Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 20 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe.Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 427

**Ujenzi wa barabara kutoka Kwasadala – Masama Mboreni na Masama Sonu**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni za mwaka 2005 pale kwenye mji wa Bomang'ombe Wilayani Hai, aliwaahidi wananchi wa Hai kuwa, barabara ya kutoka kwa Sadala kwenda Masama Mboreni na Masama kwenda Sonu yenye urefu wa km. 12.5 itajengwa kwa kiwango cha lami na kwa kuwa, umuhimu wa barabara hiyo umeongezeka zaidi kutokana na shughuli za utalii na uzalishaji mwingine kuongezeka:-

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kwasadala-Masama Mboreni na Masama kwenda Sonu yenye urefu wa km. 12.5 kwa sasa iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Barabara hii ni barabara ya udongo na changarawe. Kutoka Kwasadala hadi Masasma, barabara hii ni ya changarawe.

Sehemu hii ina idadi kubwa ya magari kwa sababu ya soko la Masama Mula, hali ambayo inayofanya matengenezo ya barabara hii kwa kiwango cha changarawe kutodumu kwa muda mrefu. Sehemu ya Masama kwenda Sonu ni ya udongo, hivyo haipitiki kwa uhakika wakati wa mvua. Barabara hii ni kati ya barabara zinazopendekezwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kilimanjaro kupandishwa hadhi kubwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais aliahidi barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami. Kuhusu kuimarishwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa, ni dhahiri kwamba iwapo itapandishwa hadhi kuwa ya mkoa Bajeti yake itaongezeka tofauti na sasa ambapo hutegemea Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Wataalam wa Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu wanatarajia kwenda kukagua barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi nchini kote ikiwemo barabara anayoizungumziwa na Mheshimiwa Mbunge. Zoezi hili linaanza kesho tarehe 21 Agosti, 2008. Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge kuvuta subira wakati zoezi nililolitaja likiendelea.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa niaba ya Serikali na hii inazidi kuonyesha jinsi Serikali ilivyo na ufuatiliaji nzuri kutokana na majibu niliyoyapata kutoka kwa Mheshimiwa Andrew Chenge akiwa Waziri na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa. Nashukuru kwa majibu mazuri. Nina swali moja tu la nyongeza.

Je, kwa sababu hiyo kazi sasa inaanza hapo kesho ya kuzipitia hizi barabara ambazo zitapandishwa madaraja na kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais anapozungumza tunaelewa fika kwamba ni agizo.

Je, hatua za kuanza kutekeleza hiyo ahadi zitachukuliwa punde tu hii kazi inapokamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema hapa ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi kuhusu hii barabara ambayo tunaizungumzia na kama tulivyosema mkakati tulionao sasa hivi ni wa kupandisha hadhi ya barabara hii ili iingie katika *TANROADS* na hivyo iweze kutengewa fedha ambazo zinalingana na mahitaji ya barabara hiyo.

Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mapema tu tutakapokuwa tumemaliza zoezi hilo na tumewasiliana na Wizara ya Miundombinu, kazi hiyo itaanza na taratibu zake ni zile za kufanya *feasibility study* na mambo mengine.

Na. 428

**Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya ya Njombe**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali ya Ilembula ina vigezo vyote vya kuwa hospitali ya Wilaya na kwa kuwa Halmashauri ya Njombe, haina kabisa hospitali ya Wilaya:-

(a) Je, Serikali haioni busara kuifanya hospitali ya Misheni ya Ilembula kuwa ya Wilaya?

(b) Je, kwa nini Halmashauri ya Njombe bado inatumia hospitali ya Kibena wakati hospitali hiyo iko chini ya Manispaa ya Njombe?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua jokofu la kuhifadhia maiti pale Ilembula-Njombe kwani kuna matukio mengi ya ajali za barabarani kati ya Mbeya na Iringa ambazo zinasababisha vifo?

**SPIKA:** Vipi majibu? Swali Na. 428 limeulizwa. Swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi ndilo linalofuata, limeelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Samahani sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na hospitali ya Serikali katika eneo lake la Utawala, Uongozi wa Halmashauri umeanza mchakato wa mazungumzo na Uongozi wa Dayosisi ya Kilutheri ya Njombe ili kuona uwezekano wa kuifanya hospitali ya Lutherani ya Ilembula kuwa hospitali Teule. Tunaamini kuwa ufanisi wa mchakato huu utapelekea huduma za afya kuwa bora zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Kibena iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Ni ukweli kwamba baada ya kuanzisha Halmashauri ya mji wa Njombe na kwa kuwa Halmashauri ya mji wa Njombe haikuwa na hospitali ya Wilaya, wananchi wamekuwa wakiendelea kutumia hospitali ya Kibena na wataendelea kutumia hospitali hiyo hadi hapo mchakato wa kuifanya hospitali ya Ilembula kuwa hospitali Teule.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia Idara ya Afya katika Bajeti ya kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya hospitali ya Ilembula. Mfano 2005/2006 zilitengwa kiasi cha Sh.36,126,068, 2006/2007 Shs.42,674,400, 2007/2008 Sh,68,768,438 na 2008/2009, Shs.43,731,600. Hivyo, ninashauri menejimenti ya hospitali ya Ilembula kuangalia suala la jokofu la kuhifadhia maiti kama kipau mbele cha wananchi na kuweka gharama za upanuzi katika Bajeti zao za mwaka.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa kibali cha tarehe 9 mwezi wa saba mwaka huu kutoka kwa Askofu Cleopa Lukilo wa Kanisa la Dayosisi ya Kusini katika vikao vyao vya utendaji kilisharidhia na kukubali kwamba hospitali ya Ilembula iwe ni Hospitali Teule ya Halmashauri ya Njombe.

Je, hapa kuna kigugumizi gani kwa Serikali kutoa maamuzi ili hospitali hii ianze mara moja?

Swali la pili, kwa kuwa sasa wananchi wana kilio kikubwa cha gharama kubwa ni kwa sababu kwamba asilimia 25 tu Serikali ndiyo inachangia. Asilimia 75 ndiyo inabeba mzigo misheni yaani Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu walau wa kuongeza mchango wake walau ufike asilimia 50 ili kupunguza makali ya gharama kubwa kwa wananchi na kupelekea huduma za afya kuwa bora zaidi?

**SPIKA:** Mhudumu hebu saidia hapo.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ningependa kwanza nimpongeze Naibu Waziri TAMISEMI kwa majibu mazuri na fasaha aliyotoa na ningependa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kevela.

Kwanza ningependa kusahihisha kwamba katika swali la msingi Mheshimiwa Mbunge ameomba Hospitali ya Ilembula iwe hospitali ya Wilaya.

Ilembula siyo Wilaya, kinachowezekana ni kwamba tutakuwa na hospitali moja tu ya Wilaya ya Njombe, lakini anachoomba ni hospitali ya Halmashauri na huo utaratibu upo na nimshukuru Askofu kwa kuridhia kwamba hospitali yake inaweza ikatumiwa na Halmashauri hasa kwa utaratibu kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba makubaliano yanaanzia kwenye Halmashauri. Wanakubaliana na Mheshimiwa Askofu halafu Wizara inakuja kuikagua hospitali hiyo kuangalia kama imekidhi vigezo vya kuweza kuchukuliwa na Serikali.

Kwa hiyo, kwa kibali hicho cha tarehe 9 kama alivyosema ni mwanzo mzuri na ningependa nimshukuru Baba Askofu. Sasa Halmashauri ilichukue hilo na kuanza kulipitisha mpaka kwenye *RCC* mpaka kuja Wizara ili tutoe kibali.

Kuhusu swali la pili amelalamika kuhusu gharama kubwa ambazo zinatolewa na wananchi. Namhakikishie kwamba hapo hospitali itakapokuwa chini ya Halmashauri, ataona ahweni katika pesa ambazo wanalipa wananchi. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Na. 429

## Utekelezaji wa Sera ya Wazee

**MHE. MARGRETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wazee bado wanakosa ulinzi wa kisheria kama Sera ya Wazee inavyoeleza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaandaa Muswada wa Sheria ili kutekeleza yale yaliyo kwenye Sera ya Wazee?

(b) Je, ni mikakati gani imeandaliwa ili kuwezesha huduma nzuri kwa wazee nchini tangu Sera ya Wazee ipitishwe mwaka 2003?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali Na. 429 lililoulizwa na Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuwa na Sera ya Taifa ya Wazee, ni kuhakikisha kuwa wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha ya kila siku kwa manufaa yao na Watanzania.

Aidha, tunalenga kuhakikisha kwamba wazee wanapata huduma zote muhimu na za msingi ambazo zitawezesha kushiriki kwa ukamilifu katika maisha ya kila siku. Nakubaliana na Mheshimiwa Mkanga kwamba Sera ilipitishwa mwaka 2003 lakini Sera bila Sheria inakuwa haina nguvu ya utekelezaji.

Baada ya kutoa maelezo hayo mafupi naomba nimjibu Mheshimiwa Margareth Mkanga, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wazee wanapata ulinzi wa kisheria kama Sera ya Taifa inavyoeleza Wizara yangu iko kwenye mchakato wa maandalizi ya rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuandaa Muswada wa Sheria pamoja na Sheria ya Watu wenye Ulemavu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utoaji wa huduma nzuri kwa wazee nchini tangu Sera hiyo ilipopitishwa mwaka 2003, Wizara yangu tayari inayo rasimu ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee na rasimu hiyo imewasilishwa kwa wadau mbalimbali ili iweze kujadiliwa na kuboreshwa baada ya kupata maoni yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchakato huu, Serikali imeendelea kuchukua baadhi ya hatua zilizomo katika rasimu ya mkakati ambazo zinalenga katika kuboresha maisha ya wazee. Kwa mfano:-

Serikali, baadhi ya Halmashauri za Wilaya na Manispaa zimeanza kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za wazee.

Serikali imetoa agizo kwa Waganga Wakuu wa Wilaya/Halmashauri na Waganga Wakuu wa Mikoa ili waanzishe kliniki za wazee kwa nia ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa kundi hili ambalo tayari sera ya uchangiaji inatoa msamaha wa kulipia matibabu.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru Serikali imekiri kwamba kwa namna fulani inachelewa kweli katika suala hili. Je, haioni kwamba inaendelea kuwanyanyasa na kutojali kundi hili kwamba Sera tangu 2003 mpaka sasa hivi ni mkakati wa rasimu, ni mkakati wa rasimu ya Sheria, rasimu hizi zitakwisha lini kama nilivyouliza lengo kwamba hivi hiyo Sheria inakuja lini? La kwanza.

Swali la pili, pamoja na kwamba kimaandishi imeelekezwa wazee waweze kupata matibabu bure kwa misamaha. Je, Serikali inafahamu kwamba mkakati huu na agizo hili hautekelezwi hapa nchini, wazee bado wanaendelea kupata shida kwenye matibabu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba Serikali haiwanyanyasi watu wenye ulemavu na wazee na kuchelewa ni kutokana na kutaka ufanisi katika shughuli zenyewe. Kwa sababu mikakati ilipoandaliwa imebidi tutafute maoni ya wadau wakiwamo wazee na kwa jinsi nchi yetu ilivyo kubwa imechukua muda kidogo. Lakini siwezi kusema ni lini hasa, tunategemea kwamba katika kipindi cha mwaka huu wa fedha hiyo sheria italetwa hapa Bungeni ili iweze kuridhiwa.

Suala la pili ilihusu matibabu ya wazee. Nimkumbushe tu kwamba Mheshimiwa Mbunge wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Afya hili lilijitokeza na hapa tulikiri kwamba tutaliangalia kwa kina kwa sababu sera iko wazi lakini kinacholalamikiwa ni utendaji. Tulisema tutatafuta mipango maalum ya kuhakikisha kwamba inatekelezwa na katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tumewaandikia Waganga Wakuu katika Halmashauri katika Wilaya na katika Mikoa kwamba watenge kliniki maalum ili tuweze kuwatambua kwa urahisi kuliko ilivyo kawaida kwamba walikuwa wanakuwa kwenye mstari pamoja na wengine. Kwa hiyo, naona utekelezaji umeanza na tutakiane kheri, wote tusimamie hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja fupi la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba *definition* ya Mzee, maana mzee hata Spika wangu kwetu akifika tutamwita mzee. Sasa naomba *definition* kamili ya neno mzee. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamruhusu Mheshimiwa Waziri kujibu, naona kumekuwa na mwelekeo au mkakati siku hizi wa kumtania tania Spika hapa. Kuna alisema Spika ana kipara. Kwa hiyo, anaweza akanyolewa, akanyofolewa kichwa. Leo mimi nawekwa ndiyo kigezo cha uzee. Basi ni vizuri tu inafurahisha, lakini angalieni wengine msije mkavuka kipimo, kiwango kwa sababu Kanuni za sasa naweza kukutoa nje kwa siku tatu. Lakini Waziri hebu tupatie majibu. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika sheria zozote zinazoletwa hapa maneno yanayotumika mara kwa mara yanatolewa ufafanuzi kwa maana ya *definition* na sheria itakapoletwa tutaleta hiyo. Lakini utekelezaji wa Sera iliyopo sasa hivi kuhusu matibabu tunazungumzia habari za wazee watu ambao wamefikisha miaka 60 na niongeze kwamba ni wale ambao wanashindwa kulipia gharama za matibabu. Lakini vile vile naomba niongeze kwamba wanasema *age* iko katika akili ya mtu. Kwa sababu unaweza ukawa na miaka 80 lakini akili yako inakwenda kama kijana wa miaka 25. Unakumbuka kila kitu lakini kuna wengine wana miaka 45 ni wazee kabisa katika kufikiri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi wako nzuri sana. Tunaendelea Waheshimiwa na swali linalofuata Wizara hiyo hiyo.

Na. 430

**Ugonjwa wa Fistula Obstetrikia**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. MASOLWA C. MASOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa *Fistula Obstetrikia* ni hatari kwa wanawake wajawazito na hasa wanaoishi vijijini ambako huduma za afya ni duni:-

(a) Je, nini chanzo, dalili,athari na tiba za ugonjwa huo?

(b) Je, ni wagonjwa wangapi nchini waliokufa au kuathirika tangu kugundulika kwa ugonjwa huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kule Zanzibar lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimaudhui swali hili linafanana na swali Na. 49 lilioulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, ambalo lililoulizwa tarehe 2 Novemba 2007 katika Mkutano wa Tisa wa Bunge. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu wakati huo, fistula ni tundu linalotokea baada ya kujifungua, tundu hilo linatokea katika misuli kati ya uke na kibofu cha mkojo au kati ya uke na njia ya haja kubwa au sehemu zote mbili.

Chanzo cha tatizo hili ni kuwa tundu hutokea kutokana na uchungu unaoendelea kwa muda mrefu na uzazi pingamizi, ambapo mgandamizo wa kichwa cha mtoto kwenye mifupa ya nyonga kwa muda mrefu katika njia ya uzazi unazuia damu kuingia na kutoka

kwenye misuli hiyo laini na kusababisha misuli hiyo kulainika na kufa na hatimaye kuachia.

Baada ya hapo hilo tundu linaloitwa (Fistula) hutokea kati ya uke na kibofu cha mkojo au kati ya uke na njia ya haja kubwa au sehemu zote mbili. Ziko sababu nyingi zinazosababisha uzazi pingamizi, baadhi yao ni mlalo mbaya wa mtoto tumboni, mtoto kuwa mkubwa, nyonga ndogo hasa kwa wanawake wenye umri mdogo chini ya miaka 20 na wanawake wafupi chini ya cm 150.

Mheshimiwa Spika, dalili za *Fistula Obstetrikia* ni kuvuja mkojo au haja kubwa kupitia njia ya uzazi wakati wote na pasipo hiari. Aidha, athari zake ni pamoja na kuchafuka, kutokwa na harufu mbaya wakati wote, kuvunjika kwa ndoa, kutengwa na jamii na kuathirika kisaikolojia na hivyo kupunguza uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Ugonjwa huu hutibiwa kwa njia ya upasuaji kwa kuziba tundu linalovujisha mkojo au haja kubwa kwenye njia ya uzazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa ya mgonjwa aliyekufa kutokana na *fistula obstetrikia* moja kwa moja kwani kwa kawaida wagonjwa wanaopata ugonjwa huu ni wale walionusurika kufa wakati wa uzazi.

(c) Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa *fistula* unajitokeza nchi zote duniani lakini hutokea kwa kiwango kikubwa katika nchi zinazoendelea, hususan zile zilizoko Barani Afrika kusini mwa jangwa la Sahara.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini naomba niulize maswali madogo kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba Mheshimiwa Waziri atueleze tatizo na ukubwa wa tatizo hili katika nchi yetu. Tatizo hili ni kubwa kwa kiasi gani?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba matibabu ya ugonjwa huu ni kwa upasuaji tu. Lakini wengi tunajua kwamba huduma za upasuaji katika nchi hii na hususan katika maeneo ya vijijini pengine hazipo kabisa.

Sasa nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba huduma za upasuaji hasa katika hospitali za Wilaya na katika vituo vya afya zinaimarishwa ili matatizo haya yanapojitokeza kwa akina mama waweze kupata matibabu hayo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ukubwa wa tatizo nadhani hili linazungumzia habari za takwimu ambazo sinazo hapa sasa hivi.

Lakini ninaweza kusema tatizo linapungua kutokana na utambuzi kwa sasa hivi akina mama wengi wanajua umuhimu wa kuzalia katika hospitali na kwa jinsi wanavyojitokeza tunaweza tukatambua wale ambao wanaweza wakapata matatizo ya

kuelemewa kwa maana ya kuwa na uzazi ambao utahitaji operesheni au kusaidiwa na hospitali.

Lakini kama ni kutafuta takwimu, hizi naweza nikazitafuta na kumpa mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuonyesha *trend* kwamba miaka iliyopita ilikuwa hivi na sasa tunaelekea wapi.

Suala la pili ilikuwa ni upatikanaji wa hizi huduma kwa watu walioko vijijini. Mkakati mzima uliopo katika mpango wa maendeleo ya Afya ya Msingi ni kuboresha huduma ya uzazi wakina mama.

Moja ya mambo ambayo yanapewa mkazo ni kwamba kina mama wajifungulie katika vituo vya huduma za hospitali. Wakifanya hivyo, tunaweza kwa urahisi kabisa kutambua kwamba mama gani atahitaji msaada na kwa maana hiyo hili tatizo litapungua sana na hivi sasa vile vile tunao madaktari wengi katika orodha yetu ambao wana uwezo wa kufanya hiyo operesheni na ni hospitali chache sana za Wilaya ambazo zinaweza zikafanya hiyo operesheni.

Kwa hiyo, pale watakapotambulika watapelekwa mahali ambapo hiyo operesheni inaweza ikafanyika.

**SPIKA:** Maswali mafupi sana ya nyongeza. Moja kutoka kwa Mbunge mwanamke na moja kutoka Upinzani. Mhesihmiwa Faida Bakar, halafu Mheshimiwa Dr. Slaa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya watu hasa wanaoishi vijijini wanauhusisha ugonjwa huu wa *fistula* na imani za kishirikina na kwa kuwa mwanamke anapopata tatizo hili huwa baadhi ya watu wanamtenga kutokana na kutokwa kile choo kidogo na kikubwa na kupelekea kunuka au kutoa harufu.

Je, Serikali inatoa tamko gani thabiti hapa Bungeni dhidi ya watu hawa wanawatenga wanawake wanaopatwa na maradhi haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwa kirefu jinsi ugonjwa wa *fistula* unavyotokea na nimechukua muda kuliko ilivyo kawaida ya maswali ili sisi kama Wabunge tuweze kuelewa na sisi kama wawakilishi wananchi tunapokwenda kwenye majimbo yetu tuweze kuwaeleza.

Ugonjwa wa *fistula* hauna uhusiano na masuala ya kishirikina ingawa sijui kishirikina ni kitu gani na kama Serikali ni vigumu kutoa tamko kwa maana ya Serikali kwamba kuanzia sasa watu wasiwatenge.

Mimi nadhani ni kuwaelewesha lakini muhimu zaidi ni kwamba hao ambao wanatengwa kwa sababu ya *fistula,* waende hospitali ili wakatibiwe na hii harufu mbaya inayotoka waweze kuondokana nayo na wataingia kwenye jamii bila matatizo.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ugonjwa wa *fistula* umeingizwa katika listi ya Shirika la Afya la Dunia *(WHO)* na kwa kuwa ugonjwa huu kwa tabia yake hawa wanaohusika hata wao wenyewe wanaogopa kujitokeza na kwa kuwa ugonjwa huu sasa umethibitika kwamba unatibika.

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuelimisha jamii yetu ili hawa akina mama wasiendelee na athari hasa ikizingatiwa kwamba unawapata wale ambao wako katika umri mdogo waweze kujitokeza na waweze kurudi kwenye maisha ya kawaida kama akina mama wengine?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Wilbroad Peter Slaa, kama ifuatavyo.

Swali lake linaenda sambamba na la Mheshimiwa Faida Bakari, ambalo nilisema hapa kwamba nia ni si Serikali peke yake, tunao mkakati na kitengo maalum cha elimu ya jamii. Na kwa jinsi mambo yanavyojitokeza tunayapangia mikakati hili ni moja ya masuala ambayo tungependa tuwaelimishe na liko katika tunaita *at netal clinic work,* kinamama wanapokuja kujifungua tunawaeleza kwamba endapo matatizo yatakupata uende mapema hospitali.

Kuna wengine wana watoto wakubwa, tunaweza tukang'amua mapema tunawashauri kwamba walale hospitali lakini kiujumla ni kwamba sisi wote tuelewe kwamba ugonjwa unatibika. Kwa hiyo hawa akina mama wasije wakaona kwamba wanabahati mbaya kwa kupata hilo suala. Muhimu ni kuzuia, lakini tukishindwa kuzuia hao ambao kwa bahati mbaya wanapata haya matatizo wajue kwamba kuna mahali pa kukimbilia ili ile adha wanayoipata iweze ikaondoshwa na madaktari wenye uwezo huo. *(Makofi)*

Na. 431

**Rasilimali Iliyomo Mkoa wa Rukwa**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Rukwa una kila aina ya rasilimali zinazoweza kupatikana mahali popote ikiwa ni pamoja na madini, mbuga za wanyama, maziwa yenye samaki wengi, na kadhalika:-

(a) Je, Serikali inausaidiaje mkoa huu ili ujulikane kwa wahisani wa nje na ndani?

(b) Kwa kuwa, Serikali ya Norway ilifanya kazi nzuri sana katika miradi mingi ya kusaidia Mkoa wa Rukwa katika Maendeleo kwa miaka ya 80. Je, kwa nini sasa Serikali isiwaombe wahisani hao, *Norway,* wakarejea tena kuendeleza kazi nzuri waliyoianza?

(c) Kwa kuwa, Wajerumani wana historia ya Mkoa, kwa boma na Ngome Kuu ya Kasanga ya Bismark. Je, kwa nini Serikali isiwaombe waje kuimarisha kivutio hicho cha utalii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Rukwa una rasilimali nyingi kama vile madini ya dhahabu, *phosphate, galena,* na kadhalika.

Pia una mbuga ya wanyama ya Katavi ambayo wanyama wake ni wakubwa kuliko wale wa kawaida na ina Twiga mweupe. Aidha, mkoa una Ziwa Tanganyika ambalo lina samaki wenye rangi za mapambo pia una ziwa Rukwa ambalo lina Mamba wengi.

Kwa vyovyote vile, Rukwa ina vivutio vingi na ni sehemu ya Tanzania, hivyo Serikali ina wajibu wa kuutangaza Mkoa huu kwa wawekezaji na wahisani mbali mbali kwa lengo la kusukuma zaidi Maendeleo. Katika kuitekeleza azma hii, mnamo tarehe 1 – 2 Juni, 2007, Serikali iliandaa Kongamano la wawekezaji kwa lengo la kutangaza vivutio vilivyomo ndani ya mkoa huu. Matokeo ya Kongamano hilo yanaweza kuwavutia wawekezaji na wahisani mbali mbali wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, (b) na (c) naomba kuyajibu kwa pamoja. Ni kweli Serikali ya Norway kwenye mwaka ya 1980, ilifanyakazi nzuri sana katika mkoa wa Rukwa na napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuishukuru sana Serikali ya Norway pamoja na wahisani wengine kwa misaada wanayoipatia nchi yetu.

Aidha napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekubaliana na wahisani wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na Serikali ya Norway na Ujerumani kwamba kuwepo na utaratibu wa pamoja wa kuchangia Maendeleo kupitia kwenye Bajeti ya Serikali, *General Budget Support.*

Utaratibu huu ambao ndio tunaoufuata unatupa fursa na uhuru wa kupanga na kutekeleza vipaumbele vyetu kwa kuzingatia matatizo yaliyopo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa maana hiyo, haitakuwa rahisi kuwaomba wahisani kurejesha utaratibu wa zamani ambao ulihudumia moja kwa moja mikoa kwasababu utaratibu tunaoendelea nao haujaonyesha matatizo.

Kwa kupitia Bunge lako Tukufu nichukue fursa hii kuziomba Wizara, Mikoa na Halmashauri kujipanga na kuandaa miradi kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na kuwasilisha Hazina kwa mazingatio.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa kuwa twiga mweupe anapatikana katika Mbuga ya Katavi ambayo ni sehemu ya jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu na ni twiga peke yake duniani ambaye anaweza kuonekana sehemu hiyo.

Lakini kwa kuwa utaratibu wa sasa wa kudhani twiga huyo ni albino wameanza kumvizia na wanataka kummaliza kabisa. Kwa msingi huo. Je, Waziri atakuwa atakubaliana nami ya kwamba kuna haja sasa kuanza kufanya sensa ya twiga hao weupe wako wangapi na pili kuhakikisha wataalamu wa mali asili wanawalinda hao ili wasije wakapotea na watu wenye uchu wa kutaka utajiri wa haraka haraka?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili. Ili kuwa na wawekezaji katika mkoa wowote ni lazima miundombinu iwepo ikiwemo barabara, maji, umeme na vitu vingine. Na kwa kuwa mkoa wa Rukwa, umepangiwa kuanza kutengeneza barabara ya lami ambayo iko chini ya *MCC* kwa mwaka huu wa fedha. Je, Waziri anatuambia ni sababu zipi za zimefanya fedha za *MCC* zimewekwa Hazina badala ya kuweka Miundombinu? Na mutuambie ni lini barabara hiyo itaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI ( MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paul Kimiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimfahamishe tu Mheshimiwa Paul Kimiti, kwa taarifa ambazo nilizonazo kwamba huyu twiga mweupe ameanza kuonekana na watoto anafuatana nao. Lakini nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kufanya hiyo sensa ili tuweze kujua kwamba hawa twiga weupe wako wangapi.

Mheshimiwa Spika, la pili kwa hilo hilo la kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna haja kwa wataalamu wetu wa maliasili kuwalinda hawa twiga weupe. Hilo ni kweli kabisa na tutawashauri wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba wataalam wao wanawalinda hawa twiga weupe ili wasije kudhuriwa na wasije kutoweka katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la nyongeza la pili aliuliza suala la fedha za barabara za *MCC* kuwekwa chini ya Wizara ya Fedha badala ya kuwekwa chini ya Miundombinu. Nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba *MCC* tuna miradi mingi sana sio miradi ya barababara tu. Tuna miradi ya umeme, tuna miradi ya barabara na tuna miradi mingine.

Kwa utaratibu wa kuanza na hizi fedha kwa makubaliano pamoja na wenzetu wamarekani ambao ndio waliotusaidia hizi fedha tumekubaliana kuanzia kwanza tuanzie na Wizara ya Fedha na tuwe na kitengo maalumu cha kusimamia. Lakini baadaye tukiendelea na mambo yetu vizuri ndio tutaanza kuzipeleka katika sekta husika.

**SPIKA:** Majibu ya ziada Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kuongezea kwenye majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Paul Kimiti kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshatoa maelekezo kwa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, *TAWIRI*, kufanya sensa ya wanyama wote kwa mwaka huu wa fedha. Miongoni mwa wanyama watakaofanyiwa sensa hiyo ni pamoja na hao twiga weupe. Kadhalika, tumeshapewa taarifa na watafiti wetu kuhusu uwepo wa twiga huyu mweupe na hatari yake ya kutoweka. Tumeshatoa maelekezo kwa idara yetu, kwa *Tanzania National Parks*, *Katavi National Park*, ili waweze kuimarisha ulinzi wa wanyama hao. Kwa hivyo nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba sensa hiyo tunaifanya. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Waziri, ametaja baadhi ya madini ambayo yanapatikanika katika mkoa wa Rukwa, lakini pia kuna vito na ulanga. Wakati tunasubiri wahisani au wafadhili au wawekezaji kuja kuendeleza mkoa wa Rukwa, wananchi wake hasa wachimbaji wadogowadogo wanaweza kuchimba vito na ulanga. Je, Wizara yako iko tayari kuwasaidia wachimbaji hawa wadogowadogo kujua masoko ya kuuza ulanga na vito?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuwasaidia wananchi wake.

Kwahivyo nakubaliana naye kabisa kwamba kama tulivyoanza kwa mkoa wa Mwanza kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo na kwa mkoa wa Rukwa nao wakati ukifika Serikali itawasaidia wachimbaji wadogo wadogo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, kongamano la wawekezaji lililofanyika Mkoani Rukwa, Mheshimiwa Waziri, amesema mkoa wa Rukwa uliwavutia sana watalii kuweza kuwekeza mkoa wa Rukwa, lakini mpaka dakika hii hakuna wawekezaji waliovutiwa sana na mkoa wa Rukwa. Hakuna hata mmoja ambaye amerudi kuja kuwekeza. Utafiti umeonyesha ni kitu gani hasa au ni vitu gani ambavyo vimewachochea wawekezaji wasirudi tena kuja kuwekeza licha ya kusema wamefurahia sana uwekezaji katika mkoa wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyami, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kongamano hili limefanyika mwaka 2007 na sasahivi tuko mwaka 2008, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba wiki iliyopita nimezungumza na Mkuu wa Mkoa, kuhakikisha kwamba ili kuelewa matokeo ya kongamano hili.

Nataka nimwambie wamejitokeza wawekezaji wanataka kuwekeza katika viwanda vya kusindika mafuta na vilevile wamejitokeza wawekezaji wanataka kuwekeza katika sekta ya utalii. Kwa maana ya kuwekeza katika hoteli. Wapo wawekezaji wa Tanzania na nje ambao wamejitokeza na baadaye naweza nikampatia orodha ya wawekezaji hao na nchi wanazotoka. *(Makofi).*

Na. 432

**Maafisa Ugani**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa mkoa wa Dodoma wameanzisha kilimo cha Korosho, Jatropha na mazao mengine mageni lakini kuna tatizo kubwa la maafisa ugani na Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 ilitarajia kuajiri maafisa ugani 2500:-

Je, ni Maafisa ugani wangapi walioajiriwa mwaka 2007/2008 na kupangiwa vituo vya kazi kwenye mkoa wa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa, ilipanga kuajiri wataalam wa ugani 2,500 mwaka 2007/2008.

Hata hivyo kutokana na upungufu wa wataalam wa ugani ambao walitegemewa kupatikana kwenye soko na hususan, katika ngazi ya Afisa Kilimo Msaidizi Daraja la pili, wataalamu walioajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika mikoa mbalimbali walikuwa 309 tu. Mkoa wa Dodoma ulipangiwa wataalam sita tu. Kati ya hao Maafisa Kilimo walikuwa wanne na Maafisa Kilimo Wasaidizi walikuwa wawili.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wizara ilitarajia kuajiri wataalam 2500 na waliopatikana ni 309 tu na mkoa wa Dodoma tukapangiwa wataalam sita tu. Je, Naibu Waziri, anaweza kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tatizo la kuwapata wataalam hao ni nini? Kwani Serikali ina vyuo vya kuwasomesha wataalamu wa kilimo katika vyuo mbalimbali hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, lengo la Serikali ni kilimo kumkomboa mkulima na kama kaulimbiu ya nane nane mwaka huu ilivyosema kwamba mkombozi wa mkulima ni *Green Revolution.* Je, wananchi wa Mkoa wa Dodoma ambao wameamua kulima mazao ya biashara kama vile korosho, jatropha, na mazao mengine, watafikia lengo la kukombolewa na mapinduzi ya kijani lini kama wataalam hao hawatoshelezi katika mikoa yetu?

**NAIBU WAZIRI KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Tatizo kubwa lililosababisha tusipate wataalam wa kutosha ni kwa sababu tulikuwa tunatumia wale wataalam wa stashahada, yaani *Diploma*. Na wale wa *diploma* hawapo wengi kwenye soko, wale wa *Degree* pia hawapo wengi kwenye soko kwa maana wanachukuliwa na makampuni binafsi na wao wenyewe wanajiajiri. Sasa tutakachokifanya mwaka huu ni kwamba tutachukua wale waliomaliza na kufaulu *form IV* ambao tutawasomesha ngazi ya astashahada, yaani cheti, kusudi waweze kwenda kutimiza lile lengo la kuajiri 2500 kwa mwaka. Mwaka huu tu, wiki mbili zijazo tutapokea wanafunzi 3000 ambao watasoma kwenye vyuo vyetu vya kilimo kusudi tuweze kupata wale 3000 na tuweze kuwaajiri 2500 kila mwaka tuweze kuziba lile pengo hadi 2011 tutakuwa tumeshawaajiri wataalamu wa ugani 11,703.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mapinduzi ya kilimo yatapatikana kwasababu tayari kwa suala hili la maafisa ugani tayari tumeshaona tatizo ni kwamba tulikuwa tunategemea zaidi *form VI* na sasa tunachukua *form IV*. Kwa hiyo, wale wako kwa wingi na tutawapata. Kwa hiyo, ni dhahiri tutapata wataalam wa ugani wa kutosha.

Na. 433

**Matatizo ya Wananchi wa Kijiji cha Tanganyika – Kilombero**

**MHE. CASTOR R. LIGALAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo kubwa linalowakabili wananchi wa kijiji cha Tanganyika Kata ya Masagati wilayani Kilombero ni ukosefu wa barabara ya kuunganisha kijiji hicho na makao makuu ya Kata Taweta, Kilometa 25, pamoja na ukosefu wa daraja la kudumu katika mto Mfuji; na kwa kuwa, ili wananchi hao waendelee kuishi katika wilaya yao ya asili, suluhu siyo kuwahamishia njombe, bali kuwatatulia matatizo sugu waliyonayo:-

(a) Je, Serikali inaweza kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, daraja la kudumu katika mto huo ambao kutokana na ukubwa wake Halmashauri haiwezi kumudu kulijenga daraja hilo?

(b) Kwa kuwa barabara ya Taweta hadi Madeke, Njombe, zimepatiwa fedha za kuitoboa. Je, Serikali itakuwa tayari kukiingiza kipande hicho cha barabara kwenye barabara ya mkoa kwa kuzingatia kwamba kutoka Njombe hadi Madeke ni barabara ya mkoa na kutoka Ifakara hadi Taweta ni barabara ya mkoa.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) pamoja na masahihisho kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, daraja la mto Mfuji lipo kwenye mtandao wa barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na inahitaji fedha nyingi kulijenga. Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu haina uwezo wa kugharimia ujenzi wa daraja hilo. Kwa hiyo tunashauri Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Halmashauri ya Kilombero ili itenge fedha katika Bajeti yake kwa awamu kukamilisha ujenzi wa daraja hilo. Wizara yangu ipo tayari kusaidia kutoa utaalamu kama utahitajika.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Taweta hadi Madeke – Njombe, yenye urefu wa kilometa 16 ni mpya na hivi sasa inachongwa kutoka kijiji cha Taweta kwa upande wa wilaya ya Kilombero hadi kijiji cha Madeke Upande wa wilaya ya Njombe, kazi hiyo inafanywa na Wizara yangu kupitia wakala wa barabara, *TANROADS,* Morogoro. Barabara hii ni moja ya barabara zilizopendekezwa na bodi ya barabara ya mkoa wa Morogoro ili zipandishwe daraja na kuwa barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kukamilisha Kanuni za sheria, *Regulations,* kwa ajili ya kupanga barabara zote katika madaraja husika kulingana na vigezo vilivyoainishwa katika Sheria. Zoezi la ukaguzi wa barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi linaanza mwezi huu wa Agosti, 2008. Hivyo basi ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wavute subira wakati kazi hiyo inaendelea kukamilishwa.

**MHE. CASTOR R. LIGALAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Naibu Waziri amesema hataweza kutusaidia kujenga hilo daraja, lakini anakuja tena anasema yuko tayari kutoa utaalamu. Je, ni utaalamu gani huo anaoweza kutusaidia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwanza napenda niishukuru Serikali kwa kutuwezesha kutupa fedha za kutoboa ile barabara, kazi inaenda vizuri bado kilometa tano.

Lakini suala la kupandisha madaraja ya barabara limeongelewa sana hapa Bungeni. Je, Waziri, atakuwa tayari kutoa *time frame* ya kumaliza mchakato wa kubadilisha kanuni ili madaraja ya barabara yaweze kupandishwa sio katika mkoa wa Morogoro tu, lakini katika nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Castor Ligalama, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaalamu niliouelezea ambao Wizara yangu iko tayari kuutoa ni ule wa kiujuzi zaidi.

Kwa hiyo, nilichokuwa nataka kueleza hapa ni kwamba endapo Wilaya ya Kilombero itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo tukizingatia kwamba pengine itahitaji utaalamu wa hali ya juu sana kuweza kushauriwa ili daraja hilo lijengwe katika kiwango kinachostahili huo utaaolamu niliouelezea kwamba Wizara itakuwa iko tayari kuutoa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu upandishaji wa madaraja. Nimeeleza hapa na asubuhi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, *TAMISEMI*, ameeleza vilevile kwamba zoezi hili la kukamilisha shughuli ya upandishaji haya madaraja ya barabara limeanza kuanzia tarehe 20 Agosti, 2008 timu za wataalam kutoka Wizarani zitapita kukagua zile barabara ambazo zimependekezwa na mikoa nchini kote ili zoezi hilo liweze kukamilika. *(Makofi).*

Na. 434

**Kutengeneza Daraja la Mto Simiyu**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa, daraja la mto Simiyu katikati ya vijiji vya Lumeji na Ng'haya jimboni Magu, linaharibika mara kwa mara kwasababu ya kuzidiwa na ukubwa wa wingi wa magari yanayopita hapo yakielekea ama yakitoka wilaya za Magu, Bariadi na Kwimba na hivyo kutishia usalama wa magari na maisha ya wananchi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inapoteza pesa nyingi zaidi kwa kukarabati daraja hilo kila baada ya muda mfupi badala ya kulijenga kabisa moja kwa moja?

(b) Je, ni lini ahadi ya kulitengeneza daraja hilo lililokuwa la muda ili liwe la kudumu, imara na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miondombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa mwanza, ililifanyia usanifu daraja la mto Simiyu katika mwaka wa fedha wa wa 2007/2008 kwa gharama ya 104,000,000/=. Kulingana na usanifu huo, kiasi cha shilingi bilioni 1.96 zinahitajika kulijenga daraja hilo. Wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha ya kujenga upya daraja hilo, Wizara yangu kupitia Wakala wa barabara Mkoa wa Mwanza, imeendelea kulifanyia matengenezo kuhakikisha kuwa linaendelea kutumika kwa usalama.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na napenda kuipongeza sana Serikali, kwa kutenga 104,000,000/= katika Bajeti iliyopita kwa ajili ya kufanya usanifu na kwamba sasa zinahitajika bilioni 1.96.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Daraja hili lilikuwa ni la muda na lilijengwa mwaka 1969 na kufunguliwa mwaka 1971 na Rais wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Abeid Amani Karume, mwaka 1971. Sasahivi ni miaka 37 imepita daraja hili lilikuwa la muda au lilikuwa la kudumu? Na katika kipindi hicho limekuwa likitumia 30,000,000/= kila mwaka kutengenezwa kwa miaka 30 hii ni kama bilioni 1.1. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuendelea kutenga fedha kidogokidogo ni kupoteza fedha za wapiga kura badala ya kutenga fedha maramoja daraja likajengwa likakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema fedha zitakapopatikana litajengwa, baada ya kujulikana sasa ni bilioni 1.9, Lakini katika Bajeti ya mwaka huu zimetengwa 150,000,000/= kwa daraja hili na mimi niliamini kwamba 150,000,000/= zimetengwa kwasababu gharama halisi ilikuwa haijajulikana, Kwa hiyo 150,000,000/= ilikuwa kama *token.* Kama linakarabatiwa kwa 30,000,000/= kila mwaka kwa mwaka huu zimetengwa 150,000,000/= maana yake ni kwamba hii ilikuwa ni kianzio tu kwamba gharama zitakapojulikana fedha zitapatikana ndani ya Bajeti ya serikali.

Je, Waziri atanihakikishia kwamba 150,000,000/= zilizotengwa ilikuwa *token* ili sasa 190,000,000/= zitafutwe katika Bajeti hii ili daraja lijengwe kuondoa adha za madhara yanayopatikana kutokana na daraja kuharibika mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miondombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Limbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu kutenga fedha kidogo kidogo kila mwaka. Kama nilivyoeleza hapo awali, kwamba huu utengaji wa fedha kidogo kidogo ni kuliwezesha tu hili daraja liweze kundelea kupitika kwa usalama wakati jitihada za kupata fedha nyingi za kulijenga kwa ukamilifu unaostahili liweze kuwa la kudumu unaendelea lakini fedha hizi kidogo kidogo zinapangwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. La sivyo kama kungekuwa na fedha za kutosha basi hili zoezi la kupanga fedha kidogo kidogo lisingekuwa linatokea na ndio maana sasahivi kazi iliyofanyika ya kulifanyia usanifu,

Sasa limeshaainisha kiasi cha fedha inayotakiwa. Kwa hiyo sasahivi zoezi linaloendelea ni la kutafuta kiasi hicho cha fedha bilioni 1.9 ili daraja hilo liweze kujengwa katika hali ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili labda tu nifafanue. Katika hizi fedha 150,000,000/= ambazo Mheshimiwa Mbunge hapa anmezielezea, fedha hizi kwa kusema kweli zilikuwa zimetengwa kwa kukusuudia kuendeleza usanifu yakinifu katika daraja lile lakini ilipoainishwa kwamba usanifu ulikuwa umekamilika fedha hizi 150,000,000/= kama itakavyofahamika kwamba mto huu Shimiyu ni mto mrefu na unagusa maeneo mengi fedha hizi sasa imeamuliwa na imeelekezwa kwamba zikatumike katika daraja la mto huu huu katika upande wa wilaya ya Kwimba kule kwenye jimbo la Sumve ili usanifu yakinifu uweze kufanyika ili nako huko fedha ziweze kuanza kutafutwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja haya.

Na. 435

**Biashara za Jinsia**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. DEVOTA M. LIKOKOLA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kukuza Sekta ya Biashara ya Jinsia:-

(a) Je, nchini kwetu kuna chama chochote cha wafanyabiashara wanawake?

(b) Je, ni nani wafanyabiashara wakubwa wanawake katika nchi yetu?

(c) Je, serikali inawasaidiaje wanawake hao wanaofanya biashara zao nzuri ili nao wawasaidie wanawake wengine?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vipo vyama vingi vya wafanyabiashara wanawake vilivyoanzishwa hapa nchini. Baadhi ya vyama hivi ni pamoja na Chama cha Wachimba Madini Wanawake kinachoitwa *Tanzania Women Miners Association (TAWOMA),* Chama cha Wasindikaji Chakula – *Tanzania Food Processing Association (TAFOPA), Imani Women Development*, Chama cha Watoa Huduma (*Service Providers Association (SEPA). Kawe Women Development Fund, Tanzania Women Development Association*, Chama cha Wanawake Katika Biashara ya Kilimo (*African Women Agribusiness Network (AWAN),* na *Federation of Association of Women Entrepreneurs Tanzania (FAWETA).*

Aidha, Wanawake wafanyabiashara wameunda Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (*Tanzania Women Chambers of Commerce (TWCC)* ambacho vyama vya wafanyabiashara Wanawake vinaweza kujiunga nacho ikiwa kama kiungo cha vyama vyote vya kibiashara vya Wanawake Tanzania.

Chama hiki ni Mwanachama wa Chama cha Wafanyabiashara, wenye viwanda na Kilimo Tanzania (*Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA)* na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)*

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu Wanawake wafanyabiashara wakubwa, nakiri kuwa utafiti wa kubaini Wanawake wafanyabiashara wakubwa haujafanyika kwa kuwa usajili wa makampuni ya biashara hauzingatii jinsia za wamiliki na hivyo takwimu za umiliki wa makampuni kwa jinsia haujaandaliwa kwa sasa.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwasaidia wafanyabiashara wote, wakiwemo Wanawake, kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, usindikaji, ufungashaji, usimammizi mzuri wa biashara, kubaini masoko ya ndani na nje, kubaini teknolojia na matumizi yake, ubora wa bidhaa, kupatikana kwa mikopo kwa ajili ya mitaji ya miradi yao na taarifa za biashara, uchumi, masoko, sera na kuwashirikisha kwenye maonyesho ya biashara ya ndani na nje. Serikali inatumaini kuwa wafanyabiashara wanawake wataitumia vema Benki au Taasisi ya Fedha ya Wanawake itakayoanza hivi karibuni kama chanzo cha mitaji ya kuboresha biashara zao.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili nadogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa ametufahamisha kwamba hakuna taarifa maalum zinazoweza kuonyesha idadi ya wafanyabiashara

wakubwa Wanawake na hivyo inasababisha kuwepo na ugumu katika kuleta mawasiliano ya karibu au *linkages* kati ya hawa wafanyabiashara wakubwa na wadogowadogo kwa maana kwamba wanapotokea wakubwa ndivyo na wadogo wanavyoweza kupata fursa.

Je, Mheshimiwa Waziri ataweza kufanya utafiti huo mapema iwezekanavyo ili kuweza kufahamu ni kwa jinsi gani Wanawake wanashiriki katika masuala ya biashara?

La pili, kwa kuwa wajasiriamali hasa waishio vijijini wanakabiliwa na matatizo au changamoto za aina mbalimbali ikiwemo hata namna ya kubuni biashara za kufanya na pia maeneo hayo ndiyo yanakuwa yana raslimali nyingi za kuweza kuibua biashara.

Na kwa kuwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *UDEC* wanatoa mafunzo hayo. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka angalau akina mama 50 kutoka kila Mkoa kuweza kupata mafunzo hayo katika chuo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, kama ifuatavyo;

La kwanza, Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, ni kweli kwamba utafiti wa kufahamu idadi ya wafanyabiashara wakubwa na wale wadogo haujafanyika.

Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba ili kuweza kuweka makundi hayo mawili kuyatenganisha ni lazima tufahamu kwamba ni vigezo gani vinavyotumika pale na kiasi cha kodi kinacholipwa, idadi ya wafanyakazi ambao wanaajiriwa katika kampuni ndiyo wanafanya kampuni inakuwa kubwa na vilevile kuna kampuni nyingine zinamilikiwa na mtu mkewe au mfanyabishara mwanamke na mwanaume.

Kwa hiyo, ni lazima kazi kubwa ifanyike hapo na Wizara yangu inaahidi kwamba inapokea hiyo kama changamoto lakini tutafanya hivi kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ili tuweze kukubaliana kuhusu vigezo vya kuweza kutenganisha wafanyabishara katika makundi hayo mawili yaani kundi kubwa na kundi dogo ili kuwafanya wafanyabishara wakubwa wakina mama waweze kuwasaidia wenzao ambao wanahitaji kusaidiwa.

La pili, kuhusu ujasiriamali vijijini. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba kada hii ya wajasiriamali kule vijijini ndiyo ambayo inahitaji kusaidiwa zaidi kwa sababu ndiyo ambayo kwa kweli ufahamu wao kuhusu ujasiriamali ni mdogo.

Kuhusu hiki kitengo cha Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho amekisemea hapa, kwanza naomba niseme kwamba kitengo hiki kimeanzishwa kutokana na jitihada za Serikali. Serikali imetambua umuhimu wa kuwasaidia wajasiriamali wote wa jinsia zote mbili na akima mama wanafaidika pale.

Kama Serikali itaamua kuwapeleke wajasiriamali 50 kutoka kila Wilaya hilo ni suala ambalo siwezi kulitolea maamuzi hapa lakini naomba nilichukue kama changamoto tuangalie na uwezo wa Serikali wa kuhakikisha kwamba hivi vitu vinafanyika.

Lakini napenda nisisitize hapa kwamba ni vema zaidi maombi ya kujiunga na taasisi hii yakaanza katika ngazi ya wajasiriamali wenyewe na Halmashauri zetu zinaombwa kusaidia katika hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ingawa muda wa maswali sasa umepita lakini naona tumalizie swali la mwisho linaloelekezwa Wizara ya Nishati na Madini na linaulizwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Jimbo la Sikonge.

Na. 436

**Hitaji la Umeme – Pangale, Mpombwe,
Mkolye na Mlogolo**

**MHE. SAIDI JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Vijiji vya Pangale, Mpombwe, Mkolye na Mlogolo vimepitiwa na gridi ya Taifa, na kwa kuwa, Vijiji hivyo havijapata umeme.

Je, ni lini vijiji hivyo vitapatiwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, napendakutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, njia ya umeme uendao Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge, ilianza kujengwa mwezi Juni, 2002 na kukamilika mwezi Desemba, 2002. Njia hiyo imepita kwenye vijiji vya Pangale na Mlogologo kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge

na vijiji vingine vilivyotajwa vya Mpombwe na Mkolye viko umbali wa kilomita moja kutoka njia hiyo ya umeme.

Wakati wa utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge vijiji vyote alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge havikupatiwa umeme. Serikali iliangalia uwezekano wa kupeleka umeme kwenye vijiji vya Pangale na Mlogolo ambapo kijiji cha Pangale kilipatiwa umeme mwaka jana yaani 2007.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Mlogolo unakadiriwa kugharimu shilingi milioni 30 na utahusisha ujenzi wa njia ndogo ya umeme wa msongo wa *KV 0.4* yenye urefu wa kilomita 2, ufungaji wa *transforma* kubwa ya *KVA 100* na kuunganisha wateja. Mradi huu umependekezwa katika utekelezaji wa Bajeti ya *TANESCO* ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Mkolye utahusisha ujenzi wa njia kubwa ya umeme ya msongo wa *KV 33* umbali wa kilomita 1.0. Ujenzi wa njia ndogo ya umeme ya msongo wa *KV 0.4* umbali wa kilometa 2, ufungaji wa *transforma* ya *KVA 50* na kuunganisha wateja. Mradi huu unakadiriwa kugharimu shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Pangale tayari kimeshapatiwa umeme. Upelekaji wa umeme katika vijiji vingine vilivyobaki vya Mpombwe, Mkolye na Mlogolo ambao gharama zake zinakadiriwa kufikia shilingi milioni 130 utafanyika kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tathmini iliyofanywa hadi hivi sasa kwa umeme uliounganishwa ni kwamba wateja waliokadiriwa kuomba kuunganishiwa umeme hawakufanya hivyo. Kwa hivyo, pamoja na kufanya Makadirio ya umeme ni vyema kufanya tathmini mpya ya mahitaji ya umeme dhidi ya gharama. Aidha, tutawashauri *TANESCO* watekeleze kwa haraka zaidi mikakati ya uhamasishaji na mauzo ya huduma ya umeme kama sehemu ya mpango wa kuongeza wateja.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwa siku za usoni kwamba kwenye sehemu ambazo kazi ya kuunganisha umeme siyo kubwa wateja watabuni mbinu za matumizi ya nishati hiyo ili kuboresha uzalishaji wa maisha ya wananchi, kuongeza ufanisi wa gharamza za uwekezaji (*Cost effectiveness* ya *investments*). Kwa upande wao *TANESCO* nao wanalazimika kuboresha mikakati ya kuvutia wateja zaidi ikiwa ni pamoja na kuwarahisishia taratibu na gharama za uunganishaji na matumizi ya umeme. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. *(Makofi)*

Matangazo, naomba mniwie radhi leo wageni ni wengi kidogo lakini ndiyo utamaduni tuliyouweka katika Bunge letu kwa sababu hili ni Bunge la watu na kuwatambulisha siyo kupoteza wakati. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib, ambao ni Bi. Ruth Mollel, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ndugu Mbarak Abdul Wakil, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mbunge amesema ni pamoja na Wakurugenzi. Kwa hiyo, naomba Wakurugenzi kwa pamoja wasimame, lakini hawakutajwa majina. Karibuni sana na ahsanteni sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Waziri wa Nchi kifanikisha majukumu yake. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Waziri wetu wa Ardhi ambaye ni Ndugu Nalaila Kiulia, aliyekuwa Mbunge na pia alikuwa Waziri wa Ujenzi. Karibu sana! Nikiwa ni mtu ambaye ninakufahamu tangu zamani, nakupa pole sana kwa yote yaliyokupata katika maisha yako. Lakini hizo ndizo gharama za sisi tunaopenda kusema ukweli. Ahsante sana na Mungu atakulipa. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Boniface Shija, Diwani wa Kata ya Bugarama, Kahama. Ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Haroub Said Masoud ni Ndugu Hassan Shaaban, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kati - Unguja. Karibu sana Mwenyekiti na ahsante sana. (*Makofi*)

Bi. Pili Amour huyu alikuwa ni Mwenyekiti wa CCM, Tawi la Machuwi kule Koani. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Eustace Osler Katagira na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, ambao ni Ndugu Costal Inyoma kutoka Jimbo la Kyerwa. Karibu sana na ahsante sana. Pia Ndugu Latifah Nassor kutoka Jimbo la Karagwe, safari yenu ni ndefu ya kutoka mpakani mwa nchi ya Rwanda huko. Karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka ni Ndugu Arafa Khamis mke wa Mheshimiwa Mbunge Mama Arafa na mwanaye Ndugu Faisal Mzeru. Ahsante sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis ni hawa wafuatao; Mheshimira Rajab Khamis Diwani wa Wadi na Magogoni Zanzibar, Mheshimiwa Ahmada Othamn Sheha wa Magogoni Unguja, Bi. Semeni Zubeir Khamis, Bi. Fatuma Abdallah Mbaruk na Mheshimiwa Salmini Subora Hajji Mjumbe wa Wilaya ya Magharibi. Inashangaza kidogo Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis kwa wale wageni ambao ni kina Mama hakutaja uhusiano wowote lakini wale wengine wote ameeleza vyeo vyao. Karibuni sana na Ahsanteni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri ni Waheshimiwa Madiwani wa CCM kutoka Manispaa ya Moshi nao ni hawa wafuatao, nitawaomba wasimame.

Bi. Modline, Ndugu Allan Kingazi, Ndugu Lameck Kaaya, Ndugu Athumani Ramole na Madiwani ambao ni Mheshimiwa Michael Mwita, Mheshimiwa Christopher

Lyimo, Mheshimiwa Zuena Bushiri. Karibuni sana Waheshimiwa kutoka Moshi, nina kumbukumbu nzuri sana za kuishi pale Moshi miaka ile ya 1990 mwanzoni, ninyi ni watu wakarimu sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' ni Dr. Renarta Mandike kutoka katika Mpango wa Kudhibiti Malaria, karibu sana Dr. Ndugu Dismal Maalim kutoka katika mpango huohuo, Dr. S. Mkude na Ndugu Faudhiah Aboud hawa ni kutoka katika mradi unaoitwa *COMIT* yaani *Communication and Malaria Initiatives.* Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Joyce Martin Masunga Viti Maalum Shinyanga, kama ifuatavyo: Ni mdogo wake ambaye anaitwa Marry Masunga amefuatana na Wanae sijui ni wana wa Mbunge ama ni wana wa mgeni lakini wasimame nao ni Allen Keffas na Odi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia Ndugu Ndifiha Mela ambaye ni *Marketing Manager* wa *St. Gasper Hotel* amefuatana na Viongozi wa *St. Gasper* ambao ni Ndugu John Kiruth - *Hotel Manager,* Ndugu Malamula ambaye ni *House Keeper* na *Father* Chesco - *Director*. Ahsante sana wageni wa *St. Gasper.* Nyakati zote mmekuwa ni mfano mzuri sana katika kupokea wageni. Hoteli yenu ni nadhifu sana, mazingira safi sana nawaomba wawekezaji waliopo hapa Dodoma watembelee *St. Gasper* waone kuna ugumu gani kuotesha nyasi vizuri, kupanda miti ikapendeza. Kwa ujumla kwa usafi ni kweli kabisa mnaongoza, ahsante sana. (*Makofi*)

Bahati njema hii hoteli ninayoisifia ni ya Kanisa Katoliki hapa Dodoma. Kwa hiyo, hamuwezi kusema nina hisa yoyote humo. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Gofrey W. Zambi ni Ndugu Andrew Namayala, Ndugu Daniel Andendekisye na Ndugu John Kipangula. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula kutoka *TANESCO* sasa hakusema ni *TANESCO* ya wapi hii, ya Dar es Salaam, Mkoa au Jimboni? Lakini ni hawa hawa wafuatao:-

Ndugu John Kasenga Kabwaye, Ndugu Filbert Kajuna, Ndugu Willy Mligo, Ndugu Manase John na Ndugu Ephrahim John. Karibuni sana. Huyu Mbunge naona yeye ana mkakati maalum maana yake ana wageni wake wa *TANESCO* kwa hiyo mradi kule vijijini kwake utakuwa si vigumu sana kutekelezwa. (*Makofi*)

Wapo wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Mlimwa wakiambatana na Walimu wao hili ni kundi lingine siyo lile la jana. Walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mlimwa, ahsante sana na karibuni sana. Tunapenda mara kwa mara kuwaona na kwa niaba ya Wabunge wote tunawatakia mafanikio katika masomo. (*Makofi*)

Wapo pia wanafunzi 15 kutoka Shule ya Msingi hii inaitwa Mlimwa 'B' karibuni sana na tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Kwa kuhitimisha orodha hii ndefu ya wageni nina heshima kuwatambulisha wageni maalum nina heshima kuwatambulisha wageni maalum wafuatao, wageni hawa walikuwepo, walishuhudia na walishiriki siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1964.

Kwanza ni Ndugu Hassan Omar Mzee kutoka Kibweni Zanzibar, ambaye kwa wakati huo alikuwa na umri wa miaka 16, alikuwa akisoma katika Chuo cha Ufindi Maisara na alitoka Umoja wa Vijana yaani Afro Shiraz Party Pioneer. Yeye ndiye aliyeshika Chungu kilichotumika kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa sasa ana umri wa miaka 60, naam! miaka 60 sasa. Ndiyo! 1964 si karibu ndiyo maana mnazungumza mambo msiyoyajua tu hapa. (*Kicheko/Makofi*)

Wa pili, ni Bi. Khadija Abbas Rashid kutoka Raha Leo Zanzibar, ambaye kwa wakati huo alikuwa na umri wa miaka 16, alikuwa anasoma *Town Primary School*, Forodhani. Yeye alishika Kibuyu kilichowekwa udongo wa Zanzibar. Umri wake ni miaka 60 na ni mama wa nyumbani. (*Makofi*)

Wa tatu ni Bibi Sifael Kunda Shuma kutoka Machame Hai Mkoa wa Kilimanjaro ambaye wakati huo alikuwa na umri wa miaka 30 na alikuwa Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Machame. Yeye siku hiyo ya Muugano alishika Kibuyu kilichowekwa udongo wa Tanganyika. (*Makofi*)

Kwa sasa umri wake ni miaka 74 na anaishi Machame na wa kuwa alifanya jambo la maana Mwenyezi Mungu anaendelea kumuweka vizuri tu mnaona? Napenda niwaashukuru sana kutuletea historia hapa. Ahsanteni sana na ninashukuru sana kwamba Mwenyezi Mungu kwa rehema zake ameweza kuwaweka hadi leo mkiwa ni mashahidi halisi wa siku muhimu sana katika historia ya nchi yetu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib ameniomba kuhusiana na hilohilo sasa muelewe kwamba katika viwanja vyetu vya maonyesho yapo maonyesho ya historia na maendeleo ya muungano wetu. Kuna nyaraka na vielelezo, kwa hiyo ni vizuri kila mkipata nafasi kwa leo muweze kufika pale. Nitamuomba Karibu pia atengeneze utaratibu ili tuweze kuwaona hao tuliowatambulisha kwa karibu zaidi hapa tunavyowaona siyo rahisi kuwatambua vizuri. ahsanteni sana.

Naendelea na matangazo mengine haya ni ya kazi sasa.

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anaomba Wajumbe wa Kamati zituatazo yaani Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati

ya Huduma za Jamii na Kamati yake ya Maendeleo ya Jamii wakutane leo saa 7:30 mchana hadi saa 10:00 katika Ukumbi wa *St. Gasper Hotel*. Kwa hiyo, Saa 7:30 Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Maendeleo ya Jamii mkutano *St. Gasper Hotel* Saa 7:30, usafiri utakuwepo katika viwanja vya Bunge kuanzia saa saba.

Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani ameomba nitangaze kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani wakutane leo Jumatano tarehe 20 saa saba mchana mara baada ya kusitishwa Kikao cha Bunge katika sehemu ambayo wao wanaijua. Unajua hawa wenzetu mambo yao ni ya kifichoficho tu hivi sijui kwa nini, hapana kuhofu ninyi mnatambuliwa ndiyo upinzani. Sasa mnavungavunga na kadhalika aah! (*Kicheko*)

Mheshimiwa George B. Simbachawene Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo wakutane leo saa tano asubuhi Ukumbi namba 2 27 Jengo la Utawala. Kamati ya Sheria Ndogo, saa tano asubuhi Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji wakutane kikao cha saa 5.30 leo asubuhi katika Ukumbi Namba 231. Kwa hiyo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji saa 5.30 asubuhi hii Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa William H. Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo ya Nishati na Madini saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi yake kama kama Mwenyekiti wa *TWGP* anaomba Wabunge Wanawake wote mkutane leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Amesisitiza kwamba mkutano ni mfupi sana na hisi labda mkutano wa jana haukuwa na mafanikio. Kwa hiyo, Wabunge Wanawake wote saa 7.00 mchana mkutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge, kutokana na ujio wa Mheshimiwa Rais kesho hapa Bungeni kutakuwa na badiliko yafuatayo.

Kwanza, hakuna wageni watakaoruhusiwa kuingia, watakaoingia ni msafara, kuna watu wengi wengine ambao wanahusika kama Viongozi mbalimbali, Makatibu Wakuu wa Wizara na kadhalika. Kwa hiyo, haitawezekana kundi la wageni wa saa tatu lipishane tena na hao wengine wanaokuja katika msafara wa Rais na wageni wengine waalikwa. Hizi ni sababu za kiusalama. Kwa hiyo, hali ndiyo itakuwa hivyo, msikaribishe au kuwapigia simu watu kuja kesho, watakaa nje tu na hata nje ni vigumu kwa sababu kutakuwa na gwaride la kumpokea Rais. Kwa hiyo, hawataingia kabisa hata katika eneo hilila Bunge kwa kesho.

Vivyo hivyo, Mheshimiwa Rais Ahmed Abdallah Sambi wa Comoro siku ya Jumatatu tarehe 25 Agosti, 2006 utaratibu utakuwa huohuo na kwa taarifa yenu tu ni kwamba Rais Sambi wa Comoro atafuatana na Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo, Rais

wa Jamhuri ya Muungano atarudi tena kumleta mgeni wake hapa Bungeni. Kwa hiyo, utaratibu huohuo hatutakuwa na wageni Jumatatu tarehe 25 Agosti, 2008.

Kesho siku ya Alhamisi tarehe 21 Agosti, 2008) Waheshimiwa Wabunge mtatoka kidogo kwa nidhamu na kurejea kwa sababu tunamtarajia Rais kwenye saa 4.30 asubuhi. Kwa hiyo, nitakapositisha shughuli kunyoosha mguu kidogo inaruhusiwa lakini urejee mara kwa sababu watakao mlaki ni Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge, kwa niaba yetu sote pale kwenye graride. Lakini wengine wote mnaombwa mbaki ili msafara unapoingia hapa ndani tuwe tumechukua nafasi zetu. Hivyohivyo siku ya Jumatatu tarehe 25 Agosti, 2008.

Ahsante sana kwa uvumilifu wenu na sasa tunaendelea na shughuli zilizopangwa. Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Ofisi ya Makamu wa Rais

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo hapa ni ndefu lakini sitaifuata kikamilifu kwa sababu hasa kwa suala la Muungano lina pande mbili. Mimi nawasihi tu mseme kadiri Kanuni zinavyoruhusu lakini tuongee kwa dhati kwa sababu mjadala huu pia unachangia kujenga ama kubomoa Muungano wetu, yaani namna tunavyojadili izingatiwe. Kauli za kubeza, kuudhiudhi, kudharau na kudharauliana yote haya hayatapendeza.

Kwa hiyo, kwa leo nalegeza kidogo ule msimamo wangu kwa suala la Zanzibar ni nchi na kadhalika kwa sababu ni mambo ya Muungano haya huwezi kuzungumza bila kugusiagusia. Lakini nitakuwa makini kweli kweli. Kwa hiyo, kwa tahadhari hizo ninapenda niwataje watakaoweza kuchangia asubuhi hii ambao wachache kati ya hao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir ndiye ataongoza, hayupo? Basi Mheshimiwa Anna Maulidah Komu tutaanza na huyo, halafu Mheshimiwa Job Y. Ndugai baada yake atakuja Mheshimiwa Mohammed Amour Chombon atafuatiwa na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami. Kisha atakuja Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda.

Namwita sasa Mheshimiwa Anna Maulidah Komu kwa mchango wake.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kujadili na kuchangia kwenye hoja ya mazingira na Muungano. Mimi naanza na mazingira, mazingira ni kitu muhimu sana kwenye maisha ya wanadamu kwa sababu mazingira yanaleta uhai na mazingira yanachangia kukosa uhai. Lakini kitu muhimu tusipoangalia njia ya kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu kuelewa nini maana ya kutunza mazingira tunapokwenda ni kubaya. Kukosa mvua katika nchi ni njaa, maradhi na kukuza watoto waliodumaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa vyovyote vile, tunaiomba Serikali ifanye bidii kuhakikisha kwamba inatoa elimu ya kutosha kabisa kuwaelimisha Watanzania waelewe umuhimu wa kutunza mazingira. Wazee wetu kule vijijini hata kama mzee wa aina gani lakini ana kiredio chake mpaka tulivibadilisha jina hivyo viredio tukaviita redio mkulima. Kwa hiyo, wanahakikisha wanasikiliza *TBC* 2 ambayo zamani ilikuwa Radio Tanzania. Kwa hiyo, tukitoa elimu ya kutosha ya mazingira wataelewa na watasikia na watahakikisha yale ambayo wanayapatia elimu wakati wanasikiliza redio hizo.

Mheshimiwa Spika, kuna hatari kubwa ya kukata miti kwa sababu ya kuchoma mkaa, kuna hatari kubwa ya kuchoma pori, wanachoma nyasi wakisema wanatafuta uwezekano wa njia ya kuingia porini ili waweze kupata kile wanachokihitaji na hakuna chochote isipokuwa kukata miti.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la kuchimba mchanga, wanachimba mchanga malori kwa malori, unapochimbwa mchanga huu ukipeleleza utakuta ni maeneo ambayo tunaharibu na tunaleta mmomonyoko. Vilevile kuna kuchimba udongo kwa ajili ya kuchoma matofali. Yote haya tunaharibu mazingira na ukiwauliza Watanzania wanaofanya hayo wanakwambia wanafanya hivyo ili waweze kujikimu katika maisha magumu waliyonayo.

Sasa kama tutasema maisha magumu ndiyo yatufanye tuharibu mazingira basi tunayafanya hayo maisha yawe magumu zaidi kwa sababu tutakapoendelea kuchoma misitu, kukata miti, kuchimba mchanga, kuharibu mazingira yetu hapo tunakwenda kwenye maisha magumu kuliko tuliyonayo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipi kitu mbadala tunapowakataza Watanzania wasichimbe mchanga, wasichome mkaa, wasichome mashamba ili wafikie kwenye hiyo miti wanayoita?

Hakuna, ni kusema, ni kusema lakini hatukai kama Serikali tukafikiria tufanye nini ili kiwe mbadala wasiendelee kukata miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, leo baba ukirudi nyumbani, ukakuta sijapika eti kwa sababu hakuna kuni, humo ndani tutakuwa hatuelewani, unakuja kuniambia nitafute jiko la moto poa. Hivi kweli moto poa kule kijijini na sufuria zetu za kijamaa kweli itawezekana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba, cha kwanza ni kuhakikisha tunatoa elimu ya kutosha kwenye redio zetu, si lazima kwenye *TV* kwa sababu wengi ambao tunahangaika na hayo maisha hatuna *TVs* lakini redio mkulima zipo. Cha pili, tuhakikishe tunawapa Watanzania vijijini mbadala ili wasikate miti, kuchoma mashamba au kufanya mambo ya kuchimba mchanga au udongo ili kuchoma matofali.

Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye Muungano. Kabla ya yote, namtakia afya njema Makamu wa Rais na namwombea Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na

busara.  Mheshimiwa Rais wetu mwezi Machi, 2006 wakati akifanya semina elekezi kule Arusha alitoa kauli ya kusema kwamba tuanzishe mfumo wa Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu wawe wanakutana, wakae kitako, waorodheshe kero za Muungano ili kero hizi zipatiwe ufumbuzi, nilifurahi.  Kufanya vikao mara tatu kwa mwaka, kuorodhesha kero za Muungano tulizonazo ambazo sisi wengine zinatuchosha na kuzipatia ufumbuzi kwa kweli niliona ni jambo zuri na lina busara.  Hakuna mtu ambaye hataki Muungano kwa sababu kwetu kuna Kiswahili kinasema mkataa wingi mchawi, hakuna mtu ambaye anasema sitaki muungano, siku zote *unity is strength* na tukiwa peke yetu hatutaweza, kwa hiyo, tukiwa wengi tutaweza.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililopo, siku zote pande zote mbili zinalalamika, sisemi kwamba unaolalamika ni upande mmoja kwa sababu tayari ninao hawa wa Muungano wa Zanzibar na hawa wa Bara ndani ya nyumba yangu.

Kwa hiyo, hawa wa bara wanalalamika wanasema ninyi Wazanzibar tunawabebeni sana lakini hamna shukrani na Wazanzibar nao wanasema kwa nini hatupewi haki ya kueleweshwa nini maana ya huu Muungano.  Nini sasa kinachohitajika?

Mheshimiwa Spika, tunazunguka lakini wanachohitaji Wazanzibar siyo mambo ya kusema tumepeleka kule haki za binadamu wala sio *TASAF* mkawape mikopo, wale akinamama Wazanzibar kule tunapokwenda kuwapa mikopo wengi wao ni hatari, watachukua hizo pesa na watafilisiwa walichonacho, sio hicho.  Kinachohitajika pale ni kueleweshwa, kitu gani ambacho Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na Mzee wetu Karume, Mungu awarehemu wote, walikaa kitako wakakubaliana.

Mheshimiwa Spika, waeleweshwe ili wajue walikubaliana kuunganisha nini katika hizo Wizara walizokubaliana kuunganisha na waliunganisha kwenye vipengele vipi na vitu gani ambavyo walisema hivi visiwe vya Muungano na kama si vya Muungano Serikali mbili zikae vipi kuzisaidia hizo ambazo si za Muungano, ni hicho tu.  Kama kutakuwa na uwazi wa kuwaambia Wazanzibar ukweli na kuwaonyesha ile hati ambayo walikaa watu wawili wakasaini wao wawili kukubaliana kwamba haya mambo yawe ya Muungano na haya yasiwe ya Muungano sidhani kama kutakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, matatizo yapo kwenye usiri.  Kuna usiri mkubwa sana ambao unafanyika, tunaficha nini kwa sababu mwenye Muungano ni mwananchi, Serikali ni mtendaji.

Sasa kama Muungano huu unamhusu mwananchi mweke wazi, mweleweshe, Wizara waliyokubaliana hawa wawili ni Wizara ya Ulinzi na Ulinzi huu moja, mbili, tatu kwa sababu nimeinukia kwetu kulikuwa hakuna jeshi la nchi, tulikuwa na Mapolisi tu, mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi na nani, kesi zinakwisha hivyo hivyo mradi tumekubaliana.  Jeshi lilikuja baada ya mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, sasa tulikubaliana nini kwenye hili Jeshi?  Juzi hapa walisimama wakati tunachangia mambo ya ulinzi, walisimama Wabunge wenzangu

wakilalamika kuhusu ajira, kuna kitu gani ambacho wazee hawa wawili walikubaliana. Wazee hawa wawili walikubaliana mambo ya ndani ni yepi, walikubaliana hili ni lipi. Ndiyo hicho tu kinachotakiwa kuwekwa wazi na kweli vikitoka vikabrasha hivyo vikaonyesha yale ambayo wazee wawili walikubaliana, wakatia saini kwamba haya tunakubaliana na haya hatukubaliani sidhani kama kutakuwa na la tatizo la Muungano.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linanisumbua, sisi wenyewe hapa ndani, jana Mheshimiwa Selelii alikuwa anachangia hapa anasema kwenye sherehe ambazo zinahusu Serikali ya Zanzibar, Rais gani huwa anakagua gwaride na Rais gani anatangulia anampokea Rais gani, kwa hiyo mbona huku bara sisi tunavumilia, tunapoona kwamba Rais wqa Tanzania anatangulia ni Rais wa Zanzibar anakwenda baadaye. Sasa hapo tunajenga nini? Kwa sababu hapo ndiyo tunasema alaa, kumbe Rais Kikwete ni wa Tanzania Bara, Rais Karume ndiyo wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hapana, Kikwete ni wa Tanzania, ni Rais wetu wote, si kwamba yeye ni Rais wa Bara. Hiyo sasa ndiyo inayofanya wananchi wanakaa na kushangaa ni nini, mimi mwenyewe nilikuwepo uwanjani Amani pale, kwenye sherehe za mapinduzi wakati fulani, nilishangaa pia kwa sababu niliona Rais Mkapa wakati ule amefika yeye kwanza kwenye uwanja, baadaye akaja Karume, nikasema alaa, hivi inakuwaje, mbona katangulia kuja Rais Mkapa halafu ndiyo anampokea Karume. Nikaambiwa, kwa sababu hizi ni sherehe za Mapinduzi Zanzibar kwa hiyo inabidi iwe hivyo. Ahaa, *protocol*, Rais wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, Zanzibar imo ndani ya Tanzania kwa hiyo Rais Mkuu pale ni Rais wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo vitu vidogo vidogo ndiyo vinafanya Wazanzibar hawaelewi na tunavijenga sisi wenyewe. Tukizungumza mambo ya gesi, Zanzibar nina masikitiko huwa unafika Zanzibar sipo, lakini Zanzibar kuna maisha magumu ya ajabu kuliko yaliyoko Tanzania Bara. Sh. 10,000/= kwa kutwa haitoshi, nikiwa na Sh. 500,000/= pale Zanzibar, nikimaliza mwezi nasema ngoja nirudi bara.

Mheshimiwa Spika, mambo ni magumu pale, sasa tunaisaidiaje kiuchumi, tunafanyaje ili wale Wazanzibar waondokane na maisha magumu waliyonayo, hakuna. Tutakaa huku tukilalamika, watu wanapiga kelele, Wazanzibar wanapiga kelele, Wabara wanapiga kelele lakini mwisho wa haya ni nini? Siku zote Madaktari wanasema unapoona kipele kimeota kwenye uso wako usikichokonoe mwisho wake ni kansa.

Sasa tujaribu kutibu hivi vipele vidogo vidogo kwa sababu sisi wengine tunapata tabu sana. Maana yake leo huniambii kwamba Muungano unavunjika, kwa sababu wewe Mzanzibar rudi ukakae Zanzibar, Komu nimwachie nani, haiwezekani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa Muungano unavunjika wewe rudi ukakae Zanzibar, wanangu nimwachie nani, haiwezekani. Kwa hiyo, huu Muungano si wa Serikali tu, hata sisi wenyewe tumeungana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba, Serikali yetu kama Serikali ambayo wananchi ndiyo wameiweka madarakani na iko madarakani kumtumikia mwananchi iwe wazi. Iwe wazi wakati wanaitumikia nchi hii, wawaeleweshe Watanzania ni kitu gani

ambacho wanachokihitaji wasikilize hizi kero wazikalie kitako, si kero za kusema tunataka kupeleka *TASAF*, tumejenga Bunge Zanzibar, si kero hizo, hizi kero ndogondogo za kijamii ndizo zinazoleta tabu.

Mheshimiwa Spika, tangu tumeanza kusikia Pemba kuna gesi mpaka leo ni miaka mingapi? Kila siku ni hadithi.

Hivi hii gesi ingejulikana ikachimbwa kule Pemba si kungekuwa mbinguni kwa sababu uchumi ungesaidia pale ambapo kile kitu kinatoka kwanza. Wapemba wangeacha kulalamika kwa sababu umaskini kidogo ungepata nafuu lakini leo ni hadithi maana yake uchumi wa Pemba uwe Pemba, uchumi wa Bara uwe Bara kwa nini uchumi wa bara uwe bara peke yake.

**SPIKA:** Ahsante sana kengele ya pili hiyo.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Nakushukuru sana lakini siungi mkono hoja kwa sababu inanitesa sana katika nafsi yangu. Ahsante. (*Makofi*)

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(1)(a). Wakati msemaji wa mwanzo akisema hapa ametumia neno la Rais wa Zanzibar na kumekuwa na matamko ya namna hii mara kwa mara ambayo nadhani nahitaji kupata ufafanuzi zaidi, hivi ni Rais wa Zanzibar au Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge yote mawili yanatumika na hayana tatizo lolote. Nadhani kila kitu katika lugha ya kawaida binadamu hawakai wakaanza kufikiria Katiba na kuzungumza tu, nadhani tukifanya hivyo tutaongeza tabu katika mjadala huu. Hili ndilo lilikuwa chimbuko kwamba unaposema Rais wa Serikali ya Mapinduzi maana yake ni Rais wa Zanzibar kwa lugha nyepesi nami nitailinda hiyo kwa sababu imezoeleka hivyo. Ahsanteni sana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja zilizo mbele yetu. Kwa kawaida mimi ni mwana mazingira na ningetumia dakika zangu zote kumi na tano kuzungumzia mazingira. Sijawahi kusimama nizungumzie habari za Muungano lakini leo nitalazimika kuzungumza kidogo kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze na kutoa salaam za pole kwa familia za wote waliopata ajali katika maeneo ya Wilaya ya Konga, maeneo ya *NARCO* Pandambili hadi eneo la Gairo ikiwa ni pamoja na familia za Mheshimiwa Severina Mwijage, familia ya Mheshimiwa Chacha Wangwe na familia ya ndugu yangu jirani yangu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Tunawatakia kila la kheri wote waliopata majeraha wapone kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nianze na mazingira kama nilivyosema kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, tumeshirikiana naye sana katika Kamati yangu kuzungumza mambo mengi yanayohusu mazingira, tumepata ushirikiano mkubwa sana, tunafanya kazi kwa karibu. Ziko changamoto nyingi za mazingira katika nchi yetu, kama tunavyojua sote jinsi ambavyo nchi yetu inaharibika kimazingira kwa kiwango kikubwa na juhudi ambazo zinahitaji si za Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira bali zetu sote.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo yana matatizo kidogo kwa mfano tafsiri ya neno chanzo cha maji, inahitaji iwekwe vizuri. Watu wengi wanafikiri ukisema chanzo cha maji unazungumzia habari ya *water source* wakati hapa nia yetu ni kuzungumzia hasa *catchment area* ambalo ni eneo pana na kubwa zaidi. Somo hili halijafika vizuri katika Halmashauri zetu na Vijiji vyetu. Mara nyingi watu wakibanwa kuhusu kuharibu mazingira kwa maana ya chanzo cha maji, wanajibu kwamba pale hakuna chanzo cha maji kumbe chanzo cha maji ni jambo pana zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili katika eneo hilo ni kuhusiana na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya mifugo kuhusiana na uharibifu wa mazingira kwa kuhakikisha kwamba malambo, malisho, madawa, mabwawa, njia za mifugo na kadhalika zinatengwa vizuri. Kutokana na funzo linalotokana na kule Ihefu Mbarali, suala hili la wafugaji na mifugo ni vizuri likawekewa sera zinazoeleweka nchi nzima na utaratibu mzuri zaidi ili wafugaji wetu waweze kufuga vizuri na mazingira yetu yaweze kuhifadhika.

Mheshimiwa Spika, la tatu katika eneo hili ni zoezi ambalo Serikali imeagiza la kupanda miti isiyopungua elfu moja kwa kila Wilaya. Zoezi hili halina usaidizi mkubwa toka Serikali zaidi ya lile agizo. Tunaomba sana Wizara ya Maliasili na Utalii itenge fedha za kupeleka kwenye Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya kununua viriba lakini vilevile Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na yenyewe itenge fedha kwa ajili ya kununua viriba.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hapa kwenye hotuba iliyo mbele yetu kwamba katika fedha tutakazopata za kutusaidia kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika utaratibu wa *National Adoption Plan of Action* ambazo zitafikia karibu Sh. 3bn/= kama si chini ya hapo zitafanya mambo fulani fulani. Ningefurahi sana kama sehemu fulani ya fedha hizi zikatumika katika kununua viriba vikagawanywa nchi nzima ili miti ikapandwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni *Lake* Natron. Tumeambiwa kwamba kuna pendekezo kiwanda kitajengwa kilomita thelathini toka kwenye Ziwa lenyewe. Tatizo halikuwa umbali wa kutoka kiwanda hadi kwenye Ziwa, nalo ni tatizo kiwanda kikiwa karibu zaidi lakini tatizo si umbali, tatizo ni athari itakayotokana na *activity* nzima tunaamini kabisa itafanyika athari ya kuangalia mazingira ya *Lake Natron* yataharibika kiasi gani?

Ziwa lile ni muhimu sana kwa ndege wale flamingo ambao wanatawanyika Afrika Mashariki nzima lakini wote wakiwa wanazaliwa pale *Lake Natron.* Tukiharibu pale kimazingira tutakuwa tumetenda jambo ambalo kwa kweli si jema, kwa hiyo utafiti

unatakiwa ufanyike kwa kina sana ili tuweze kujiridhisha kwamba kinachofanyika *is a win will situation.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nihamie kule ambako nilisema toka mwanzo huwa sizungumzii lakini nalazimika kwa sababu ni mwaka wa nane sasa nipo Bungeni nasikia kila kukicha baadhi ya Wabunge hasa kutoka upande wa pili wakisimama ni kulaumu kuhusu Muungano na hasa ripoti rasmi za Upinzani na kama alivyosema Mbunge aliyeongea kabla yangu ambaye kasema maneno mengi sana.

Sasa najiuliza kwa mfano, aliyetangulia anasema kuna usiri mkubwa sana kwenye mambo haya ya Muungano, usiri upi? Nani anaficha mambo haya?

Mheshimiwa Spika, niseme ukweli, ukinipa *a clean sheet of paper* na Wabunge wengi tu hapa ukasame hebu andika kero za Muungano kwa neno kero ninavyolijua, ni kitu kinakufanya usijisikie vizuri muda wote, kinakukereketa, nafikiri naweza kukurudishia bila kuwa nimeandika chochote. Tumeungana muda mrefu na leo ni bahati nzuri sana tumepata waasisi vijana mashahidi waliokuwepo wakati ule tendo hilo likifanyika, hongereni sana na karibu sana Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuliokuwa wadogo sana wakati huo hatukuona wala kusikia, tunafurahi sana kuona ushahidi huo na Mheshimiwa aliyeongea kabla yangu ameimarisha Muungano kwa kuolewa na upande wa pili na kaka yangu Komu, jambo ambalo ni jema sana. Nilitarajia katika mazingira haya tungekuwa sote tunaongea katika kuelekea kwenye Muungano ikiwezekana wa Serikali moja. Hayo ndiyo matarajio yangu. Hii inanikumbusha wakati fulani nilikuwa nikisoma nchi fulani ya ng’ambo, tukawepo Watanzania na wanafunzi wa nchi nyingine, miaka kumi iliyopita, tukawa tunaalikwa wakati kwa wakati labda kwa Meya wa Mji ule au mahali pengine, sisi wa Tanzania na wa kutoka sehemu nyingine hasa wa kutoka nchi maskini.

Mheshimiwa Spika, sherehe ile ikifanyika tunaambiwa tujitambulishe, Wanigeria wanajitambulisha, Wazambia wanajitambulisha na wengineo.

Tukifika sisi Watanzania tunasimama, tunasema mimi fulani natoka Tanzania, wakatokea wanafunzi wenzetu wengine wanaotoka Zanzibar wanasema mimi fulani natoka Zanzibar, hii ikatuletea mgogoro miongoni mwa wanafunzi, tunapoanza kurudi kwenye basi tunaulizana hivi nyie mnaposema mnatoka Zanzibar hamtoki Tanzania nyie na palepale wale wenyeji wetu wanaanza kuuliza kwani Zanzibar si sehemu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, yaani inaanzisha mjadala ambao wala haukuwepo, ni jambo la siku nyingi lakini lipo, wapo wenzetu ambao hawajisikii tu kusema Watanzania. Sasa ndugu zangu niwahakikishieni kwa vijana hawa wa sasa kwa lugha hii inayoendelea kila wakati ya upande mmoja kuwa kazi yake ni lawama, hakuna jema, hivi kweli bara kazi yao ni kuwaonea Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, sisi wote ni Wabunge, Wabunge wengi wa Bara hatuijui Zanzibar, hatujafika kuitembelea thoroughly lakini Wabunge wengi wa Zanzibar

mmetembelea Bara mnaifahamu.  Juzi Mheshimiwa Spika alipofanya kikao kule Kiwengwa ndiyo mara ya kwanza nimetembea tembea kwa maana ya kupelekwa kule upande wa pili kwenye hoteli.

Nilichokiona sikuamini macho yangu, Zanzibar kuna Maendeleo makubwa huwezi kulinganisha na Dodoma, umaskini niliouona kule si kama wa Dodoma.  Sikuona tembe kule, nyumba zote karibu ni za bati na ukiona ya makuti lakini bado ina ubora na hadhi fulani, Zanzibar kimaendeleo iko mbali, huo ndiyoukweli, piga vigezo vyote vya umeme, mgawo wa barabara, simu, mawasiliano na kadhalika linganisha Zanzibar na huku bara hasa hii Dodoma ya kwangu, kweli iko sawa?

**MBUNGE FULANI:** Tofauti.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Tofauti, Zanzibar iko mbali.  Sasa kwa nini mnairudisha nyuma kila dakika, kwa nini mnajidharau nyie wenyewe.  Zanzibar iko mbali.  Kongwa ina watu laki tatu, ina Mbunge mmoja katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mimi niliyesimama hapa.

Pemba ina watu laki tatu, ina Wabunge wangapi hapa ndani.  Wanafika hata thelathini.  Nimewahi kusimama nikalalamika hapa.  Kwa nini mnadhani kwamba kila kinachozungumzwa hapa ni kuionea Zanzibar.  Huku tunakoelekea ni kubaya zaidi kuliko tunakotoka. Watanzania wanazidi kuchoka, kusikia kila wakati.

Mheshimiwa Spika, aliwahi kuongea Rais Mwinyi wakati fulani alipokuwa kiongozi, kiongozi mmoja wa UWT akiwa ni Mwenyekiti wakati ule, alitamka jambo fulani la kuhusu ndoa kwamba iwekwe sheria iwe mke mmoja nchi nzima, kule Zanzibar baadhi ya watu wakakasirika wakaandamana, nakumbuka nilikuwa bado kijana mdogo lakini Rais Mwinyi alisema hivi, ninyi mnakasirika kwani yule Mwenyekiti wa UWT ni Waziri wa Serikali, si katoa maoni yake, sasa mnakasirika nini ndugu zangu na kweli wakaacha maandamano.

Sasa leo hii kiongozi Waziri Zanzibar sio mwananchi wa kawaida anatoa matamshi ya kumdharau Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, Waziri katika Serikali ya Mapinduzi, mnategemea sisi tukae tunashangilia kwani huyu ni kiongozi wa UWT. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Waziri anapozungumza maana yake ni kwamba wamekubaliana kule, mambo haya si ya afya hata kidogo, hatuwezi kukaa tukaona Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akidharauliwa na Waziri.

Katika taratibu za mahusiano ya Serikali kwa Serikali hata Waziri wa Tanzania katika Mawaziri wetu hawa haruhusiwi kumdharau Waziri Mkuu wa Kenya Raila Odinga ovyo ovyo tu, mahusiano hayaruhusu, diplomasia hairuhusu.

Kwa hiyo, hata wenzetu wanaosimama na kuunga mkono mwenendo huu sidhani kama wanatutakia mema. Hawa wana lao jambo. Huwezi kuendekeza utaratibu huo wa Mawaziri kujisemea ovyo ovyo lazima kuwe na utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Tatu, Rais Mkapa aliwahi kuja Bungeni katika Bunge lililopita akatoa mfano mmoja, akasema kulikuwa na walevi watatu wamelewa pombe, wanatembea huku wanabishana, wanaulizana hili jua au mwezi, hawakubaliani kama ni jua au ni mwezi lakini ni saa sita mchana. Wakakutana na mlevi mwenzao wa tatu, wakamwuliza hili jua au mwezi akasema sijui.

Sasa ndiyo hawa ambao kazi yao kudharau kinachoendelea Zanzibar na Maendeleo ya Zanzibar na Muungano wetu, wanashindwa kujua hili jua au mwezi, saa sita mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kusema kwamba mwendo sasa tuelekee kwenye Serikali moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele yako ili nitoe mchango wangu kidogo katika suala hili au mada iliyo mbele yetu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja katika,.....

**SPIKA:** Samahani nilighafirika kidogo. Keti tafadhali, naomba kuelezea jambo nililoulizwa na Mheshimiwa Dr. Chegeni. Waheshimiwa Wabunge msingi wa Katiba Ibara ya 103 unasema hivi kuhusu Rais wa Zanzibar:

"Kutakuwa na kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye ndiye atakayekuwa Rais wa Zanzibar".

Kwa hiyo, lipo wazi kabisa wala siyo hisia kwamba ukisema ni Rais wa Zanzibar umekosea, si kweli kwa sababu ndivyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyomtamka kwenye Ibara ya 103. Endelea Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Afadhali kwa hilo umenisaidia maana yake nilikuwa nataka kuliweka wazi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, mimi ni mmoja kati ya Watanzania wachache ambao Muungano umewakuta.

Mheshimiwa Spika, wakati Muungano unaundwa nilikuwa na miaka kumi na moja. Kwa hiyo, mimi ni muumini mkubwa wa Muungano naujua faida yake na niko tayari kuulinda kwa gharama yoyote ile.

Kwa yote ninayotaka kusema hapa ni kwa sababu au kwa madhumuni ya kuudumisha Muungano. Nisingependa au ningewashauri Watanzania wenzangu kwa wakati huu ambao kumetokea mikwaruzo katika Muungano wetu kauli zetu tunazokuwa tunazizungumza tujaribu kuzungumza kwa nia ya kujenga. Tusivae ngozi ya kondoo kumbe sisi ni chui. Kuna kauli zinazojitokeza kuona kwamba watu wanaumwa sana na Muungano kumbe vile hawana nia nzuri hasa hizi kauli za kukebihiana ni jambo baya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Pwani hasa Wazanzibar kumwambia mtu mzima kwamba wewe ni mkosefu wa nidhamu ni tusi. Kuna lugha nyingine ya kumrekebisha ni sawa sawa na kumwambia mtu mzima wewe mwongo, lakini unaweza kumwambia siyo kweli akaelewa na watu wakaeleweka.

Sembuse Viongozi wa Serikali anatoka Mheshimiwa na akawaambia viongozi au Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawana nidhamu kwa kweli si jambo zuri na wala si jambo la kujenga Muungano. Ingetumika lugha nzuri kama kakosea binadamu hakuna aliyekamilika ikatumika lugha ya kuweza kujenga Muungano na tukaweza tukaenda sambamba kama madhumuni yetu yalivyo.

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba hakukosea au sisemi kwamba hakuna makosa lakini kauli tunazoweza kujaribu kurekebishana tujue kauli za namna gani ya kuweza kujenga. Mtu mwenye busara na mwenye uchungu wa Muungano kama mimi nisingeweza hata siku moja kutoa kauli ya kuweza kukashifu au kutukana upande wa pili wa Muungano ningetoa kauli ya kuweza kurekebisha kwamba kilichotokea kule siyo sahihi.

Lakini mimi naamini Wazanzibar ni watu madhubutu na wanajua na wana thamini Muungano, na ndiyo maana wakakubali kuitoa *sovereignty* ya nchi Kuungana na wenzetu wa Bara kuwa nchi moja ambayo inaitambua Zanzibar ipo, hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja kimataifa, lakini inaeleweka kwamba ndani ya Tanzania ipo Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa ndiyo inapofika wakati mimi nashangaa tunajiuliza majawabu kwa sababu tunayojiuliza ni majawabu si maswali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitaungana na kauli yako siku moja ulisema kwamba Zanzibar tuna Rais, tuna Baraza la Wawakilishi, tuna wimbo wa Taifa, tuna Mawaziri, tuna Bendera, bado tunajiuliza sisi ni nchi, Wazanzibar tusijiulize majawabu. Jawabu lipo wazi hiyo kwa msemo wa kwetu kule Zanzibar haitakiwi tochi kwamba lazima umulike. Tuache hapo. Matatizo yote hayo yanayojitokeza kuuliza majawabu ni yale masuala tunayoita kero za Muungano. Kero za Muungano zinakuja pale ambapo Wizara au

Vikao/Mikutano inayohusika kutokuchukua hatua zile ambazo watu wanasema hizi ni kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyepita kuchangia amesema wewe ukimpa karatasi kuziweka kero za Muungano hataweza kuandika. Sishangai kwa sababu ndiyo mara ya kwanza kuvuka bahari kwenda huko kwenye upande wa pili wa Muungano na yeye kafika kule kapokelewa kalala *Kempiski Hotel. (Makofi)*

Wanaopata kero za Muungano ni Wazanzibar wanaotoka kule kuingia upande wa pili wa Muungano, lakini mtu yeyote wa Tanzania Bara anayetoka huku kwenda Zanzibar hapati kabisa kero ya Muungano *never ever*. Kero kubwa zinapotokea ni pale pa kuingilia Tanzania Bara kutokea Zanzibar kwa maana bandarini au *airport*. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina nia safi na ina sera safi lakini kuna watendaji wake wenye mamlaka ya kusimamia yale mambo hao ndio wakorofi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya Uchumi wa Zanzibar kama kisiwa na kama visiwa vingine vyote sisi hatuna uwezo wa kutegemea kwamba tukasema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Zanzibar, hatuna ardhi, hatuna madini. Zanzibar ni kisiwa na kwa asili yake ni harakati za kibiashara, harakati za huduma ndiyo tu zitakazoleta faida au maslahi ya maisha ya watu wa Zanzibar, bila hivyo hakuna kitu. Ndugu zetu ninyi mna ardhi ya kutosha, tunashukuru sisi wengine tuko huku na tunalima na tuna ndugu zetu wengine wafanyabiashara Wazanzibar wako bara, wako kila kona na wabara wako Zanzibar. Tunashukuru.

Lakini tatizo tunalozungumza hapa kero zipo na bila kuchukua hatua zinazofaa hizi kero ndiyo inapofika wakati ambapo tunajiuliza majawabu. Ninachotaka kusema na nataka kuwashauri Wazanzibar kwamba sisi tujiamini na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umefika wakati sasa hivi kutolumbana haya mambo tuchukue hatua ya kuokoa au kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na umaskini huu ambao unawakabili. Hali hiyo, ni kuweza kuweka au kutekeleza ile sera yetu au sera ya Mapinduzi kuifanya ile Zanzibar iwe bandari huru bila ya hilo hakuna mtaji utakaotupeleka huko pengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni huu ambapo juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyokuwa anatoa ripoti yake hapa makusanyo ya shilingi bilioni 20, asilimia 96 zimekuwa *exemption* kwa sababu bila ya kufanya *exemption* hataweza kumiliki mtu kilo ya mchele pale. Mambo haya hayakuanza leo mambo haya yameanza toka zamani kama nilivyokuambia mimi nimefaidi Muungano wakati wa Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Zanzibar hayati Mheshimiwa Abeid Amani Karume kulikuwa kuna shirika moja linaitwa bizanje, shirika la bizanje lilikuwa linaagiza bidhaa zote muhimu kule Zanzibar lilivyokuwa linaagiza mimi nilikuwa nafanyakazi bizanje, lakini Serikali ilikuwa inafidia gharama za kodi kwa sababu ya kuweza kuwafanya Wazanzibar wamiliki kuweza kununua kwa sababu ingekuwa inatozwa kodi kwa mujibu ilivyo wasingeweza kuhimili hili.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi kuna biashara huru, Serikali haiwezi kufidia kuwalipia wafanyabiashara ndiyo inatoa *exemption* kuwezesha wananchi kumiliki hali ile. Kwa hiyo, hii inadhihirisha wazi kwamba hakuna sababu hata moja ya kuweza kuwa na kodi pale, iwe bandari huru, bidhaa ikiingia pale ikitoka ikija huku itachajiwa ushuru kama inavyotakiwa. Harakati za kibiashara zikiwa pale Zanzibar ndiyo zitakazoweza kuwanyanyua Wazanzibar hatuna ardhi ya kulima. Sasa hivi zile sehemu za kulima zote watu wanakata miti wanajenga nyumba za kuishi. Sasa niambie kinachosaidia ni kwamba wana hizo bahati Wazanzibar wametimka nje ya nchi, wanachuma huku wanakuja kujenga kwao lakini Wazanzibar wako pale sisi Wabunge tunaoishi Zanzibar sisi tunaishi ndani ya majimbo yetu na tunaishi na wananchi wanakila wao ndiyo tunachokila sisi. Kwa kawaida binadamu huwa anakula milo mitatu. Lakini ili uweze kukaa na wananchi wako vizuri wewe Mbunge lazima ule mlo mmoja na nusu na mlo mmoja na nusu uwaachia wananchi wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninyi huku wenzetu inaweza kuwa uko Dar es Salaam Jimbo liko Kagera, liko Ruvuma liko wapi lakini sisi asubuhi na jioni tuna watu wetu, tunachokizungumza sasa nawashauri Wazanzibar, naishauri Serikali ya Muungano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Zanzibar tuifanye Zanzibar inyanyuke kiuchumi siyo mtuletee fedha tuna uwezo wa kutafuta fedha sisi, hizo 4% tunaweza tukazisahau kabisa tukiwa na fursa ya kuweza kufanya kitu kama hicho. Hatujakuwa walemavu kwamba tuletewe fedha tuna uwezo kabisa na mnawajua Wazanzibar kwa kufanyakazi. Nawasihi ilikuwa ni njia mojawapo ya kuweza kutafuta maisha bora kwa Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, *OIC* sasa wenzetu huku ikakataliwa. Kujiunga Zanzibar sisi tusigeuke nyoka wa mdimu, wewe nyoka umekaa kwenye mdimu huli ndimu unataka kumtisha binadamu asichume ndimu, faida gani, hamuwezi, tuacheni sisi tufanye. Hii inawezekana tuikoe Zanzibar katika hali ya uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Zanzibar yanayojitokeza kuuliza maswali watu hawana kazi ya kufanya wamekaa. Kuna wakati fulani mimi nimekaa na vijana wanajiuliza hivi mimi hapa ni kwetu kaandika *slogan* kwenye kikao chao na kama siyo kwetu mimi kwetu wapi kwa sababu alitegemea kwamba pale kwao ndiyo apate yale aliyoyategemea lakini anaona tu, maana *north* haoni mwisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili niongee, mara nyingi sana mimi nitacheza na Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maneno yangu yatakuwa machache, mengi yatakuwa ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nikianza na kero za Muungano ningependa kufahamu mpaka dakika hii ziwekewa utaratibu gani hasa? Kwa mfano, kama vile hisa katika *BOT* tatizo lipo wapi, na ninaomba niweze kupatiwa maelezo sahihi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 134 inaelezea masuala ya Tume ya Pamoja ya Fedha inayotokana na sheria ya mwaka 1984 Namba 15 kwenye Ibara yake 42.

Ibara ya Katiba inasema kifungu kidogo cha (1) “Kutakuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye wajumbe wasiozidi 7 ambao watateuliwa na Rais kwa mujibu wa Ibara hii na masharti ya sheria iliyowekwa na Bunge.” Tume hii tayari imekwishaundwa. Lakini ningependa kufahamu mpaka dakika hii imefikia wapi? Pia ninaomba kujua mgawanyo wa mapato yanayohusiana na gharama za Muungano. Je, mkataba umekwishakamilika kutokana na hiyo Tume?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 133 ya Katiba inataja akaunti ya fedha ya pamoja na hii ipo kwenye Sheria hiyo hiyo ya mwaka 1984 namba 15 kwenye Ibara ya 42. Naomba kunukuu:-

“Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa akaunti ya fedha ya pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambao kutakuwa na fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano.” Mwisho wa kunukuu.

Je, Mfuko huu tayari upo, na kama haupo haijakiukwa Katiba kwa sababu hili lipo katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa Tanzania. Mimi nadhani la muhimu hapa tuimarishe Muungano wetu kikamilifu. Ninawashangaa baadhi ya viongozi ambao wamelishikilia bango kujaribu naweza kusema pengine ni kama kutaka kuwachochea wananchi badala ya kuwaelimisha, na mbaya zaidi ni pale ambapo Mheshimiwa Mbunge anaweza akasimama Bungeni akaanza kuisemea vibaya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo kwa mujibu wa Ibara 68 ya Katiba hii ameapa kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano, na aliapa kwa kusema mimi fulani bin fulani naapa kwamba nitaitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuilinda na kadhalika na kadhalika akaishia kwa maneno ya kusema ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.

Ukishindwa kuitetea Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mambo yote yaliyoandikwa humo ndani wewe unakiuka na hupaswi kuwa Mbunge, ukitaka nenda kayasemee huko nje na siyo ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kila mtu anafahamu kwamba mwezi Desemba, 1961 iliyokuwa inaitwa Tanganyika ilipatikana, na mwaka 1963 iliyokuwa inaitwa Zanzibar ilipatikana na mapinduzi yake mwaka 1964. Ilipofika tarehe 26 Aprili, 1964 na kwa ushahidi ambao tumeonyeshwa hapa Bungeni tunawaona wale waasisi waliounganisha udongo uliochukuliwa kutoka iliyoitwa Zanzibar na udongo uliochukuliwa kwa ile iliyoitwa Tanganyika ukaunganishwa pamoja kuwa nchi moja kwa mujibu wa Ibara ya

Katiba ya Jamhuri ya Muungano namba moja Sura ya kwanza, Ibara ya Kwanza, ikaitwa Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano ndivyo ilivyoitwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii iliyoitwa Tanganyika bado jina la Ziwa Tanganyika lipo, na leo hii iliyoitwa Zanzibar hatuwezi tukakataa kuna Mji wa Zanzibar, na ndani ya Zanzibar kuna Unguja na kuna Pemba. Kutoka Tanganyika zilichukuliwa herufi (Tan) na kutoka Zanzibar zilichukuliwa herufi (Zan), ikachukuliwa herufi (i) toka kwenye Zanzibar, na ile (i) na (a) iliyoishi (ka) kwenye Tanganyika ikaitwa Tanzania si Tanganyika na si Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Sura ya Pili ya Katiba kifungu kidogo cha kwanza, na cha pili, naweza kukisoma. Naomba kunukuu: "Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo." Kifungu kidogo cha pili, "Kwa ajili ya kutekeleza utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Rais aweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa, Wilaya, na maeneo mengineyo kwa kufuatana na utaratibu uliowekwa na Sheria au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapeleke katika Katiba ya Ibara 102. Ibara ya 102(1) inasema hivi:-

"Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama alama za mtajo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar." Kule tumetazama Ibara ya kwanza nchi ya Tanzania, na huku tumetazama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mapinduzi ya Zanzibar, inaendelea ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar katika mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge, takriban hamsini na zaidi wanaotoka Zanzibar kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar ambayo ina wananchi wasiofika milioni moja, Tanzania Bara ina Watanzania wanaozidi milioni 35 na zaidi, na kama vile haitoshi kuna wawakilishi wa Baraza hilo la Mapinduzi watano wanaoingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Baraza la Wawakilishi siyo Baraza la Mapinduzi.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, samahani Baraza la Wawakilishi naomba kurekebisha, watano wanaoingia kwenye Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, hakuna Waheshimiwa Wabunge wowote wanaotoka kwenye Bunge hili pengine tukasema Tanzania Bara wakaingia kwenye Baraza la Wawakilishi, na hakuna malalamiko, lakini wenzetu wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, wakati Muungano unakuja na ninaomba wawaulize hao waasisi waliopo, hayati Sheikh Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema huko peponi alimwambia hayati Mwalimu Julius Nyerere ushahidi tunao hapa *live* ningefurahi kama Muungano huu ungekuwa wa mia kwa mia kwa maana

ya kwamba badala ya kuwa na hizi Serikali mbili tuwe na Serikali moja tu, na mimi nipo tayari kuwa Makamu wako, mashahidi wapo hapa muwaulize wote wawili wanaotoka Tanzania Bara na wanaotoka Tanzania Zanzibar waliokuwa wanachanganya mchanga huo. Hayati Mwalimu Julius Nyerere alisema hivi haina tatizo lakini bado tunaweza tukaenda polepole lengo letu ni kufikia Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, ningefurahi sana kwa mtu ambaye anapenda Muungano mzuri bila pengine kuwa na ubinafsi tukaongelea Serikali moja kulikoni wengine wanaongelea Serikali tatu, mtakumbuka na nyie mtaelewa ndugu zangu sisi ni Tanzania moja.

Mheshimiwa Spika, hapa alipokuwa anatambulisha wale waasisi walioweka mchanga, tulipokuwa tunashangilia, nilichokiona mimi sijui kama wengine walikiona wenzetu wa Kambi ya Upinzani hasa wanaotoka Chama kimoja fulani cha Zanzibar kwa wale wanaotoka Zanzibar hawakushangilia, na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Zanzibar mmoja mmoja hawakushangilia, nilipata picha nikasema ala kumbe ni mambo ya siasa, na siyo kweli kuhusiana na Muungano.

Mheshimiwa Spika, ninadhani kama Muungano kwa bahati mbaya utakuja kuvunjika chokochoko hii itakuwa imevunjwa na baadhi ya watu wanaotoka Zanzibar siyo wote. Maana wao wanaona Uzanzibari wao ni muhimu sana kulikoni sisi tunaodhani Utanganyika wetu ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi ambacho ahaa nisije nikasema sielewi nilisikia tu, sina uhakika kama kuna ukweli, baadhi ya mambo ambayo hata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikikwama bado Serikali ya Muungano husaidia wanachotaka ni nini? Ninayajua sana na kwa sababu nimesoma historia, na bahati mbaya kipindi fulani Zanzibar haikufundishwa historia sisi tuliichimbua zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kupata *challenge* hiyo kwa sababu nimewafahamu maadui wetu. Kwa hiyo, ninawaomba wenzetu Wazanzibari tuongelee Utanzania zaidi, hii mambo ya kusema sijui kuna bendera, sijui kuna Katiba, sijui kuna nini, pengine tu ni makosa ambayo yalifanyika tunaweza tukayarekebisha baadaye. Ni makosa tu yaliyofanyika ambayo tunaweza tukayarekebisha baadaye.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja kwa maana ya kwamba Tanzania ni nchi moja tu na siyo vinginevyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Abubakar Bakary atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda na wakati huo huo Dr. Ali Tarab Ali ajiandae.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo tu katika masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme tu kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 100 pamoja na *the Parliamentary Immunities Powers and Privileges Act* ya mwaka 1998 sheria namba 3 Mbunge au Mjumbe yeyote katika Bunge hili ana uwezo na ana haki na analindwa na sheria hizi nilizozisema ya kusema chochote ambacho anahisi kwa mawazo yake anayo.

Pale ambapo Mbunge mwingine anasema kwamba anaposema kiongozi kwa mfano Waziri Mkuu au Waziri kwamba hawezi kwenda kinyume na maelezo anayosema kwa hiyo, nafikiri Mbunge huyo ama hafahamu hii sheria au hafahamu kanuni na katiba. Kwa maana hiyo, naomba radhi sana na kumtaka Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kwamba aliyoyasema alikuwa anakwenda kinyume na utaratibu na kinyume na sheria hizo ni lazima aombe radhi kwa yale aliyoyasema. Asiombe radhi kwa Mawaziri na wananchi wa Zanzibar tu lakini aombe radhi hata kwa wanasheria wenzake. Mimi uzoefu wangu wa sheria nilionao mdogo wa miaka 33 inaonyesha kwamba Dr. Harrison Mwakyembe alikosea na kwa kweli alidhalilisha fani hii ya kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kulisema ni kwamba katika Katiba nina vifungu zaidi ya vitano au sita, ibara 103, 107, 46 (b) 3, ibara ya 54 na kadhalika zote zinazungumzia Rais wa Zanzibar katika Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa naomba nije katika suala muhimu la Muungano. Kwanza nasikitika sana kwa sababu kitabu hiki kilicholetwa na Mawaziri wetu wawili kina kurasa karibu 100 ambazo zinazungumzia masuala ya Muungano na masuala ya mazingira lakini ukikisoma masuala ya Muungano yamekuwa covered katika kurasa 12 tu, kurasa zote 88 zilizobakia ni mazingira. Sasa mimi nauliza hivi Waziri haoni kwamba suala hili ni muhimu na nyeti ambalo angelipaswa alizungumze kwa kina? Alikuwa anatakiwa anazungumzia matatizo yaliyopo ya Muungano, mafanikio yaliyopatikana, jinsi baadhi ya matatizo yalivyotatuliwa na changamoto ambazo zipo katika suala hili la Muungano. Lakini nasikitika sana kwamba hakufanya hivyo. Hii ina maana mbili ama alificha ule ukweli ambao tunataka sisi Wabunge na Watanzania kwa ujumla tujue au alikuwa anafanya hivyo pengine sijui kwa sababu gani.

Nikija katika masuala ya Muungano sote tunajua kwamba Zanzibar ilikuwa nchi huru na ambayo ni *sovereign* ni *independent state with sovereignty*. *Tanganyika* hivyo hivyo ilikuwa ni nchi huru na *sovereignty* yake na nchi hizi mbili katika mwaka wa 1964 ndipo zilipoungana. Wakati wa kuungana kitu kilichopotea ni *sovereignty* ya Zanzibar na *sovereignty* ya Tanganyika, yaliyobakia ni Zanzibar na Tanganyika zilikuwepo Zanzibar kama ni nchi *sovereignty* yake iliondoka na Tanganyika kama ni nchi *Sovereignty* yake ilipotea. Sasa unaposema kwamba Zanzibar si nchi mimi nashangaa sana. Lakini sasa nini cha kutazama, tunachotakiwa tutazame ni suala zima la kile chanzo cha Muungano.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha Muungano ni *articles of union*, a*rticles of union* ndiyo tunachosema kwamba hiyo ndiyo sheria kuu ndiyo *grand norm*. Sasa *articles of union* haziwezi kuwa chini kuliko Katiba ya Jamhuri ya Muungano wala Katiba ya Zanzibar. *Articles of union* ndiyo kama Katiba Kuu ya Muungano huu. Sasa twendeni

kwenye *articles of union* tutazame ni kitu gani kilichotakiwa, kitu gani kina kasoro na kitu gani ambacho tumekikiuka. Tukifanya hivyo naamini kwamba Muungano wetu utakuwa ni mzuri na tunaweza tukarekebisha yale matatizo ambayo hivi sasa yapo.

Mheshimiwa Spika, katika *articles of union* hizo za mwaka 1964 kuna mambo 11 ambayo yaliwekwa kama ni mambo ya Muungano. Bahati mbaya mambo yale yalikuwa yanaongezeka kama uyoga, yanaongezeka mara kwa mara kinyume na matakwa ya *articles of union*. Mpaka sasa tunayo mambo 23. Lakini hakuna hata siku moja tuliosema kwamba katika mambo haya 11 au 12 au 13 yaliyopo basi jambo hili kweli lina matatizo na tuliondoe katika suala hili la Muungano, hakuna. Mambo hayo yalikuwa yakiongezeka tu sasa *issue* ni nini.

Mimi nilikuwa nina wasiwasi nikasema ikiwa hivyo ndivyo basi pengine kulikuwa kuna *hidden agenda* ya kusema kwamba haya mambo tuyachukue kidogo kidogo hatimaye Zanzibar iwe haina Mamlaka yoyote haina nguvu ya kisheria ya jambo lolote na hii utaona kwamba ….

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Kanuni ya 64 (2) Mheshimiwa Spika, msemaji wa sasa mtiririko wake wa mjadala ni mzuri sana, isipokuwa hapa alipofikia kwamba hii agenda iliyofichika ya siri kuhusu mambo ya Muungano yaliyoongezeka toka yale ya 11 mpaka sasa 22, pengine ndugu yangu angefuta usemi huo. Kwa sababu alianza vizuri sana alisema nchi huru mbili *sovereign states* Tanganyika na Zanzibar zikaungana kukawa na *sovereignty* moja.

Kwa ajili hiyo tulikuwa katika Jumuiya ile ya Afrika Mashariki ya mwanzo kama nchi moja kama *one sovereignty state.* Kwa bahati mbaya Jumuiya ikavunjika na tulikuwa wanachama katika Jumuiya ile kama nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye *sovereignty* moja.

Mambo yale yaliyoko katika Jumuia ya Afrika Mashariki tulikuwa tunaendesha kama nchi *soverency* Jamhuri ya Uganda, Jamhuri ya Kenya ana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuvunjia Jumuiya basi yale mambo ambayo yalikuwa kwenye Jumuiya na ilirejeshwa kwenye nchi husika, kwenye *sovereignty state* husika na yale ambayo kwa upande wa Tanzania yalirejeshwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa hapa ila iko wapi?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nimechukua na mimi muda kutazama orodha ya masuala ya Muungano ambayo ni nyongeza ya kwanza ya Katiba yetu. Nimeangalia na kanuni nadhani Mheshimiwa Abubakar aliposema kuongezeka huku kunatokana na nia mbaya kwa mujibu wa kanuni zetu amesingizia jambo ambalo si la kweli. Kwa sababu haliwezi kufika hapa bila pande mbili kuridhiana, haya yanayoingia hapa hayawekwi kichochoroni usiku yanapitishwa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, kusema kuongezeka ni agenda ya siri hakika hii haipendezi inazua hisia ambazo si njema. Pengine kwa tafsiri hiyo inawezekana yeye ndio ana agenda ya siri. Kwa sababu hivi kuna athari gani masuala ya anga yakawa ya pamoja hii inaitwa athari kila anapoongezeka ni athari kwa Zanzibar kweli. Mimi nilipokuwa Serikalini suala la elimu ya juu lililetwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa hapo nani alikuwa na agenda ya siri.

Kwa hiyo, nadhani haya mambo ndiyo nasema tuyaangalie kwa vizuri. Mimi najua yote haya yana nia njema nimekuwapo nimekaa na wazee wale wanapozungumza isitokee hisia kwamba yanapoongezeka masuala yanayoimarisha Muungano basi hiyo nayo tena ni kero, hiyo itatufikisha mahali ambapo sasa tutasema ukisema kwa mfano turudi kwenye yale yale 11 ndio tunaimarisha Muungano.

Kwa dhati mtu unaipenda Tanzania unaweza kusema hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Abubakar naomba ufute usemi kwamba kuna agenda ya siri kwa sababu haipo.

**MHE. ABUBAKARKHAMIS BAKARY**: Mheshimiwa Spika, naomba kufuta usemi huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante bado Mheshimiwa Issa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, toka alipokaa Mheshimiwa Mchangiaji Ndugu Nyami akili yangu haijakaa sawa kidogo. Ibara ya 64 naona bora nitoe jasho langu. “Atatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli”. Mimi nimepata wasi wasi baada ya kusema kwamba ameshawajua maadui Zanzibar, kwa kweli nimepata *muhuma* mkubwa sana kwa sababu hapa tuko Bungeni tuna wajibu wa kuchangia na mtu kutoa mawazo yake. Sasa leo kwamba mtu anatoa mawazo halafu inakuwa ni kama adui. Tungelipata maelezo?

Lakini la pili zaidi ambalo anasema kwa bahati mbaya kuweko maana yake kama bendera yake Zanzibar tena kwa kejeli, sasa kwa bahati mbaya maana yake hili jambo hakukuwa na uongozi na ukapanga na ukakubaliana kwamba mnaweza kuwa na bendera yenu. Kwa hivyo suala hilo kwa kweli akili yangu haijakaa sawa Mheshimiwa Spika. Mimi naomba afute usemi wake.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado nasema tujaribu kuvumiliana suala hili ni kubwa na zito. Sasa kwa kiwango kile alichosema Mheshimiwa Ponsiano Nyami kwamba kuna maadui humu hilo ameteleza na hilo nitaomba alirekebishe. Lakini anaposema bahati mbaya kuna bendera ya Zanzibar hayo ni maoni yake. Hilo hakuna haja mtu kuna watu, wapo watu wengi sana wanaona kuongezeka kwa hisia za Zanzibar kujichomoza kama ni sehemu ya pekee kabisa ambayo lazima daima dumu iwe hivyo hivyo.

Kama ukifuatilia alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivi mtu unakaa unajiuliza hivi Afrika nzima ikiungana, Zanzibar peke yake ndiyo itakuwa ni nchi ya pekee, unajiuliza maswali kama haya. Kwa sababu kama lengo la Afrika ni kuwa na nchi moja watu kama Nyami wanaona hii kusisitiza upekee pekee wa Zanzibar uwe ni wa kudumu maisha milele ni tatizo, hao nao muwasikilize. Kwa hiyo, kwa hilo sitamwomba aombe radhi. Lakini lile la kwanza la kusema tuna maadui hilo lina kasoro naomba uliondoe.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kunipa nafasi hii ingawa nilipokuwa nachangia nilikuwa naambiwa kaa wewe mtoto mdogo hujui na mimi niliona ndio nilitamka kwamba aah kumbe nimeshawajua maadui wangu sio maadui wa Muungano. Lakini kama limeeleweka vibaya kwa nini nisifute hayo maneno. Nayaondoa. (*Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kama nilivyosema mwanzo ni kwamba kuna hili suala la *articles of unions* ambazo hizi zina matatizo na hizi ndizo zilizozaa kero nyingi sana za Muungano. Kwa mfano kuna suala la *TRA*, *TRA* ina matatizo na hayo yamesemwa hatujapata ufafanuzi. Nilifikiria kwamba Waziri atatuambia katika suala la *TRA* matatizo yake ni yapi na limepata ufumbuzi gani? Kuna mchango na mgawanyo wa mapato kwa mujibu wa ibara 133 ya Katiba haijapata ufumbuzi.

Kuna Tume ya Pamoja haijapata ufumbuzi, kuna Mikutano ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, mikutano hii ipo kila siku mimi nilifikiria kwamba angalau siku moja Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wangelikaa wakasema kwamba katika matatizo ambayo tumeyazungumza basi ufumbuzi wake tatizo (a) ni hili, ufumbuzi wake tatizo (b) ni hili.

Tatizo (c) lina matatizo haya na haya tunalifikiria, lakini wote Waziri Kiongozi, Waziri Mkuu wanakaa kwa muda gani. Kwa hivyo haya ndiyo yanayofanya Wazanzibar na Watanganyika kuwa na matatizo katika kusema kwamba kuna kero na kero hizi nafikiri vyombo vinavyohusika wangelisema.

Mheshimiwa Spika, kuna kero za mafuta hazijapata matatizo, kero za gesi hazijapata matatizo, ingawa msemaji wa jana hapa alisema kwamba

**SPIKA:** Hazijapata ufumbuzi au matatizo?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Hazijapata ufumbuzi, ingawa msemaji wa jana alisema kwa sababu Zanzibar kuna mafuta hatutaki. Sasa hapa Tanganyika kuna gesi mmeshaanza kuchimba mwaka wa sita huu Zanzibar haimo kwani hili ni tatizo kwa nini hamsemi hayo. Kuna masuala ya vyombo vya Muungano *ATC* kwa mfano toka ilipoanzishwa *ATC* ambayo naambiwa ni ya Muungano hatujui faidayake, hatujui hasara yake hatujui mambo mengine yanayohusiana na hayo. Hayo ni matatizo ambayo nilifikiria kwamba Waziri angetuambia.

Mheshimiwa Spika, katika Katiba vile vile katika nyongeza ya pili orodha ya kwanza utaona kwamba kuna suala linalosema kwamba sheria ambazo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote na sheria hii kwa mfano Sheria ya Kuthibitisha Mapato ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa nini sheria hii ambayo ni Kuthibitisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge, kwa nini isiungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wa Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, orodha ya pili vile vile kuna mambo ambayo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya watu wote ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar, kwa mfano madaraka ya Serikali ya Zanzibar. Madaraka ya Serikali ya Zanzibar kwa nini yaungwe mkono hapa na Bunge hili, kwa nini isiwe ni suala la Zanzibar peke yake.

Orodha ya mambo ya madaraka Serikalini au idadi ya orodha ya mambo ya Muungano na Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa nini Mahakama Kuu ya Zanzibar iungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar, hili ni suala la Zanzibar. Hayo na mengine mengi ndiyo mambo ambayo tunayasema ni kero za Muungano. Tanzania Bara vile kuna kero na ndiyo maana pengine katika mwaka wa 1993 kulikuwa na hili azimio la kusema kwamba *G55* wakasema na wao wanataka kuwa na Tanganyika ni sawa, kwa sababu sisi tulipoungana tulikuwa na Zanzibar yetu wao wakasema Tanganyika yao hawaitaki. Baada ya kuona kwamba kuna matatizo wakarudi kati ya mwaka 1993 wakasema wanataka kuwa na Tanganyika yao.

Mheshimiwa Spika, sasa hili ni tatizo kwa nini hatukai tukayatatua matatizo haya kwa niaba au kwa faida ya Watanzania wote. Baada ya azimio hilo baadae lilifutwa nakumbuka katika kikao cha tarehe 23 Agosti, 1994 na likaletwa azimio lingine azimio lililosema kwamba wanafuta azimio la Serikali ya Tanganyika na msimamo wao ni Serikali mbili kuelekea moja, sasa azimio hili litaleta matatizo. Litaleta matatizo Wazanzibar hawako tayari kuwa na Serikali moja. Wazanzibar tuko tayari kuudumisha Muungano kwa njia yoyote ile,

**SPIKA:** Hata Afrika nzima ikiungana mbaki nyinyi tu?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, sio hivyo.

**SPIKA:** Nakuongeza dakika zako 2 maana yake tumekukatiza katiza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninachotaka kusema ni kwamba sisi Wazanzibar tunasema Muungano ni mzuri lakini katika uzuri wenyewe tukaeni tutazame matatizo ambayo yanakabili Muungano wetu. Matatizo haya yatatatuliwa tu na viongozi wanapokutana wakatoa yale mambo ambayo wameyajadili lakini tokea Waziri Mkuu akae na Waziri Kiongozi mwaka wa ngapi hatujapata chochote kusikia kwamba kuna suala hili ambalo limeamuliwa. Tokea Kamati

nyingine zikae mwaka wa ngapi hatujapata kusikia chochote kwamba suala hili limeamuliwa. Sasa hayo kwa heshima kubwa sana naomba tuyatazame, tuyatatue ili tuweze kuondoa kero za Muungano. Vinginevyo kama hatukuondoa kero za Muungano basi hali haitorudi kama tunavyofikiria.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba murua iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na kwa kuanza tu naomba niseme kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo ya Zanzibar au Unguja au wapi mimi ni mtoto, nasema mtoto, sitaki, sintasema, nitasema mambo ya mazingira. Kwa sababu gani nimeshagundua kwamba wanachokitaka hawa kipo na kama kipo sijui kitu gani na sitaki kabisa kusema. (*Makofi)*

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mambo ya mazingira tuchukue katika mpango wa kisayansi. Kuna kitu kinaitwa *paleogiology, paliontology, palioclimatic*, vitu kama hivi mkiviangalia kwa undani kabisa mtakuja kugundua kwamba kitu gani tunachotakiwa kukizungumza katika maeneo hayo.

Kwa mfano katika Mlima wa Kilimanjaro kweli watu wengi wanavunjavunja miti, wanaharibu mimea, kule miti mingi inakatwa eti kunakosekana mvua, lakini habari niliyonayo mimi niliyekuwa Bwana Maji nasema kwamba mvua nyingi inanyesha sana kule juu kuliko hata chini ya Mlima ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano hata kusema kwamba kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro ndio kunakochangia maji ya mto Kikuletwa na mengine mengine Pangani tukasema labda pengine ndio sababu kubwa mimi bado nasema sivyo. Iliyopo ni kwamba mvua inayonyeshwa kwenye msitu mkubwa ulioko kule ambao unaelekea upande wa kilele ukishanyesha unaingia chini ya ardhi, ukishaingia chini ya ardhi kuna kitu kinaitwa *residence time. Residence time* ni muda ambao unatokea wakati maji ya mvua inaponyesha mpaka yanapokuja kutoka kwa namna ya ziwa, chemchem na kadhalika na kwa mfano huo naweza kusema kwamba ukienda kwa mfano kama *Lake Jipe* ukienda kama pale Soko ukienda Weru Weru ukienda Shiri yaani vile vitu utaona wakati wa kiangazi maji yanapungua na wakati wa masika maji yanaongezeka ni kwa nini ni kwa sababu ya *residence time* na wakati wa uhai wa macho yangu nilishawahi kufanya *research* pale nikagundua kwamba muda unaotumia maji kutembea kutoka kunako *recharge* mpaka kunako *discharge* ni karibu siku 60 ambazo zinakuja kuvamia kwenye muda mwingine wa *climatic* ambayo tunaijua sasa hivi.

Ndugu zangu nataka kuzungumza suala la ukataji wa miti na mkaa. Mkaa kusema kweli ndiyo nakubali kwamba unaharibu mazingira kwa sababu inaharibu uoto wa asili, ni sawa sawa. Lakini kuna kitu kinaitwa *climatic change global warming* vitu hivyo ndio vitu vya kuzungumzia vya msingi. Dunia hii imegawanywa katika misingi, kuna *lithosphere*, kuna *atmosphere* na mambo mengi tu mambo yanayotendeka hapa duniani ni ya binadamu kwa wingi wake na mambo hayo kusema kweli ndiyo yanayoweza kuwa *regulated.*

Lakini yanayotokea na muundo wa dunia *you can't bit it never* na nasema hivyo kwa sababu kwamba kule Kioto wenzetu Wamerikani walipokataa kutia saini walikuwa na maana yao na sisi tulipotia saini tulikuwa na maana yetu, sasa tuache. Ninachosema kuni kutumika kusema kweli tutumie lakini kwa namna ambayo ni endelevu. Mikaa tukate kwa namna ambayo ni endelevu na kila kitu tutumie kwa namna ambayo ni endelevu.

Lakini sio kusema kwamba kuanzia leo miti marufuku kukwata, kuanzia leo sijui nini nashangaa kabisa kwa sababu hiyo kitu kwa mfano kwenye *lithosphere* kuna gesi, gesi ni chanzo kizuri sana cha kuleta moto kwa maana ya kwamba tunaweza tukatumia gesi katika kupikia na mambo mengine.

Tunayo gesi tungeweza kuitumia kwa ukamilifu tukapunguza matumizi ya kukata miti hiyo mimi ningefurahi sana kuiona na agenda hiyo ingetolewa ningeifurahia kwa makini kabisa na ningeichangia kwa nguvu zangu zote.

Lakini kusema kwamba wasikate miti, sijui wasifanye nini hii naona ndiyo, ni sawa sawa lakini isitiliwe mkazo sana wakati wanaacha kusema habari za *Arzonilayer* ambayo inabomoka kule ambayo ndiyo inayoharibu mazingira ya dunia yetu badala yake tunaanza kuzungumzia kuni. Akinamama wanakwenda kukata kuni *Arzonilayer* wanakwenda mijabali mikubwa, Mimarekani, Mirusi wanatoboa kule kama wanavyotaka kumekuwa kama sijui nisemeje.

Lakini badala ya kuzungumzia hayo au kwa sababu ya udogo wetu kama ninavyokataa kuzungumza habari ya Zanzibar mimi kwa udogo wangu au sijui kuna nini. Maana yake ardhi yetu imejigawa, kuna mambo ambayo tungeweza tukazungumza habari za *wetlands* jinsi tulivyogawa, tunaweza tukazungumza mambo ya chanzo cha maji kwa mfano Wami Ruvu kwa nini imeitwa Wami Ruvu, kumbe ule Mto Wami umetokea Makotopora vitu kama hivyo na uchafuzi tunaotaka kuuzungumza wa mazingira unaweza ukapatikana hapa ukaenda chini kwa chini ukatokea mpaka Wami na ukaenda.

Halafu Zanzibar pale jiografia inasemaje ilikuwa wapi, imeanzaanzaje, nafikiri ningekuwa na uwezo kidogo ningeweza kutoa *lecture* ya jinsi Pemba, Unguja na Visiwa vingine vidogo vidogo jinsi vilivyoanzishwa. Maana yake makelele yote haya

mkiyaweka kwenye *jiology* elimu ya miamba hivi vyote ni vidogo na waasisi wetu wamevijua hivyo.

Kwa hiyo, nasema acheni, kama mnataka kufanya kitu cha siri au kama sikosei basi jiumbueni tuone. Maana yake nini sisi hatutaki mambo ya chini chini, ya chini chini tuwaachie wale wanaopenda vitu vya chini chini.

Sisi watu ni wa wazi tutakuwa wazi na tutaelekeza mambo yetu yaende wazi na tunaunga mkono Muungano kwa asilimia mia moja. Msemao vinginevyo na mlie. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi labda kwanza niseme kwamba historia ni Mwalimu, ni mwalimu ambaye anatufunza. Ikiwa ni mwanadamu, ikiwa ni taifa pale ambapo tumejikwaa kule nyuma basi tujerekebishe ili tukipita pale tusijikwae tena. Ikiwa ni sisi ikiwa ni wengine kwa hivyo mimi naona nienze kwenye historia. *(Makofi)*

Nataka niwarejeshe nyuma katika historia ya ulimwengu wetu huu kama miaka 20, 30 nyuma hivi. Katika dunia yetu kulikuwa na Taifa moja lenye nguvu sana hili likitambiana sana na wenzake. Lilikuwa taifa ambalo ni moja kati ya majogoo au katika viranja wa Ulimwengu huu kwa kiingereza linaitwa *Super Power*. Taifa hili hivi leo halipo, lilikuwa linaitwa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti.

Mheshimiwa Spika, wakati linaundwa taifa hilo, wazee waliounda taifa hilo na hata muda mrefu baada ya kufa kwao ilikuwa wananchi hawaruhusiwi kuhoji, usiulize, hata ukifikiri tu hata hujafungua mdomo basi tayari, umeshanyakuliwa, umeondolewa umesahauliwa. Ndivyo ilivyokuwa. Kwa hiyo hii tabia ya kuzuia, ya kutishana, kukandamiza, kukataza, kukemea, hii itaweza kutufikisha pabaya.

Mheshimiwa Spika, taifa hili lilidumu mwaka 74, mwaka wa 1985 uliingia uongozi wa vijana wakati ule na kidogo wakaregeza masharti. Kwa hiyo lile joto ambalo lilikuwa likikandamizwa wakati wote, likizuiwa, likikemewa lililipuka kama unapofungua mfuniko wa *pressure cooker*. Lilipuka kweli kweli na ilipofika mwaka 1991 nchi ile ikasambaratika kama nyumba ya karata inavyoanguka wakati wa upepo. Hiyo ni moja ziko nyingi. Yugoslavia, tunajua vita vya Balkan miaka kumi iliyopita ilikuwa vivyo hivyo. Yugoslavia ilianguka ikavunjika vipande vipande kama sahani unayoidondosha juu chini ya ardhi au kwenye sakafu inavyodondoka na tena mbali ya kudondoka na kuvunjika iliambatana na vita vikubwa vya kikatili kabisa na mauaji ya kishenzi kabisa.

Mheshimiwa Spika, huo ni mfano mwingine kwa mimi ningeiita Jamhuri au Muungano ambazo zimeundwa ikiwa na misingi yake imejengenga kwa hoja ya nguvu. Miungano hiyo imejengwa na wanasiasa na ikabomolewa na wanasiasa. Wananchi kwa hali yoyote hawakujumuishwa katika miaka yote na mifano iko mingi. Tulisikia Senegambia, tulisikia Eritrea na Ethiopia zilivyovunjika, tumesikia Indonesia na Timor Mashariki ilivyovunjika, yote hiyo ni mifano historia inatufundisha.

Mheshimiwa Spika, na hata kama hakuna kuvunjika basi kuna migogoro ya kila siku. Nitoe mfano ya China na Tibet au China na Jimbo lake la Xin jian au India na Kashmir au Urusi na Chechnya, hiyo yote ni mifano historia inatufunza. Kwa hivyo mimi kwa maono yangu ni kwamba kwa kweli imefika wakati tuwashirikishe wananchi, tuibue mijadala ya kitaifa kwa nia nzuri tu kidugu, kwa nia njema tu ili baadae tufike kwenye muungano ambao tunauhitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeangalia upande mmoja wa sarafu, ngoja niangalie upande wa pili. Kuna aina ya Muungano katika Ulimwengu huu. Umekuwa ukidumu siku zote. Canada, ni Shirikisho la Majimbo 10. Jimbo moja katika hayo Quebec wakazi wake wanaongea kifaransa wakati wengine wanaongea kiingereza na hata utamaduni wao ni tofauti kidogo. Kwa hiyo pametokea na misuguano wakati mwingine lakini wakati wote inapotokea misuguano hiyo paliibuliwa mijadala ya kitaifa. Watu wakaongea, wanasiasa wakaongea na hata ikafikia kupiga kura ya maoni. Lakini wananchi wakaamua kuibakisha Quebec katika Canada; mijadala ya kitaifa. Hii ni aina ya muungano ambao umejengwa kwa nguvu ya hoja ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, aina nyingine Denmark, ni nchi ya Kifalme. Lakini katika Denmark kuna Visiwa, mfano Fore Islands na Greenland. Kwa mfano Fore Islands kutokea mwaka 1948 ilipata uhuru mkubwa tu na Greenland katika mwaka 1979 nayo ikpata uhuru mkubwa tu, lakini ikiwa katika Ufalme wa Denmark. Naambiwa hata Visiwa hivi katika Balozi zao za nje wanao wawakilishi wao. Wanadiplomasia wao ambao wanaamua yale tu ambayo yanahusu visiwa vyao. Lakini leo Zanzibar ushiriki wetu katika medani ya kimataifa hata hapa East Africa jamani tusionekane? Hii ndiyo inayotuuma.

Mheshimiwa Spika, nirudi nyumbani nimetembea sana huko nje. Nirudi nyumbani, tumeungana Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 ni jambo zuri sana na tunaliunga mkono sana na tunawashukuru sana wazee wetu.

Lakini nirejee kwenye Kitabu cha *Pan-Africanism or Pragmatism? Lessons of Tanganyika - Zanzibar Union.* Ni kitabu ambacho kimeandikwa hivi karibuni tu na msomi mkubwa sana hapa nyumbani Profesa Issa Shivji na kimekuja kwa wakati kwa kweli.

Sasa yeye katika ukurasa wa 97 wa Kitabu chake anasema hivi. "*In sum an interim Constitutional and Legal framework for the Union was established by amending the existing Constitution of Tanganyika and extending the relevant laws of Tanganyika to Zanzibar. The power to do so was exercised by the President, that is to say, the head of union executive, who was also, by law, the head of Tanganyika executive. In effect it could be said that the first Constitution of the Union albeit Interim, was promulgated by one man, the President, and by one side of the union, Tanganyika. Even Karume was not consulted." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yangu ambayo siyo ya kitaalam inasema hivi; *"Kwa kifupi Katiba ya muda na mfumo wa Sheria ya Muungano ulianzishwa kwa kurekebisha iliyokuwa Katiba za Tanganyika na kuzifanya Sheria mahususi za Tanganyika zitumike Zanzibar pia. Haya yalifanywa na Rais, yaani Mkuu wa Serikali ya Muungano, ambaye pia alikuwa kwa mujibu wa Sheria, Mkuu wa Serikali ya Tanganyika. Kwa maantiki hii, inaweza kusemwa kuwa Katiba ya mwanzo ya Muungano, pomoja na kuwa ilikuwa ni Katiba ya muda, iliundwa na mtu mmoja, ambaye ni Rais, na upande mmoja wa Muungano yaani Tanganyika na hata Karume hakushirikishwa au hakushauriwa."*

Mheshimiwa Spika, mimi baada ya kusema hayo nirejee kwa maneno aliyosema Mheshimiwa Marmo. Mheshimiwa Marmo wakati inajadiliwa *OIC* hapa Bungeni katika Mkutano wa Kumi tarehe 23/2/1993, Mheshimiwa Marmo akiwa Mwenyekiti wa Mambo ya Katiba na Sheria alisema hivi. …*Nne Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imedhihirika kwamba bado yapo matatizo muhimu yanayohusu Muungano wa Tanzania na ili kukidhi utashi wa sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katiba ya Muungano iangaliwe tena ili kuchunguzwa upya muundo wa Muungano mapendekezo ya Tume ya Nyalali na mapendekezo ya Kamati ya Ndugu Mark Bomani"* Mwisho wa kunukuu maneno ya Mheshimiwa Marmo.

Kwa kweli ingekuwa tumefuata ushauri mzuri wa Mheshimiwa Marmo kwa kweli tusingekuwa na matatizo hivi leo. Lakini matatizo haya yamekuwa yakirejea. Miaka ya themenini kulikuwa na uchafuzi wa hali ya hewa ya kisiasa Tanzania Zanzibar, miaka ya tisini kulikuwa ni kutingisha kibiriti. Hivi sasa kuna mambo ya nchi si nchi na tukiachia baada ya miaka mitano kumi yatarejea mengine hatujui.

Mheshimiwa Spika, tuna njia mbili tu. Kwanza mie hata sitaki kuifikiria. Tuendelee kukandamiza, kuzuia, kukataza tusiseme tuje tuishie kule ilikoishia Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti, Mungu aepushe. Pili tukae tuibue mjadala wa kitaifa. *(Makofi)*

Hivi leo mimi nafikiri kwa kweli hakuna Mtanzania mwenye akili yake atasema hatotaka muungano hakuna au kama wapo ni wachache. Lakini waulize watanzania hao hao je, mna uafiki huu muungano tulionao? Watakwambia ahh! Muungano huu hatuuafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna tatizo. Bahati mbaya muda umekwisha ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Pole sana mjadala mtamu huo ingawa Doctor wewe unasema kuna kukandamizwa na nini wakati unachangia kwa uhuru kabisa halafu unasema unakandamizwa, sasa sijui. Lakini tunaendelea sasa namwita Mheshimiwa Mudhihir atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi siku tunapata uhuru kutoka kwa Muingereza nilikuwa mwanafunzi wa darasa la nne nikiwa na miaka 12 tu. Tunaungana mwaka 1964, tunaipoteza Tanganyika kwa nia njema ya kujenga Tanzania nilikuwa darasa la sita bado kijana mdogo sana. Nakusudia kusema nini?

Katika maisha yangu naijua zaidi Tanzania kuliko Tanganyika. Lakini hata kwa wale ambao walikuwa wakubwa kwangu kwa umri kama kaka yangu Kapuya hata na yeye kaifaidi Tanganyika kwa miaka mitatu tu. Kwa hiyo anaijua zaidi Tanzania kuliko anavyoijua Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakusudia kusema hivi kwa sababu mtafaruku tunaouona humu ndani kati ya Wazanzibar na Watanzania Bara ni mtafaruku wa mazoea. Sisi tulishalisahau jina la Tanganyika ambalo tulikaanalo kwa miaka mitatu tu.

Lakini wenzetu wamekuwa nalo jina la Zanzibar tangu Muungano mpaka leo ni kazi ngumu kwa kweli ukimwambia aachane nalo ghafla ghafla.

Kazi ngumu sana wameshakaanalo muda mrefu limekuwa ni sehemu ya utamaduni wao, imekuwa ni sehemu ya maisha yao. Kwa hiyo wapo Wazanzibar wanaochukia kuisahau Zanzibar kwa sababu ya mazoea. Lakini wapo Wazanzibar wengine wanaoitaka Zanzibar kwa maana nyingine kabisa tofauti na nitaeleza kwa kirefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuna sababu ya kugombea majina, sisi ni viongozi wakubwa na tunajukumu kubwa kwelikweli kwa watanzania wenzetu; na ndiyo maana wakati tunaapa tumeshika na vitabu vyetu vya dini kwa kumweka Mungu mbele. Leo itakuwa ni kichekesho mimi nisimame hapa nigombee Tanganyika, kwanza aliyetoa jina la Tanganyika simjui wala ukimuuliza maana yake ni nini Tanganyika, mimi sijui na sijui kama kuna anayejua Tanganyika maana yake humu ndani. Wala si busara kugombea neno Zanzibar maana hata huyo aliyelitoa hakumshirikisha Mzanzibar na sijui kama tunajua maana yake nini. Kwa hiyo jukumu letu kubwa sisi ni kuangalia wananchi wa pande zote mbili za Muungano ndiyo jukumu la msingi.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nataka niongeze kusema; maingiliano ya wananchi wa Tanganyika na wananchi wa Zanzibar hayakuanza mwaka 1964. Tulikuwa na maingiliano haya kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Ndiyo maana leo ukienda kule Kiboje Zanzibar utafikiri Wilaya ya Mgeta, Waluguru watupu, ndiyo maana ukienda Bungi pale Zanzibar kuna Wamakonde Msumbiji hawakujui, ndiyo maana ukija huku Tanzania Bara kila kona utawakuta Ndugu zetu wa kutoka Zanzibar wanafanyabiashara. Tumeoleana, tunazaliana, sisi ni watu wamoja tu Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukikaa ukapanga faida na hasara za Muungano, huhitaji kuwa na digrii ya chuo kikuu kugundua mara moja kwamba muungano unafaida kubwa sana. Kufutika kwa Tanganyika huku Tanzania Bara, ndiyo kumezima ukanda, ndiyo

kumezima ukabila ndiyo au Wasukuma na Wanyamwezi kwa wingi wao kama tungekuwa na Tanganyika bado tunayoyaona Unguja na Pemba tungeweza kuyaona hapa.

Lakini watu hapa hatuna habari ya ukabila, ukizungumzia *Mtwara Corridor sijui Central Corridor* tunazungumzia maendeleo ya wananchi, sio Kiongozi Mkuu wa Nchi hajatoka Ukanda huu, hatuzungumzi hilo.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa mvutano huu tunaouona leo kati ya Unguja na Pemba mpaka wengine wanaitana vibua, wengine makanadi ni kwa sababu ya Serikali tu wala sio wananchi. Kuwepo kwa ile Serikali ndiko kunawafanya watu wavutane makundi. Ndugu yangu Ali Salum jana alikuwa anazungumzia huu Muungano wa Tanzania mfano wake uko wapi? Waziri uje utuambie. Nenda tu Uingereza na Northern Ireland ndiyo mfano wake. *Northern Ireland* wana Serikali yao lakini ni sehemu ya *United Kingdom of Great Britain*.

Muingereza walikuwa marafiki wakubwa wa Anglikana wa Northern Ireland lakini si Wakatoliki. Lakini Wakatoliki na Waangalikana wanapofika kutetea Ireland yao wanakuwa kitu hiki kimoja. Zanzibar tunajua kuna mvutano mkubwa kweli kweli kati ya *CUF* na CCM. Lakini unapofikia suala la Zanzibar *CUF* na CCM Zanzibar wanakuwa kitu hiki kimoja. Nilitaka kutoa mfano huu alioutaka kuujua ndugu yangu Bin Salim pale. Sasa mimi hili ndilo linanitisha. Linanitisha sana kwa sababu kero nyingi za Muungano tunazozizungumza sio kero zinazoibuliwa na wananchi wa Zanzibar au wananchi wa Tanzania Bara. Ni kero zinazoibuliwa na sisi viongozi kwa sababu tu ya tamaa ya kutawala basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana inafikia mahali viongozi wa pande hizi mbili wakasimama hadharani kutoleana maneno ya kudharauliana. Mwanadamu akijenga nyumba anahakikisha anajenga na chumba mle ndani. Chumba kile madhumuni yake sio kumficha mwanadamu wewe unaonekana tu, unaenda kazini unakuja Bungeni. Unajificha mle ndani kwa ajili ya maneno yako na vitendo vyako, viwe vizuri au vibaya lakini kuna vitendo na maneno yanayohitaji faragha na viongozi mnayo maneno ya kusema hadharani ya kuhamasisha wananchi kufanya jambo jema. Mnapotaka kuzungumzia maneno ya kutaka kukosoana kaeni kwenye falagha zenu na vikao vyenu. Mkisimama hadharani na kuanza kubomoana mnatuyumbisha mnaotuongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo sikutarajia mimi kama jambo lile lilokuwa limezungumzwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu lingekuwa linaendelea kukaa kwenye midomo yetu mpaka leo. Kama wangetafuta utaratibu wa kukaa kwenye vikao vyao ambavyo vipo ninauhakika haya yasingetokea. Lakini haya maneno yanayotoka Zanzibar yote yetu? Mimi nilipata bahati kusoma kitabu kinaitwa Zanzibar Ukweli ni Huu. Kitabu hiki kimetungwa na Thani Feiruzi ambaye alikuwa *Hizibou Youth League Secretary General* kabla ya Mapinduzi. Thani Feiruzi anasema mambo makubwa yafuatayo:-

Moja anasema 1964 Zanzibar hakukuwepo Mapinduzi lakini kulikuwepo uvamizi kutoka Tanganyika na anatoa ushahidi katika lile Baraza la watu kumi na nne, kulikuwa na Watanganyika. Akamtaja Mzee Nassoro Moyo kutoka kule Songea, Mzee

Mfaranyaki, amemtaja Mzee wangu wa kutoka Tunduru Mzee Hamis Darwesh, kamtaja Mzee Natepe, anasema hawa wote walikuwa ni wavamizi kutoka Tanganyika. Kwa hiyo, yeye hayatambui Mapinduzi. Nikimsikia Mzanzibar anazungumza kwamba hayatambui Mapinduzi ya Zanzibar najua hayo si maneno yake ni maneno ya Thani Feiruzi ambaye wakati anaandika kitabu huki alikuwa ndiyo Mwenyekiti wa *Zanzibar Association* yenye Makao Makuu yake Dubai. Dubai na Zanzibar. Sasa mimi naweza kujiuliza wakati mwingine kama mtu kutoka Tanganyika huku Tanzania Bara kwenda Zanzibar alionekana mvamizi na yule aliyepinduliwa ambaye alitoka Oman mvamizi ni nani? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini haya maneno ambayo ameyanukuu sasa hivi ndugu yangu hapa yamo kwenye kitabu cha Feiruz, kwamba Muungano wa Tanganyika na Unguja ulitengenezwa na Mwalimu Nyerere na ndiyo maana alipeleka Polisi kwenda kusaidia Mapinduzi. Polisi hawakwenda kusaidia Mapinduzi Zanzibar, Polisi walikwenda kulinda amani baada ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mapinduzi ya Zanzibar yalitengenezwa na Wazanzibar wenyewe baada ya kuchoka kutawaliwa. Lakini leo tunasema Mwalimu Nyerere ndiyo alileta haya, haya mambo hayawezi kuwa sahihi, Nyerere peke yake asingeweza kwenda kuivaavaa tu Zanzibar ambayo wakati huo wametoka kunawa damu za Mapinduzi.

Lakini tunaposema kuna zile *Item 11* ndiyo Msahafu, ndiyo Biblia, ukibadili umekufuru, sisi wanadamu wa Tanzania sio jiwe. Maana jiwe kila likikaa likipigwa jua na mvua linakwisha. Sisi kama wanadamu tunaongezeka kwa uwingi wetu lakini tunaongezeka kwa busara zetu. Mnataka kazu ambayo mimi niliyoivaa siku natoka jandoni ndiyo niivae leo? Si nitakuwa kinyago, itanienea? Lazima mahitaji yangu yataongezeka kadri ninavyokuwa. Sasa kuongezeka kwa *articles of the union* kuna tegemea mahitaji yetu kama Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba mnaotupigia kelele kutaka Tanganyika tuanzishe Serikali yetu hebu tuacheni. Sisi tumeshasahau habari ya Tanganyika na wala hatuna ugomvi na jina sisi. Wala alililoleta jina la Tanganyika sisi hakutushauri tunawaleteeni Tanganyika sisi tumelikuta tu. Tunagombea kitu gani? Lakini sisi tubaki bado kuwa Watanzania na Mwenyezi Mungu anasema nini katika hilo? Mimi naomba ninukuu Surat-l-hujurat kwa Kiswahili; Mungu anasema hivi, "*Hakika tulikuumbeni ninyi kutokana na Mwanaume mmoja na Mwanamke mmoja*" bila shaka anakusudia Adam na Hawa. "*Tukawawekeeni mataifa na makabila ili mpate kutambuana tu. Aliyebora miongoni mwenu ni yule mwenye kunicha mimi*." Mwisho wa kunukuu.

Kumcha Mwenyezi Mungu ni pamoja na kumtendea mwanadamu mwenzako mema, kumletea kheri na sio shari. Kero za muungano lazima ziwepo sisi watu. Lakini dawa ya kero za muungano sio vurugu wala si maneno ya ovyo ovyo. Ni busara na hekima kwa viongozi wetu tukiwemo na sisi wenyewe maana na sisi ni viongozi.

Lakini kama kuna dawa nzuri ni chungu. Maana dawa siku zote ni chungu, ukipata bahati ya kupata dawa tamu ugonjwa wako wewe wa bahati sana. Faida tuliyoiona Tanzania Bara ya umoja wetu ni kutokana na kuvunjika kwa Tanganyika.

Tukiweza kufuta na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar taratibu wala si kwa nguvu dawa ya Utanzania itakuwa imepatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pasitumike jeshi, pasitumike kutukanana katika kuwaonyesha wenzetu wa Zanzibar kwamba sasa tumefikia wakati wa kuwa na Serikali moja. Kutumike busara tuzungumze tu. *(Makofi)*

Tutawa-care wale Watanzania tena wawe wenye raha zaidi, hata hili vurumai hili la Pemba na Unguja litakwisha. Kwamba kila siku Rais anatoka Kisiwa hicho tu huku sisi atatoka lini? Mbona sisi hatusemi kila siku Rais anatoka huko lini atatoka Unyamwezini ambapo kuna watu wengi?

Hatuna sisi mambo hayo huku yamepotea zamani. Ndugu zanguni dawa sasa ni kuelekea kwenye Serikali moja na ningewashauri Wazanzibar wana-CCM wenzangu maneno ya Thani Feruzi tutakapokuwa tunatetea Uzanzibar wetu tusiyakumbatie.

Wale wanataka kurudi kule, nyie mlimwaga damu kuipata Zanzibar yenu. Msipigiwe zumari nyimbo hamuijui mkaanza kuhemkwa. Ni hatari kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mimi nilikuwa na hayo machache ya kusema na nakushukuru tena maana yake ilibidi nijitoe mahali fulani niingie mahali fulani ili kupata nafasi hii lakini umenisamehe nakushukuru sana ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Namwita sasa Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud atafatiwa na Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD**: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini pia nikupongeze kwa kutumia jina lako kuipatia sifa nchi yetu kuwa Rais wa *CPA.* Niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada walizonazo katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mie nianze kwa kukuomba kubadilisha jina la kero za muungano. Hii inaonyesha dhahiri tafsiri ya neno kero wengi hawaelewi. Sasa nakuomba kwanza hii Kamati ya Makamu ambaye ndiye Mwenyekiti ibadilishwe jina iwe Kamati ya kuboresha muungano.

Mheshimiwa Spika, humu ndani tafsiri ya kero haijulikani kwa sababu kuna Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wao ndiyo walikuwa mstari wa mbele kukisaidia Chama cha Mapinduzi ili kishinde na tumefanikiwa kimeshika madaraka.

Lakini wao ndio wa mwanzo kuzitakaa baadhi ya Bajeti ya Serikali yao. Sasa wangelikuwa wanajua maana ya kero hayo wanayofanya wasiunge mkono ndiyo kero hizo.

Lakini kwa kuwa hawaelewi maana ya kero sasa bora libadilishwe jina. Hizi kero wanazozitoa za ndani ya Majimbo yao zingekuwa zimewekwa katika jina la kero ya muungano basi labda wangeelewa kero ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, elimu iwepo ya kuelimisha neno kero, lakini pamoja na hayo, ipo haja jina likabadilika kwa sababu ndilo linaloleta matatizo. Matatizo yanakuja kutokana na jina kwamba, lolote linalozungumzwa na Mbunge wa Zanzibar basi kero, lakini jimbo lolote lingine lililoko Bara likizungumza, likipinga hoja, kisa hajatimiziwa aliyoyataka, ameomba barabara, ameomba *dispensary*, ameomba vitu vingi ambavyo anataka apatiwe ndani ya jimbo lake; lakini kwa kuwa hakupata anasema siungi mkono hoja hii. Sasa kama tafsiri ya kero haijulikani, hiyo ndiyo kero ambayo kila mtu ana kero yake. Narudia kuomba hii tafsiri ya neno kero iondoke, tuweke maboresho, labda tukiweka hivyo tunaweza kwenda sambamba. Kwa sababu ukinitaka mimi Mbunge wa Zanzibar nizungumzie Zahanati ya Nzega kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Selelii, ambaye ndiye anaongoza hapa katika kutokuunga mkono kwa sababu zake mwenyewe, lakini ndiye wa kwanza asiyejua kero, namshangaa sana! Napenda tuyaweke sawa ili twende sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulifikiria Zanzibar kwa wakati huo kwamba, tukisikia mfadhili ametaka mwenyewe kujenga kitu fulani mahalai fulani, tulisema tunaonewa sana. Mwenyezi Mungu, mambo kama haya huyaweka bayana. Sasa humu ndani tunalumbana sisi wenyewe, Kaskazini kuna maendeleo zaidi kuliko Kusini; yanayofanya hivyo ni kero hizo! Kwa hiyo, imekuja sasa imefika wakati aliyeko Kaskazini anasema mimi sijapata kitu na aliyeko Kusini anasema wewe umepata, mimi sijapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tulidhani kwamba, mfadhili anataka mwenyewe, labda hataki kuja kujenga Zanzibar tu, kumbe hata huku Bara yapo na yanajitokeza humu ndani. Sasa kwa tafsiri rahisi hizo ndio kero. Tusitoe kipaumbele sana kwa sababu inazungumzwa kero ya Muungano ikawa ndiyo *slogan*, ikawa ndiyo *point* ya kuzungumzwa. Nani hana kero ndani ya jimbo lake? Mimi nipo hapa tangu mwaka 2000, sijasikia hata siku moja Serikali kuthibitisha kwamba, sasa tumepata pesa za kutosha, semeni wananchi mnataka nini! Siku zote Serikali inasema hali yetu ya uchumi ni mbaya na kweli lazima tukubali kutokana na hali ilivyo na tugawane kutokana na hali ilivyo. Kwa maana hiyo, kero zitaendelea kuwepo hata ndani ya majimbo yetu iwe Bara au Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa tukibadilisha hili neno tukasema kuboresha, labda tutaelewana. Mimi nasema tunazungumza Kiswahili kimoja, lakini sijui kwa nini hatufahamiani! Hapa ndipo ninapopata tabu mimi. Kisa kinachofanya tusifahamiane mimi sikielewi! Pananipa tabu sana, lakini tukifikia kubadilisha jina tukaweka kuboresha, basi naona tutapata mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kubwa lililoko hapa ni choyo ya maendeleo na choyo ya maendeleo ndiyo choyo inayotakiwa. Choyo ina aina mbili, choyo sawa sawa na kisu. Choyo ya maendeleo basi ni nzuri! Wewe ukinunua Mark II, mimi nanunua Range

Rover, choyo ya maendeleo! Lakini siyo mimi nanunua Range Rover, wewe unakuja kukata mipira (matairi), hiyo siyo choyo ya maendeleo. Ukimuuliza mtu atakwambia kisu ni kibaya, lakini ni kizuri, inategemea wewe unakitumia vipi! Ukimenya chungwa, ukimenyea mhogo, kina ubaya gani kisu? Lakini ukienda kumchinja mtu siyo kisu kilichochinja ni wewe uliyemchinja!

Mheshimiwa Spika, sasa tusilumbane kwenye matumizi yaliyo sahihi. Wanzanzibari wanadai mambo yenye msingi. Tukae tukubaliane katika mambo yenye msingi. Nakubaliana sana na kaka yangu Mheshimiwa Mudhihir, mtindo unaotumika kwa viongozi wetu kuwaona kwenye magazeti, tena basi bahati mbaya sana ni Viongozi wa Juu na wa Chama Kimoja. Wakati wana vikao vingi sana vya kukaa wakakosoana, wakaelezana, lakini utakuta kwenye magazeti huyu kasema na huyu kajibu. Hakuna faida, ukweli ni upotoshaji tu unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi sana hapa wamenukuu Katiba, lakini wamenukuu kwa maslahi yao, hawanukuu ilivyo. Leo Mbunge anahoji; kwa nini hakuna anayekwenda kwenye Baraza la Wawakilishi? Hasomi Katiba, angeisoma asingehoji hapa kwa nini hatoki Mbunge, wanatoka Wawakilishi kuja huku! Nasema tuwasamehe hawajui wafanyalo, wangelikuwa wanajua Katiba ipo wazi na sehemu pekee ya kurekebisha Katiba ni Bunge hili. Wao wana matatizo hayo, kwa nini hawaji hapa ikarekebishwa Katiba kama kuna matatizo ya kurekebisha? Lakini kukaa hapa mtu akachukua Katiba, akaisoma kama anaijua sana, kama kaitengeneza yeye kumbe hajui chochote ni kupotosha tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kitu kizuri, kiongozi umechaguliwa na watu wewe Mbunge, unaisoma Katiba kinyume nyume kwa faida yako mwenyewe! Kwa hiyo, ningeomba Wabunge wenzangu tusome Katiba tuijue vizuri; kama tuna matatizo chombo chenyewe ndiyo hiki. Katiba haipitishwi chini ya miembe, inapitishwa ndani ya chombo hiki! Sasa kama yupo mwenye matatizo na Katiba, tuna njia nyingi tu: Lete hoja binafsi, omba mwenyewe unakotaka kuomba, lete hapa tucheze nayo ngoma tuone lipi litafanikiwa, lipi litaharibika. Lakini kukaa ukainua Katiba, ukafanya wewe unaijua sana na kumbe hujui chochote ni tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunarudi kwenye choyo ya maendeleo. Mzunguko wa kifedha na ajira, ukweli Zanzibar ni tatizo kubwa. Hatuna pa kukimbilia ila kwa kaka yetu Jamhuri ya Muungano, inayo haki ya kuisaidia Zanzibar, si msaada ni wajibu wake. Zanzibar kuna bahati nzuri ya matunda msimu hadi msimu, yaani likitoka shokishoki, litaingia chungwa, likitoka chungwa litaingia nanasi, mzunguko huo unaendelea kwa mwaka mzima. Bado hatujafikiria kama ipo haja angalau kutuombea tukapata kiwanda tukaweza kusindika haya mazao, vijana wetu wakapata kazi. Vijana wengi hawana kazi! Haya yote yanayokuja, yanakuja kwa sababu hiyo, vijana wengi wanazunguka tu hawana lolote la kufanya.

Ukija kwa wavuvi ndiyo wanasikitisha zaidi; mvuvi akienda baharini akipata samaki mmoja, kila boti ikija na samaki mmoja, basi siku hiyo watapata pesa nyingi sana. Maboti yote yakijaza, basi siku hiyo hawapati pesa kwa sababu inabidi wauze kwa bei

yoyote, kama hawakuuza wataoza matokeo yake hawana wanachokipata. Sasa akijaza boti anasema leo nimepata samaki wengi lakini pesa hakuna. Siku anayopata samaki mmoja, tunanyang'anyana anapata pesa nzuri zaidi. Yote ni ajira na ninaamini Serikali ya Muungano ina uwezo wa kutusaidia tukaweza kuondokana na hayo.

Mheshimiwa Spika, si hayo tu, hata misaada inayokuja inayozungumzwa ya 4.5, mfano kama Serikali ya Muungano itatupa lami kadiri ya mgao unavyokuja, mwisho tutasamehe sisi kwa sababu nchi yetu ndogo, tutaweka lami mwisho inakuja tunasema jamani sisi hatutaki tena hii lami, chukueni ninyi lakini haifanyiki hivyo!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Soud. Sasa namwita Mheshimiwa Marombwa na nitatumia Kanuni ya 28 kuongeza muda wa dakika kama kumi ili Mheshimiwa Hafidh Ali aliyekuwa awe msemaji wa kwanza, sasa mekuja nataka nimpe nafasi.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Awali ya yote, niseme tu kwamba, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumza kuhusiana na Muungano. Kwa upande wangu mimi nataka nichukue muda mrefu kidogo, kuzungumzia masuala ya mazingira. Ninalizungumzia hili kwa sababu kwenye Jimbo langu la Kibiti, kuna eneo kubwa sana la Hifadhi ya Miti ya Mikoko na ni enelo la Ramsar *(Ramsar Site),* ambalo limewekwa rasmi kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira yetu, kila mwaka katika nchi yetu hii tumeweka Siku Maalum ya upandaji wa miti. Siku hii ni muhimu sana na kila Wilaya, kila kata, kila kijiji kinatakiwa kipande miti. Toka tuanze kampeni hiyo ya upandaji miti kwa siku ya mazingira duniani, mpaka hivi sasa mimi binafsi sijaiona tija yake. Hii miti inayopandwa kila mwaka mbona haionekani? Jangwa linazidi kuenea, tatizo ni nini? Mimi naiomba Serikali, inapokea kila mwaka taarifa kwamba mwaka huu Wilaya fulani imepanda miti 10000/20000, mwaka mwingine miti 15000 au 30000. Ninaomba Serikali, hii miti inayopandwa yote iweze kuratibiwa na Wilaya inapotoa taarifa yake kwamba mwaka huu tumepanda miti fulani, basi ieleze kwa miaka mitano nyuma kwamba, mwaka pengine 2004 tulipanda miti kadhaa, kati ya miti hiyo iliyokua ni kadhaa, iliyokufa ni kadhaa. Mwaka unaofuatia vile vile kwa miaka mitano nyuma. Watuonyeshe kwamba tulipanda ekari 30, lakini hadi sasa tumeshapanda ekari pengine 100, tuzione hizo ekari ambazo miti hiyo imepandwa kuliko kupokea taarifa ambazo hazitoi usahihi wa takwimu halisi za miti iliyopandwa katika mazingira yetu katika Wilaya na Mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la kwanza kuhusu upandaji wa miti. La pili, kwenye upandaji wa miti, mimi nawashukuru sana vijana wengi katika nchi yetu wanajihusisha na utengenezaji au uoteshaji wa miti, mijini wapo na hata vijijini wapo. Je, Serikali inawatambua vijana hawa? Vijana hawa wanawasaidiaje? Kijana mmoja ukienda maeneo ya Dar es Salaam, anaweza kuwa na vitalu vya miche ya miti zaidi ya

5000/6000. Serikali inawasaidiaje vikundi hivi kwa kuviunganisha halafu na hatimaye zile mbegu ambazo zinaoteshwa ziweze kutawanywa katika maeneo mengine ili kuboresha hali ya mazingira yetu hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibiti, kuna kikundi kinachoitwa *Rufiji Environmental Group*, ambacho kinaotesha miti ya asili. Kile kikundi kina miche zaidi ya 800,000 na miche hiyo mingi ni ile miti iliyoanza kupotea hasa miti ya Mikongo. Wameotesha miche mingi, lakini kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha, wanashindwa kuitoa kutoka kwenye vitalu vile ambavyo vina zaidi ya miti 800,000 na kuipeleka katika maeneo yasiyokuwa na miti ili waweze kuipanda na kuzidi kuimarisha na kuboresha mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri anayehusika, hebu ajaribu kukitembelea kile kikundi pale Kibiti. Jitihada wanazozifanya, naamini kabisa itakuwa ni mfano mzuri wa kuweza kukisaidia kikundi hiki kiweze kupata fedha ya kutoa vitalu vilivyooteshwa na kwenda kupandwa katika maeneo yasiyokuwa na miti.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza, hivi Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), pamoja na Mazingira, inaishia wapi? Watendaji wake wote wanaishia wapi? Mwongozo au Muundo wake ukoje? Kwenye ngazi ya Mkoa, kwenye ngazi ya Wilaya, kwenye ngazi ya kata, hivi tunamkuta nani ambaye anasimamia suala la Mazingira ambaye Ofisi ya Makamu wa Rais inamtambua? Ninamwomba Waziri katika majumuisho yake, atufahamishe Muundo mzima wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, nizungumzie masuala ya *Ramsar Site*, eneo la mikoko kule Delta. Mikoko katika nchi yetu ya Tanzania, inapatikana kwa wingi kwenye Jimbo la Kibiti katika Wilaya ya Rufiji. Eneo lile wananchi kwa sasa baada ya kukatwa miti, wameamua kupanda miti kwa wingi. Hivi Serikali inawasaidiaje wananchi hawa? Kweli miti iliharibiwa kiasi, lakini kwa jitihada kubwa za Serikali hasa ya Wilaya na Serikali za Vijiji vinavyozunguka eneo lile, miti inapandwa vizuri.

Sasa hivi miti ya Mikoko inapandwa kwa mistari, inaoteshwa vizuri na inakua vizuri, tunawasaidiaje? Naiomba Serikali iende ikaangalie namna ya kuwasaidia wananchi wa eneo lile ili waweze kupanda miti hii ya Mikoko ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, labda sasa nizungumzie ufinyu wa bajeti hii. Nilikuwa naangalia fedha za maendeleo zilizotengwa katika Wizara nzima, nimeona ni shilingi milioni 98; hivi hizi ndio fedha za maendeleo katika Ofisi ya Makamu wa Rais? Fedha hizi zitaendeleza kitu gani, kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji peke yake fedha za maendeleo inapata zaidi ya shilingi bilioni mbili au tatu? Ofisi kubwa kama ya Makamu wa Rais, inapata fedha za maendeleo shilingi milioni 98; zinasaidia nini? Zitafanya kazi gani fedha kama hizi? Ninaiomba Serikali iliangalie hilo kwa kuongeza wingi wa fedha katika miradi ya maendeleo itakayofanywa na Ofisi hii ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki cha Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwenye ukurasa wa 34 unazungumzia warsha zilizofanyika katika kanda mbalimbali. Kuna kanda ya bahari ambayo ni ukanda wa pwani, mazingira ya bahari ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa. Hivi Wabunge wameshirikishwa kwenye warsha hizi ili na wao waweze kutoa michango yao?

Namwomba Waziri mhusika wa Mazingira, warsha nyingi ambazo zinatolewa na Wizara yako, hebu jaribuni kuwashirikisha Wabunge. Wabunge ni wadau wa mazingira na wao waweze kuchangia namna ya kuboresha mazingira katika Wilaya zao. Wao ndio wanaojua vijiji vyote, wao ndio wanaojua vitongoji vyote, wataalam waliopo kwenye ngazi ya Wilaya hawajui vijiji vyote, wataalam waliopo katika ngazi ya mkoa hawajui vile vile vijiji vyote. Mbunge ndiye anayejua vijiji vyote katika jimbo lake, anajua vitongoji vyote katika jimbo lake.

Kwa hiyo, ukimshirikisha yeye, kuna uwezekano mkubwa sana wa kuweza kuboresha mazingira katika maeneo ya Wilaya zetu. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri, warsha nyingine zitakazofuata, ziweze kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge ili waweze kuchangia namna ya kuboresha mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 33 na wa 34, kuna changamoto nyingi zimejitokeza katika warsha hizo. Zile changamoto ni nyingi sana, zipo zaidi ya 20 katika maeneo mbalimbali. Maelezo ya namna gani ya kutatua changamoto zilizopo, yameandikwa kwa sentensi sentensi mbili.

Mheshimiwa Spika, nanukuu kwamba, "Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, uhamasishaji wa jamii kuhusu nafasi ya kila mmoja katika utekelezaji wa mikakati utafanywa."

Sentensi ya pili ambayo inamalizia inasema; "Mikakati ya muda mfupi kama vile utoaji wa matamko yanayohusu hatua za haraka katika maeneo hayo zitachukuliwa." Ni utoaji wa matamko tu! Zile changamoto ni nyingi sana, mimi nadhani kila changamoto moja iliyowekwa pale ilitakiwa ipewe majibu yake kwamba, utatuzi wake itakiwa ni nini! Haiwezekani changamoto zote zilizowekwa kwenye ukurasa ule zikajibiwa kwa sentensi mbili tu pale mwishoni mwa ukurasa ule wa 34. Hii haipendezi, mimi nadhani kila changamoto iliyokuwepo na namna gani ya kutatua changamoto hiyo ilikuwa ni ya muhimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie tu jambo dogo sana ambalo linahusu kero za Muungano. Kuhusiana na kero za Muungano, kama wenzangu wengi walivyozungumza, lakini na mimi niseme tuna kero nyingi hata na sisi wa Bara, siyo kwamba hizi kero za Muungano zipo Zanzibar peke yake. Wakati mimi jimbo langu nina wapigakura zaidi ya 70,000, mwenzangu anakuwa na wapigakura 5,000 tu; ni kero kubwa. Wakati posho yangu ninayopata mimi ndio ile ile anayopata Mbunge mwenzangu mwenye wananchi 5,000 tu; ni kero kubwa! Wakati jimbo langu linanichukua zaidi ya mwezi mmoja na siku kumi, karibu siku 40 kulizungukia, mwenzangu anazunguka jimbo lake kwa siku tatu tu au moja, amemaliza jimbo lake; hii ni kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uvumilivu ndio unaotakiwa kuwepo; kero tunazo nyingi na changamoto tunazo nyingi pia. Tunaiomba Serikali yetu, mimi binafsi naiomba Serikali yetu iziangalie kero hizi kwa undani zaidi na itafute mbinu nzuri ya kuweza kuzitatua bila ya kuchafuana na kuumizana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuchukua nafasi hii, kuomba radhi kwa kuchelewa kidogo kuingia hapa Bungeni, kwa sababu nilikuwa jimboni kutokana na sababu zisizozuilika ilibidi niende huko.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo; kwanza, nitamke tu kwamba, naunga mkono hoja kwa sababu kati ya Waasisi wa Muungano huu mimi ni mmojawapo. Nimezaliwa ndani ya Mapinduzi na nikaingia kwenye hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sina haja ya kusema mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa ninalotaka kusema, pamekuwa na matatizo tangu tulipoanza Muungano huu kiasi miaka 44 iliyopita. Mbali ya matatizo hayo, wakati wengine tukiwa tunaushangilia Muungano huu na kuutakia kila la heri katika utaratibu huu tulionao wa Serikali mbili, kuna wenzetu wengine wamejipa mamlaka ya kuwa na hati miliki ya Muungano huu.

Sasa Mtanzania mmoja kujifanya ana hati miliki ya Muungano na ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa maelezo yake atuambie, hivi alipokufa Karume mwaka 1972, akafa na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere; nani alikabidhiwa hati miliki ya Muungano huu akawa yeye ndiye msemaji mkubwa na anayeleta maudhi katika Muungano kiasi ambacho katufikisha hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu ni mambo ambayo yanakera katika Muungano huu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao umeunganisha Tanganyika na Zanzibar. Siyo vizuri katika Muungano huu tukaonyeshana vidole. Akianza mwenzetu mmoja kuonyesha vidole kule Zanzibar na wa Zanzibar akionyesha kidole Bara, ndio tutaingia katika matatizo yaliyoko sasa hivi. Cha kufanya, hivi sasa nafikiri tutazame matatizo yetu yako wapi na tunatakiwa tufanye nini. Hapo tukikaa kuzungumza haya tunaweza kufika mahali ambapo itasaidia sana vizazi vinavyokuja katika Jamhuri hii ya Muungano na Muungano wenyewe utakaa sawa.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu jambo tu la kuonyeshana vidole. Ndani ya Bunge hili, kuna Mbunge mmoja alikuwa akichangia na ninaomba ninukuu maelezo ambayo aliyatoa anasema: “Sasa ukiangalia Muswada ulioletwa inaonekana haugusi Zanzibar, maana ripoti ya leo ya CAG tuliyonayo, haizungumzii Zanzibar na Zanzibar imekuwa ni chanzo cha matatizo makubwa katika Muungano wetu miaka nenda rudi.” Narudia tena, tusionyeshane vidole! Hii ni *Hansard* na ninamkuu Mheshimiwa Mkono aliyekuwa anazungumza. Nasema tusinyosheane vidole, kama matatizo hayapo Zanzibar

peke yake na ndiyo maana tuna kero hizi tunazozizungumza hivi sasa. Sasa kuna jambo lipo, lipeleke katika ngazi zinazohusika lizungumzwe lipate ufumbuzi. Huwezi ukazungumza hapa ukasema sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano imekuwa na matatizo tangu kuasisiwa Muungano huu! Hivi Bara hakuna matatizo; sasa mbona watu wanasimama humu wanalalamika?

Mheshimiwa Spika, lakini la ajabu, Mbunge huyu anazungumza kwamba, Zanibar ina matatizo miaka nenda rudi. Hivi sasa anagombea Uenyekiti wa Wazazi na kura za Zanzibar ndizo zitakazofanya awe Mwenyekiti wa Wazazi. Zanzibar ina matatizo miaka nenda rudi asahau; narudia tena, asahau kwa sababu tufika mahali tuondoshe matatizo ya miaka nenda rudi, halafu tutampa Uenyekiti wa Wazazi. Hawezi kuunyoshea vidole upande mmoja wa Jamhuri tunategemeana.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaloliomba sana na hawa Wazee wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya miaka 44 hivi sasa kuna haja ya kuangalia vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa vinavyohusu Muungano. Narudia tena, hasa vinavyohusu Muungano; kwa sababu manung'uniko mengi yanayotoka Bara na Zanzibar bado yanakwenda katika vifungu hivi. Mimi nikizungumza kama Mzanzibari, nitazungumza upande wangu kwa sababu na mimi nina kero zangu za Muungano. Ndugu yangu hapa amesema tusiite kero, lakini mpaka sasa hivi tuite kero maana hazijabadilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanatakiwa yaangaliwe, naomba ninukuu katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukurasa wa 33(34): "Kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano na pia juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara."

Mheshimiwa Spika, mimi hapa ndipo nilipopata matatizo na ukisikia manung'uniko hii Katiba imejifunga mno na inaonekana kama kuna ujanja ujanja, kwa sababu ulivyosema mambo yote yanayohusu Tanzania Bara, tunavyofahamu sisi Tanganyika ilikubali kuondosha hadhi yake ikaingia kwenye Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuonyesha hadhi hiyo maana yake imo kwenye Muungano, Tanganyika ni nini na Tanzania Bara ni nini, si unabadilisha tu mkono wa kushoto unakwenda kulia? Kama hiyo haitoshi ni lazima tuangalie vifungu vyetu vinavyosema maneno hayo na hapo tunapofika ndiyo tunapata matatizo. Juzi Mheshimiwa Kikwete, alipokuwa akiweka jiwe la msingi kule kwa vijana wa biashara ndogondogo Ilala ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kikwete ndiyo nani?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA**: Aah unamzungumzia Rais? Sawa.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa anaweka jiwe la msingi kule alitoa mfano akasema *you can not eat your cake and have it.* Anasema huwezi kuila keki yako mwenyewe uliyonayo, ukishamaliza halafu unasema kwamba, bado unayo haiwezekani. Tanganyika imejiondosha lakini tunaambiwa kuna Tanzania Bara, Zanzibar katika Katiba hii inaambiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haina lake. Sasa Zanzibar haijala keki wala haina, Tanganyika imekula keki na bado ipo maana Tanzania Bara ipo, sasa tuangalie mambo kama haya yanayojitokeza, ukisikia manung'uniko yanayotokea kama hivi hilo moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunasema tu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sawa, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuna mambo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamo ndani ya Katiba hii. Tunaambiwa Muungano ulipoanza kulikuwa na mambo 11, sasa hivi tupo miaka zaidi ya kumi na moja; tunaposema haya ni mambo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yale yaliyobakia mwenyewe ni nani?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akija aniambie maana Tanganyika haipo, kuna Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; sasa mambo kumi na moja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yale mengine yaliyobakia mwenyewe ni ya Serikali gani? Ndiyo maana tumefika mahali, Marehemu Mwalimu Nyerere, akatoa onyo katika suala hili maana kuna wenzetu kule wengine alisema wakorofi; wakorofi kwa mujibu wa ilani yetu na utaratibu wetu mimi nakubali. Anasema kwamba, Zanzibar na Tanganyika ni Serikali tatu, akaona ajabu akasema moja na moja tatu! Kumbe wale wakorofi walisema Zanzibar na Tanganyika ni Serikali tatu, Mwalimu akakataa na mimi naendelea kusema kwamba, ana haki ya kukataa lakini tukatae katika misingi basi mbona hii tatu ipo gizani?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie haya mambo mengine yaliyokuwa si ya Muungano nani anayasimamia? Kinachokera zaidi, Wazanzibari ni pale unapoona kwa mfano, mambo ya miundombinu na mengine, wenzetu wanapoomba misaada kutoka nje hawaombi kwa jina la Tanganyika, wanaomba kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa unapoomba kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumesema wenyewe kwenye Katiba kwamba, Zanzibar ni sehemu ya Muungano wa Tanzania mbona haviji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii afya ni nani anaisimamia na nyingine nani anaisimamia? Tunasema kuna matatizo kidogo ni lazima tukae tuzungumze angalau tufike mahali tuwe tunajua basi tunakwenda vipi. Matatizo na manung'uniko mengi hivi sasa yanakuja inaonekana watu wasema kuna mtu kafa, lakini kumbe hakufa yu hai. Sasa huyu aliye hai ndiyo tunamtaka tujue yukoje, tuwe wawazi kidogo? Muungano ni mfano katika ulimwengu lakini Muungano wetu una matatizo ndani ya Jamhuri yetu ya Muungano na una matatizo kwa sababu kuna udanganyifu na ujanja; sasa huo ujanja tuuzungumze ili tuondoshe haya matatizo. Hakuna Mzanzibari hata mmoja ambaye hapendi kuona Jamhuri ya Muungano, sote tunataka tuwe na Jamhuri ya Muungano ni

sifa yetu lakini tuondoshe matatizo ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, unaposema kwamba, Zanzibar watakuwa peke yao; watakuwa peke yao katika mambo gani? Kuna mambo kumi na moja hayo, tangu yameanza mpaka leo bado kuna kero za Muungano, miaka 44 sasa hivi! Tusije tukaenda kwenye ule msemo wa Marehemu Mzee Karume, maana alisema maneno mawili; kwanza, alisema Azimio la Arusha mwisho Jumbe na alikuja Zanzibar, halafu akaja akasema huu Muungano ni sawasawa na koti, ukiwa na koti ukilitoa likikubana livue litupilie mbali. Kwa nini tunakwenda huko?

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwenda huko, ndugu yangu Mheshimiwa Mudhihir kazungumza hapa kwamba, kile kikoti cha udogoni kile mpaka leo anavaa? Huu ni mfano hai na mimi nakubaliana naye, hatuwezi tukavaa vilevile tu; kuna mambo ni lazima tuyazungumze kuondoka hapa tuache watu ambao wanakaa ndani wazungumze. Waziri Mkuu, ana mamlaka, Waziri Kiongozi hana mamlaka au Serikali ya Mapinduzi ipo hivi hapana; ni lazima tukae tuzungumze mambo yetu. Tatizo lililopo hatujanukuu vifungu vyetu vya Katiba kuona Jamhuri yetu ya Muungano hivi sasa imesimama wapi, nini matatizo ya upande wa pili wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa Zanzibar kuhusu Muungano, wenzetu wamekumbatia kila kitu na yale yaliyokuwa ya Muungano na ambayo si ya Muungano pia wameyachukua wao; nitakupa mfano mwingine.

Mheshimiwa Spika, siku mmoja ulinizuia hapa ukasema kwamba, Sheria itafanya kazi yake; ni suala la Michezo halimo katika mambo ya Muungano na ndani ya Katiba inazungumza hiyo. Lakini tangu tumeanza kuungana mpaka leo, wenzetu hawa wakaidi hatari; sijapata kuona watu wakaidi kama hawa! (*Kicheko*)

Mhehsimiwa Spika, hawataki kuifuata hii Katiba kwa sababu ingekuwa kuna kitu kingine Katiba inasema hivyo kwamba, mambo ya michezo si ya Muungano, mbona wanang'ang'ania wao tu; sasa ni miaka 44, kama miaka 44 imepita sasa hivi zamu yetu Zanzibar kuongoza, watupe sisi *International.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana hawa wanaongoza bila kibali chetu, hatukuwaambia watuendeshe sisi katika mambo ya michezo, haimo kwenye Katiba; wao wanafanyaje mambo ya ajabu? Sasa hili Mheshimiwa Waziri ulikuwa Waziri wa Michezo na hili unalijua hukulisimamia, sasa hivi bahati mbaya iliyokuwepo ni kwamba, yule mchawi ndiyo kapewa mtoto alee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii haiwezekani, Waziri huyu wa Zanzibar alipewa Wizara ya Michezo hakufanya kitu, kapewa Muungano sasa hivi sijui atakwenda kwenye vifungu au vipi; maana unapopewa jambo na wewe ulitazame kwa sababu mchawi kapewa mtoto alee atamuua, haiwezekani ni lazima tuangalie mambo ya Muungano. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, akifa mtoto huyu atakufa kwenye mikono yake, maana siku moja Waziri Mkuu hapa alituambia kwamba, hayupo tayari Muungano huu ufe mikononi

mwake; mimi namuunga mkono, ukifa mikononi mwake historia itajijenga. Mheshimiwa Waziri. Muungano usife mikononi mwako; Kiti cha Uzini utakuwa hukipata. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Mimi nadhani nitatafuta nafasi tufanye semina kuhusu Muungano, maana sisi ambao tunaujua vizuri, baadhi ya maelezo humu ni ya ajabu kabisa. Nadhani kwanza Wabunge tuelewe Muungano ulipotoka, jinsi unavyoendelea na ulikusudiwa ufike wapi. Leo mmewaona wale waliokuwa vijana wadogo wakati ule, lakini nadhani tunahitaji pia wazee wetu; akina Mzee Kingunge, leo amekaa kimya tu na wengine tusaidiane. Tutakaa pale Pius Msekwa tuweze kuelewana vizuri, kwa sababu wengine wanakwenda nje ya mstari, lakini nilikuwa naheshimu Kanuni ya 100 kwamba, wana uhuru wa kusema hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea saa kumi na moja. Nitamwita Mheshimiwa Issa Kassim Issa na tutahitimisha na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Bahati mbaya hao kama ilivyo kawaida, saa kumi na moja mara kwa mara nawaona mnakuwa na shida kidogo; kama hawatatokea basi nitamwita Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na Mheshimiwa Shah, ambaye hata hivi sasa hayupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, lakini nafasi ni mbili tu, atakayechelewa moja kwa moja tutaanza na yeyote kati ya hawa atakayekuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea hadi saa kumi na moja na nusu, nitamwita Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mheshimiwa Dr. Burian, ambaye atajibu hoja kwa dakika arobaini na tano; hiyo itatufikisha saa kumi na mbili na robo jioni, ambapo nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib ili aelezee masuala ya Muungano kwa nusu saa; saa kumi na dakika arobaini na tano tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi, nadhani saa moja itatutosha.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge, ningependa kusema kwamba, wageni wetu niliowatambulisha ambao walikuwepo tarehe 26 na kushiriki katika kuchanganya mchanga kutoka pande mbili za Muungano, wataelekea sehemu ya maonyesho hivi sasa; tukitoka hapa ni vizuri sana mkaenda kusalimiana nao. Wabunge wachanga kabisa kama akina Mheshimiwa Mhonga si fursa nzuri kuikosa. Pia Mbunge wa Kibakwe yupo, Mheshimiwa George Simbachawene, ndiyo vijana hao mkasalimiane. Mmesikia, mmoja ana miaka 74 atawapeni maelezo pengine itasaidia. Watakuwepo pale ili kusalimiana na Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, wakati natambulisha wageni, nilipitiwa sikuweza kumtambulisha mwanawe Mheshimiwa Waziri Mohammed Seif, yeye anaitwa Seif Mohammed Seif. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa tutaendelea saa kumi na moja na muda umepita, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 07.19 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya jioni, niweze kuchangia katika Wizara hii. Jambo la kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu na pili, leo kama kanuni ina uwezo wa kutupa nafasi ya kuweza kuwakumbuka Waasisi wa Muungano huu, basi ningeomba Kanuni iweze kuturuhusu tusimame dakika moja kuwakumbuka wazee wetu; Hayati Julius Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume, lakini nadhani Kanuni haituruhusu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, huruhusiwi kutoa hoja kama hiyo. Spika angeweza kufanya hivyo.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu habari ya Muungano, jambo la kwanza kabla sijaendelea ingelitolewa elimu mashuleni kwa elimu ya Muungano na tatizo hasa kwa wenzetu kwa elimu ya mambo yaliyopita ya mapinduzi wameyafuta. Sasa hili lingelirejeshwa mashuleni, lingeweza kutusaidia na kutuondoa katika matatizo madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakalolizungumza na mimi ni Mwanachama wa Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi kinaeleza Serikali mbili; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hili sina tatizo nalo. Tatizo langu ni Serikali tatu na Serikali moja sisi witiri hizi hazitufai kabisa.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kuna kiongozi au Mheshimiwa Mbunge, anasimama anazungumza kwamba, huu Muungano hautambui ukoje! Eeeh Muungano una miaka 44, leo unasema Muungano huutambui; ni nchi gani iliyokuwa na Muungano kama huu si tuupe hongera Muungano kama huu. Muungano wa nchi yetu uliokuwa madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaopinga Serikali mbili na wanaotaka Serikali tatu na moja wana siri ya ajenda. Waheshimiwa Wabunge, lazima tujitahadhari na watu kama hao. Wana kitu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepatikana kwa kupinduliwa, wao wakaambiwa tu bwana tayari mapinduzi wakakaribishwa. Wenzetu ninyi mmepata Serikali kwa kura, sisi tulipiga kura tukakoseshwa na hali tumeshinda na mtawala ilikuwa akienda Pemba anafikia kunako meli hateremki. Sasa haya lazima tuyakumbuke, wanataka kutupeleka mahali pabaya uchaguzi tayari mwaka 2010. Tujitahadhari sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi na watu kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Muungano, panapo uzuri na kasoro hutokea. Mwenyezi Mungu, ametuumba wanene na wembamba, wadogo na wakubwa, lazima tuwe na ustahimilivu na tuvumiliane.

Mheshimiwa Spika, Wazanzibari wapo milioni moja, lakini hali za Wazanzibari zinaeleweka; usifike kule Kempiski ukaona maisha ya Wazanzibari wanaoishi kama wanaoishi watalii wa Kempiski**,** wana maisha magumu na Muungano huu ndiyo unaoweza kutusababisha sisi tukawa na maisha mazuri. Tukae kwa kusikilizana si vyema Viongozi Wakuu mkanyosheana vidole wakati wake. Sasa hivi ni wakati wetu kukaa kitako kujadiliana, tukae kwenye meza moja tujue nini Muungano wetu tuuboreshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawahakikishieni wazi sisi tunaonewa choyo kwa Muungano huu na hakuna atakayethubutu kuvunja Muungano huu. Tusijidanganye, hapa sisi Waheshimiwa Wabunge tumewekwa na nani? Wengine tunatoka Chokocho, wengine tunatoka Uroa, wengine tunatoka Tabora, tumekuwa ndugu siyo ndugu wa hivi tu ni ndugu wa damu na ndiyo lengo na dhamira ya viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo chokochoko hizi zinatokea wapi? Tukae na tahadhari na wenzetu hawa Wapinzani, sana na Wapinzani wana ajenda ya siri kuhusu Muungano na lengo lao ni kuuvunja Muungano. Hapa wana maneno matamu kama sukari, lakini si kweli wana mambo yao tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninashangaa kitu kimoja; utasimama mwana-CCM unasema unataka Serikali moja ahaa! Haya makubwa tena wewe baada ya kusema unataka ile Suna ya rakaa mbili unataka rakaa moja, ambayo haigawiki, witiri; jamani tunaelekea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba, wananchi wanatusikiliza sisi wanasiasa tusiwapotoshe, tumefika mahali tunawapotosha wananchi wetu. Wananchi wetu wametulia, wanahitaji usalama na amani, siyo chokochoko. Hawa hawana la kushika kwa sababu wanaona mkono unatingishika na wanaona unakatika yagunju**,** mkono wa CCM haukatiki upo madhubuti na CCM itawaletea maendeleo wananchi wake wa Tanzania bila ya ubaguzi. Sasa mnataka nini jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zanguni mnataka nini? Mkataa ya Mussa hupata ya firauni**,** tuondokane na huko**.** Watu wanakaa kindugu, jamaa tunazaliana, tunataka nini; kwa nini tusirudi katika meza moja kuondoa zile kasoro wanazozilalamikia?

Mheshimiwa Spika, haya matatizo ya kuchelewa kutoa maamuzi katika masuala ya kero, ndiyo yanayoleta tafaruku humu ndani. Hebu wafanyeni wawe na maamuzi na wawe wanawajulisha wananchi wetu hatua moja baada ya nyingine, tunazozifanya katika masuala ya kutatua yale matatizo. Wazanzibari ni watu wakarimu sana na wataratibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mtu akifika mahali akasema ujue kwamba, anaumia huyo. Maana mimi huwezi kunilinganisha niwe sawasawa na Mheshimiwa Mgana Msindai, ndiyo Mwenyezi Mungu alivyotuumba. Mheshimiwa Mgana Msindai ni mnene, ndiyo Mwenyezi Mungu alivyomuumba. Mimi ni mwembamba ndiyo hali kadhalika nchi yetu tustahimiliane. Utakaponikanyaga lazima niseme na nitakaposema ndipo nitakaposikika kwamba ninaumia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, matatizo yapo na lazima tukubali kwamba, matatizo yapo, lakini tunayo nafasi ya kuyatatua. Sasa hivi kumekutokea kero, unateremka *Airport Dar es Salaam transit* kwenda Zanzibar kwa *Emirates*, unatakiwa mzigo uulipie; je, Zanzibar hakuna *custom*? Mimi safari yangu haijafika.

Mheshimiwa Spika, halafu sasa ni muda mrefu, nimesimama hapa nikasema kuhusu gawio; jamani na sisi tunakua si wadogo tena, tukaeni kitako tuyatatue hayo matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani leo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kaka yangu na pembeni kuna shemeji yangu, ninaloliomba Wizara hii ameongezwa Makamu kukaa kitako kujadili habari ya Muungano katika kutatua matatizo ya Muungano. Makamu ametoka Zanzibar, Waziri ametoka Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoka Tanzania Bara ndiyo kapungua. Msimchoshe Rais wetu, kila kitu tena Rais ndiye aingilie kati, hamumuonei huruma? Muoneeni huruma Rais wetu ana kazi nyingi huyo, ana majukumu makubwa. Sasa na ninyi onyesheni mfano kwamba mna lengo na dhamira nzuri kabisa ya kuondoa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawahakikishieni mkienda kwa *speed* kali kama aliyokwenda nayo Spika kwenye Bunge hili, matatizo haya yatakuwa hayapo. Tumieni muda mtatue hili tatizo, kuna tatizo la umeme sasa, watendaji pia wanawaharibu, nadhani ndani ya Chama cha Mapinduzi hamkuapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umeme Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu alilifikisha katika hatua nzuri. Juzi walipelekewa barua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanalipa asilimia 80 ya deni lililokuwepo, Serikali ya Muungano inachangia asilimia 20, Wananchi wabaki pale pale katika asilimia 21.7. Je, jamani tulikaa juzi hapa tukalitatua, leo limekwisharudi tena limekuwa kero linakuja kuwekwa kwenye Muungano hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu tukaeni tustahimilianeni, tukubaliane tunakwenda mwendo wa *slow much* au wa harakati. Mwendo wa *slow much* sasa hivi haufai, uchaguzi mwaka 2010 Wapinzani wanachukua hii *slogan;* lazima muelewe Wapinzani sasa hivi wametaka kudaka wamekaa kinyonyozi kule Pwani kwetu, tupa chambo tu wanakiokota, wala yeye humpati. *(Kicheko)*

Lazima muelewe wazi, wazee wangu tukae tutanabahi nini tunafanya katika nchi kuwaletea maisha bora wananchi wetu wakiwemo wa Zanzibar wana maisha magumu. Muungano wa Serikali mbili, mimi sina matatizo nao kwa sababu ndiyo ulionilea mpaka

umri huu. Nakwenda kifua mbele kwa sababu ya Muungano. Hawa waliokuwa hawaufahamu Muungano ndiyo wanaotuletea matatizo katika nchi hii, wapeni elimu, ipelekeni mpaka vyuo vikuu tutaondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo kwa leo usinipigie kengele ya mwisho, mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii. Kwanza, napenda niseme kwamba, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda niseme kwamba, kinachoendelea kujiri sasa hivi hapa nchini na hata kwenye Bunge lako Tukufu ni kitu ambacho hakifurahishi hata kidogo. Watanzania tunakoelekea kama ni kwa *speed* hii, nadhani siyo kuzuri tunaelekea pabaya.

Hivi ni wapi dunia ya leo tunafikiria kwamba Muungano ufe? Watu sasa hivi wanataka tuungane kwa kila kitu, *is a global village.* Dunia inataka tuungane kwa kila namna, leo kuna Watanzania wanafikiria kwamba pengine Muungano huu ufe! Mimi nafikiri dhana hii, ningependa tuiondoe kabisa katika mawazo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekerwa sana na baadhi ya matamshi ya viongozi wenzetu. Matamshi haya ukiyachukulia haraka haraka unaona ni mepesi, lakini uzito wake mimi nasikitika sana. Hivi leo suala la kwamba, Zanzibar ni nchi au si nchi linatoka wapi? Mwaka 1964 mimi nilikuwa bado sijazaliwa, nimezaliwa nimekuta hakuna Tanganyika, nimekuta Tanzania. Kwa hiyo, ndiyo maana ukisema kuna Tanganyika ifufuke sielewi Tanganyika iko wapi? Mimi nilizaliwa nikakuta Tanzania na Watanzania wote wa pande mbili, upande wa visiwani na bara ni ndugu na tunaishi katika nchi moja inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa hii inapoanza kujitokeza kwamba, kuna suala la nchi, kuna madaraka kamili, kuna Rais, Bunge, Katiba na vitu vingine. Mimi nafikiri ni kupotosha Katiba jinsi ilivyo. Ibara ya kwanza imesema wazi na naomba niinukuu hapa ibara ya kwanza ya Katiba imesema kwamba: “Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano na ibara ya pili imeelezea mipaka ya Tanzania.” Sasa huwezi ukawa na nchi ndani ya nchi. Watanzania tunakwenda wapi, tunasema kwamba, nadhani kama kuna kasoro basi tuendelee kuzungumza. Waasisi wamezungumza miaka nenda rudi na sisi tumekutana na hali ya namna hiyo, jamani tuendelee kuzungumza. Hivi leo kila mmoja akianza kueleza masikitiko au akianza kueleza kwamba, yeye ana tatizo gani tuulizane humu Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Busega napata *resources* sawa sawa na Mbunge wa jimbo lolote la kutoka upande wa Zanzibar. Hivi na sisi tukianza kulalamika kwamba, kwa nini Wabunge wa Bara tunapewa *resources* ambazo haziendani na uwiano wa majimbo yetu ukilinganisha na wenzetu wa upande wa pili, mbona hatujasema. Tunaamini kwamba, Mbunge ni Mbunge anatekeleza wajibu wake

kwa mujibu wa Katiba. Sasa nashangaa Wabunge wanaanza kusema kwamba, unajua hivi kila mmoja akisema unajua, tutakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, ningependa sana kushauri na ninasikitika sana na maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa na wenzangu, lakini viongozi ambao hawastahili kutamka. Kwa mujibu wa Katibu hii hapa, Waziri Mkuu ni Kiongozi Mkuu namba tatu. Rais anapokuwa hayupo, Makamu wa Rais anachukua madaraka, kama hayupo ina maana kwamba Waziri Mkuu atakaimu Urais wa nchi hii, akikaimu Urais wa nchi hii maana yake ni kwamba mpaka Zanzibar atakuwa anakaimu, hakaimu huku Bara peke yake. Sasa ninaomba jamani Watanzania tufike mahali tusianze kuwayumbisha viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, kingine hebu tuangalie, Watanzania sote ni ndugu; hivi toka lini Mtanzania wa Pemba au Msukuma ukawatofautisha? Sasa hivi ukitembea hapa Tanzania si Wapemba wamezagaa Tanzania nzima, si Wa Unguja wamezaa na kuzaliana na kuzaana mahali popote pale. Si Wasukuma ukienda kule Zanzibar unawakuta, ukienda Pemba unawakuta. Leo Watanzania tunaanza chuki ya kusema wewe unajua unakula zaidi kuliko mimi, unajua wewe; hii dhambi alisema Mwalimu Nyerere kwamba, tukianza namna kunyosheana vidole hatutafika tunakokwenda. Naomba Watanzania wenzangu tuache mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kusema hili, kitu ambacho nakiona hapa tusipoangalia kwa mujibu wa Katiba hii, mtu anayesema kwamba kuna nchi ndani ya nchi, yeye ni muasi kwa mujibu wa Katiba hii. Mtu anayesema kwamba, kuna nchi ndani ya nchi ni muasi. Sasa mtu wa namna hiyo tumshughulikie. Wanaosema namna hii watoke kwanza wao, sisi Muungano tunautaka, watupishe tuendelee nao. Hakuna sababu yoyote ya msingi leo hii Watanzania tuanze kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nina kumbukumbu hapa ambayo ni *Government Gazette* ya tarehe 26 Aprili, ikizungumzia *Article of Union* na jinsi ambavyo Bunge la kwanza la tarehe 22 mpaka 25 Mei, 1964 liliridhia kuwepo na Muungano. Leo tunaanza kuzungumza suala la Muungano, Zanzibar nchi si nchi; kitu gani Waziri Mkuu hana mamlaka huku? Hivi kweli katika Katiba hii ni wapi Waziri Kiongozi ameelezwa kwamba atakuwa ni Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Katiba ya Zanzibar inatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa mmesema namna gani jamani? Naomba viongozi wenzangu na Waheshimiwa Wabunge, katika hili tusiwapotoshe Watanzania. Ninaamini Muungano huu kama sisi viongozi tumechoka, basi tuwaulize wananchi kama wanautaka Muungano au hawautaki. Hii ndiyo njia pekee ya kuweza kuridhia Muungano huu.

Kwa sababu Wabara tutasema ohoo; unajua tunawa-*finance* sana Wazanzibari, kila kitu wanategemea huku na sisi tuanze kudai ya kwetu. Mwaka 1994 kulikuwa na hoja ya G55, mambo ya Tanganyika. Tukasema hivi haina tija kwa Watanzania? Masuala ya kusema Serikali mbili, tuvunje tuwe na Serikali tatu, sasa Tanganyika atafufuka wapi, wengine hatukumwona huyu Tanganyika? Tutamfufua kwenye kaburi lipi? Mimi nafikiri katika hili, aidha, kama kweli tumechoka ninaomba tuwaulize

wananchi wao waamue wanataka Muungano au hawautaki. Muungano wa Serikali moja au wa Serikali mbili uendelee. Katika msingi wowote, Watanzania leo hii watapenda kuona Muungano huu tunauendeleza.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho mimi ningependa kusisitiza ni kuhusu kauli za viongozi. Unajua mambo unapoyaachia kidogo yanazungumzwa, yanakeleketa, lakini tunahitaji tusikie kauli. Wenzetu wa Zanzibar walitoa tamko wakimwambia mwenzetu hapa aombe radhi, limetoka kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nilitegemea kwamba, kauli kama hiyo si ya kuibeza, nina maana kwamba kulikuwa na makusudio ya kusema vile.

Sasa kama ndiyo hivyo, basi tunaomba Viongozi Wakuu watoe tamko, watuambie jamani kinachosemwa ndiyo hicho, kwa sababu haiwezekani kuendelea kufukuta maneno namna hii.

Mheshimiwa Spika, ulitumia busara zako wakati ule ukasema mjadala huu tuuahirishe lakini leo umesema kabisa kwamba, hapana tuuzungumze. Watanzania nadhani ni vyema tufikie mahali, hili suala tujaribu kujiepusha. Leo hii ukirudi huku, kwa mfano, tuna mambo ambayo tumeungana sisi Watanzania, lakini kuna mambo ambayo yanakwenda nje ya Muungano; kwa mfano, kuna Mawaziri ambao wanashika Wizara zisizokuwa hata za Muungano, hakuna wa Bara anayelalamika hata kidogo. Kuna Watanzania wangapi wa kutoka visiwani waliopo huku Bara wanafanya kazi, hakuna aliyelalamika hata kidogo.

Kwa nini sasa tunaanza hii chokochoko; kuna nini; kama kuna viongozi wamechoka basi ni bora watupishe? Mimi nasema Muungano wetu tuendelee nao, hatuna sababu yoyote ya msingi ya kumwogopa mtu. Ufike wakati sasa tuanze kuambizana ukweli. Haya mambo ya longolongo tuachane nayo. Mtu akiweza kushika kama ni moto aungue, Jumbe aliwajibishwa hapa Dodoma kwa sababu ya mambo haya haya; tunaona ni madogo lakini ni makubwa. Kama kuna viongozi ambao wanadiriki kuubeza Muungano huu, lazima wachukuliwe hatua za msingi ndani ya Chama cha Mapinduzi. Nasema kama kuna viongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi, lazima tuwawajibishe. Hatuwezi kuangalia hali ya namna hii. Sera ya CCM ni ya Serikali mbili. CCM inasema sera yake ina Serikali mbili hatujaibadilisha sera hiyo. Mnaotaka kufufua Tanganyika hiyo, basi muitafute nyingine. Naomba katika hili, Watanzania wenzangu mnisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine katika hili ni kuhusu gharama za uendeshaji. Mimi naamini Watanzania kama wakiweza kuridhia aina ya Muungano tunaoutaka, tujaribu kuwa nao sasa hivi tuangalie kumekuwa na kero za aina gani, tukae chini na viongozi mtumie hekima na busara mlete tuweze kufikia maamuzi ambayo yana tija kwa taifa hili. Hatuna sababu ya kutwisha wananchi mzigo mkubwa sana. Leo hii ukiangalia Watanzania kila kukicha tunalalamika maisha magumu, hivi tutalalamika mpaka lini?

Sasa ninawaambia ndugu zangu wa upande wa visiwani, *Wallahi* kama leo hii tunaamua kutengana kesho kutwa itakuwa kama Comoro au Biafra. Hamuwezi ku-*survive* kila mmoja anamuhitaji mwenzake; wa Bara tunawahitaji Wazanzibari,

Wazanzibari wanahitaji wa Bara. Hatuwezi kuacha hivi sasa, twende kwenye shirikisho la Afrika Mashariki tukiwa kama nchi moja ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Watanzania wengi wameoa na kuolewa Zanzibar na Bara. Hawa wamedumisha Muungano na ndiyo raha ya Muungano. Leo miaka 44 tunasema eti tunafikiria kuchokana; kuchokana kwa lipi wakati sisi wote ni damu moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi napenda nirejee kwamba, jambani katika nchi za Maziwa Makuu, tunahitaji amani zaidi, tusichezee amani. Watanzania wenzangu nawaambia na narejea tena, kama kuna watu wanadhani kwamba, kupitia chokochoko hii wanaweza kuruvuga amani ya Watanzania ni bora Watanzania tukasimama imara zaidi. Bunge kama hili ni vyema tukakaa imara. Sisi sote hapa inashangaza kuona tunaweza kusema kwamba, unajua huyu hajui kusoma Katiba, huyu anajua kusoma Katiba, nchi inaongozwa kiujanja ujanja. Ujanja upi? Kama kuna tatizo basi useme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa hotuba nzuri. Bila kusita naunga mkono hoja.

Naomba kuchangia yafuatayo, kwanza ni kuhusu mazingira. Wilaya ya Lushoto ni ya milima, misitu na wakazi wengi, miti inakatwa lakini inayopandwa ni michache sana kutokana na wananchi kushindwa bei kubwa ya miche na viriba. Naishauri Serikali ikubali kusambaza miche na viriba bure au kwa bei nafuu ili wananchi wengi wapande miti kwa wingi kunusuru misitu na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano, katika kuimarisha Muungano ngazi ya Bunge na Baraza la Wawakilishi nashauri Katiba irekebishwe ili Wabunge toka Zanzibar na Wawakilishi wawe wale wale badala ya utaratibu wa sasa ambapo ni watu tofauti ukiacha wale watano wa sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Natron ni Ziwa la pekee hapa nchini, pamoja na kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na maziwa mengi yanayotuzunguka lakini Ziwa hili ni la kipekee lenye rasilimali ya kipekee kwa Afrika nzima.

Mheshimiwa Spika, Ziwa hili ni mazalia ya ndege wa aina ya *Heroe* wadogo *(lesser flamingos)* zaidi ya million nne. Ndege hawa wanazunguka Afrika nzima lakini lazima warudi pale Ziwa Natron kuzaliana. Ni bahati ya pekee ulimwenguni Mungu ametoa hapa kwetu Tanzania, rasilimali hii ni kivutio kikubwa kwa watalii hapa nchini ni utajiri mkubwa kwa maendeleo ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo hili lipo kwenye mkataba wa Ardhi Oevu *(Ramsar Site)* chini ya Shirika la *UNESCO.* Tangu Tanzania iingie mkataba huu hakuna utafiti wowote uliyofanywa kwenye eneo hili kujua *monitoring data base* za eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Idara ya wanyamapori ndiyo ilikuwa inajipanga kuweza kufanya utafiti huo ili kujua jiolojia, baiolojia na haidrolojia ya eneo. Pia taadhari ya mazingira haijafanyika kuona athari zinazoweza kutokea kutokana na uwekezaji unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo Serikali imeridhia uwekezaji wa kiwanda hiki bila kufanya yote niliyoyaeleza hapo juu. Mara nyingi hapa Bungeni katika majibu ya maswali mbalimbali Mawaziri wanaelewa wakitamka kwamba Serikali ina mpango/utaratibu wa kujenga *extension* ya reli kwenda *Lake Natron* kwa ajili ya kiwanda cha magadi!

Mheshimiwa Spika, hili linatishia uhai wa *resource* zilizopo eneo hili. Naomba kuiuliza Serikali swali. Hata kama kiwanda kitajengwa Mto wa Mbu au Arusha je, malighafi ya kiwanda itatoka wapi? Siyo ndani ya Ziwa hili? Barabara na reli hizo zinajengwa zitapita hewani?

Mheshimiwa Spika, neema hizi tulizozikuta zinatunzwa/zinalindwa na waliotutangulia ni muhimu tukazitunza kwa ajili ya watoto wetu/vizazi vijavyo siyo kuziharibu kwa tamaa za pesa kana kwamba hiki ni kizazi cha mwisho. Tunazo njia nyingine za kuongeza kipato chetu na siyo kuharibu maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, upo uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na watu/wawekezaji wa viwanda kutumia kuni na magogo katika kuendesha viwanda vyao badala ya kutumia umeme. Kuna kiwanda kilichopo Morogoro ambacho mwenye kiwanda kwa kukwepa kulipia umeme, Kiwanda chake kinaendeshwa kwa kutumia magogo/kuni, kwa siku moja kiwanda hiki kinatumia *minimum* tani 30 za magogo/kuni.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kufuatilia kiwanda hiki kinachomilikiwa na kiongozi mkubwa tu ambaye alitakiwa yeye ndiye aelimishe na kusaidia kuhifadhi mazingira. Pia ningependa mwenye kiwanda aonyeshe shamba la miti analokata magogo hayo na pia aonyeshe ni miche mingapi ya miti anapanda kila mwaka kwa matumizi ya hicho kiwanda. Kiwanda hiki kinatengeneza nguo na kipo eneo la Kihonda Magharibi.

Mheshimiwa Spika, vikundi vya mazingira Morogoro kikiwepo kikundi cha *Morogoro Environment Conservation Action Group (MECA)* wamekuwa wanalipigia

kelele lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.  Naomba Waziri atueleze ni hatua gani zimechukuliwa kwa kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo tatizo kubwa la juhudi za Serikali za kupambana na uharibufu wa mazingira kukwamishwa na wanasiasa.  Serikali inapotoa maagizo, watendaji wakiagiza kutekeleza maagizo hayo, wanasiasa wanaingilia juhudi hizo kwa kusema sisi ndiyo viongozi wenu hivyo asiwasumbue mtu.

Mheshimiwa Spika, mfano ni uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu wanaoishi kwenye milima ya Uluguru huko Morogoro.  Serikali imeshatoa agizo kuwa wananchi wanaoishi kule juu kwenye milima ambao wanafanya shughuli za kilimo na ukataji wa mkaa waondolewe.  Watendaji kwa maana ya maafisa misitu wa Wilaya na Kata walianza juhudi za kukaa na wananchi hao na kuwaelimisha na wengine walishaanza kuhama. Lakini wanasiasa walienda na kuwarejesha wananchi hao na kusema asiwaguse mtu.

Mheshimiwa Spika, hadi leo milima ya Uluguru kila leo inaunguzwa moto na hata hali ya hewa ya Uluguru sasa imebadilika na kuwa ya joto wakati ilikuwa ya baridi kwa mwaka mzima. Masuala ya utendaji yabaki kuwa ya utendaji na yasichukuliwe kisiasa. Wanasiasa watumie nafasi zao kujenga na sio kubomoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchomaji mkaa, uharibifu unaosababishwa na uchomaji wa mkaa umeongezeka kwa kasi kubwa sana baada ya hali ya maisha kupanda. Sijui kama Serikali imefanya tathmini ya suala hili/uharibifu huu lakini hali ndivyo ilivyo.  Mwaka 2006 mkaa gunia hapa Dodoma ilikuwa shilingi 5,000/= hadi shilingi 7,000/=.  Leo mwaka 2008 mkaa hapa Dodoma ni shilingi 10,000/= hadi shilingi 13,000/=.  Huko Dar es Salaam inasemekana gunia ni shilingi 28,000/= hadi shilingi 35,000/=.  Kutokana na gharama za nishati nyingine kama umeme, mafuta ya taa kupanda, wananchi wengi wanatumia mkaa.

Mheshimiwa Spika, kupunguzwa ushuru kwa mafuta mazito (Moto Poa) pamoja na gesi kwa kupikia hakujatoa matunda makubwa. Bila Serikali kuingilia kati bei za umeme zinazopanda kila leo na mafuta zinazopanda kila leo misitu yetu itateketea na juhudi za kupanda miti mingine ni ndogo sana.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulizaliwa mwaka 1964 na maraisi wawili ambao kwa sasa hawapo tena duniani, kwa vile nchi ambazo zimeungana kwa baadhi ya mambo tu, ingetegemewa kuwa vikao rasmi vilivyotambuliwa na Katiba na Sheria za nchi na wala sio sahihi kuwa na Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kuondoa kero za Muungano kwa kuwepo na sheria ambayo washiriki wawe na uwezo wa kuamua, kuongeza, kupunguza mambo ya Muungano na wakiwa na uwezo sawa na nguvu ya uamuzi.  Hakuna kikao kinachotambulika kisheria kinachozikutanisha pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, mambo ya Muungano kiutawala na kisera yanaamuliwa na Baraza la Mawaziri la Serikali ya Muungano, Zanzibar haiwakilishwi ndani ya Baraza

hilo, Rais wa Zanzibar anaingia kama mjumbe na sio kama upande mmoja wa chombo hicho ambacho kinaruhusiwa kutetea msimamo wa Zanzibar. Hivyo hawakilishi Zanzibar kwa vile ndani ya Baraza hilo yeye anawajibika kwa Rais na hata Mawaziri wa Zanzibar na wao wanawajibika vile vile kwa Rais wa Jamhuri, hivyo hawawezi kutetea Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, inapotokea Zanzibar kushirikishwa kama Zanzibar katika masuala ya Muungano ni kwa njia ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutakiwa kutoa maoni. Hivyo maoni hayo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao baadhi ya wakati huandaliwa na Baraza la Mapinduzi, mara nyingi hukataliwa na hata Mkurugenzi tu wa Serikali ya Muungano au Katibu Mkuu au Waziri.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mfano mashuhuri ni uanzishaji wa Benki Kuu mwaka 1965, marekebisho ya Benki Kuu mwaka 1995, uanzishaji wa Mamlaka ya Mapato na sera ya mambo ya nje. Ahsante.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Buriani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha ya mwaka 2008/2009, naona hotuba yao ni nzuri na imegusia maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni hasa kuhusu kwanza umuhimu wa mipango endelevu katika elimu juu ya utunzaji wa mazingira (usafi) hasa katika maeneo ya miji yetu, hasa katika kingo za barabara na mabega yake na umuhimu wa kuwashirikisha wenye nyumba zinazopakana na barabara au maeneo ya wazi.

Pili, ni suala la Muungano ni *delicate* na linastahili kuangaliwa kwa umakini. Ni vyema vipengele vyote vikapitiwa kwa uangalifu na kupata suluhisho la kudumu kwa pande zote. Ila naomba waulizwe wenzetu wa upinzani, wakati kikao cha *NEC*, CCM Butiama kilipoazimia suala la muafaka lirudishwe kwa wanachi wenzetu waliandamana *(CUF),*sasa wanasema suala la Muungano lirudishwe kwa wananchi. Je, ni wakati gani wananchi wanafaa au ni muhimu kutoa maoni yao? Ni pale wanayoridhia wao tu? Japo katika hilo pia sipingi.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wao hawazungumzii kifungu cha 64(1) wanazungumzia vifungu vya (ii) na kuendelea kwa nini? Pia naona kuna kuchanganya kati ya masuala ya Muungano na yasiyo. Basi labda ni vyema kupitia upya ili kuona mapungufu yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kutuongoza vizuri katika Kambi yetu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba yao nzuri pamoja na wale wote walioshirikiana katika kuiandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mazingira ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu na viumbe hai. Katika kuonyesha kuwa mazingira ndio shina katika shughuli za binadamu kwa uhifadhi wake ni muhimu kama vile maji na mazingira, ardhi, misitu na mazingira, hewa na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umaskini wa wananchi wetu hasa vijijini unachangia uharibifu wa vyanzo vya maji kwa wakulima kukata miti kwa kuchoma mkaa na kuni na kuchoma misitu kwa wakulima, wapo wafugaji huchoma moto kwa ajili ya kuota majani mapya ili walishe mifugo yao. Kwa uharibifu huo unachangia kuleta njaa na kuleta ukame na kukauka kwa maji hali inayoleta shida kwa wafugaji kuhangaika kwenda masafa marefu kutafuta maji kwa ajili ya mifugo yao na wanawake pia kuwa ni mzigo kwao kufuata huduma hiyo masafa marefu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itilie mkazo sheria iliyopo ili wanaokwenda kinyume wachukuliwe hatua ili ikomeshwe hujuma hii. Naipongeza Serikali kwa kuweka siku ya Kitaifa ya kupanda miti, huu ni mfano kwa Serikali yetu kuwa inatilia mkazo kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, Muungano kama tunavyojua kuwa Muungano ni kuungana kwa nchi mbili, Zanzibar na Tanganyika ndio tukapata Jamhuri ya Muungano na jina lake tukapata Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuungana ni jambo zuri sana na linaleta upendo, kukaa pamoja na kupanga mipango yetu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mambo ya Muungano ni 22 hili ni tatizo kwa sababu waliokubaliana ilikuwa ni mambo 11 tu haya mengine ndio yanayoleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Rais wake asiwe Makamu wa Rais kwa sababu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano ametoka Bara kwa maana ya Baba wa Taifa na Makamu angetoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (kama Rais) kama mama? Hiyo inamfanya kuwa Rais wa Zanzibar akija Bara ni sawa na Waziri asiyekuwa na Wizara?

Mheshimiwa Spika, tunaomba mambo yanayoleta kero yashughulikiwe ili tuweze kuudumisha Muungano wetu, tusilete migogoro ili vizazi vyetu waweze kuishi vizuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi inayochimbwa Tanzania Bara inajulikana kuwa ni suala la Muungano.

Je, Zanzibar inafaidika nini kutokea kuchimbwa gesi hiyo na matumizi yake? Naomba Waziri anijibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, nawaombea kheri wote Mawaziri wawili na nawaombea na afya njema.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote nichukue fursa kumpongeza Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa hotuba yake nzuri kuhusu Wizara inayoshughulikia masuala ya Muungano na Wizara inayoshughulikia masuala ya mazingira.

Napenda pia nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kutayarisha hotuba ya masuala ya mazingira kisayansi na kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, napenda pia niwapongeze kwa dhati Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, wakuu wa idara, watendaji wengine wa Ofisi ya Makamu wa Rais na mashirika mbalimbali yanayofanya kazi kwa ushirikiano na ofisi hii kwa kazi yao kubwa katika kuboresha mazingira na mshikamano katika Muungano wa Jamhuri yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la utunzaji wa mazingira na mustakabali wa uhai wa viumbe ikiwemo mimea na wanyama mbalimbali wakiwemo binadamu ni la kufa na kupona. Sisi wenyewe katika muda wa uhai wetu tumekwishashuhudia mabadiliko mbalimbali ya hali ya nchi katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu kwa mfano kukauka kwa vijito vilivyokuwa vinatiririsha maji kwa mwaka mzima katika maeneo mbalimbali ukiwemo Mji wa Mbeya, kutoweka kwa misitu na miti ya asili katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa na Kati wa nchi hii na hivyo kusababisha hali inayoashiria ujio wa jangwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhakikisha hali hii haiendelei kutokea kwa kufanya tafiti mbalimbali na kuanzisha mipango ya hifadhi za mazingira katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa katika vijiji vichache vya Bonde la Ufa la Rukwa, Wilayani Mbozi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kushirikiana na *NEMC* na wadau wengine itoe kipaumbele maalum ili kuepusha hali ya uharibifu wa mazingira ambayo inaashiria kutokea jangwa kwenye eneo la Bonde la Ufa la Rukwa linalojumuisha vyanzo na kwenye maeneo inayopitia mito Mpemba, Muko, Nkana na Momba katika kata za Chiwezi, Ndalambo, Kapela, Myunga, Msangano, Chitete, Chilulumo, Ivuna na Kamsamba, jimboni Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa za eneo hili kukumbwa na hali hii ni ujio wa wafugaji na makundi makubwa ya mifugo kutoka mikoa ya Ziwa na Bonde la Ihefu katika miaka ya hivi karibuni ambao wamesababisha *overgrazing* na ukataji mkubwa wa miti ya asili.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye vyanzo vya mto Nkana pale *Mbozi Mission* na Mjini Vwawa (eneo la Ichenjezya) kunatokea ujenzi wa nyumba na upandaji wa mianzi ambao umesababisha chemchemi hizo kukauka na kusababisha ukame mkubwa kwenye maeneo ya Bonde la Ufa katika Kata za Chiwezi, Msangano, Chitete, Chilulumo na Kamsamba. Mbali na hilo wakulima wa eneo hilo vyanzo vya mto huo vinasababisha madhara makubwa kiafya kwa wananchi wa bondeni kwa kulima mazao kama nyanya na mahindi kwa kutumia mbolea za viwandani zenye kusababisha magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ombi la wananchi wa Mbozi Magharibi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ni kupanua harakati za hifadhi ya mazingira hadi kwenye bonde la ufa la *Msangano Trough.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizipongeze juhusu za Ofisi ya Makamu wa Rais, masuala ya Muungano kwa kufanya kazi bila kuchoka katika kuhakikisha Muungano wetu unaimarika siku hadi siku. Ni imani yangu na wananchi wa Mbozi Magharibi kwa jumla, kuwa Muungano wetu utaendelea kuwa mfano bora katika Afrika na dunia nzima. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, pamoja na watendaji wote wa ofisi yake kwa kazi wanazozifanya katika kupunguza kero za Muungano na kuhakikisha kuwa Muungano wetu unadumu. Nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, kwa kazi nzuri ya kulinda na uboreshaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ndiyo yenye jukumu la kuishauri Serikali kuhusu masuala ya mazingira. Naiomba Ofisi hii kuishauri Serikali ipasavyo kuhusu ujenzi wa kiwanda cha uvunaji magadi kinachotarajiwa kujengwa eneo la Ziwa Natron na Shirika la *TATA Chemicals* la India.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Natron ni ziwa lenye maji yenye magadi na maji yake ni ya kipekee Afrika. Ndege aina ya *Lesser Flamingo* kutoka sehemu mbalimbali Afrika hutaga mayai na kuzaliana katika ziwa hili. Ndege huyo huzaa mara moja tu kwa muda wa miaka mitano hivyo kufanya ziwa hili la Natron kuwa na historia ya kipekee sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kujua je, utafiti umefanyika vya kutosha na hasa katika kuwashirikisha wataalamu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kujua kama ujenzi wa kiwanda hicho kitaathiri kuzaliana kwa ndege hao? Mimi ni mwana mazingira na ni mmoja kati ya wanaofuatilia sana uhai wa ndege hao aina ya *Lesser Flamingo.* Kwani ni lazima kiwanda hicho kujengwa karibu na Ziwa Natron? Mbona Tanzania hii kuna maeneo mengi?

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu sasa una umri mkubwa sana kiasi kwamba tunatakiwa kupiga hatua sasa na hatua tunayotakiwa kupiga ni kuwa na Serikali moja. Tutakapokuwa na Serikali moja makelele ya wananchi wa Zanzibar kuonewa yatakwisha. Hawaonewi na hawamtaji anayewaonea, bora Serikali iwe moja.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza na kumaliza kabisa malalamiko ya Muungano ni Serikali moja kwa sababu Zanzibar idadi ya watu ni ndogo sana haifiki hata milioni. Je, kuna haja kweli ya kuendelea kuwa na Serikali mbili? Tuonyeshe mfano kwa nchi zingine za Afrika kwa kuwa na Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Muungano na wa Mazingira, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutuletea hotuba nzuri inayoleta matumaini kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano na pia upande wa kutunza mazingira endelevu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza ni kuhusu kero za Muungano. Serikali ifanye makongamano ya kuwaelimisha wananchi hasa wale wa Pemba. Si sahihi hata kidogo kwamba mpinzani au mwananchi wa Pemba kila akisimama Bungeni kazi yake ni kukejeli Muungano na misingi yake. Muungano ni uhai wetu. Bila Muungano ni hasara kubwa pande zote za Muungano. Tutakuwa hatuna usalama wala mustakabali wa Taifa. Waarabu waliopinduliwa Zanzibar wanataka kurudi kwa kupitia mlango wa nyuma wa kibaraka wao.

Mheshimiwa Spika, tuwaelimishe Wapemba kuwa Muungano ni maisha yetu na iwe marufuku kuukejeli Muungano wetu. Jambo hili sasa litungiwe sheria kwamba ni jambo la uhaini kuukejeli Muungano na adhabu zake ziaInishwe. Bado nakubali turekebishe kasoro zilizopo kwa mazungumzo *(positive discussions)* sio kuonekana kana kwamba waasisi wetu wazee Sheikh Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hawakufanya jambo kubwa kwetu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu mazingira yetu. Mazingira na utunzaji wa mazingira ni maisha yetu. Mheshimiwa Waziri napenda kukutia hamasa kubwa kwa minajili ya kukutia moyo kwa kazi kubwa iliyo mbele yako.

Kuhusu elimu, naomba Serikali ifanye programu ya kusomesha umuhimu wa mazingira katika nchi yetu na dunia nzima. Kuwe na *syllabus* juu ya mazingira tangu shule za msingi hadi Chuo Kikuu na mazingira liwe somo la lazima kwa kila mwanafunzi. Pia kuajiriwe maafisa mazingira wa kila halmashauri, kila ofisi ya Serikali katika nchi yetu. Kuwe na *guideline* inayowafanya maafisa hao wawe wanazungumza lugha moja. Waweze kufanya *Environmental Audit* nchi nzima na kuwe na ufuatiliaji wa karibu wa *trends.* Je, mazingira ya nchi yetu yanaharibika zaidi na kwa kiasi gani? Ama

mazingira yanaendelea vipi *positive* au *negatively* kuwepo na msisitizo wa kisheria na kwa kutoa adhabu kali kwa maana *(potuter pays)* kwa wakosaji wote.

Kuhusu kuhama hama kwa wafugaji wetu kunahitaji udhibiti mkubwa. Sheria itungwe kuweka ukomo wa wanyama (ng'ombe) kwa kila mfugaji. Kuhama hama kupigwe marufuku kabisa. Tusije tukaongeza ukubwa na jangwa kama ilivyotokea Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu Rufiji, Mheshimiwa Waziri misitu ya asili imekatwa na hasa kufyekwa kwa ajili ya kupata magogo. Nakuomba ufanywe utafiti kwa maana ya kupanga utaratibu wa *Afforestation* ya sehemu tupu iliyofyekwa ipate kupandwa miti kule Rufiji.

Mheshimiwa Spika, Bajeti finyu. Naomba Serikali kuu iongeze Bajeti ya Wizara hii ya Mazingira kwa sababu shughuli nilizoainishwa hapo juu zinahitaji matumizi ya fedha nyingi. Kwa kuwa mazingira ni uhai wetu basi Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii zaidi ya mara nne.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja. Namuomba Mheshimiwa Waziri azingatie hoja ya tatu. Ahsante sana.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Nawapongeza Mawaziri hawa pamoja na wataalam wao kwa hotuba hizi na kuwa hata matumaini ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua zinazochukuliwa kwa kuhifadhi mazingira na juhudi kubwa za uhamasishaji wa mazingira, bado kuna tatizo kubwa la wananchi wenyewe katika kuweka mazingira yao ya kila siku kuwa katika hali safi. Mfano katika Jiji la Dar es Salaam vyoo vinatiririka maji taka mitaani au kuchimba shimo dogo nyuma ya nyumba kutiririsha majina linakuwa wazi, ni vizuri uhamasishaji wa kupanda miti kwenye majangwa na kulinda vyanzo vya maji uende sambamba na uhamasishaji wa mazingira jamii katika maeneo ya wanayoishi wananchi.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya mazingira endelevu ni muhimu sana, mfano kumekuwa na uharibifu wa fukwe za Bahari ya Hindi ambao umekuwa ukiendelea katika baadhi ya maeneo, bahari inakula ardhi ya nchi kavu kwa kasi, pia ujenzi usiozingatia utaratibu wa sheria zilizopo na kuharibu mazingira, jambo lingine ni viwanda vikubwa na vidogo kutupa ovyo taka za sumu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi imeingia katika malumbano ya Muungano na kwa muda mrefu, baadhi ya wananchi wanadai kuwa Muungano una kero na suala hili limepelekea kuwa gumzo nchini ni vyema basi jambo hili liwekwe bayana na hizo kero kama zipo zitatuliwe ili kuondoa joto hili ambalo linaitikisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, pongezi, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kuandaa na kuwasilisha Bajeti yao.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha pesa za Bajeti, napendekeza kwa Bajeti zijazo Serikali iitengee Wizara hii Bajeti ya kutosha hasa sekta ya mazingira tofauti na sasa ambapo Bajeti ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nishati mbadala ya kuni, pamoja na jitihada zinazofanywa tayari, kasi iongezwe ili kuwezesha na kushawishi ili Watanzania tutumie nishati mbadala ya kuni. Tuweze kutumia gesi ambayo tunayo, hasa mijini kwa kuanzia. Hii itasiaidia kulinda misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Muungano na pia Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, Waziri wa Mazingira, Katibu Mkuu, Lucy Mollel na watalaam wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa maandalizi na hatimaye kuiwasilisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie na Mazingira, moja ya uzalishaji wa vitu mbalimbali hususan vile vilivyotokana na kilimo basi ni kutokana na kuboresha mazingira. Kwa hivi sasa sura halisi ya nchi yetu iliyoshamiri misitu na chemichemi za maji kwa sehemu mbalimbali hivi sasa nuru inatoweka kutokana na hali ya uharibifu wa mazingira. Mazingira yanaharibiwa kutokana na ukataji miti hovyo na wanyama wafugwao hususan ng’ombe na kadhalika kutumia ardhi kwa malisho kiholela.

Mheshimiwa Spika, kwa suala kama hili Wizara lazima ifanye kazi na Wizara nyingine ikiwa ni hatua ya kukuza uhai wa mazingira yetu ili kuwa na uhakika wa mvua ya kutosha itakayotunza maji na baadae kusaidia kwa kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mlima Sekenke sasa ni eneo tengefu kwa msitu ambalo naamini kwa kiwango kikubwa likiboreshwa litasaidia uboreshaji wa mazingira. Naomba Waziri awasaidie wananchi kwa kuwapatia mtaalam ili kuwapa elimu wananchi hao waweze kushiriki katika kutunza mazingira ya Mlima Sekenke ili hali ya kiuchumi ya wananchi yakue katika maeneo hayo.

Pia Waziri atembelee Ziwa Kitangiri kwa kuwa hali ya Ziwa inaendelea kuwa tope kutokana na kuchafuliwa kwa mazingira juhudi zinahitajika za kitaalam kuokoa Ziwa hilo (Kitangiri) ambalo ni nguzo ya kiuchumi kwa wananchi wa Doromani, Kidaru, Tulya na Ntwake.

Kuhusu Muungano, Wizara ione umuhimu kuainisha yale yote yanayoonekana kulalamikiwa na wananchi kuhusu Muungano. Wananchi walio wengi waelimishwe vya kutosha juu ya Muungano kwa kuwa walio wengi hawauelewi.

**MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza sana Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa uwasilishaji hotuba zao za Bajeti uliokuwa makini na uliojikita katika maeneo muhimu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, leo nitachangia kidogo kuhusu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kabla sijaanza kuchangia nianze na ku-*declare interest* kwamba mimi ni mfanyakazi wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama Afisa Utumishi ambae nipo likizo bila malipo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalolikabili Baraza la Mazingira ni Bajeti ndogo inayofanya ishindwe kutimiza majukumu yake ipasavyo. Baraza hili linawajibika kwa Taifa zima linatakiwa kufanya kazi na sekta zingine ikiwa ni pamoja na halmashauri za Wilaya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, matatizo muhimu ambayo yanahitaji kutafutiwa ufumbuzi ni Baraza halina jengo la ofisi ambayo ni muhimu sana kwa majukumu ya Baraza, ukosefu wa nyenzo za kazi kiasi cha kushindwa kuyafikia maeneo mengi nchini kwa mfano Ziwa Natron, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa na kadhalika. Pia watumishi wa Baraza ni wachache sana kulingana na ikama na mahitaji yao na zimeanzishwa *zone* mbalimbali za utekelezaji wa kazi ambazo bado ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo niliyoyataja ufumbuzi wake ni kuongeza Bajeti ya Baraza, hivyo namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian ambaye ni mtu mahiri na ni chapakazi asaidie ili Bajeti ijayo Baraza lipate fedha zaidi lakini wakati tukitarajia Bajeti ijayo namuomba Waziri aendelee kutafuta vyanzo vingine kwa ajili ya kuisaidia *NEMC* ili iweze kutekeleza vyema sheria ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mola kwa kuniwezesha kuamka nikiwa mzima nasema *Allhamdullillah.* Pia nimpongeze Mheshimwa Waziri kwa hotuba yake yenye nia njema kwa Watanzania pia umahiri wake wakati akiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba nitoe mchango wangu katika hotuba husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali ya umuhimu wa mazingira ni vyema Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kutekeleza mkakati wa kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji nchini, pia ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, misitu ni chanzo cha mvua na pia kuiweka ardhi katika hali ya unyevu. Kinachoendelea sasa katika misitu yetu ni watu kuivamia misitu hiyo kwa njia ya kufanyia mkaa na wengine kuitia moto kwa njia ya uwindaji haramu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaokata miti kwa kutoa mkaa ni vyema Serikali ingejizatiti kufanikisha nishati mbadala kama vile umeme, gesi asilia pia makaa ya mawe. Je, Serikali itakamilisha lini utafiti wake juu ya mkaa wa mawe? Azma hii itapelekea kunusuru misitu yetu pia ikamsaidia Mtanzania aepukane na gharama kubwa ya matumizi, tukijua hali ya watu wetu kiumasikini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bonde la Ziwa Tanganyika. Maumbile ya bonde hili lina sura ya mtazamo wa eneo la ushirika kati ya nchi na nchi. Miundombinu ya bonde lile kwa upande wetu Tanzania ni mibovu. Je, kuna mpango gani wa Serikali kuweka barabara za kileo katika maeneo ya kwenda katika bonde la Ziwa Tanganyika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, mara nyingi uchafuzi wa mazingira husababishwa na viwanda jambo ambalo huhatarisha usalama wa raia. Je, Serikali imechukua hatua gani katika maeneo ya viwanda kunusuru afya za watu na mipango miji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo nasema ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mawaziri wote kwa hotuba nzuri ambayo imezingatia hali halisi ya mazingira tuliyonayo. Aidha, napenda kuwapongeza watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu maeneo yafuatayo, kwanza ni *Ramsar Sites.* Nchi yetu ni moja ya nchi duniani ambazo ziliridhia mkataba wa *Ramsar* ambao uliainisha maeneo yenye ardhi oevu. Katika wilaya yangu ya Kilombero kama ilivyo katika Bonde la Ihefu, Bonde la Mto Kilombero kwa maana ya wilaya ya Ulanga na Kilombero ni maeneo yaliyotambulika kama *Ramsar Site.*

Mheshimiwa Spika, katika waraka wa Mheshimiwa Makamu wa Rais alioutoa mwezi Januari, 2006 aliainisha hatua za kuchukuliwa katika kuhifadhi mazingira katika wilaya yangu ili kukidhi vigezo vya *Ramsar Sites.* Mpaka hivi leo waraka huo haujatekelezwa ipasavyo na kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi hasa kuhusu matumizi bora ya ardhi. Naomba kupitia Wizara hii waraka ule upitiwe upya kwa kuwa wananchi waliosambaziwa na kuelewa.

Kuhusu Muungano wa Tanganyika na Unguja, Muungano wetu una umri wa takribani miaka 44. Katika muda wote huu, Tanzania imekuwa ni nchi ya amani, kama waasisi wetu wa Muungano walivyotuasa. Leo hii yamekuja mawazo mapya baina ya watu ambayo kama hatutakuwa waangalifu, amani yetu itatoweka. Msingi mkubwa wa mmomonyoko huu nionavyo mimi ni uchu wa madaraka uliopo miongoni mwa nafsi za watu hao.

Napendekeza kama vile hatua zilivyochukuliwa huko nyuma kwa wote waliotaka kuleta chokochoko za kuua Muungano kinyume cha matakwa ya wengi. Hatua za kinidhamu zichukuliwe. Pia napendekeza ziainishwe kero zote za Muungano kwa uwazi ili hatimaye pande zote mbili za Muungano ziweze kuzishughulikia pia kwa uwazi, ikizingatia pia mawazo ya wananchi. Kwa hali ilivyo sasa hivi kutokana na mjadala uliopo wa Zanzibar kuwa au kutokuwa nchi, pamejitokeza mawazo ambayo lengo lake linaonekana dhahiri ni kuvunja Muungano. Wizara hii upande wa Muungano, isiruhusu kabisa watu wachache hao. Badala yake msimamo wetu uwe kulenga kuwa na Serikali moja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais Muungano na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri wanayofanya kwa faida ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema wazi kwamba ni jukumu la kila Mtanzania kuulinda Muungano wetu ambao ulianzishwa kwa faida yetu Watanzania wote kuanzishwa kwa Muungano huu uliwekwa bayana na ukaingizwa kwenye Katiba yetu ambayo inaeleza wazi kwamba Muungano wetu utakuwa wa Serikali mbili yaani Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar na ulianzishwa baada ya kuzivunjwa Serikali za Tanganyika na Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wanaopinga Muungano ni watu wachache na wanafanya hivi kwa maslahi yao binafsi au ya kikundi. Wakati tunaingia kwenye Muungano kulikuwa na makubaliano kwamba Bara na Visiwani tumeunda nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na hayo maana yake Serikali zote za zamani zitavunjwa na kutengeneza Serikali moja. Kwa hiyo, sasa hivi tunayo nchi moja tu ya Tanzania hakuna Tanganyika wala Zanzibar linalotakiwa ni wanasheria wetu kuwaelimisha hawa wanaojidai hawafamu na kudai kwamba Zanzibar ni nchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira namuomba sana Waziri pamoja na kazi nzuri anayofanya bado kuna matatizo makubwa ya miradi mikubwa hasa ya hoteli za kitalii kujengwa kwenye vyanzo vya maji, kwenye njia za wanyamapori au kwenye sehemu ambazo wanyama nyeti kama simba huishi na kuzaliana.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, Serikali isikubali kujenga Kiwanda cha Magadi Ziwa Natron kwa sababu kwa kweli tutakuwa tumeingilia maeneo ambayo ndege aina ya flamingo huzaliana. Hii isije ikatokea kwa maziwa mengine ya Manyara na Eyasi.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati idara ya mazingira ijitume na kufika hadi mikoani na wilayani. Kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira bado unaendelea huko, inakuwa vigumu kusimamia kutokana na kutokuwa na uwakilishi huko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA**: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wahemishiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib (Muungano) na Mheshimiwa Dr. Batilda S. Buriani (Mazingira), pamoja na watendaji wakuu na wasaidizi wao kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la hifadhi ya mazingira, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada kubwa za ufuatiliaji na mafanikio makubwa nchini. Pamoja na pongezi hizo, naiomba Serikali iteue timu ya wataalam washauri waliobobea katika masuala ya *river training* na mafuriko ili wakafanye utafiti wa kina kuhusu kuongezeka kwa mafuriko makubwa ya mto Mkondoa yanayojirudia na kusababisha uharibifu mkubwa wa nyumba, mashamba, madaraja na miundombinu katika mji wa Kilosa na vijiji jirani.

Mheshimiwa Spika, mto Mkondoa ni mto korofi sana na usiotabirika kila msimu wa mvua na ndio ulioliboma daraja la mto huo na kusababisha ajali kubwa ya treni ya abiria kutumbukia katika mto huo miaka zaidi ya saba iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mafuriko haribifu, inasadikiwa ni kutokana na *deposit* kubwa sana ya mchanga kwa kuwa eneo lote la Kilosa ni *low flat plain* kipindi uharibifu wa mazingira ulipokithiri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio makubwa ya hifadhi ya mazingira mto Mkondoa umeongeza kwa kiasi kikubwa *volume* na *flow rate* ya maji ambayo kila msimu wa mvua unapasua kingo za mto katika maeneo mbalimbali na kusababisha madhara makubwa ambayo hufikia kutenganisha wananchi wa baadhi ya kata na hata kuwazuia wanafunzi na walimu wa upande mmoja kushindwa kwenda shule upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo, namuomba Mheshimiwa Waziri awatume wataalam Kilosa kutafiti hali niliyoieleza ili kuepusha madhara ya muda mrefu kwa kutafuta ufumbuzi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri atoe kauli, wakati akijumuisha hoja za Wabunge, kuhusu kulikubali ombi langu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu Muungano baina ya Zanzibar na Tanganyika, ninasikitishwa sana na dhamira mbaya inayoonyeshwa na baadhi ya wananchi wa Tanzania wenye asili ya Zanzibar inayodhoofisha juhudi endelevu za kuimarisha Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha zaidi ni kuona kuwa hata baadhi ya Wabunge wanaotoka Zanzibar, wakiwa ni wawakilishi wa wananchi wao, wanadiriki kuchochea hisia kwa wananchi wao kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano inawaonea na inawakandamiza. Dhana hii ni potofu na haina ukweli.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa mazingira mbalimbali kidunia ya wakati ule Muungano ulipoundwa ni tofauti na wakati tulionao sasa, ikiwa ni pamoja na upeo wa elimu, uwezo wa uchambuzi wa mambo pamoja na idadi ya walioelimika kuweza kuchambua mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hali hii ndio iliyoibua kero za Muungano zilizotamkwa kwa nyakati tofauti. Viongozi wa juu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari wanaendelea kuzitafutia ufumbuzi wa kero mbalimbali za Muungano kwa sababu hiyo sisi Wabunge wote tungeungana kuwaomba viongozi wetu wa Serikali kuharakisha kasi ya kujadiliana na kupata ufumbuzi muafaka wa kero zote za Muungano, ili umoja wetu uimarike.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi wakati mwingine napata hisia, kutokana na matamshi ya baadhi ya Wabunge, kuwa labda wananchi wa Zanzibar walio wengi hawapendi Muungano uendelee!

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri alielimishe Bunge lako Tukufu, hivi kweli kwa bahati mbaya sana Muungano ukivunjika ni upande upi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakayoathirika zaidi? Na ni hatari zipi zinaweza kuibuka ku-*destabilize* ujirani mwema na ndugu tuliokuwa nao hadi leo.

Mheshimiwa Spika, namuomba pia Mheshimiwa Waziri, atuelimishe ni kwa vigezo gani na sababu zipi zilizosababisha idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar waliomo Bungeni kutozingatia *proportionality* ya ukubwa wa maeneo na idadi ya watu, kama ilivyo Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Muungano, baada ya kufikia muafaka wa kuondoa kero za Muungano, naishauri Serikali hatua za makusudi, zichukuliwe kuendeleza *propaganda* zenye lengo mahsusi la kuwaelimisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano, historia na faida kubwa za Muungano. Hatua za aina hii zitarithisha imani na udugu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa nguvu zote na kuwaomba Wabunge wote tutambue umuhimu usioepukika wa kuulinda na kuudumisha Muungano wetu kwa gharama zozote, la sivyo tutakuja juta.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Nchi, Muungano na Waziri wa Nchi, Mazingira kwa kushirikiana na watendaji wote wa Wizara hizo kwa kazi kubwa tena ngumu wanazofanya. Pamoja na pongezi hizo nina maoni yafuatayo, kwanza ni kuhusu upandaji wa miti. Kwa kuwa kumekuwa na hali ya kutosimamia vizuri zoezi la upandaji wa miti ingawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa agizo mwaka 2006 la kupanda miti kwa wingi na alitumia lugha ya tupande miti kama wendawazimu, lakini agizo hili halionekani kuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, ingefaa kuwe na mfumo mzuri utakaosimamia upandaji wa miti kwa kuzingatia ubora wa miche ya miti, umri (urefu wa mita mbili) ndio utumike

kupanda kuliko ilivyo hivi sasa miti hupandwa bila kuzingatia umri na ubora wa miche, hali ambayo husababisha miche kutokuwa kwa kukosa maji, mbolea na usimamizi wa karibu. Hali ya kutosimamia kwa karibu upandaji wa miti na ukuaji wake unasababishia Serikali kutenga fedha kila mwaka ambazo hazileti tija. Serikali iwe na kitengo maalum kitakachosimamia upandaji wa miche na maua na usimamiaji wa ukuaji wake.

Pili ni kuhusu uchafuzi wa mazingira. Kumekuwa na udhaifu wa kutosimamia vizuri uchafuzi wa mazingira katika mabonde na mito yote iliyoko katika mkoa wa Dar es Salaam. Ukanda wote wa mito na mabonde ya mkoa huu wananchi wameamua kufanya ni eneo la kutupa takataka hali ambayo imeharibu vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali na hasa katika mito na mabonde ya mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, ombi, tunaomba kuwe na kitengo maalum kitakachosimamia maeneo hayo ili kulinda na kuhifadhi mito na mabonde na kuhifadhi mazingira kwa ujumla. Kubwa zaidi, ni kuzingatia kauli ya Mheshimiwa Rais ya kupanda miti kwa wingi zaidi kwa kuzingatia maeneo na hali ya hewa ya kila mkoa. Hii iwe ni ajenda ya kufa na kupona. Vijana wengi wapo tayari kujihusisha na upandaji wa miti na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa mchanga, vijana wengi wanachimba mchanga mahali popote bila woga na viongozi wa vijiji na mitaa wapo hawachukuliwi hatua yoyote. Naiomba Serikali itoe waraka wa kuzuia uchimbaji wa mchanga kwa viongozi wa vijiji na mitaa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba hii katika eneo la mazingira. Eneo hili ni pana na linahitaji uangalizi maalum ili vizazi vyetu vijavyo visije kutulaumu ukataji wa miti umeongezeka sana na kusababisha jangwa kutoka katika maeneo mengi nchini kwetu. Lakini upandaji wa miti mingine ni mdogo mno. Hii ni hatari.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie kwa makini namna ya kurudishia uoto wa asili unaotoweka siku hadi siku. Ushauri wangu ni kuwa siku ya mazingira duniani ambayo ni mahsusi kwa upandaji miti basi kila Wilaya ipewe idadi kamili ya miti ya kupanda na itoe taarifa juu ya miti iliyopandwa mwaka uliopita inaendeleaje! Taarifa za sasa nyingi ni za kupika na sio sahihi. Kama kweli miti inayopandwa kila mwaka ingekua vizuri, basi nchi yetu ingekuwa na miti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rufiji hususan Jimbo la Kibiti katika mji wa Kibiti kuna kikundi cha mazingira kiitwacho *Rufiji Environmental Group* ambacho kimeotesha miti ya asili zaidi ya laki tano ambayo inahitajika kupandwa. Tatizo lililokuwepo ni ukosefu wa fedha wa kuhamisha miti hiyo kutoka kitaluni kwenda kuipanda katika eneo linalokusudiwa. Naiomba Serikali ikisaidie kikundi hiki kwani miti yake mingi ni ya asili hasa miti ya Mikongo ambayo kwa sasa imeanza kupotea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na warsha ambazo zinafanyika kuhusu uboreshaji wa mazingira, warsha hizi ni vizuri wakishirikishwa na Wabunge ambao ni wadau muhimu katika uboreshaji wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na muundo wa Wizara hii. Hivi kwenye ngazi ya wilaya ni nani anayehusika na Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, eneo la *Delta* ambalo lina miti mingi ya Mikoko inabidi lipewe kipaumbele ya kuboreshwa. Eneo hili ni *Ramsar Site* na ni tajiri kwa Mikoko na ndilo eneo kubwa kabisa la Mikoko hapa nchini. Hapo nyuma wananchi wanaozunguka eneo hilo pamoja na wengine kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Rufiji walianza kuishambulia miti hiyo. Lakini kwa sasa wananchi hao wameelimishwa na kuelimika na wameanza kupanda miti hiyo kwa wingi. Naishauri Serikali izidi kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi hao ili wazidi kupanda kwa wingi miti hii na hivyo kuboresha mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, naishauri Serikali kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni kidogo sana. Mfano mwaka 2008/2009 zimetengwa shilingi 98,000,000/=. Hiki ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA**: Mheshimiwa Spika, naanza na pongezi kwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na watendaji wote kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Muungano wa zaidi ya nchi moja una faida nyingi kama vile masuala ya uchumi mpana (soko) na ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi na raia na mali zao. Soko dogo siku zote si rafiki wa uwekezaji mkubwa. Ili tuweze kupata wawekezaji wakubwa katika nchi zetu na manufaa yake ya ajira na kadhalika, inapendeza nchi zetu ndogo ndogo kuungana. Bidhaa nyingi hazipatikani ndani ya mipaka ya nchi zetu ndogo ndogo na zinapatikana kwa urahisi ndani ya nchi zilizoungana.

Kuhusu ulinzi na usalama, kujenga jeshi (majeshi) imara ya ulinzi na usalama ni gharama kubwa ambazo nchi ndogo ndogo peke yake si rahisi kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, Comoro ni visiwa ambavyo kwa kiasi kikubwa havijitegemei katika maeneo ya ulinzi/usalama na upatikanaji wa bidhaa mbalimbali kama vile vyakula na vifaa vya ujenzi. Sehemu kubwa ya mahitaji ya visiwa hivi yanatoka nje pamoja na Tanzania. Majeshi yetu yako huko pia, sababu hizi pamoja na nyingine ndiyo chachu ya sisi kuendelea kuuenzi Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mazingira. Rais Mstaafu Alhaj Alli Hassan Mwinyi alipata kusema uharibifu wa mazingira na umaskini ni watoto pacha. Kwa hiyo, kwa dhamira yetu ya kupambana na umaskini chini ya sera yetu ya mkukuta ni dhahiri kwamba

tunawajibika sana kuyatunza mazingira yetu. Aidha, sambamba na kuyatunza mazingira yetu ili yawe endelevu, hatuna budi kuhakikisha kwamba sera zetu mbalimbali zinazogusa mazingira hazishindani na sera nyingine za kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, *Lake Natron.* Kwa mfano mradi wa uchimbaji wa magadi katika Ziwa Natron usikwamishwe kwa dhana ya kuhifadhi mazingira. Napongeza juhudi za kufanya tathmini ya athari ya mazingira zitokanazo na mradi huu ili kufikia maamuzi mazuri kwa manufaa ya kutunza mazingira na maendeleo ya mradi wa magadi nchini.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni muhimu sana kwa uchumi wetu kama ilivyo kwa uwepo wa ndege flamingo, ndiyo maana nasisitiza ndege flamingo waendelee kuwepo na mradi wa magadi nao utekelezwe pia.

Kuhusu misitu, hifadhi ya misitu yetu kwa ajili ya kupata mvua za kutosha na pia kuweza kuwa na vyanzo vya maji endelevu kwa manufaa ya uchumi wetu. Matumizi ya nyumbani, viwandani kuzalisha umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuni na makaa. Hizi ndiyo nishati kubwa kwa matumizi ya wananchi. Kwa hiyo, upatikanaji wa nishati hizi ni muhimu kwa maisha ya Watanzania. Lakini ukataji kuni na uchomaji mkaa, unachangia sana uharibifu wa misitu yetu. Kwa mantiki hii ni vyema Serikali ikabuni upatikanaji wa nishati mbadala ili kuepusha ukataji wa miti hovyo kwa ajili ya kuni na makaa.

Kwa mfano, Tanzania ina hazina kubwa ya gesi asilia. Kwa nini Serikali haiweki mkazo mkubwa na wa haraka wa kuendeleza matumizi ya gesi asilia kama nishati mbadala? Kazi ya kutekeleza mradi huo wa matumizi ya gesi asilia majumbani si kuwa kulingana na athari za kuendelea kukata miti.

Aidha, gesi asilia ikianza kutumiwa kama nishati mbadala kwa ajili ya kuendesha magari itasaidia sana kupunguza athari za uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi ya petroli na hasa dizeli.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, shukrani, ahsante sana kwa fursa hii. Pongezi, nawapongeza sana Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa hotuba yao nzuri sana.

Aidha, nawapongeza sana watendaji wote wakubwa na wadogo katika Ofisi na Wizara hizi kwa ushirikiano unaoonekana wameutoa kwa Mawaziri hawa hata hotuba hii nzuri ikawa kama inavyoonekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na pongezi hizi naomba nitoe machache katika maeneo mawili tu.

Kwanza ni kuhusu Muungano. Binafsi ninaogopa kila hoja ya Muungano inapoanza kujadiliwa, baadhi ya wasemaji wanaongea bila mipaka na staha. Mimi nashauri mambo mawili, kwanza, wasemaji kuwa waangalifu. Kauli ni tamu kuzitamka

lakini mtu huwa hana uwezo tena wa kumiliki athari na nguvu ya kauli yake mara inapomtoka. Ni vyema kila mtu awe na ufahamu kuwa si vyema mtu akawasha moto asiokuwa na uhakika na uwezo wa kuuzima moto huo mara utakapowaka!

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu Muungano. Mambo mengi ya Muungano yanaoneshwa na baadhi ya wasemaji kuwa ni kero kwa kuwa hawana ufahamu wa kweli au kupotosha ukweli waujuao na kupiga kelele sana kuonyesha kuwa yale wasemayo ndiyo ukweli mtupu. Wanayasema hayo kwa kupotosha ukweli waujuao au kutokana na wasiyoyajua vizuri.

Naomba sana kwa nguvu nyingi sana elimu itolewe kwa wananchi wetu na viongozi wengi. Ni vyema faida za Muungano ziwe bayana, aidha, kero na jinsi zinavyoshughulikiwa nazo ziwe bayana kwa wananchi wote ili kila linaloendelea kila mwananchi aliye na mapenzi mema na Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni mzuri na unahitaji kulindwa. Muungano unahitaji kuaminiana, kuheshimiana na kuvumiliana. Muungano wowote unahitaji upendo wa dhati waliomo katika Muungano huu. Naamini elimu ikitolewa kwa wananchi wetu tutauendeleza Muungano wetu na kuudumisha. Ni dhahiri hata maadui wa Muungano wetu kuwa bayana na itakuwa rahisi kuwasiliana nao.

Mheshimiwa Spika, mazingira**.** Mazingira ni muhimu sana kwa uhai na maendeleo ya wananchi wetu. Tatizo kubwa nililonalo mimi ni upungufu wa elimu ya mazingira kwa wananchi wetu. Kwa watu wengi masuala ya mazingira ni kupanda miti, kuzuia kukata miti na kuondoa uchafu barabarani na vitu kama hivyo. Binafsi naamini masuala ya mazingira yanaanzia katika fikra za elimu juu ya mazingira. Mtu kutambua kile akitendacho mtu kina athari gani kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ndiyo wawe na mpango kabambe wa kuwaelimisha maendeleo ya jamii hadi ngazi za kata na vijiji ili waweze kufanya kazi za uhamasishaji kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, mpango kama huo ufanywe kwa maafisa wote mijini, kata na vijiji ili waweze kusimamia masuala ya mazingira katika maeneo yao. Hakuna sababu ya kuajiri watu wengine. Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima afya na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwako wewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti kwa kuliongoza vizuri Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa kutuongoza vizuri. Pia shukrani ziwafikie viongozi wa chama chetu, Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa imani zao na uongozi wao ulio bora. Vile vile natoa shukrani kwa wananchi na wanachama wa *CUF* Jimbo la Mtambwe kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, ukuajia wa uchumi pamoja na maendeleo ya nchi yanategemea udhibiti na uhifadhi wa mazingira. Mazingira ni pamoja na ardhi, maji, misitu, hali ya hewa na kadhalika. Serikali inapaswa kuwa makini kuhakikisha kwamba sekta hizi muhimu katika mazingira zinadhibitiwa na kuhifadhiwa ili zisiharibiwe na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi pamoja na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, upandaji wa miti unaweza kusaidia hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji, kuboresha misitu, ardhi pamoja na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, *NEMC* inapaswa kuwa makini katika kusimamia na kuhifadhi mazingira kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji, misitu kwa ukataji miti ya kujengea, kuchoma mkaa pamoja na kuchoma moto.

Mheshimiwa Spika, Tanganyika imo katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano lakini Serikali ya Zanzibar haimo. Je, ni nani *partners* wa Muungano wa Tanzania, hapa kuna utata *(confusion).* Kuondoa utata huu ni kuwepo kwa Serikali tatu. Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kila Serikali itashughulikia mambo yake yenyewe na Serikali ya Muungano itashughulikia mambo ya Muungano tu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali ya Zanzibar haiwezi kujiunga moja kwa moja na Jumuiya za Kimataifa bila ya kupata idhini ya Serikali ya Muungano jambo ambalo linainyima Zanzibar fursa mbalimbali zinazoweza kusaidia kunyanyua uchumi wa Zanzibar na kuleta maendeleo. Hii inatokana na mfumo wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964 Rais wa Zanzibar alikuwa Makamu wa Rais, lakini hivi sasa ni Waziri asiyekuwa na Wizara. Mabadiliko haya ni ya kumdhalilisha Rais wa Zanzibar na hivyo pia kuidhalilisha Zanzibar. Hili linapaswa kuangaliwa upya ili kuirudishia Zanzibar hadhi yake iliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, kuna nyongeza zisizopungua kumi na moja katika mambo ya Muungano. Miongoni mwa nyongeza hizo zinaonekana kuinyima Zanzibar fursa mbalimbali pamoja na hadhi yake. Hivyo kuna haja ya baadhi ya mambo kuangaliwa upya kwa maslahi ya pande mbili za Muungano. Wakati wa kuundwa kwa Katiba mpya umefika ili kuondoa kero mbalimbali ambazo sasa zimekuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la hivi sasa kuwa Zanzibar si nchi. Hili ni tatizo ambalo kwa muda wote wa Muungano lilikuwa halieleweki wala halielezwi waziwazi kwa wananchi hasa wa Zanzibar. Ndio maana baada ya Wazanzibar kujua hilo kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni kuwa Zanzibar si nchi kumetokea malumbano makubwa kutoka kwa wananchi mbalimbali wa pande mbili za Muungano wakiwemo Wabunge, Wawakilishi na viongozi mbalimbali. Hili linatokana na mfumo wa Muungano uliopo. Hivyo *solution* ni kubadili mfumo wa Muungano kutoka Serikali mbili na kuwa na mfumo wa Muungano wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi kadhaa za kutekelezwa kwa muafaka baina ya *CUF* na CCM na hivyo kumaliza mpasuko wa kisiasa Zanzibar, lakini hadi leo hii halijatekelezwa na hivi sasa imekuwa ni kimya kabisa. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala la muafaka na ahadi kadhaa za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Zanzibar kutokana na misaada ya wafadhili Serikali inasema hivi sasa ipo katika mchakato wa kutafuta *formula* ya kudumu ya kugawana mapato yatokanayo na vyanzo vya mapato vya Muungano na kuchangia gharama za Muungano, je, kwa muda wote huo Serikali imekuwa ikifanya nini kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ina nafasi gani katika Benki Kuu ya Tanzania katika uanzishwaji wake pamoja na umiliki wa hisa? Ahsante.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE**: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Nchi kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri pamoja na watendaji wote katika Wizara hii kwa kuandaa Bajeti ambayo kwa kiasi kikubwa imelenga katika kuboresha mazingira ya nchi yetu ambayo kwa hivi sasa mazingira ya maeneo ya nchi yameharibiwa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu limekuwa ni jambo la kawaida kwa wananchi kutupa taka ovyo, kujisaidia ovyo, kutumia maeneo ya wazi ovyo hasa maeneo ya miji, hata kama kuna alama za kuzuia vitendo hivyo katika maeneo hayo bado kwa wananchi limekuwa jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, natambua wazi kuwa ipo sheria ambayo inawabana watu wanaokiuka sheria hii, je, kweli sheria hii inatumika? Na kama inatumika ni adhabu gani wanapewa watu hawa? Kwani nimeona pia vijijini watu wamekuwa wakichoma moto ovyo katika misitu hali ambayo imeathiri sana uoto wa asili, wanyama wadogo, vyanzo vya maji na kadhalika. Je, sheria iliyopo adhabu yake ni ndogo na ndio maana watu hawaoni, sababu ya kuacha vitendo hivyo ambavyo vinaathiri mazingira kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, kama ndivyo Wizara haioni iko haja ya kurekebisha sheria hii? Na kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kuelimika na kuacha kabisa vitendo vinavyoathiri mazingira?

Mheshimiwa Spika, katika suala la mazingira limekuwa ni mtambuka hivyo utakuta katika Wizara nyingine wanakuwa na fungu na mazingira, je, Serikali haioni mafungu yote yanayogusa mazingira ingeachiwa Wizara hii ili iweze kutenda vizuri kazi zake na kuwa na usimamizi hadi ngazi za chini? Naomba Serikali ingeangalia suala hili kwa umakini na kulipatia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikiwahimiza wananchi kuwa na vikundi vya ujasiriamali ili kuweza kumudu gharama za maisha na kuondokana na umaskini, katika kutekeleza ili akinamama na vijana mkoani Mtwara wamekuwa wakijishughulisha sana na kazi za mikono kwa kutumia rasilimali za asili zinazopatikana katika mkoa wetu kwa mfano miaa kwa kazi za ususi, mianzi kwa kutengeneza mapambo mbalimbali, miti kwa kazi za uchongaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, watu hawa wamekuwa wakipata shida sana wanapokutana na maafisa maliasili na pengine kunyang'anywa vitu vyao au kutozwa faini kubwa wakiambiwa wanaharibu mazingira. Je, hatuoni jambo hili hatuwatendei haki akinamama hawa ambao kipato chao hutegemea shughuli ndogo ndogo zinazotokana na mazao ya misitu? Ingawa wanakata leseni ndogo lakini wanahangaishwa sana hasa wanapotaka kusafirisha bidhaa zao. Je, Serikali kwa kuwa maafisa maliasili huwasumbua wananchi hawa kwa kosa la kuharibu mazingira je, Wizara hii inasemaje juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la uharibifu wa mazingira ambao umetokea katika Bonde la Ihefu kutokana na wafugaji. Natambua wazi kuwa Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya kuangalia uharibifu huo na nisingependa kulisemea jambo hilo kwa hivi sasa lakini hoja yangu ya msingi ni kwamba wafugaji hawa wamehamishwa wakapelekwa katika maeneo mbalimbali ukiwemo mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, kwa jambo hili ningependa kutoa ushauri kwa Serikali, kuhakikisha kuwa taratibu zilizowekwa kwa wafugaji hawa zinasimamiwa kikamilifu na zinafuatwa ili kuzuia uharibifu mkubwa ambao unaweza kutokea na migogoro kati ya wakulima na wafugaji hatimaye Serikali kuja kutumia gharama kubwa katika kutatua migogoro na utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA**: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Makamu wa Rais mwenyewe kwa kazi kubwa na nzuri iliyoendelea kufanywa na yeye mwenyewe pamoja na Mawaziri wa Nchi wawili na maafisa wote.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kero zimeendelea kushughulikiwa na mafanikio yanaonekana, ikiwemo mvuto wa wananchi wengi kutaka kuuelewa na kupendekeza, hata kupitia maswali mbalimbali, namna wanavyopenda Muungano huu uimarishwe. Suala la msingi hapa ni kupanua wigo wa namna ya kushughulikia kero za Muungano ili kutoa fursa ya kuzingatia hisia na maoni ya Watanzania kwa upana zaidi. Ofisi ya mkoa na Wilaya zinaweza kusaidia kupitia katika hata *RCC* na *DCC* zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri kwa kazi ngumu na nzuri. Suala la Muungano linazidi kuwa nyeti. Mimi nadhani moja ya sababu ni kuwa watu wasioelewa vipi Muungano wetu ulikuja wanazidi

kuongezeka na wote waliokuwapo Muungano ulipoanzishwa wanazidi kupungua. Sababu nyingine ni kuwa Wizara hii ambayo ndiyo inasimamia Muungano haionekani kuwa imechangamka vya kutosha kuwaelimisha wananchi hasa kizazi cha leo nini maana ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, tusisahau kuwa tangu kuzaliwa kwake Muungano umekuwa na maadui na watu ambao wangependa ufe sasa hivi wala siyo kesho. Baadhi ya hoja zinazotolewa hata kama zinaombwa kwa maneno matamu kama sukari zina lengo la kuona Muungano wetu unakufa. Kwa sababu hiyo ipo kila haja na ulazima wa kuchukua hatua siyo tu kuulinda Muungano bali pia kuona wananchi hawapotoshwi na maadui wa Muungano. Katika kufanya hivyo yapo mambo yanahitaji maelezo ya wazi na sahihi na yapo mambo yanahitaji marekebisho.

Kwa mfano hili suala lililokuwa hivi sasa la Zanzibar ni nchi au siyo, siyo la kulibeza kwa maneno kuwa mjadala wake hauna tija. Watu ni lazima waelezwe kwa usahihi kwa vigezo vyetu vya Kitaifa na Kimatifa upi ni usahihi. Tukitumia maneno ya Kiingereza ya *State* na *Sovereign* Zanzibar ni *State* lakini Jamhuri ya Muungano ndiyo *Sovereign State* siyo Zanzibar wala Tanganyika sasa je, neno *State* kwa Kiswahili tuite *State?* Ni nini Kiswahili cha *sovereign state?* Mimi nadhani watu ni lazima wapatiwe usahihi unaokubalika Kimataifa na pande zote mbili za Taifa letu, vinginevyo tutaendelea kutoa mwanya kwa maadui wa Muungano kuwavuruga mawazo watu, mimi naona ni wajibu wa Wizara hii kutoa maelezo sahihi.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni suala la kwa nini Rais wa Zanzibar siyo Makamu lakini ni Mzanzibari na wengine ni Makamu. Watu wanapotoshwa kama mabadiliko haya yalikuja kinyemela tena yalifanywa na Tanzania Bara peke yao siyo sahihi. Ukweli ni kuwa mabadiliko hayo yalifanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano tena kwa utaratibu uliowekwa na Katiba. Wabunge wa kila upande walipiga kura ili kupata theluthi mbili za Wabunge wa kila upande ndipo mabadiliko yakapita, ukweli ni upande wa Zanzibar walipinga Wabunge wawili tu wote kutoka Kaskazini Unguja mmoja Msanifu (Marekani) na mmoja Mheshimiwa Ussi Yahaya wote sasa siyo Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wa Zanzibar walikubali kwa theluthi mbili na mabadiliko haya yalifanywa kutokana na haja za msingi ambazo zipo na ni muhimu kuzingatiwa, na ili kuweka sura ya Muungano ndiyo maana iliwekwa utaratibu wa *running route* ili Rais wa Jamhuri akitoka upande mmoja wa Muungano Makamu atoke upande wa pili. Wanaopinga utaratibu huu wana hoja za siri ambazo hazina uhusiano na kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli pia yapo mambo ya kuwekwa sawa katika Katiba zetu mbili na kuondoa utata. Hakuna nchi hata za Muungano ambazo zinakuwa Amiri Jeshi Mkuu zaidi ya mmoja. Amiri jeshi Mkuu anakuwa wa yale majeshi ya nchi ambayo ni *Sovereign State.* Lakini hapa kwetu Katiba ya Zanzibar inamtaja Rais wa Zanzibar kuwa ni Amiri Jeshi Mkuu wa vikosi maalum. Hili ni tatizo kwani Amiri Jeshi

Mkuu ni wa Jamhuri ya Muungano. Utata wa namna hii ndio imetoa mwanya kwa watu wabaya kuvuruga hali ya hewa ya kisiasa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ya mwisho ni juu ya zile zinazoitwa kero za Muungano. Ni lazima tukiri kuwa Serikali zetu zimekuwa nzito mno kufikia maamuzi juu ya baadhi ya kero hizo.

Mheshimiwa Spika, tuchukue suala la asilimia inayofaa kugawana misaada kutoka nje. Hata baada ya tume ya pamoja kufanya kazi yake bado hakuna matokeo Serikali mbili zimeafikiana nini. Ucheleweshaji wa mambo muhimu kama haya yanatoa mbolea kwa wapinzani wa Muungano kuhuwisha mimea yao ya chuki dhidi ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara hii iwe na utaratibu wa kudumu wa kutoa elimu kuhusu Muungano faida zake kwa Taifa letu, kwa njia ya mijadala ya mara kwa mara katika *TV* na redio na siyo kusubiri wakati wa sherehe tu za kila mwaka na ikiwa uwezo wa pesa unaruhusu kutoa vijarida au gazeti kukuza ufahamu wa Muungano.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza kabisa nampongeza Mawaziri kwa hotuba zao nzuri zenye kueleweka. Kwa upande wa mazingira yote yaliozungumzwa kuhusu mambo ya mazingira yanaeleweka lakini nashauri izidi kutolewa elimu kwa njia ya redio, *TV*, mashuleni, magazeti, vipeperushi kuhusu mazingira, kwa suala la mazingira ni suala mtambuka linaingia kila sehemu mpaka maofisini, sehemu za kazi, viwandani yakiwemo mazingira ya kufanya usafi, sehemu kuwa wazi na kuonekana, mazingira ya kupanda miti, kulimia majani, kupanda maua na kuweka safi viwanja mbalimbali.

Vile vile haya magereji ambayo yamo mitaani yangehamishwa na kutafutiwa nafasi ambayo nje na makazi ya watu kwani nayo yanahatarisha afya za watu na kuharibu mazingira na hatimaye yanaweza kuleta maradhi ya aina mbalimbali, hata hii minara ya simu iliyoenea mpaka kwenye viwanja vya nyumba sijui itachukuliwa hatua gani kwani wachunguzi wa sayansi wanasema yana madhara na tayari yameshaenea maeneo yote katika nchi yetu sijui sasa yatafanywaje au itachukuliwa hatua gani kudhibiti mambo haya, kama sehemu za watu wengi pia zinahitaja usafi wa kujengwa vyoo, mfano sokoni, vituoni na sehemu mbalimbali zenye mkusanyiko wa watu, ili wasiharibu mazingira kwa kujisaidia ovyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muungano napongeza maelezo yote yalioelezwa na mikakati iliyowekwa na shughuli mbalimbali zilizofanyika na zitakazofanyika, na kuhusu kero za Muungano ambazo tayari zimeorodheshwa na ambazo nyingine zitajitokeza zifanyiwe kazi ili kuondoa haya malumbano na migogoro iliyopo kutokana na hao wasioutakia mema Muungano wetu ambao wanawatukana wakunga na uzazi ungalipo kwani Muungano umeleta faida nyingi na wengi wetu tumefaidika na huu Muungano nikiwemo mimi mwenyewe tangu kielimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia watu wengi wa Bara na Visiwani wote ni wamoja tunahusiana kidamu, kiasili, wengine babu katoka Bara, bibi katoka Visiwani au mama

katoka Bara, baba katoka Visiwani na hii imetokea tangu hakuna Muungano na bado tunazidi kuoana na kushirikiana na kuzaliana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Katiba kama kuna vifungu vinahitajika marekebisho basi yafanyiwe marekebisho hayo kwa mujibu wa sheria na kuhusu Muungano nataka uwe kama ulivyo sasa na uendelee na uzidi kuimarisha kwani wengi wanauonea wivu na choyo. Naitakia kila la kheri Bajeti hii na kazi njema.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU**: Mheshimiwa Spika, napenda kusema naunga mkono mia kwa mia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza sana Mheshimiwa Lucas Selelii wa Nzega aliyesema jana kuhusu suala la Muungano. Muungano huu wetu wa Tanganyika na Zanzibar kufanya nchi moja Tanzania yenye Serikali mbili.

Mheshimiwa Spika, naona Muungano huu kama tumefunga ndoa na mfano huu kwenye ndoa bwana, kuna vitu watu wa Zanzibar hawavipendi na kuna vitu pia Watanganyika *in that particular sense* hawavitaki au hawavipendi kwa misingi hiyo basi sisi wote lazima tuvumiliane na sio upande mmoja tu upande mmoja kuvumilia au kuendelea kuvumilia na bado wote sisi tunataka Muungano na unatufaa sisi wote. Hivyo basi isiwe kisebusebu na kiroho papo, sisi wote tunahitaji Muungano, hivyo lazima tuuenzi Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, kero hatukatai zipo hata kwenye ndoa zipo, ukizichambua sana waswahili husema ukichambua kuku humli, maana kuku anakula hata makamasi na uchafu zaidi. Kwa misingi hiyo naomba tusichambue sana kila upande una vitu ambavyo havimridhishi, lakini ndio hivyo wote tuvumiliane. La msingi tuiachie Serikali ishughulikie kero ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kila Jimbo lina Mbunge mmoja, lakini tuna Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi, hii ni moja ya kero toka upande mwingine. Kwa nini sasa tuna wengine zaidi? Majimbo ya Zanzibar ni madogo sana kama kata za huku yanawakilisha watu wachache. Yote haya tunamezea tu kwa ajili ya Muungano. Ni kama kwenye ndoa kama wataka ndoa iendelee, basi lazima kuyavumilia na kuvumilia ni wote sio upande mmoja. Ikiwa upande mmoja mwisho upande huo utachoka, iweje sasa? Kwa msingi hiyo, naomba tuvumilie/tuvumiliane wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mazingira, lazima tusisitizie kutunza vyanzo vya maji. Tupande miti mingi sasa ikiwezekana tupate miti ya kivuli na matunda ambayo baadaye yanaleta mvua. Tuhamasishe zaidi upandaji wa miti.

Mheshimiwa Spika, naomba tuhamasishe upandaji wa miti ya kuni, kwani miti mingi sana inavunjwa kwa ajili ya kuni/mkaa na hivyo kutuletea jangwa na upungufu wa mvua na hivyo njaa yaani upungufu wa chakula na kwa biashara kupitia kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba mbinu za kilimo cha miti ya kuni uendelezwe/ufundishwe nchi nzima ili tuepukane na hayo niliyoyataja hapo juu. Najua kuna mashamba ya miti ya kuni Zanzibar, naomba mbinu hii wafundishwe akinamama wote wa Tanzania yote na ni watumiaji wa kuni wazuri. Naomba elimu hii iendelezwe na isambazwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. TATU M. NTIMIZI**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashangaa Wabunge kuchangia kwa jazba na kusanifu Muungano, hasa wale watokao Pemba. Hivi wanajua kupitia Muungano huu ndio Wapemba wamepata nguvu na wengi kuhamia Bara? Hakuna mkoa usimuone Mpemba sasa kama hali hiyo hawataki, basi warudi kwao ili wakajinafasi. Lakini wajue kuwa Wasukuma wengi walioko Zanzibar wamekuweko huko kabla ya Muungano ndio maana wameendelea kuhamasisha kilimo na kutoa chakula cha kutoka huko visiwani. Kumbukeni, tusitukane wakunga wakati uzazi ungalipo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo, kama wenzetu wameona wanapunjwa kwa lolote lile bila kuona faida yake, basi waanze kupendekeza kuvunjwa kwa Muungano. Ikiwa Muungano uendelee basi aina ya Muungano tuendelee nao la sivyo kila mmoja akae na ustaarabu wake. Ajenda ya Muungano ifungwe, hao wanao usanifu, wana yao ambayo si kwa manufaa ya wananchi walio wengi, hakuna mtu kati yetu anayejipendekeza bali ni ustaarabu tu na kuvumiliana.

Kuhusu mazingira, uongozi wa Wizara au *NEMC* hawajafika Jimboni Igalula kusaidia na kukemea uharibifu wa mazingira. Hii ni kuiongezea nguvu siyo kusema Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji wameshindwa, lakini kufika kwenu ni kutia hamasa zaidi na uelewa, pia ndugu zangu Wasukuma, wamehamia Jimboni kwangu na ajenda yao ni kukata miti bila kujali aina, kukimea ukiondoka tu wanarudi kazi ni ile ile. Kutokuwa na mbadala wa nishati ndiyo maana kuni na mkaa vinatumika sana, sasa leteni umeme na gesi Igalula ili miti isitirike.

Kuhusu vibali vya kuvuna mbao kutoka Wizara ya utalii viache kuletwa jimboni kwangu, kwani watasababisha jangwa katika ardhi yetu, kwa mfano, wahamiaji Wasukuma wanakata miti ovyo na vibali vya uvunaji miti, magogo, mbao zitoke jimboni, sasa wananchi wetu waishi vipi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Buriani, MaKatibu Wakuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri na yenye mwelekeo wa kuboresha Muungano wetu pamoja mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda kumtamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia na nawaombea kwa

Mwenyezi Mungu awape nguvu, afya na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao barabara.

Mheshimiwa Spika, naungana na Serikali kuwa nishati ya mkaa inaharibu mazingira yetu kwani miti inakwisha hivyo basi naungana na Serikali kuzuia uchomaji wa mkaa bali naiomba Serikali itoe elimu juu ya nishati mbadala inayotakiwa kutumika sasa ili wananchi wasiendelee kutumia mkaa.

Mheshimiwa Spika, naungana na Serikali kuwa miti ya Mikaratusi inanyonya maji mengi sana. Hivyo inasababisha vyanzo vya maji kukauka na kufanya ardhi isistawishe mazao yanayolimwa kwa wingi na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilishatoa agizo miti hii kuvunwa ili kuondoa tatizo la vyanzo vya maji kukauka na kwa kuwa zoezi hili linatekelezwa pole pole sana, vile vile miti mbadala inapandwa kidogo sana. Naiomba Serikali kutoa mkakati mzito kuvuna miti hii na kupanda miti mingine hasa tatizo lipo Singida Mjini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kurudia tena kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia na kuomba suala la Muungano kutazamwa upya ili kuondoa migogoro inayojitokeza hususani shughuli za maendeleo ambazo tunashirikiana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na programu maalumu ya kutafuta teknolojia ambayo itapunguza ukataji wa miti hasa kwa ajili ya kuni za kukaushia tumbaku na chai.

Pia kufanyike utafiti ambao miti ambayo ina soko kubwa nje ili ilimwe kama ni mradi wa kupunguza umaskini na kuliongezea fedha za kigeni nchi yetu. Nashauri mshauriane na Wizara ya maji ili tuweze kuvuna maji ya mvua ili kuongeza matumizi ya maji salama.

Kuhusu Muungano, wakati umefika kuanzisha mjadala wa Muungano ili tupate ridhaa ya wananchi. Ushauri wa Kamati iliongozwa na Mheshimiwa Philip Marmo bado haujatekelezwa ni vyema ukatekelezwa. Ni vyema yale aliyoagiza Waziri Mkuu ya Wanasheria wa pande mbili kukutana, wigo upanuliwe kwa madhumuni ya kutekeleza hilo pendekezo langu la mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Waziri akaelezea je, mfumo wa Serikali unaotakiwa iwe ni sera ya vyama au ni uamuzi wa wananchi? Kwa mtazamo wangu suala la mfumo wa Muungano kwa wananchi na vyama vya siasa katika Katiba zao uonyeshe namna gani vitaimarisha mfumo huo. Ukiangalia Azimio la Bunge la tarehe 24 Agosti,1993 ni Azimio la Bunge liliidhinishwa na chama.

Naomba unieleleze utekelezaji wa azimio hilo, lakini naomba uzingatie ushauri wangu kuwa ni vyema tukapata kura ya maoni juu ya mfumo wa Muungano au tulipeleke suala hili kwenye mahakama ya Katiba. Nashukuru.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI**: Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi nilitaka maelezo au ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa mkakati wa hifadhi ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa kufanya uperembaji kutika mikoa kadhaa. Nilihoji kuwa hakuna *baseline data* iliyoandaliwa, uperembaji hauwezi kutekelezwa. Kadhalika nilihoji Serikali kushindwa kutafsiri *(definition)* ya chanzo cha maji. Mwisho nilihoji mantiki ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye moto poa na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa mazingira ni mtambuka na sehemu kubwa ya shughuli za mazingira zinategemewa kutekelezwa na sekta husika, ndiyo maana fedha nyingi za mazingira huelekezwa huko hususan kwenye halmashauri. Kwa bahati mbaya wataalam na mwamko wa mazingira kwenye sekta hizo ni kidogo, kwa hiyo, utekelezaji wa shughuli hizo ni hafifu, duni na matokeo hayajitokezi kwa uwazi.

Je, Serikali haioni kuna kasoro katika muundo wake kuhusu mahusiano ya kiutendaji kati ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu inayovuruga mtiririko wa maagizo ya kiutendaji na fedha kutoka ngazi ya juu hadi vijijini na kwamba hali hii inatakiwa kurekebishwa?

Mheshimiwa Spika, tumepokea barua kutoka *NEMC* ikitutaka Ludewa tuainishe masuala ya mazingira yanayohitaji ufumbuzi wa haraka katika Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, suala muhimu ni migogoro ya matumizi ya ardhi itakayotokana na miradi ya mchuchuma na Liganga itakayounganishwa na ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara na bandari. Migogoro hiyo itatokana na ongezeko kubwa la watu kutoka nje ya Ludewa na kushinikiza mahitaji ya ardhi ya makazi, kilimo na ufugaji. Ili kuepusha migogoro hiyo, napendekeza Wizara hii ishirikiane na Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Nishati na Madini, Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Halmashauri ya Ludewa kufanya *SEA* na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi.

Suala lingine ni shinikizo *(pressure)* kwenye mahitaji ya rasilimali mbalimbali kutokana na ongezeko la watu kwa sababu ya miradi ya Mchuchuma wa Liganga na kuathiri rasilimali hizo hususan za Ziwa Nyasa (samaki) na fukwe zake, maji na misitu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya dharura, Wizara hii ishirikishe Wizara za maliasili na utalii, Mifugo na Uvuvi; pamoja na halmashauri ya Ludewa kuainisha hali *(status)* ya rasilimali hizo na kundaa mpango wa matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho inasikitisha kuona kuwa licha ya neno mazingira kutamkwa mara kwa mara na Watanzania kuna uelewa mdogo wa maana ya mazingira kwa ngazi zote za jamii pamoja na viongozi wa ngazi za juu wa nchi. Wengi wanahusisha mazingira na miti tu na wengine hutafsiri mazingira kama ucheleweshaji au uzuiaji wa maendeleo yenyewe, huu ni mtazamo potofu na mawazo finyu. Mara nyingine nawasikia viongozi wetu pamoja na Mawaziri wakibeza na kupuuza umuhimu

wa *EIA* na *SEA* kama *tools* muhimu za kusaidia kufikia maamuzi kuhusu miradi au programu za maendeleo.

Hali inasikitisha zaidi inapotokea hata viongozi mwenye dhamana ya kusimamia mazingira naye anaegemea kwenye maendeleo zaidi kuliko mazingira na kufanya sekta ya mazingira ionekane kama haina mtetezi. Hali hii ikiachwa kuendelea ni hatari kwa mazingira ya leo na hususan ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, haja ya Wizara hii na taasisi zake kuanzisha mipango endelevu ya kutoa elimu ya mazingira kwa Watanzania na hasa wale wenye mamlaka wa mazingira niko tayari kutoa semina fupi kuhusu mazingira, hususan *SEA* na *EIA* kwa Waheshimiwa Wabunge kama ofisi ya Bunge itakuwa tayari kufanya maandalizi yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 27, kifungu 42, kuna programu ya *UDEM* Ofisi ya Makamu wa Rais inayosaidia Wilaya kuandaa Ripoti ya Hali ya Mazingira *(Environmental Management Profile).* Kutokana na kuanza miradi ya Mchuchuma na Liganga (Ludewa) na matatizo ya mazingira yanayotegemewa, naomba programu hii ya *UDEM*, itumike kuandaa ripoti ya Hali ya Mazingira Ludewa kabla miradi hii ya Mchuchuma na Liganga haijashika kasi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 30, Kifungu 47, Mikoa, Wilaya na sekta mbalimbali ziendelee kutekeleza majukumu yao ya mkakati. Kati ya vijiji 500 vinavyotarajiwa kupimwa na kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi zake, naomba vijiji vinavyozunguka migodi ya Liganga na Mchuchuma vifanyiwe mipango ya matumizi ya ardhi.

Ukurasa 80, Kifungu cha 102, inaonyesha kuwa *NEMC* ilikamilisha tathmini ya mifumo ya kiikolojia ya milima ya *Livingstone* katika Wilaya ya Mbinga tu wakati milima hiyo inaanzia Tukuyu kupitia Makete na Ludewa. Je, utafiti huo sasa utafanywa kwenye safu za milima yote ya *Livingstone* pamoja na iliyopo Ludewa.

**MHE. USSI AMME PANDU**: Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wa Wizara hiyo kwa Bajeti yao nzuri na yenye kutia matumaini kwa wananchi, lakini pia nipongeze Wizara hii pamoja na Serikali kwa kudumisha Muungano wetu huu ambao umekuwa ni mfano katika Bara la Afrika na duniani kote. Naupongeza sana sana.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilijenga barabara ya Amani hadi Mtoni Jeshini kwa awamu ya kwanza barabara hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu wa Tatu wakati wa Kampeni ya Uchaguzi mwaka 2005 Mheshimiwa Benjamini William Mkapa. Katika ufunguzi wa barabara hiyo Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ya pili utamalizwa na Serikali ya Muungano kabla ya kuondoka kwake madarakani.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho anieleze kupitia Bunge hili ni lini utekelezaji wa ahadi hii utaanza?

Wananchi wanasubiri kwa hamu utekelezaji wa ahadi hii na wanasubiri majibu baada ya miaka karibu mitatu kupita.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja hii na nitashika mshahara wa Waziri kama sitopata majibu ya kuridhisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA**: Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira kuna tafiti nyingi zimefanyika na zinaonyesha Mlima Kilimanjaro theluji yake inayeyuka na baada ya miaka kadhaa ijayo itapotea kabisa. Mlima Kilimanjaro kule *Hein Glacier* watu walikuwa wanatumia njia ile kupanda lakini kwa sasa hivi njia ile imefungwa kwa ile barafu kuyeyuka kabisa pale. Tayari hapa tumeshapoteza fedha kwenye uchumi wetu.

Ushauri wangu, Wizara iangalie ni jinsi gani ya hata kuelimisha wale *tour operator* wenye kupeleka wageni kupanda mlima pamoja na wenyeji wenye kuishi kuzunguka mlima wapande miti mingi na wasikate miti kwa ajili ya kuni. Hii kwa namna moja au nyingine itasaidia kuunusuru msitu wa mlima Kilimanjaro na kusaidia barafu isizidi kuyeyuka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya *plastic* lakini bado mifuko hii ipo madukani inabidi Serikali ifanye msako maalum na atakayebainika na mifuko ile atozwe faini au hata kufungiwa biashara yake.

Mheshimiwa Spika, jiji letu la Dar es Salaam ni kioo cha nchi yetu. Lakini cha kusikitisha mji wetu ni mchafu sana kimazingira. Kwa mfano mitaro ya maji machafu yote yapo wazi na watu wasiokuwa na uaminifu wanatumia mitaro ile kutupia taka chafu hata mifuko ya rambo na kadhalika. Ushauri wa ngu ni kuwa, Serikali ifunike mitaro ile. Sio hilo tu hata magari ya kuzolea taka katika mji wa Dar es Salaam pamoja na yale ya *breakdown* yote haya yanachangia katika kuharibu mazingira, yale magari mabovu yanatoa moshi mweusi ambao unaharibnu mazingira. Duniani pote kwa sasa hivi magari mengi yanayotumiwa sasa hivi yanatumia gesi ili kutunza mazingira. Swali, je, Serikali ina mikakati gani kwa kuanzia kuhakikisha magari haya hayapo barabarani njiani Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spik,a kuna haja ya kuwapa elimu wanavijiji kule kwenye vyanzo vyote vya maji panapopandwa miti na wakulima hawalimi katika vyanzo vile. Mfano pale Moshi kuna chemchem ya njiani. Watu wanaosha magari, wanatumia chemchem ile kuoshea magari. Watu hawa hakipata elimu ya uhakika hawatumia vyanzo hivi vibaya.

Kuhusu kero za Muungano, kwa kuwa Tume ya Jaji Nyalali na Jaji Kisanga iliundwa ili kuchunguza kero za Muungano na nina uhakika Tume hizo zilitoa mapendekezo, je, ni mapendekezo gani yaliyotokea? Na je, Serikali ipo tayari kutumia mapendekezo yake katika kutatua kero hizo?

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI**: Mheshimiwa Spika, naupongeza uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi wanayofanya juu ya shughuli za Muungano na mambo ya Mazingira.

Naomba kumkumbuka sana Marehemu Dr. Omar Ali Juma aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungo wa Tanzania kutokana na kazi kubwa aliyoifanya akiwa Makamu wa Rais katika kusimamia Muungano na masuala ya mazingira nchini. Kwa hakika kiongozi wetu huyu anastahili kuwekewa kumbukumbu maalum. Amekuwa mstari wa mbele kuelimisha umma juu ya kemikali, tabia nchi, utumiaji wa vyazo vya maji, upandaji miti na juu ya umuhimu wa tathmini za mazingira *(EIA).* Naamini Ofisi ya Makamu wa Rais yenyewe inaelewa zaidi ya haya juu ya Marehemu Dr. Omar Ali Juma, kiutendaji.

Nashauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuangalia uwezekano wa kuweka jina lake, aidha, kupitia mifuko yake ya mazingira au utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la uchafuzi wa mazingira katika maeneo yafuatayo, kwanza, Kata ya Mbagala, Wilaya ya Temeke kuna tatizo la uchafuzi wa mazingira kutokana na Moshi unaosumbua wananchi unaotokana na wazalishaji wa vibiriti unaofanywa na kiwanda cha *Alfa Match.* Vile vile kuna tatizo la umwagaji wa maji machafu ovyo unaofanywa na Kiwanda cha Nondo. Haya yote nimeyawasilisha kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na wananchi wanasubiri majibu ya *NEMC* katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo lingine na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na *Tazama Pipelines* ambao wanamwanga mabaki ya mafuta sehemu isiyostahili eneo la *TIPPER* na kusababisha uchafuzi wa maji safi ya visima katika kata ya Wijibweni, mtaa wa Kisiwani, kueneo kwa harufu mbaya na kusababisha mmomonyoko wa ardhi.

Naomba kuelewa *NEMC* kupitia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira wamefikia wapi katika kufuatilia jambo hili. Naomba majibu Bungeni.

Aidha, kuna tatizo kubwa la uharibifu wa mikoko unaofanywa kwa makusudi na watu binafsi, tarafa ya Kigamboni. *NEMC* wanalielewa, tunaomba kujua hatua zilizochukuliwa. Sheria zilizopo juu ya mikoko na utunzaji wake zisimamiwe.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha kitengo cha Muungano Zanzibar ilikuwa nia ya kuratibu kwa karibu sana majukumu ya idara ya Muungano kwa mara ya kwanza kuwekwa Mratibu wa Muungano Zanzibar. Suala la Zanzibar kuwezeshwa kukopa nje lipewe msukumo wa kutosha na sekta husika za pande zote mbili zikutane kwa haraka kujadiliana na kutia mwongozo wa kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa ofisi ya Faragha na *State lodge* wanafanya kazi kubwa ya kumsaidia na kumhudumia Makamu wa Rais na muda wao mwingi kwa siku unatumika katika majukumu ya kazi. Hivyo naomba Serikali kuboresha posho za mazingira magumu ya kazi kwa watumishi na wasaidizi wa Makamu wa Rais, hii ni kuzingatia kwamba hawana muda wa kuweza kujiongezea kipato baada ya saa za kazi kutokana na maelezo ya hapo juu.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiongea na Wabunge wa Bunge jipya la mwaka 2005 – 2010 katika hotuba yake alitoa wito wa zile Wizara zisizo za Muungano nazo kuangalia uwezekano wa kushirikiana na kuzisaidia Wizara zisizo za Muungano. Wananchi wa Kigamboni wanapenda kujua utekelezaji wa agizo hilo la Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwa ni mratibu wa Muungano. Naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN**: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii na kuwapongeza Mawaziri na watendaji wote wa ofisi hii, naomba nipate maelezo ya kina kuhusu suala la mazingira katika eneo la Kigogo Sambusa ambalo limejengwa ukuta mkubwa sana, eneo hilo kuna mto Msimbazi ambao mara nyingi wakati wa mvua huwa na mafuriko makubwa na maji hujaa katika eneo la Kigogo Sambusa ambalo limejengwa ukuta mkubwa sana, eneo hilo kuna mto Msimbazi ambao mara nyingi wakati wa mvua huwa na mafuriko makubwa na maji hujaa katika eneo hilo hivyo kunusuru maisha ya wananchi wanaoishi eneo hilo lakini kwa kuwa eneo hilo hivi sasa limejengwa ukuta mkubwa na kujazwa kifusi hivyo wakati wa mvua na mafuriko kutokea maji yaliyokuwa yakijaa eneo hilo yataingia kwenye maeneo ya makazi ya watu hivyo kusababisha maafa makubwa.

Naomba Waziri anipe maelezo na awaeleze wakazi wa eneo hilo la Kigogo ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kuhusu usalama wao wakati wa mafuriko? Je, ilifanyika tathmini ya mazingira na mjenzi kupata kibali? Na kama *NEMC* ilitoa kibali ni kwa nini wananchi wa eneo hilo hawakushirikishwa? Na kama kweli *NEMC* imeridhia ujenzi ndani ya mkondo wa Mto Msimbazi yatakapotokea madhara, wakati wa mafuriko mtakuwa tayari kuwajibika na kulipa fidia kwa waathirika? Je, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira wameishauri Wizara ya Ardhi kuhusu kumilikisha eneo hilo la Kigogo Sambusa mmiliki huyo kwa kumpa hati ya kumiliki mpaka Mto Msimbazi ili hati hiyo ifanyiwe marekebisho ili kupunguza urefu wa eneo hilo mita 198 na kuwezesha eneo lote la mto huo kuwa wazi na kutomilikiwa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na nikiamini kabisa kuwa ofisi hii itahakikisha kuwa suala hili la mazingira linapewa uhumimu wa pekee kwani mazingira ni uhai.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia tena kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE K. MALECELA**: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo yote mawili kwa pamoja nianze na mazingira. Ili Wilaya ya Same iendelee kuwepo kikamilifu ni lazima msitu wa Shengena uwepo. Sasa hivi msitu huu umevamiwa vibaya sana na majangili wanaovuna mbao ovyo na kutafuta dhahabu.

Mheshimiwa Spika, hali hii sio nzuri na kila siku hali inakuwa mbaya. Mheshimiwa Waziri ningeomba aelewe kuvamiwa kwa msitu huo kunaua Same na nitaomba Waziri wa Mazingira alitolee kauli wakati anahitimisha ili na majangili wale wajue Serikali imejua na inachukua hatua madhubuti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, jambo lolote huku duniani linapokosa upendo na uvumilivu linakosa nguvu na linaharibika. Muungano wetu ni muhimu sana kwa nchi yetu. Tunalohitaji hapa ni sisi viongozi kuwa na upendo, uvumilivu, busara na hekima. Mahali popote penye kuungana pana kukwazana, sasa tupendane, tuvumiliane ili Muungano wetu udumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA**: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Ziwa Rukwa hasa upande wa Kusini mwa Ziwa hili limeathirika kiasi cha kima cha maji kupungua sana na Ziwa lenyewe umbali wa zaidi ya kilometa saba. Mbona kwenye hotuba zote hakuna kilichozungumzwa kuhusu uharibifu unaofanyika kwenye Ziwa hilo?

Mheshimiwa Spika, pili, kwenye Ziwa Rukwa wapo wavuvi wadogo wadogo wanaoishi kwa kazi hiyo, je, ule mfuko wa dunia wa mazingira *(GEF)* unawezaje kusaidia wavuvi hao wadogo wadogo kunufaika na mfuko huo?

Tatu, Wilayani Chunya kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi ambao hawana elimu yoyote ya utunzaji wa mazingira. Matokeo yake wamesababisha uharibifu mkubwa sana kwenye mazingira. Kwa kutumia Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF)*, je, haiwezekani kukaandaliwa mpango wa makusudi wa kunusuru mazingira husika kwa kutoa elimu kwa wachimbaji hao wadogo wadogo?

Mheshimiwa Spika, nne, miaka ya hivi karibuni kumezuka tabia ya madereva wa magari kukata miti na kuitandaza barabani ikiwa ni ishara ya kuwa gari limeharibika huko mbele, je, hiyo ndiyo sera ya mazingira? Tano, kwenye Jimbo la Songwe – Chunya yamegundulika machimbo ya makaa ya mawe yaliyokuwa yakitumiwa na Wajerumani enzi hizo kwenye Kijiji cha Magamba. Ili kunusuru uharibifu wa ukataji miti ovyo kwa ajili ya matumizi ya nishati majumbani, je, makaa ya mawe yaliyopatikana kwenye Kijiji cha magamba?

Mheshimiwa Spika, sita ni kuhusu Muungano. Mbona Serikali haijatoa tamko rasmi kutokana na utata unaoendelea hivi sasa juu ya utambuzi wa Zanzibar kama ni nchi au la?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA**: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kazi nzuri ya kusimamia kitengo cha mazingira. Kazi nzuri na nyingi zilizofanywa na zilizopangwa zinaonekana; *keep it up!* Pongezi pia kwa Katibu Mkuu na watendaji wote wa masuala ya mazingira. Nawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu hali ya mazingira mijini ni changamoto kubwa. Mipango mizuri ya kuboresha miji ipo, imeonyeshwa. Hata hivyo, naomba niongezee suala moja kwa ushauri ili kuboresha miji yetu.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni utengaji wa maeneo ya bustani mijini. Ili kuboresha hali ya miji ili kuifanya ivutie na kuwa na hewa safi, mipango miji ijumuishe utengaji wa maeneo ya bustani. Haiwezekani miji yetu iachwe inakuwa bila ya kuwa na maeneo ya bustani. Angalia jiji la Dar es Salaam lisivyo na maeneo ya bustani, angalia miji mingine mingi. Hali hii haikubaliki katika maana ya kuwa na mazingira bora. Hata Dar es Salaam, mpango unatakiwa kubadili hali iliyopo kwa kutenga maeneo ya bustani.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kuna mpango wa *UDEM* ambao fedha zake zinaweza kutumika kutengeneza bustani za miji pale palipo na maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Mfano Manispaa ya Shinyanga ina maeneo zaidi ya matatu kwa ajili ya burudani. Maeneo hayo hayajaendelezwa kwa sababu ya fedha. Nashauri Serikali iruhusu matumizi ya fedha za *UDEM* kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya bustani mijini (Shinyanga Mjini) pale palipotengwa kwa ajili hiyo. Miji mingine ihimizwe kutenga maeneo ya bustani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya mabadiliko ya uoto. Naendelea kushauri haja ya kufanya tathmini ya mabadiliko ya uoto kati ya miaka 1960/1970 na sasa. Hii itatuwezesha kuona ni kwa kiasi gani na kazi ipi mabadiliko yametokea, ili hatimaye tuweze kutabiri tunakoelekea na kuchukua hatua za kurekebisha pale utabiri utaonyesha hali mbaya tarajiwa. Ni muhimu tuwe na dira sahihi ya hali ya mazingira kwa siku za usoni. Dira sahihi tutaiweka kwa kuangalia tulikotoka tukilinganisha na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, sina shaka na uongozi bora wa Waziri wa Mazingira. Naunga mkono tena hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii kujua hasa kuhusu mazingira kwenye Ziwa Victoria.

Kuhusu magugu maji yaliyotanda ziwa lote mpaka Mialo yote imekuwa kama uchafu. Naomba kujua ni kifungu gani kilichotengwa kuhusu mazingira hayo kufanyiwa kazi? Naomba kuuliza ni lini Serikali itatenga kifungu cha kutoa elimu kuhusu vyanzo vya maji ili wananchi waelewe umuhimu na faida na madhara yake. Serikali imetenga kifungu au tunaendelea kuwalaumu tu?

Mheshimiwa Spika, wenyewe wanatafuta sehemu ya maji kulima ili wapate mazao, kumwaga uchafu ovyo ovyo kwa mfano kumwaga kinyesi baharini, kuchoma uchafu ovyo, mitaro hasa mitaro yote ya Dar es Salaam, mitaro yote imejaa uchafu, hawana aibu ndio maana ugonjwa wa kipindupindu unaenea kwenye mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona au hapana kama inaona, Wizara ina majukumu gani. Mama ntilie wanapika vyakula humo humo, vyombo vya usafiri vya majini kutupa uchafu, kufungua vinyesi majini na baharini na ziwani; tunagetemea samaki humo humo je, magonjwa yataisha? Pamoja na hayo Serikali iko tayari kutoa huduma za dawa kama sivyo naomba nipatiwe majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina mikakati gani kuhusu ofisi ya Ardhi iache kugawa viwanja sehemu ya vyanzo vya maji na wenyewe wanasababisha kutoa viwango. Baadaye wanakuwa wamejenga ndipo wanawaambiwa waondoke na hawalipwi je, huo ni uungwana, sio unyanyasaji huo? Je, unamtoa aende wapi hayo ndiyo niliyo nayo machache nitaomba nijibiwe kifasaha kwenye mchango wangu mdogo sana . Nawatakia Bajeti njema.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuungana na Wabunge wenzangu katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Kwanza napenda kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Riziki Omari Juma, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetupa mwanga Watanzania wengi kufahamu vizuri kuhusu Muungano. Pili, naomba Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho naomba anijibu mambo yafuatayo, kwanza kuna tatizo gani kama Muungano wetu ungekuwa na Serikali tatu.

Mheshimiwa Spika, maana ya kuuliza hili ningependa kujua pia, Bunge hili ni la Muungano na Bajeti tunazopitisha humu ni za Muungano wakati kuna Wizara ambazo si za Muungano na zinapitisha Bajeti zao katika Bunge hili, hivi Serikali haioni kama haitendi haki kwa kutokuwa na Serikali ya Tanganyika? Na Bunge au Baraza la Tanganyika ndiyo lingejadili Bajeti ya Tanganyika kama ambavyo Baraza la Wawalikilishi linavyojadili. Bajeti ya Zanzibar, hapa ndipo vyama vya Upinzani kama *CUF* wanapopendekeza kuwa na Muungano wenye mfumo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Muungano tulionao sasa unahatarisha kupoteza historia ya Tanganyika, kwani huenda vizazi vijavyo, vikashindwa kujua historia ya nchi yetu. Inaonyesha bayana kuwa historia ya Tanganyika iko njiani kutoweka kwa kutofuatilia hiyo historia. Mtoto wa darasa la sita hajui kama nchi hii hapo awali iliitwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kidogo masuala ya mazingira. Uwekezaji wa wachimba madini, umekuwa ni waharibifu wakubwa wa mazingira, sasa Serikali inasema nini juu ya mashimo ambayo wanatuachia? Mimi nashauri Wizara au Serikali, ihakikishe mashimo hayo yanafukiwa mara tu wanapohama eneo hilo au mashimo hayo yatengenezwe kuwa mabwawa kwa ajili ya kilimo na wanapokuwa wanakwenda mbele zaidi huku wanakotoka wafanye kama nilivyoshauri kwani kwa kufanya hivyo tunaweza kupata mabwawa ya kunyweshea mifugo kwani kuacha mashimo bila kuyafukia au kuyatengeneza kama mabwawa huu ndiyo uharibifu mkubwa. Serikali ijue kama wachimbaji wachimbao ni bora pia kufukia mashimo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali imekuwa inahimiza upandaji wa miti ili tutunze mazingira, ardhi na vyanzo vya maji. Wananchi wamekuwa wakiitikia wito huo na miti mingi imeshapandwa, jambo ambalo linanitia mashaka juu ya zoezi hili ni pale idadi ya miti inayokatwa au kuvunwa. Kwa mwaka, inazidi idadi ya miti inayopandwa. Lakini la pili suala zima la utunzaji wa miti mipya inayopandwa kufikia hatua ya kukomaa Serikali haina budi basi kuongeza juhudi ya kuhamasisha na

kusimamia upandaji miti na kuandaa mikakati madhubuti kuhakikisha miti inayopandwa inatunzwa, kwa asilimia kuwa ifikie kiwango cha kukomaa.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi nyingi hasa zinazoendelea zimekuwa zinajikita katika matumizi ya tiba asilia *(alternative medicine)* na kuachana na dawa zenye mchanganyiko wa kemikali. Nchi yetu ni tajiri sana wa miti ya asili ambayo hutumiwa katika tiba asilia. Lakini kasi ya uvunaji wa miti hii imekuwa ni kubwa inayotishia baadhi ya miti hiyo kutoweka. Naishauri Serikali kuandaa programu maalum ya kuwashawishа waganga na miti ya asili kuanzisha mashamba makubwa ya kuotesha miti hiyo. Kwanza kwa madhumuni ya kujipatia dawa, lakini la pili kutunza mazingira ya ardhi.

**MHE. ALI SAID SALIM**: Mheshimiwa Spika, naomba maelezo juu ya nishati ya mafuta ambayo kuna fununu kuwa yapo ya Zanzibar, je, ni kwa nini madini kama Almasi, dhahabu, *Tanzanite* na kadhalika ambayo hupatikana Tanzania Bara kwa nini yasiwe ya Muungano?

Mheshimiwa Spika, miezi michache iliyopita Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipewa na Serikali ya Marekani karibu dola milioni 700 au dola milioni 680, hivi dola za Kimarekani pamoja na kuahidiwa vyandarua milioni tano je, kwa upande wa Zanzibar walipewa kiasi gani cha fedha hizo na vyandarua vingapi vimepelekwa Zanzibar kama mgao wake?

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano zinaongezeka siku hadi siku badala ya kupungua je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kuongezeka kwa kero hizi pamoja na vikao kadhaa vilivyofanyika kati ya pande mbili husika? Je, Serikali inaonaje kuwashirikisha wananchi katika kutatua kero hizi?

Kuhusu nafasi ya Zanzibar ndani ya *BOT*, kumekuwa na utata juu ya nafasi ya Zanzibar katika Benki Kuu ya Tanzania katika uanzishwaji wa umiliki wake wa hisa, kumekuwa na maneno mengi kuwa Zanzibar haikutoa mchango wowote katika kuanzishwa *BOT* na kwa hivyo haimiliki chochote katika hisa, je, Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali anasemaji katika suala hili na nini msimamo wa Serikali katika suala hili?

**MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo leo hii kutoa mchango wangu wa maandishi kwa Wizara hii ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano anao uwezo mzuri kwa nafasi aliyopewa lakini wasiwasi wangu ni je, anayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba Muungano wetu udumu kwa Serikali mbili au ni kuudidimiza kuelekea Serikali moja?

Mheshimiwa Spika, kusema hivyo ni kwa sababu ifuatayo, kwanza, tarehe 24 Agosti, 1993, Bunge lilipitisha kwa kauli moja Azimio la kutaka iundwe Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano ili kuwa na muundo wenye Serikali tatu. Lakini tarehe 6

Agosti, 1994, Rais wa Jamhuri ya Muungano aliwasilisha kwa Wabunge wakiwa katika Kikao rasmi cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Azimio la Halmashauri Kuu ya Taifa kwamba Sera ya Chama cha Mapindizi ni muundo wa Muungano wenye Serikali mbili yenye mwelekeo na upeo wa muda mrefu wa muundo wa Muungano wenye Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, Bunge katika Mkutano wake wa Kumi na Sita uliofanyika Dar es Salaam, mwaka 1994 iliazimia kwa kauli moja kufuta azimio la kutaka iundwe Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano na badala yake kuweka Azimio la Muungano wenye Serikali mbili yenye mwelekeo na upeo wa muda mrefu wa muundo wa Muungano wenye Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, hali hii Wazanzibar wanaburuzwa tena kiujanja sana ili waamini Serikali mbili, lakini wanaelekezwa kwenye Serikali moja. Sasa Mheshimiwa Waziri anawahakikishiaje Wazanzibar kuwa azma bado ni Serikali mbili zilizo na ujanja wa kuelekea Serikali moja hasa ukizingatia kwamba katika Wizara yake Wazanzibar hawazidi watatu, ni juzi tu katika Wizara za Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi yalitokea malalamiko kuwa Wazanzibar wanachukuliwa nafasi zao na vijana kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Afrika Mashariki hakuna Mzanzibar yoyote hii ni hutokana na majibu ya Naibu Waziri wa Wizara hiyo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha na nakushukuru sana, ahsante.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kabla sijaanza kuchangia kwa niaba yangu na wananchi wangu wa jimbo langu la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii kwa maelekezo yake. Mimi kwanza nitazungumzia kuhusu kero za Muungano kwa vile kero hizi zinazungumzwa kwa muda mrefu sasa ipo haja ya kumalizwa ili Muungano usilalamikiwe kwa kero hizo. Kwa hivyo, kwa kila wataokaa kwenye vikao vya kero ya Muungano kila kero watakayoipatia suluhisho itangazwe.

Kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar, ilivyokuwa huu ni Muungano wa pande mbili basi ni vyema Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar ijengwe na kuwe na huduma zote kwenye ofisi hiyo ili wananchi wa Zanzibar waweze kuhudumiwa na ofisi hiyo kwa mambo yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa fedha, ni muda mrefu sana sasa tunatumiwa hesabu ile ile ya 4.5% ambayo imepitwa na wakati, kwa hivyo sasa ni wakati wa kukaa na kutizama upya ili mgao huo kwa upande wa Zanzibar uzidi kutokana na muda mrefu uliotumika hesabu ya mgao huo.

Mheshimiwa Spika, lazima nipongeze na kushukuru kwa mazuri yaliyomo kwenye Muungano huu, ni dhahiri kuwa Muungano huu umeleta sifa kubwa ulimwengu mzima na hasa nchi za Bara la Afrika, kwa jinsi Muungano huu uliodumu na ambao unaendelea kwa amani na usalama. Pia kwa wale ambao wanafikiria Muungano huu utavunjika basi wamechelewa Muungano ni daima dumu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa *TASAF* kwenye Jimbo langu la Mwanakwerewe kwa kunipatia mradi wa maji ambao yanapatikana kiasi, kwa hali hii natoa shukrani za dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, nizidi kukushuru kwa kuniruhusu kuchangia na nazidi kuunga mkono hoja hii.

**MHE. MWANAHAMISI KASSIM SAID**: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na Muungano.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuwa na Muungano hili sio jambo la kuchezewa hata siku moja kwani dunia sasa ina mwelekeo wa kuwa nchi moja kwa kuleta maendeleo. Hivyo nashauri kwa Wizara ya Muungano kwa pamoja ifanye busara ya kuhakikisha jambo hili linapambana kwa busara kwa hivi karibuni Afrika katika historia ya dunia, mikutano wa kulifanya bara la Afrika ulifanyika Arusha, je, leo hii tunajadi Muungano wa miaka 40 kwanza hilo si jema.

Pili, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais ifanye mpango maalumu katika kuwaenzi viongozi wa Muungano basi ionyeshe mfano mkubwa kwa Marehemu Dr. Omar Ali Juma, kwani alifariki akiwa kiongozi wa juu wa nchi, naomba Waziri aangalie na atoe tamko juu ya nini kinaweza kufanyika juu ya Marehemu Dr. Omar Ali Juma.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye mpango maalum wa kuwapatia *scholarships* za nafasi ya masomo nje ya nchi ili vijana wa Zanzibar kupata nafasi zaidi ambazo zinakuja na kuona wao pia ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na kukuza nafasi ya kupata wataalam pande zote za Tanzania, ili kuwa na nafasi ya kutetea Muungano huu huko mbele.

Mheshimiwa Spika, nafasi za ajira katika nafasi za Wizara mbalimbali utaratibu wa kuzitangaza katika vyombo ambavyo watapata nafasi za kuziona lakini pia wapewe kipaumbele zaidi ili kuongeza wigo na nafasi za vijana kwani wao ndio Taifa la kesho kwa hiyo, bila ya kuwapa nafasi ya vijana katika nchi.

Kuhusu elimu juu ya masuala ya mazingira pamoja na Muungano suala hili limekuwa likizungumzwa tu lakini kwa mpango maalum wa kuwafundisha vijana Muungano huu umetoka wapi na sasa upo wapi bila ya hivyo kasoro zitakuwa zinazidi kila siku. Kuna haja ya kuanzisha mpango ambao rika la vijana wataelewa zaidi ni hasa kulitokea mpaka leo hii Muungano unatimiza miaka 40 ya uhai wake.

Kwa upande wa kasoro, hilo jambo lisiwe ndio kigezo kikubwa cha kuwa faida yake ni ndogo, nashauri sasa tuwape nafasi ya ushauri zaidi, wasomi, vijana ili kasoro zinazoonekana zisiwe na chanzo cha kukashifu Muungano wetu na sasa ukidumu kwa heshima na amani chini ya Serikali zetu za CCM za Bara na Visiwani.

Kwa hiyo, kutokana na mchango huu naomba kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa asilimia mia bila ya pingamizi.

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Spika, Afrika inarudi nyuma kuhusu ajenda ya Muungano, wakati Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umetimiza miaka 44 hakuna nchi zilizojitokeza Afrika. Kuiga mfano huu mzuri, Muungano wa Senegal na Gambia ulikuwa mfano huu lakini Senegambia haikudumu hata mwaka mmoja.

Kwa mimi mkristo na maandiko ya kitabu cha Daniel kuhusu ndoto ya Mfalme Nebukadnizer juu ya himaya yake ambayo utabiri ulionyesha kwamba utasambaratika na kubaki vipande vipande. Kwamba himaya zote duniani zitabakia vinchi, toka enzi ya Nebukadnizer hadi leo himaya zimekuja na kuondoka na kadri himaya zinavyotokomea kinachobakia ni vinchi vidogo vidogo, *USSR* ni mfano hai. *Nationalistic sentiments* huzuka na kuzusha mambo.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi bila Serikali moja hakuna atakayezuia malumbano yatokanayo na *nationalistic sentiments. People are always nostalgic they tend to look back nostalgically* na Serikali moja haiwezi kuja kwenye sahani *(plate).*

Mheshimiwa Spika, George Washington, Abraham Lincoln waliiunganisha Amerika kwa nguvu. Hali kadhalika Afrika haiwezi kuungana kwa kupitia mikataba ya uchumi, *SADC, COMESA, ECOWAS, NEPAD, East African Common market* na kadhalika. Haiwezi kuungana kwa utashi wa kisiasa, *solution* kwa Afrika kuungana ni *military solution* nchi zenye mtazamo mmoja ziunde jeshi la pamoja na zitoe wito wa kuungana, kwa kutumia *platform* ya kisiasa, kama nchi zingine zitaendelea kukaidi basi zitakabiliwa kijeshi, ndipo tutapata *United States of Africa* ndipo masuala mengine ya uchumi, siasa yatakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni uchu wa madaraka wa viongozi wetu wa Afrika, hakuna tofauti na suala la Muungano wetu unahujumiwa na uchu wa madaraka wa viongozi na si wananchi, viongozi hawa wenye uchu wakabiliwe bila woga/muhali, vinginevyo tutaendelea kukumbana miaka nenda rudi wakati huo ikimomonyoa misingi ya mmoja wetu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hatua za haraka zichukuliwe dhidi ya viongozi wote wanaopinga Muungano, viongozi hawa ni wanafiki sana kwa kujifanya wanaupenda Muungano ili kuwa na kero. Kuendelea kulumbana bila kuchukua hatua kwa kisingizio cha demokrasia, ni sawa na kukoleza moto kwa petroli, watu hawa wachukuliwe hatua. Vinginevyo tukubali kuwa maandiko ya kitabu cha Daniel na ndoto ya Mfalme Nebukadnizer yaachwe yachukue mkondo wake kwa nchi hizi mbili kurejea *status quo* ya tarehe 9 Desemba,1961 na tarehe 12 Januari,1964 *respectively.* Nawasilisha.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake. Aidha, nakubali na kuunga mkono hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Zanzibar ni nchi au si nchi, nasema kwa hali ya Tanzania, Zanzibar na Tanganyika siyo nchi, nchi ni Tanzania. Kwa vile suala la Serikali mbili inaelekea linakwaza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, njia iliyopo ni kwenda Serikali moja. Hiyo ni njia sahihi na ambayo ilikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. MOHAMED ALI SAIDI**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchangia kuhusu kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, bado hapajakuwa na nia thabiti ya kuondoa kero za Muungano kwani hili ni suala la nchi mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Ndani ya nchi hizi pia pana mfumo wa vyama vingi vya siasa, kwa hiyo, yangekuwa vyema kero hizi zishughulikiwe na vyama vya siasa na sio kuwa lishughulikiwe na chama kimoja tu cha siasa yaani CCM. Hivyo nikufanya CCM pekee Tanzania ndicho chama chenye maamuzi ya nchi, kufanya hivyo kwa CCM nikuendesha nchi kwa udikteta.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina watu wengi wenye vyama tofauti na wengine wasiokuwa na vyama tena wenye mawazo mazuri. Kwa hiyo, masuala haya ni vyema yahusishwe watu wote na sio CCM pekee.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu huu una kasoro kubwa, mimi naomba Katiba ya Jamhuri ya Muungano itengenezwe upya. Suala la Rais wa Zanzibar kuwa asiwe Makamu wa Rais hii ni kasoro, kwani ni kumnyima Rais wa Zanzibar madaraka. Kwa hiyo, Katiba itengenezwe upya ili Zanzibar irejeshewe madaraka yake na suala pekee litakaloirejeshea Zanzibar madaraka yake ni kuwa Tanzania iwe na Serikali tatu, yaani ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar. Kwani sasa hivi pana Serikali ya Tanganyika tu iliyojificha chini ya kivuli cha Muungano.

Mheshimiwa Spika, naiomba CCM ibadilishe sera yake ya Serikali mbili kuelekea kwenye Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, suala la Afrika Mashariki, Zanzibar ilikuwa ni mwanachana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, lakini sasa hivi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa. Kwa hiyo, ingekuwa vyema Zanzibar ingeshiriki kama Zanzibar pamoja na Serikali ya Muungano. Basi uwakilishi wetu ungekuwa mzuri sana.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hakuna haja ya kugombana juu ya kuwa Zanzibar ni nchi au la, tuyazungumze mambo yetu katika vikao husika kwa uwazi na ukweli. Hakuna Muungano ulio kamili usiopitia misukosuko, hili linazungumzika. Kero zetu ni lazima sasa zijadiliwe kwa ukweli na uwazi bila kuoneana haya, bila kutupiana madongo, lengo letu likiwa ni kurekebisha dosari zilizopo. *Once for all.*

Mheshimiwa Spika, tusimeze ndoana na nyimbo za wasiotutakia mema, je, wananchi wetu wanasema wamechoka na Muungano? Je, kweli Muungano wetu hauna mema yaliyofanywa? Wale wanaopenda kujikweza ili waonekane wanaguswa sana na nchi kuliko wengine na kuanza maneno ya uchochezi wapuuzwe. Viongozi wahimili wa chama na wengine wachunge sana kauli zinazoweza kutuparanganya. Kama hatutaki jambo vipo vikao vya kuvizungumzia hilo jambo na si ndani ya vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, ulimi unaua, kalamu inaua kuliko kisu, tujihadhari tusije tukaharibikiwa, kero za Muungano zitatuliwe kimatendo.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ushirikiano mwema na kuwasilisha Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Muungano ni mzuri kwa nchi zilizoungana lakini naiomba Serikali kuzingatia vizuri masharti, mikataba na mambo mengine yanayotaka kuharibu Muungano kwa hiyo, mikakati iwepo ya kumaliza baadhi ya kero ya Muungano, pia kuwe na mipango ya ziada ya ulinzi na usalama kwenye Muungno huu wa Serikali mbili, Zanzibar na Tanganyika na Zanzibar iwe mamlaka kamili. Serikali yake na baadhi ya sheria zimepitwa na wakati ziangaliwe upya kwa faida ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna matatizo ya biashara ndani ya nchi zetu Zanzibar na Tanzania Bara wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla hulalamika kuwa wanasumbuliwa kibiashara, wanapofanya biashara zao wanapofika bandarini Dar es Salaam na *TRA*, polisi na wengine. Naiomba Serikali yasiwepo na yasimamiwe kuondoa manung'uniko na tofauti, isiwepo ili kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi mwenyewe, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa hotuba yake ambayo lau kama dhamira ya yale aliyoyaandika yanatekelezwa basi haya yanayotokea leo ya malumbano kuhusu Muungano wetu, yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, mara tunapozungumza Muungano ni kwa nia ya kuboresha na sio kuuvunja kama vile wengine wanavyodhani na ndio maana tunayataja yale yanayoonekana kuwa ni kero na kasoro za Muungano wetu. Mfano, kodi ya mapato na ushauri wa forodha ni shughuli za Muungano kwa hiyo mwenye mamlaka maalum kutangaza kodi hizo, kushusha, kupandisha au kusamehe ni Waziri wa Fedha wa Muungano yule tunayemwita Waziri wa Fedha wa Zanzibar hana mamlaka wala uwezo

huo. Waziri wa Fedha za Zanzibar alipeleka Muswada kwenye Baraza la Wawakilishi kule Pemba lilizuiwa usijadiliwe na haukujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, madini si shughuli ya Muungano lakini *petrolium* ni shughuli ya Muungano, hii ni wazi kwamba chetu ni chetu lakini chako pia ni chetu. Tamaa ya kupatikana petroli Zanzibar ipo, lakini tamaa ya kupatikana madini haipo. Madini ni mali ya Tanzania Bara ambayo imo ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Petroli ikipatikana Zanzibar ni mali ya Muungano si ya Zanzibar pekee. Je, hivi si vichekesho? Lakini hivi ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kuwa Zanzibar ina hadhi mbili *(status)* kwenye vyombo vya Muungano. Moja ni kwenye vyombo ambavyo iliingia kwa kutoa mchango au hisa mbalimbali ya mchango wa Serikali ya Muungano wenyewe. Mfano Benki Kuu ya Tanzania na *Air Tanzania Cor-oporation (ATC),* kuna vyombo vya Muungano ambavyo Zanzibar ni *shareholder by virtue of being partner in the Union,* mfano Benki ya Taifa ya Biashara *(NMB)* na *Tanzania Port Authourity (TPA)* nilichosema ni kwamba *dividends* za vyombo ambavyo Zanzibar imechangia kama Zanzibar basi Zanzibar inapaswa na ina haki ya kupata fungu lake ama vyombo ambavyo Zanzibar ni *shareholder* kwa kuwa ni *partner* tu kwenye Muungano basi *dividends* ziende kwenye Serikali ya Muungano kuhudumia vyombo vya Muungano.

Mheshimiwa Spika, migongano *(confusion)* kama hii imesababishwa na kutokuwepo kwa Serikali ya Tanganyika/Tanzania Bara kama ilivyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kusema Tanzania Bara imo ndani ya Serikali ya Muungano ni kubabaisha mambo kama Serikali ya Tanzania Bara imo kwenye Serikali ya Muungano, je, Serikali ya Zanzibar haimo kwenye Muungano? Ni nani *partner* kwenye Muungano huu? Ni vyema Serikali tatu zikiwekwa wazi ili kila Serikali ikashughulikia mambo yake wenyewe na yale ya Muungano yakashughulikiwa na Serikali ya Muungano. Hivi tumesahau kwamba tulikuwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Waziri wakati kila nchi ilikuwa na Mabunge yake na Mawaziri wake? Kulikoni?

Mheshimiwa Spika, hayo mengine mengi yanafaa kuangaliwa na kufanyiwa marekebisho kwa nia ile ile ya kuboresha na kudumisha Muungano wetu. Nakutakia heri katika kuboresha Muungano wetu.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima mimi pamoja na Wabunge wote tuliohudhuria kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kazi nzuri wanayoifanya katika ofisi hii. Aidha, niwapongeze watendaji wote kwa ushirikiano mzuri waliokuwa nao na kukamilisha kitabu cha Bajeti kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nina mchango mdogo tu unaohusu Muungano. Muungano wetu ni mzuri sana na wakupigiwa mfano ndani na nje ya nchi. Muungano wetu huu

umeleta udugu na kumuwezesha Mtanzania kuishi popote anapopenda kati ya Bara na Visiwani na kusababisha Muungano wa kidamu kati ya wananchi wake (wameoleana).

Mheshimiwa Spika, Muungano huu unapendwa sana licha ya kasoro ndogo ndogo zinazoonekana kuwa ni kero za Muungano. Mheshimiwa Waziri amesema kasoro hizo zitamalizika kwa njia ya vikao (mazungumzo) nakubaliana naye, lakini ni muda mrefu sasa mazungumzo hayo tunaelezwa yanaendelea bila kuarifiwa ni yapi yamepatikana ufumbuzi na ufumbuzi wake uko vipi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuhakikisha mazungumzo hayo yanafanyika kwa haraka na kutolea uamuzi yale yaliyokubaliwa kwa sababu yale yote yanayozungumzwa kuwa ni kero hakuna lisilowezekana kupatiwa uamuzi na kila tukichelewa kutoa uamuzi Serikali ndiyo inayokaribisha malumbano na kuwapa njia wale wasioutakia kheri Muungano kwa kuuchafua na kuonekana Muungano haufai na unaendeshwa kiubabaishaji na kudhulumu upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwaenzi waasisi wa Muungano na kuwaenzi kwetu ni kudumisha Muungano waliotuachia, pale ambapo pameonekana pana tatizo tuwe wepesi kutatua tatizo kwani waswahili wanasema mzarau la mkuu huvunjika guu, pia mtemewa mate na wengi mwisho hulowa. Idumu Tanzania na udumu Muungano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI**: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuchangia japo kidogo juu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ambao ulizaa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa umeshatimia takriban miaka 44. Lakini bado tunazo kero nyingi ambazo hado hazijatatuliwa pamoja na kwamba tunaambiwa vikao vinakaliwa na kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninajiuliza hivi hivyo vikao vinavyokaa huwa vinafanya nini? Je, ni kero ngapi mpaka Juni, 2008 tayari zimeshatatuliwa?

Mheshimiwa Spika, mimi mawazo yangu naona kero kubwa ya Muungano ni muundo wa Muungano wenyewe, vipi utakuwa na Serikali ya Zanzibar ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano lakini Serikali ya Tanganyika haipo? Haipo kimaandishi tu, bali ipo imejificha ndani ya Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali ya Jamhuri ya Muungano inachangiwa na nani katika kujiendesha? Kama wadau wakubwa wa Muungano huu ni Zanzibar na Tanganyika na kama Zanzibar inachangia mambo ya Muungano, je, ni kwa namna gani na yule mdau wa pili anachangia maendeleo ya Serikali ya Muungano ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu kwa kuwa malalamiko na kero za Muungano zimekuwa nyingi na zinaongezeka kila kukicha, suluhu inayofaa wa kadhia hizi zote ni kuwa na Muugano wa mfumo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Spika, inajulikana kwamba katika mkataba wa awali kwa Muungano ulikuwa na mambo kumi na moja tu (hati 11 za Muungano) lakini sasa yamefikia 22 hii ni utaratibu gani unaotumika kwa kuongeza mambo hayo ya Muungano? Je, Serikali haijui kwamba kadri mambo hayo ya Muungano yanavyoongezeka ndivyo zinavyoongezeka kero za Muungano?

Mheshimiwa Spika, Mungu Ibariki Zanzibar, Ibariki Tanzania. Ahsante sana.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, siasa za leo ni za kiuchumi zaidi baina ya nchi na nchi, Muugano wa hiari pekee kwa dunia ya leo haufai. Kwa vile Muungano wetu wa nchi mbili umeifanya nchi moja iwe inategemea kupata ruzuku kutoka Serikali nyingine baada ya kupewa mamlaka Serikali hiyo kujitafutia misaada na mikopo ipo haja ya kuuangalia upya Muungano huu. Njia itakayofanya Zanzibar nayo kupata misaada na mikopo moja kwa moja ni kuwa na Serikali tatu.

Mheshimiwa Spika, yale malalamiko juu ya Muungano kwa kuwa ni Serikali tatu yatakuwa hayapo. Leo hii Muungano huu umetufikisha hata kama Tanzania hupoteza nguvu za maamuzi kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki pale Zanzibar hukosa kuwa mwanajumuia wa Afrika ya Mashariki. Kama Zanzibar ilikuwa mwanachama wa Afrika ya Mashariki. Tanzania ingekuwa na Wabunge 18 hivyo kweli Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Tanzania ingapoteza nini.

Mheshimiwa Spika, nadhani umefika wakati Muungano wetu tuuangalie kwa kufanikisha kuongezeka uchumi wa nchi haraka badala ya kuendelea na utashi wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ni miaka mingi majadiliano ya mgawanyo na mchango kwa Serikali ya Muungano haujapata maamuzi wakati mgawanyo wa mapato yatokanayo na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia maamuzi yake yatafikiwa Desemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri utendaji wa aina hii hauimarishi Muungano na pengine utendaji wa aina hiyo umetokea kwa sababu Zanzibar ndio inayolalamika juu ya ugavi wa asilimia 4.5 na pengine ingekuwa ni Tanzania Bara inayolalamika basi suala hilo la mgawanyo wa fedha za misaada na kutoka na vyanzo vingine vya mapato labda lingalkishapatiwa ufumbuzi.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA**: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara hii kwa utumishi wake uliotukuka kwa heshima kubwa viongozi wake wa juu katika ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuupongeza Muungano wetu tangu uasisiwe una historia ya aina yake kwa Afrika na pia ni kielelezo kizuri katika ustawi wa mshikamano kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu chochote kizuri ambacho kitakuwa hakina msongo wa upinzani hasa ukizingatia upande mmoja wa Muungano ulipatikana kwa Mapinduzi. Hivyo ikumbukwe waliopinduliwa hawapo radhi kuondoka katika ufalme na hata vizazi vyao haviridhiki na hilo, hivyo kupelekea ama wao ama kuwatumia vibaraka vyao kuona kwamba maelezo ya matakwa yao yanaendelezwa kwa hila za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi naomba sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano lazima isimame kidete kusimamia wosia wa viongozi wetu waasisi yaendelezwe, hapa ninachoona mimi wapo watu wanaolalamikia kwa sababu mbalimbali ambazo baadhi yake hazina sababu  za msingi ila kinachotakiwa hapa ni kuchosha Serikali ya Jamhuri ili iachane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivyo kutoa mwanya kwa maadui wa Muungano, hivyo mimi bado nakubaliana na mawazo ya waasisi wetu Rais atakayechaguliwa lazima awe ana uchungu wa Muungano kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa yapo malumbano ambayo kimsingi yamo ndani ya maadili ambayo kila kiongozi anapaswa awe nayo kwa 99% hivyo kimsingi kabla ya kuongea lolote                inatakiwa kuzingatia mapema kabla ya kuleta utata, athari na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mfano Mheshimiwa Waziri Mkuu katika nchi hii ni mmoja tu ambaye anastahili heshima yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakosolewa kwa *style* ya aina yake hata atakapokosea kibinadamu.  Lakini pia ieleweke kwamba Zanzibar kama Serikali na ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Waziri Mkuu hastahili kubezwa au kuonekana hana mamlaka yoyote kwa upande wa pili wa Muungano hilo si sahihi kwani kwa busara za kawaida ana sauti ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mfano, sisi Wabunge wa Zanzibar ndani ya majimbo yetu wapo Wawakilishi wa Baraza  lakini kimaadili mimi Mbunge nitakuwa na *style* yangu ya uzito kwa sababu uwakilishi wangu ni mzito kwa sababu natumikia Jamhuri ya Muungano kwa maana mchango wangu hauna mipaka ndani ya Jamhuri, kwa

fursa hii nampongeza Mheshimiwa Spika, kutoa maelekezo ya ziada ndani ya Bunge kwamba Mbunge yeyote ajibiwe kadri ya atakavyohoji ndani ya Serikali ya Jamhuri, wakati mimi nilivyohoji kutaka kujua shamba la Zanzibar ambalo lipo Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, mazingira katika nchi yetu ni suala muhimu sana, ukizingatia dunia nzima inaweka mkazo katika suala hili mimi mchango wangu ningeomba ziundwe mamlaka zaidi za kusimamia mazingira kwa kuyaboresha kwani suala la mazingira zaidi limo vijijini ambako pengine elimu ni ndogo kwa wananchi wetu, mfano bado watu wengi vijijini wanaamini kutia moto ndio njia sahihi ya kusafisha mashamba au kuzuia kuongezeka kwa bahari ni dhambi na kadhalika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumehitimisha michango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge; ni wakati ambapo Mawaziri watapitia hoja zenu moja baada ya nyingine na nikumbushe tu kwamba, tuna Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wawili; mmoja sasa anashughulikia masuala ya Mazingira na mwingine anashughulikia masuala ya Muungano. Wenyewe walivyopanga kwa dakika zao hizi 75, atatangulia Mheshimiwa Dr. Burian kwa dakika 45 halafu atahitimisha Mheshimiwa Muhammed Seif kwa dakika 30. Kwa hiyo, namwita sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ambaye kwa taarifa yenu, yeye anatoka Arusha lakini kaolewa Zanzibar. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nianze kwa shukrani. Shukrani za kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai na afya njema na kuniwezesha mimi kusimama hapa leo kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Kwa mara nyingine tena, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu na kwa kunikabidhi jukumu la kusimamia masuala ya mazingira chini ya Makamu wa Rais. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa uongozi wake, maelekezo na kwa hazina kubwa ya hekima ambayo nimekuwa nikiichota kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nihusiane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kunipa nguvu katika kazi yangu na hasa ninapotoa mapendekezo ya maeneo ya utekelezaji na ufuatiliaji katika sekta nyingine nje ya sekta yangu. Naomba pia nimshukuru aliyekuwa Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam, kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuniachia misingi mizuri ya kuiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuishukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Job Ndugai, kwa ushirikiano wao mkubwa na kwa maoni na michango ya msingi ambayo kwa kiasi kikubwa tumeizingatia katika mipango ya bajeti hii. Napenda nimpongeze shemeji yangu, Mheshimiwa Ali Seif Salum, kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Waziri Kivuli, Mazingira na ninapenda nimhakikishie ushirikiano wangu katika kazi hii. Aidha, namshukuru kwa

michango mizuri na mapendekezo aliyowasilisha kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati ya moyo wangu, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na Wabunge wote kwa ujumla, kwa ushirikiano wenu mkubwa mlionipatia katika kipindi chote cha takriban mwaka mmoja ambao nimekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, nikishughulikia masuala ya Bunge. Mlifanya kazi yangu ngumu na nzito nikaiona nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitatenda haki kama sitamshukuru kwa dhati ya moyo yangu, Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Ngoyayi Lowassa, kwa kuniongoza na kuniimarisha kiutendaji katika kipindi chote nikiwa Waziri wa Nchi, chini ya Ofisi yake. Naomba niseme kwa ninyi nyote kwamba, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kufuatia mapenzi na heshima kubwa waliyonipa akina mama wa Mkoa wa Arusha. Naomba niwashukuru na niwahakikishie kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa hali na mali. Lengo ni kuunga mkono jitihada za akina mama hawa katika kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuhitimisha salamu hizi kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Nafasi hii imeiongezea heshima nchi yetu na hata sisi Mawaziri tunapokuwa katika mikutano ya kimataifa, wenzetu wa Afrika hutupa heshima ya kuwa Wenyeviti katika kokasi za Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Nimalizie kwa kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa *CPA.* Nafasi hii imezidi kuipa chati nchi yetu. Baada ya pongezi hizi, naomba kwa masikitiko makubwa, nitoe salamu zangu za pole kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, kufuatia kipo cha Mheshimiwa Levi Mwanawasa, aliyekuwa Rais wa Zambia. Ama kweli Bara la Afrika limempoteza kiongozi shujaa na mwadilifu. Salamu zangu za pole pia ni kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Waziri Kivuli wa Mazingira. Alinipa ushirikiano mkubwa na kwa kweli tulikubaliana katika maeneo mengi. Naomba Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema Peponi. Amina.

Natomba nitoe pole kwa familia ya ndugu yangu, Mheshimiwa Ismaili Ali Kaole, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Kaloleni, Manispaa ya Arusha, ambaye amezikwa jioni hii ya leo baada ya kufariki juzi kwa matatizo ya moyo. Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya mpendwa wetu huyu mahali pema peponi. Natoa pole kwa familia za Wabunge wote waliotangulia mbele ya haki na kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu na jamaa, nawaombea wote hao waliotutangulia mbele za haki, pepo ya Manani. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

**SPIKA:** Huoni Mheshimiwa Waziri, ingekuwa vyema ukamshukuru mumeo ambaye… *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nilipanga nimalizie kwa hilo, lakini kwa vile umenipa fursa hii, naomba basi kwa dhati ya moyo wangu, nimshukuru mume wangu, Bwana Othuman Masoud Othuman, ambaye ni Mkurugenzi wa Upelelezi wa Zanzibar, kwa uvumilivu mkubwa na kunitia moyo katika kazi yangu. Kwa hiyo, mashemeji zangu wote wa Zanzibar, Pemba, mimi suala la Muungano sitaki kulizungumzia, kwa sababu nalipenda na tayari kuna muungano umeshaunganika na hivyo msinitafutie kurudi tena Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba sasa nijibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Hoja hii ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, masuala ya Mazingira, ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wapatao 42. Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja atawataja wote kwa ujumla. Hata hivyo, mimi nitawatambua tu kila nitakapokuwa najibu hoja zao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mazingira ni uwanja mpana sana, ambao umejielekeza katika maeneo yanayomzunguka binadamu. Kwa hiyo, unazungumzia masuala ya ardhi, maji kwa maana ya bahari, maziwa, mito, mabwawa, pamoja na viumbe vilivyomo mle ndani. Lakini pia tunazungumzia rasilimali ya asili kama vile misitu, ukijumlisha wanyama, wadudu na mimea. Hewa na maeneo ya makazi ya binadamu. Kwa hiyo, kimsingi sekta yoyote ile haiwezi kusema kwamba, haihusiki na masuala ya mazingira na hivyo usimamizi na udhibiti hauwezi ukaachiwa tu Ofisi yetu hii na Baraza la Mazingira. Kwa kutambua dhana hii nzima ya Sekta ya Mazingira kama sekta mtambuka, ndiyo maana basi kila sekta sasa hivi imeanzisha dawati na kuteua Afisa Mazingira kama ilivyo katika masuala ya UKIMWI na Jinsia.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ameshauri kuwa, kuna haja ya kutumia taratibu mbalimbali za ushawishi kama kampeni tunazozifanya wakati wa uchaguzi ili kuleta ushindi. Tuzitumie kufanya jamii iwe na uchungu wa hali ya uchafu wa mazingira na kuweza kudhibiti hali hiyo. Mimi nakubaliana kabisa na suala hili na ndiyo maana CCM imeweka katika Ilani yake, umuhimu wa mazingira na mikakati ya kuchukua na ndiyo maana masuala yote ya mazingira yamewekwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile ndiyo maana Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge jipya, pamoja na mambo mengine, alisisitiza sana umuhimu wa masuala ya mazingira na mazingira imeendelea kuwa ni ajenda muhimu kwa viongozi wote wa Serikali. Hivyo basi, naomba wenzangu wa Kambi ya Upinzani tushirikiane kwa hili.

Mheshimiwa Spika, tubishane kwa sera na itikadi, lakini tuungane kwenye hili la mazingira, kwani ni mustakabali wetu sisi wenyewe na vizazi vyetu vijavyo na hii ndiyo dhana nzima ya maendeleo endelevu. Mimi nawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote, nitatoa ushirikiano wangu kikamilifu, nitawashirikisha katika masuala mbalimbali na kupitia kuwasilisha bajeti hii, ninawaagiza Wataalam wangu pale wanapofanya semina na warsha mbalimbali katika Halmashauri, waweze kuwahusisha Waheshimiwa Wabunge katika semina hizo. Pia kuwe na uwakilishi unaolingana na Waheshimiwa Madiwani, kufuatana na bajeti ile ambayo itapangwa. Viongozi hawa wa siasa wana

umuhimu wa kipekee katika kupeleka ajenda nzima hii ya mazingira kueleweka. Ajenda hii ya mazingira inaweza kuwa ni ya kudumu tu kama Wabunge watashirikishwa na ni kupitia maswali mtakayotoa Waheshimiwa Wabunge na kupitia mikataba itakayopitishwa hapa Bungeni. Zaidi ni kupitia katika kubana sekta zote zinazohusika katika masuala ya mazingira na kuyahoji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilitegemea suala la mazingira lingeweza kujitokeza wakati wa bajeti zile zilizokwishapita, lakini bahati tulisubiriwa kuja kutoa suala hili la mazingira. Sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, niwakumbushe tu Mheshimiwa Rais alipokuwa akitoa hotuba ya uzinduzi wa Bunge tarehe 30 Desemba, 2005, alitoa maagizo tisa ya msingi. Kwa ruhusa yako na kwa faida ya jamii, naomba niyataje maagizo hayo tisa:-

"Kwanza, kila kijiji kipande miti katika vyanzo vya maji. Pili, Wizara ya Ujenzi ihakikishe miti inapandwa pembeni mwa barabara na katika maeneo ya karibu na daraja. Tatu, Wizara yenye dhamana ya Maliasili, iweke utaratibu mzuri utakaofuatilia na unaopimika upandaji wa miti na majani. Wizara ya Ardhi, ihakikishe machimbo ya michanga na kokoto hayapo katika maeneo karibu na vyanzo vya maji na katika mabonde. Wizara ya Madini ihakikishe inasimamia vizuri na kutoa taarifa ya kila mara ya maeneo yote ya machimbo ya madini ili kufuatilia na kujihakikishia kuwa, wachimbaji wale wanazingatia matakwa ya leseni zao lakini hasa masharti ya mazingira.

Sita, wananchi wanaoishi katika maeneo yenye viwango vizuri vya kutosha vya mvua, waongeze bidii na kasi ya kupanda miti. Saba, Wizara yetu sasa yenye dhamana ya mazingira iandae ripoti ya kila mwaka kuhusu hali ya mazingira nchini, kujumlisha mafanikio na changamoto. Nane, Halmashauri za Miji, Manispaa na Miji, zitekeleze kwa vitendo agizo la siku nyingi la kupanda miti ya vivuli na matunda.

Mheshimiwa Spika, tisa, watu binafsi, mmoja mmoja au katika kikundi, waanzishe kampeni ya kupanda miti kama zao la biashara."

Lengo la kunukuu maagizo haya ya Mheshimiwa Rais katika majuisho yangu ni kutoa tu picha ili tuweze kukumbushana na kutambua ni makundi gani yaliyopo katika uwajibikaji wa masuala mazima ya mazingira. Bahati mbaya tu bajeti hii imekuja mwisho, baada ya Wizara husika kuweza kuwasilisha. Nategemea Waheshimiwa Wabunge, tutashirikiana kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba, suala hili la mazingira halitasubiri tu Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini tunaweza kuuliza masuala ya mazingira katika sekta zote pale zinapowasilisha bajeti zao na pale tutakapokuwa tunafanya mapitio ya utekelezaji katika kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpanda, alitueleza umuhimu wa masuala ya elimu na masuala ya mabadiliko ya tabia nchi. Hili liliungwa mkono na Mheshimiwa Bujiku Sakila katika mchango wake wa maandishi aliposema kuwa, wananchi wengi wanadhani mazingira ni masuala ya kuondoa uchafu tu. Masuala haya katika nchi nyingi sasa hivi hayazungumzwi tena; ni masuala ambayo tayari yamehusishwa katika kazi za

siku hadi siku za utekelezaji katika Halmashauri ya Miji na Majiji. Kwa hiyo na sisi tupo katika jitihada za kuongeza weledi na kuongeza elimu ya masuala mazima ya mazingira ili masuala ya mazingira yafanywe kwa ushirikiano mkubwa na Wizara yenye dhamana ya mazingira, tutabaki kama wasimamizi wa sera. Mikakati ya kitaifa na mikataba na masuala mazima ya usimamizi na udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja mbalimbali zilizowasilishwa, nianze tu kwa kukiri kwamba, hata kama nitapenda sitaweza kutokana na ufinyu wa muda kuweza kupitia hoja zote kwa ukamilifu wake. Nipitie tu sasa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Suala kubwa lililojitokeza katika hoja ya Kamati ni kwamba, ipo haja ya kutoa maana halisi ya chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa na kwanza niseme tu mimi nakushukuru kwa kunipa Kamati ambayo ina Wataalam waliobobea. Kamati ile imesheheni wataalam wa masuala mazima ya mazingira katika nyanja mbalimbali na wamekuwa na mchango mkubwa sana katika Ofisi yetu. Sasa chanzo cha maji kama tunavyoelewa kwanza, kuna tofauti ya chanzo cha maji kwa maana ya *water source,* lakini kuna chanzo cha maji kinachotambulika kwa maana ya *water catchment* au *water shade.* Sasa kutokana na ufinyu wa maneno yetu ya Kiswahili, maneno hayo yote mawili ambayo yapo kwa Lugha ya Kiingereza, kwa Kiswahili tunatumia kama neno moja.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tumeamua kwamba, chanzo cha maji kwa maana ya *water catchment* tuseme ni eneo la bonde na chanzo cha maji kwa maana ya *water source* ibaki kama chanzo cha maji. Kwa hiyo basi, nitoe maelezo kwamba, hii ni sehemu au mahali penye rasilimali ya maji katika uasili wake, ambayo yanaweza yakachukuliwa kwa matumizi mbalimbali ya jamii na maendeleo kwa ujumla. Unaweza ukapata maji haya kwa njia ya kuchepua, njia ya kukinga, njia ya kutega, kuchimba, kuelekeza na kuvuta kwa pampu. Kwa hiyo, kuna aina nyingi ya vyanzo vya maji, yaani *water source* kama vile visima, chemchemi, vijito, miti na malambo. Pia kuna *water source* ile kwa maana ya eneo ambalo ni la mabonde, linalokuwa linatusaidia katika upatikanaji wa maji hayo. Sasa unaweza ukasema kwa nini kwa mfano, Mradi wa *Nile River Basine* ambao una maji ndiyo chanzo cha maji cha Ziwa Victoria, lakini unaambiwa kwamba *catchment area* yake inafika mpaka DRC, Congo, inafika mpaka Burundi, Rwanda, Ethiopia na maeneo mpaka ya Sudan, Tanzania? Kwa hiyo, eneo la *catchment* linakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilieleza kwamba, Serikali iharakishe mchakato wa kuweza kutekeleza Mradi wa *Lake Tanganyika.* Sisi tunasema, kama mtatujalia tukapitisha bajeti yetu leo, basi mradi utaanza, kwa sababu tulikuwa tunasubiri tupate dola za kimarekani 300,000 tulizoweka kwenye mpango ili tuweze kuutekeleza Mradi huo. Vile vile mmetuambia kwamba, kuna matatizo ya uharibifu wa mazingira unaotokana na chumvi ya Uvinza. Ni kweli kabisa kiwanda hiki cha Chumvi, kinatumia miti mingi katika kutengeneza chumvi. Katika ufuatiliaji tulioufanya, tumeona kwamba waweke mikakati ya mazingira wa uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Kwa hiyo, Ofisi yetu ilikutana na Uongozi wa Kiwanda na kuelekeza kubuni nishati mbadala. Kiwanda kimeanza matumizi ya nishati ya jua. Hata hivyo, mkakati unaendelea ili hatimaye wapande mashamba ya miti na akishindwa kufanya hivyo aweze

kupata kibali cha kukata miti. Tunafuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba, tunaweka sasa *time table* ya kuweza kuhakikisha anafuata kama ilivyokusudiwa, lakini kuna suala zima la matumizi ya makaa ya mawe. Hii ni sera yetu na ipo katika Ilani yetu ya uchaguzi. Sisi katika bajeti hii tumesema kwamba, mwaka huu ndiyo mwisho. Tutashirikiana na Waziri anayeshughulika na masuala ya Sayansi na Teknolojia, kwa sababu tafiti hizi zinafanywa na watu wake wa COSTECH kuhakikisha kwamba, tafiti zinakuwa wazi na zinaweza kuwafikia wananchi na kuweza sasa kutumika.

Mara ya mwisho, tafiti zilionyesha kwamba, makaa yale ya kupikia yalikuwa yanawaka kwa muda mrefu zaidi ya saa mbili. Moto wake ulikuwa ni mkali sana wa kuweza hata kuunguza sufuria na pia kulikuwa kuna aina fulani ya gesi chafu ambayo ilikuwa inatoka na ilikadiriwa kwamba, ingeweza kuwa na athari kwa binadamu kwa masuala ya kansa na kadhalika. Sasa hivi wanafanya tafiti za mwisho ili kuona jinsi gani wanaweza kurekebisha na wanaangalia yale makaa ya mawe ambayo tayari mkaa umekwishatengenezwa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu makubwa kwamba, sasa hivi hizi tafiti zinaweza kuwa nzuri na kuweza kutumika kwenye programu hii.

Wabunge wengi wamezungmzia masuala ya uoto wa asili na sisi tumesema tuna mikakati ya makusudi na ni utekelezaji wa mkakati wetu, lakini pia ni utekelezaji wa malengo ya milenia katika lengo la saba la kuhakikisha kwamba, tunapunguza uharibifu. Kulikuwa kuna masuala mazima ya umuhimu wa *environmental impact assessment.* Kikubwa kilichozungumziwa ni suala la uwekezaji katika Ziwa Natron. Napenda tu niseme kwamba, Serikali haijatoa idhini ya uwekezaji huo kuanza, idhini iliyotolewa ni ya kiwanda kuweza kufanya tathmini ya athari ya mazingira. Hata hivyo, sisi wenyewe kwa kujiridhisha tumemteua Mtaalam Mwekezaji mzalendo, ambaye atafanya tathmini ya kuweza kujua athari ya mradi ule kwa maana ya kuangalia ekolojia ya maji na *chemistry* ya ziwa lile.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililojitokeza lilikuwa ni suala la *NEMC*, kuweza kuwa na Ofisi za Kanda na sisi tayari tumeshasema tuna Ofisi za Kanda Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza. Lengo ni kuweza kuifikia nchi nzima na tutaweza kufikia hivyo kwa kuwa na wale Maafisa Mazingira ambao sasa hivi ni wajibu kila Halmashauri kuwa na Afisa Mazingira. Moja ya vipengele ambavyo tutavizuia katika utumiaji wa fedha zile za mpango endelevu wa mazingira ya miji ni kuhakikisha kwamba, wanakuwa na Afisa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilizungumzia mambo mengi ambayo yanalingana na yale ya Kamati. Moja lililokuwa limezungumzwa ni suala zima la umuhimu wa kuwa na hati zile za tathmini ya mazingira katika maeneo na kuweza kuepusha uchafuzi unaotokana na viwanda vya saruji. Niseme tu kwamba, tathmini imekwishafanyika katika maeneo yale na tumeelekeza maeneo ya kurekebisha na tutaendelea kuwaelekeza zaidi ili kuepusha madhara hayo.

Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, alizungumzia masuala mengi muhimu na ninampongeza sana kwa sababu amekuwa ni mwanamazingira wa mfano katika Bunge

hili na amekuwa akichangia masuala ya mazingira katika bajeti za Wizara mbalimbali. Naomba nimhakikishie suala zima la *UDEM* kuweza kufanyika katika Halmashauri yake. Tumesema tutalizingatia, tutatumia programu yetu ile ya *UDEM* kumwezesha awe na *environmental profile* kwa eneo la Ludewa. Nimweleze tu kwamba, tulikuwa na mazungumzo naye kuhusu uanzishwaji wa programu endelevu ya Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa. Mwingine aliyechangia programu hii ni Mheshimiwa Dr. Luca Siyame na mimi niwaleze kwamba, Waheshimiwa Wabunge, kufuatia mazungumzo yangu niliyofanya na Mwakilishi wa Benki ya Dunia, tumekubaliana kimsingi kwamba, watafadhili mradi endelevu kwa maana ya *catchment* kwa ajili ya kusaidia bonde lile lisiendelee kuharibika.

Hatua ya ziada kwa maana ya kuwasaidia wavuvi na programu nyingine zitafuatia baada ya kukamilisha matatizo ya mpaka ambayo tunayo kati yetu sisi na nchi ya Malawi na Mozambique. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya utekelezaji wa mradi hatimaye tumefanikiwa kupata ufadhili. Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda alituambia kuna umuhimu wa kuwa na mradi katika Ziwa Rukwa, hasa kufuatia mabadiliko makubwa ya tabia nchi ambayo imeathiri ziwa lile. Napenda kumweleza Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda kwamba, sasa hivi tuna mkakati wa kitaifa wa uhifadhi wa ukanda wa pwani, bahari, maziwa, mito na mabwawa na katika moja ya mambo ambayo tutayaangalia ni ziwa hili la Rukwa. Sisi tutaangalia uwezekano wa Benki ya Dunia kuongeza ufadhili wake kutoka kufadhili Ziwa Nyasa lakini pia kufadhili Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia masuala mbalimbali ni Mheshimiwa Savelina Mwijage, ambaye alielezea kuhusu magugu ya Ziwa Victoria. Nimweleze tu ya kwamba, suala hili bado linaendelea kushughulikiwa na mradi huu sasa hivi upo chini ya Wizara ya Maji na Mipango ya Usafi na Uondoaji wa Magugu unafanyika.

Mheshimiwa Dr. Mlingwa, alizungumzia kuhusu uboreshaji wa mazingira mijini. Kimsingi tumezungumza na Waziri anayeshughulikia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani, kuhusu matumizi ya fedha zile za kuendeleza mazingira ya mijini. Moja ya eneo ni katika kuendeleza bustani zetu mijini. Tumekubaliana kwamba, *botanic garden* ni eneo muhimu. Kwa hiyo, fedha hizo katika Manispaa ya Shinyanga Mjini, mimi nashauri kwamba zielekezwe ili kutekeleza ombi hilo la Mheshimiwa Mbunge la kuanzisha bustani katika maeneo yaliyopangwa na maeneo mengine ya mazingira ambayo yanakusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, ambaye alielezea kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mito katika vyanzo vya maji na kuangalia uwezekano wa kuvuna miti ya mikaratusi ambayo ipo katika maeneo hayo ya vyanzo vya maji. Sisi tunasema tutashirikiana na Wizara inayoshughulika na Maliasili na Utalii, kwa maana ya kuja kufanya maelekezo katika maeneo hayo ambayo yana miti. Tuseme kwamba, miti ya mikaratusi siyo yote ina athari. Kuna aina ya miti ambayo haina madhara na kuna aina ya miti ambayo ina madhara. Kwa hiyo, tutashirikiana na wataalam waweze kuyafuatilia hayo.

Niseme tu kwamba, mara nyingi shughuli kama hizi zinapofanywa, watu wanaona kwamba sasa wamepata mwanya. Uvamizi katika eneo lile la misitu ya Shengena pamoja na mambo mengine; watu wanasema kwamba, kumegundulika dhahabu na kadhalika. Chanzo kilichoanzia ni baada ya kutoa idhini ya kwenda kuvuna miti hiyo ya mikaratusi kwa maana ya kwamba, ilikuwa athari kwa mazingira. Kwa hiyo, baada ya pale maeneo yakaanza kukatwa zaidi na zaidi na kabla ya kumaliza hoja hii, nitatoa kauli kufuatia kitendo hicho kinachoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mbunge wa Kibiti. Mimi nasema sisi tutashirikiana na vikundi vyote vya kijamii na *NGOs* ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika mazingira. Tutashirikiana nao kupitia kuwawezesha, kupata uelewa wa kuandika miradi midogo midogo kwa ajili ya kupata ufadhili wa *GF* na kupitia fedha za *UNDP*. Tutaangalia pia suala zima hili la *Ramsar Site* ya eneo ambalo anatoka ili kuweza kuboresha zaidi. Mimi nimesema kwamba, nimepanga kuja kutembelea maeneo hayo na ni katika hatua nzima ya kuanza utekelezaji wa mkakati wetu wa uhifadhi wa ukanda wa pwani, maziwa, bahari, mito na mabwawa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, tupange mikakati ya jinsi gani basi mimi na yeye tutaweza kuongozana kwenda huko Kibiti.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la Mheshimiwa Mosi Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kuhusu muundo mzima wa usimamizi wa mazingira. Hili nimesema kwamba, sasa hivi kutakuwa na Maafisa Mazingira ambao ndiyo watakuwa wasimamizi wa mazingira. Kutakuwa na mtaalam wa usimamizi wa mazingira katika Mkoa, ambaye atakuwa na wajibu wa kuzishauri Serikali za Mitaa kuhusu masuala mazima ya mazingira na hili limezungimzwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Profesa Idri Ali Mtulia, Mbunge wa Rujifi na wote hao niseme kwamba, mikakati ipo na kutakuwa na hao wataalam kutoka ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid, Mbunge wa Wawi naye alizungumzia masuala mazima ya kuweza kuangalia teknolojia rahisi ya kuweza kutumika katika maeneo ya viwanda. Sisi tumesema tutashirikiana naye katika masuala haya na kama tulivyosema, tunatoa wito kwamba watu waachane na matumizi ya kuni ama wawe na mashamba ya kuni, vinginevyo wafuate teknolojia ambayo ni rahisi inayoweza kutumika. Hizo teknolojia sasa hivi zipo.

Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, ametupa ushauri mzuri kwamba,katika moja ya mikakati sasa hivi tuangalie pia jinsi ya kuweza kupata mafunzo ya *river training*, pamoja na kuangalia masuala ya mafuriko. Sisi tumesema hilo tutalifuatilia na katika moja ya semina na warsha tutakazozifanya, tutahusisha maeneo hayo. Ni kweli kwamba, Bonde la Mto Kilombero ni *Ramsar Site* na linatakiwa liwe na mpango wa hifadhi ya mazingira. Sisi tutafuatilia na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa sababu wao ndiyo wanasimamia *Ramsar Site* japokuwa sisi ndiyo tunasimamia *Ramsar Convention*, ambayo ndiyo inakuwa na masuala yote ya mazingira ya *Ramsar*. Wale wanasimamia *Ramsar Site* kwa sababu yapo katika eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mariam Kasembe, amezungumzia mambo mengi sana ya msingi. Ninapenda kumshukuru, katika masuala aliyoyazungumzia kulikuwa kuna haja ya kutenga maeneo ya wafugaji ili matatizo yanayotokea Ihefu yasijirudie tena. Sisi tumesema tumejifunza kutokana na matatizo yaliyojitokeza, tutazidi kuimarisha uratibu na timu ambayo sasa hivi tunayo ya kisekta, itafanya mikakati mahususi kuona uhamishaji wa mifugo utakwenda baada ya kuwa na matayarisho ya kutosha na kuwa na mashauriano ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, alizungumzia masuala ya kuwa na Maafisa Mazingira kutoka Wizarani na Baraza kutembelea ili kuhamasisha elimu ya mazingira katika Mikoa. Sisi tunasema, tutazidi kushirikiana naye kuweza kutembelea maeneo mbalimbali kutoa hamasa zaidi kwa viongozi wetu ambao wanafanya kazi hii ya elimu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala zima la Mbunge wa Kibiti, nimeshalielezea. Mheshimiwa Dr. Siyame amezungumzia masuala ya uhifadhi kwenda mpaka eneo la Msangano. Mimi nimesema kwamba, hilo litazingatiwa. Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora, naye amezungumzia masuala ya msingi kabisa, hasa matumizi ya gesi asili. Sisi tunasema tayari *EWURA* imeshaanza tafiti na inaanza kuzungumzia matumizi ya gesi ya asili kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa magari.

Kwa hiyo, baada ya muda kutakuwa na kifaa ambacho unaweza ukanunua kwa dola kama 1,000, ambacho kingeweza kubadilishwa ili baadaye watu waweze kutumia hii. Tutashirikiana nao kuona kama hiki kitu kinaweza kikaendelezwa ili kiweze kutumia kifaa hicho. Vilevile kulikuwa kuna suala zima la uendelezaji wa mradi ule wa magadi soda, yeye alikuwa analiangalia katika maana ya maendeleo. Sisi tunakubaliana kwamba, maendeleo ni muhimu lakini pia mazingira ni muhimu zaidi. Kwa hiyo, tutashirikiana na kampuni ile watakapoleta ile tathmini yao tutaona, kama haitaturidhisha basi itabidi waangalie maeneo ambayo tutaelekeza ya kuondoa hayo maeneo kama yatakayokuwepo lakini kama itashindikana kabisa basi haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, Mbunge mwingine kutoka Kyerwa, Mheshimiwa Katagira naye alizungumzia masuala mazima ya ujangili unaofanyika katika misitu yetu. Kwa kweli suala hili tunasema tutazidi kufanya *patrol.* Ofisi yangu imeshaanza kuongea na baadhi ya mabalozi kupata helkopta kwa ajili ya kuliwezesha baraza letu kupita kufanya *surveillance* na kuangalia hali nzima ya mazingira, hasa katika maeneo ya miinuko na maeneo ambayo yana misitu minene. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba, tunafuatilia hili ili tuweze kuwa na nguvu ya kufika maeneo mbalimabli. Mheshimiwa Profesa Mtulia, amezungumzia masuala ya umuhimu wa mazingira ya nchi yetu na hasa dhana nzima ya *polluter pay.* Katika moja ya mikakati yetu tumesema kwamba, tumeanzisha nyenzo ya kiuchumi ambayo inaitwa *Economic Instrument for Environment* na hii inajengeka katika dhana nzima ya kuhakikisha kwamba, ambaye anachafua mazingira basi analipia. Nilisahau, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, alitaka kujua kama bado tunayo *baseline data.* Katika mkakati wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, zimeainishwa hatua mbalimbali za muda mfupi, muda wa kati na za muda mrefu. Hatua hizi ni kama vile

kuainisha maeneo yanayohitajika katika malambo, kutoa mafunzo kwa wafugaji na watumiaji mbalimbali, kuwaondoa wavamizi katika maeneo ya miinuko na safu za milima na kubainisha vyanzo vya maji na hali ya mazingira yake.

Kwa hiyo, kwa ujumla, baada ya kufanikiwa kupata hivi, hii inakuwa ni kama takwimu ya kwanza, lakini baada ya pale takwimu hii ndio inakwenda kujenga taarifa ya hali ya mazingira ambayo ofisi yetu inatakiwa itoe kila baada ya miaka miwili. Baada ya hapo, kila Halmashauri sasa hivi inatakiwa itengeneze kama vile ulivyoomba kwa Ludewa, basi kila Halmashauri itatengeneza *profile* yake ya mazingira na kutoka pale ndio tutakuwa na *baseline data* ambayo itaweza kutumika. Kwa hiyo, tunasema kwamba, suala hili la kufanya uperembaji ni lazima ufanyike kupitia *data* na takwimu zilizokuwepo tayari, lakini zitaimarika zaidi baada ya hizo na zote kwisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mbunge wa Kinondoni, alizungumzia suala la maeneo ya Kigogo Sambusa, ambako kumejengwa ukuta. Alitaka kujua kwa nini tunamwachia huyo muwekezaji ajenge ukuta karibu na Mto Msimbazi; Je, tathmini ya mazingira ilifanyika? Baraza lilipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Mtaa wa Kigogo Sambusa,kuhusu ujenzi huo. Sasa hatua zilizofanyika; kwanza, Baraza lilifuatilia Manispaa ya Ilala na kugundua kwamba, mjenzi mwenye ukuta huo ilikuwa ni kampuni ya KONOIKE iliyopata hati ya kumiliki kiwanja hicho mwaka 1998, wakati wa ujenzi wa Daraja la Kigogo katika eneo la Kawawa.

Baada ya kujengwa kwa daraja hilo, mto umekuwa ukipanuka na baada ya mvua hizi za *El-Nino*, ulivuka kingo zake za asili na kuingia kwenye kiwanja cha KONOIKE. Kwa hiyo, Baraza liliitisha kikao cha pamoja kati ya Uongozi wa Serikali za Mitaa wa Kigogo Sambusa na muwekezaji. Katika kikao hicho, Baraza lilikubaliana yafuatayo: Kwamba, KONOIKE isizidi kujenga ukuta wake huo zaidi ya kiwango ilichokuwa imefikia. Pili, wajenge ukuta kwenye ukingo wa mto ili kurejesha mto huo katika mkondo wake wa asili. KONOIKE wainue ukuta ulioko upande wa makazi ya wananchi ngalau kwa mita moja zaidi ili kuhakikisha kwamba, maji ya mto huo hayaingii katika makazi ya watu. Pia tulisema kwamba, KONOIKE baada ya kujenga kuta hizo watasafisha mto huo ili kuondoa taka zote zilizolundikana mtoni kuufanya mto huo utiririke kama inavyostahili. Wananchi wa Mtaa wa Kigogo Sambusa, walielekezwa waache kutupa takataka katika Mto Msimbazi na KONOIKE walielekezwa wafanye taratibu za kusajili mradi wao kwa baraza la kufanya ukaguzi wa mazingira, kwa sababu mradi huu ulikuwa umekwisha anza kabla ya sheria yetu ya mazingira ya mwaka 2004. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, hayo ndio yaliyokuwa yamejiri, tutashirikiana na wewe kama kutakuwa na jambo lingine ambalo unadhani litakuwa halikuelekea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgana Msindai, katika hoja zake alitaka kujua kwa nini Serikali inaachia ujenzi wa hoteli kubwa za kitalii katika maeneo ambayo kuna vyanzo vya maji, maeneo yanayofunga njia za wanyamapori. Kwa ujumla, kuna miradi ambayo ilijengwa kabla ya sheria ya mazingira, sasa hivi tunachoweza kufanya ni ukaguzi. Miradi ambayo imejengwa kuanzia 2004 na kuendelea, inahitaji kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira na ndio maana mradi ule uliokuwa na matatizo katika

eneo la *RIM*, haukuweza kupata tathmini ya athari ya mazingira. Vilevile alizungumzia kuhusu Ziwa Natron na nimeshalielezea.

Mheshimiwa Mariam Kasembe, katika moja ya mambo aliyotaka kujibiwa pia ni kwamba, kwa nini nchi yetu inaharibiwa kunakuwa na utupaji taka ovyo na kuenea kuvamiwa kwa maeneo ya wazi na kadhalika? Sheria ya mazingira inatamka wazi chini ya kifungu cha 120, ni wajibu wa kila mwananchi kusimamia maeneo yanayomzunguka kuhakikisha kuwa, hakuna utupaji taka ovyo. Yeyote anayekiuka sheria, anavunja sheria na endapo atatiwa hatiani, anastahili kulipa faini ya papo kwa papo ya kuanzia Sh. 50,000, lakini pia kama atapelekwa mahakamani, inabidi pia alipe faini na faini hii inafika Sh. 50,000,000. Hii ni kwa viwanda na kadhalika. Baraza linaendelea pia na juhudi za kutoa elimu kwa umma kwa ujumla, kuhusu masuala mazima ya usimamizi wa taka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felister Bura, alitaka kujua je, utafiti umefanyika wa kutosha kuhusu athari ya mazingira kuhusu ziwa lile? Nimhakikishie tu ya kwamba, tathmini ya kwanza ilifanyika na bado tumewapa kazi kampuni iendelee kufanya tathmini zake. Mheshimiwa Lyamba, Mbunge wa Mikumi, alizungumzia Serikali kuteua wataalamu washauri kutafuta chanzo cha mafuriko ya mito; alisema kwamba, kuna huu Mto Kondoa ambao ni korofi sana. Mimi nimesema kupitia mkakati wetu huu wa kuangalia masuala ya mito, maziwa na mabwawa, tutafika maeneo hayo na tutaangalia ni jinsi gani tunaweza kuudhibiti huu mto korofi, lakini pia tunachukua ushauri wako kuhusu masuala ya elimu katika mambo ya mafuriko. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Ofisi yetu tumeweza kutoa fedha kwa ajili ya kupata vifaa kwa mamlaka ya hali ya hewa ili waweze kupata vifaa bora zaidi kwa ajili ya kutuwezesha kuwa na taarifa nzuri za hali ya hewa.

Mheshimiwa Nchimbi, amezungumzia masuala ya kuiwezesha *NEMC* kuwa na jengo lake. Tumesema *NEMC* tayari wameshapata eneo watajenga. Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, ameeleza kwamba, *NEMC* iwe makini katika kusimamia masuala yote. Tunasema tutaendelea kusimamia kwa umakini. Mheshimiwa Stella Manyanya, amezungumzia masuala ya mipango endelevu, tunasema mipango endelevu itaendelea kutekelezwa na sasa hivi tunafanya *Strategic Environmental Impact Assessment.* Mheshimiwa Lucy Owenya, ameeleza kwamba, Serikali iangalie utaratibu wa kufanya mafunzo ya *tour operators* katika masuala ya mabadiliko ya tabia nchi. Tutashirikiana na Wizara ya Maliasili kuweza kuona kama *TANAPA* au sisi tutashirikiana wapate elimu hiyo.

Mheheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ania Chaurembo, amezungumzia masuala ya taka. Mheshimiwa Zuleikha Haji, amezungumzia masuala hayo yote ya elimu kwa ujumla na tunasema, tutaimarisha elimu na kwa safari hii tumepanga kuwa na elimu ya kimkakati, elimu endelevu na tutakuwa na vipindi vya kuhusisha wenzetu waandishi wa habari, vyama vya kijamii na vituo vya habari kutoka katika mikoa na kanda mbalimbali ili habari iweze kutawanyika na kufika vijijini.

Mheshimiwa Msomi, Mbunge wa Kigamboni, alitaka kujua tumefanya nini katika masuala yake makuu yafuatayo: Kwanza, kulikuwa kuna uchafuzi wa *alphamatch*, kulikuwa na uchafuzi wa kiwanda cha nondo na kwa ujumla *NEMC* ilifanya kazi hiyo na kuangalia ukaguzi. Tumewapa mikakati ya kuweza kurekebisha na *NEMC* itafuatilia utekelezaji kutokana na *time* tuliyowapa ya kuweza kurekebisha. Mheshimiwa Msomi, alitupa pia wazo zuri na tumelichukua; alitoa wazo kwamba, kwa kuwa Marehemu Mheshimiwa Dr. Omar Ali Juma, aliitumikia Ofisi ya Makamu wa Rais na alifanya mchango mkubwa sana katika masuala ya mzingira; aliuliza je, tunaweza kuwa na utaratibu gani wa kuenzi mchango wake huu kwa kuwa na tuzo kwa ajili ya marehemu au kuwa na suala lingine ambalo litaweza kusaidia? Mimi nasema, wazo hilo tunalipokea, tunashukuru na tutaangalia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru nyote. Navishukuru vyama vyote vya kijamii, vinavyounga mkono jitihada za kuelimisha mazingira. Nawashukuru vijana ambao juzi wamefanya semina na makongamano kuhusu hali ya mabadiliko ya tabia nchi. Nakishukuru Chama cha Waandishi wa Habari - *JET*, kwa mchango wao mkubwa. Navishukuru vyama vyote. Naishukuru hata Haki Elimu, kupitia kipindi chao kile cha kuangalia masuala ya elimu wameweza kutumia dhana nzima ya mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa joto duniani. Kwa hiyo, hilo tangazo lao linafanya wananchi wengi sasa wajue mabadiliko ya tabia ya nchi ni nini na ongezeko la joto duniani ni nini. Nawashukuru wafadhili mbalimbali, Mabalozi wamekuwa wakichangia kama alivyotaja Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa kauli kufuatia kitendo cha majangili waliovamia Msitu wa Shengena. Naomba kutoa hoja na kusema kwamba, wavamizi hao wahame mara moja na sisi tutawafuatilia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Masuala ya Mazingira. Sasa namwita mtoa hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Masuala ya Muungano, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo imeanza jana. Kabla sijaanza kujibu hoja hizo, naomba uniruhusu niwatambue Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na kuandika. Jumla yao ni Wabunge 60. Kwa upande wa Wabunge waliozungumza ni Mheshimiwa James Wambura, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mohamed Chombo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Issa Kassim Issa na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia kwa kuandika hoja zote mbili hizi ni Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaya, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed.

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Kimwanga, sio Kimwaya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, samahani. Mheshimiwa Kimwanga, samahani sana nakuangukia kwenye miguu yako unisamehe.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Brigedia Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Usi Ameir Pandu, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Maua Abeid Dftari, Mheshimiwa Dr. James Msekela. Wakati Waziri mwenzangu anachangia hapa, alikosea jina la Mheshimiwa Castor Ligallama akatamja Lyamba, kwa hiyo, naomba kusahihisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, natarajia muda huu hautakuwemo katika katika dakika 30 maana yake nazo si nyingi hata kidogo.

**SPIKA:** Lilikosewa jina pia la Mheshimiwa Lucy Owenya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba lisahihishwe, leo mbona siku mbaya kwangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nikushukuru sana wewe binafsi, kwa kutupa nafasi ya hoja yangu kuzungumzwa kwa siku moja na nusu. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamekuwepo hapa toka jana, wale waliozungumza na waliosikiliza wote walichangia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, kuna baadhi yenu muashindwa kunong’ona mnaongea kabisa. Haipendezi na ni kinyume cha kanuni. Mhesimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba sana kukushukuru wewe binafsi, Naibu wako na Wenyeviti, kwa kutupa heshima hii ya kuwasilisha bajeti yetu kwa siku moja na nusu. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamekuwa hapa toka jana; wale ambao wamezungumza, waliosikiliza, walioandika, wote wamechangia hoja hii kwa upande wake. Pia namshukuru sana Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, dada yangu, kwa mchango wake mzuri sana wa kujenga muungano wetu. Namshukuru sana Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Pindi Chana, kwa mchango wake, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uongozi wake kwangu mimi na kwa Wizara yetu, zaidi kwa kunisaidia mara kwa mara kuonja kiti chake mara moja moja, huwa nafurahi kidogo nahesabu siku ili baadaye zinisaidie kwenye *CV* yangu siku zijazo hizo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sio kweli, unahofu sana kukaa pale, huwa unakaa karibu yake tu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo karibu karibu tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kuniamini kunipa heshima ya nafasi hii ya kuwa Waziri katika Wizara hii, ninamuahidi kwamba, nitakuwa mtii, muaminifu na mchapa kazi ili nifanikishe majukumu yake.

Nimeambiwa kuwa nimesahau kutaja jina la Mheshimiwa Diana Chilolo, naomba samahani. Ningependa niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Uzini, najua muda mrefu sikuwepo Jimboni nilikuwa kazini hapa na wengine wanapita pita huko; waambieni mwenyewe bado nipo na ninaahidi kwamba, baada ya Bunge hili nitakuja kutembelea na kuonana nao ndugu zangu wa Uzini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu zaidi ilikuwa suala la Muungano. Mtakubaliana na mimi kwamba, hoja ya msingi ilikuwa ni juu ya Muungano wetu; faida zake, hasara zake, kero zake na muundo wake. Kwa hiyo, mtanisamehe sitataja mmoja mmoja kwa sababu najua nyote mlilizungumza jambo hili moja tu si kama mwenzangu ambaye hali yake imechanganyika sana. Niseme kwamba, Waheshimiwa Wabunge, wamechangia toka jana; wengine kwa jazba sana, wengine kwa munkari kabisa, wengine kwa mori kabisa, lakini wengine kwa maneno ya upole ambayo ndani yake kuna vijembe. Wote napokea maoni yenu kwa maneno mazuri na ninaamini kwamba, nia yenu ilikuwa njema kabisa. Niseme kwamba, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuweke utaifa mbele, tuweke uzalendo mbele, tuache ubinafsi, tuzungumze lakini tujue kwamba, Taifa ndio muhimu zaidi kuliko mtu mmoja tu.

Kwa hiyo, naamini kwamba, mazungumzo yenu yatasaidia sana na ninaomba tuungane na baada ya mazungumzo haya ya siku moja na nusu, turejee katika hali ya kawaida. Kwa sababu kumekuwa na upande wa Bara na wa Visiwani; Pemba na Unguja; Wapinzani na *CCM*, tuachane huko bwana yamekwisha sasa hivi. Mmezungumza, mmetoa joto limekwisha sasa tujenge nchi, kwa sababu sote tumetumwa hapa na wananchi ili kuwatumikia mambo ya msingi. Watu wana shida, kuna njaa, umasikini na shida, hayo ni ya muhimu zaidi. Kwa hiyo, nasema huu Muungano utatusaidia

kutekeleza hayo mambo. Naomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa turejee kwenye hali ya kawaida na hasa kwa sababu tumepata uhuru mkubwa sana. Watu wamezungumza tani yao, watu wamezungumza kiasi chao; kila mmoja kazungumza anavyotaka mwenyewe tu bila kuzuiwa hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nafikiri kuna mtu mmoja amesema kwamba, hapa hatuna uhuru wa kusema; yeye mwenyewe anazungumza kwa nguvu kabisa. Sidhani kama kuna nchi katika Afrika, ambayo ina uhuru wa kuzungumza na kuandika kama nchi hii ya Tanzania. Tuutumie uhuru huu kwa ajili ya kujenga sio kubomoa. Sisi tumo ndani ya Muungano huu halafu tunataka kuubomoa tuzame, haiwezekani hata kidogo. Kwa hiyo, nasema kwamba, uhuru tunao lakini uwe na mipaka yake Waheshimiwa Wabunge. Wewe ni Mbunge una nafasi yako katika Bunge, ni huru kuzungumza, lakini je, mipaka yako ni nini? Kauli zako haziharibu? Hazibomoi? Lazima tuwe na hadhari kwamba, hili ninalolizungumza hili halitabomoa taifa letu bali litajenga, tuikosoe Serikali lakini hatimaye tuone mazungumzo yetu ni lazima yajenge Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuahidi kwamba, tumesikia mengi, Serikali ina masikio, tumeona mengi, mmetoa mifano mingi sana, yote haya tumeyachukua na ninaamini kwamba, nia yenu ilikuwa njema. Nyote kabisa nia yenu ni njema ya kutaka kujenga umoja wa Tanzania, Muungano wa Tanzania imara kabisa. Tunaahidi kwamba tutasaidia. Mambo mengine haya, jamani nisije nikasahu, wengine ambao nimewasahau hapa ni Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamisi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi. Naomba samahani sana, msitoe shilingi kwa jambo dogo kama hili tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi hapa ni Muungano wetu tu na mimi ninaamini kwamba, sote tunakubali kwamba, Muungano huu ulikuwa halali kwa mujibu wa taratibu zake za Kibunge; nafikiri hakuna anyehoji. Muungano ambao umekuja kwa hiyari ya watu wenyewe, watu wametoa mfano hapa wa Urusi na Yugoslavia, haulingani na wa Tanzania hata kidogo; vitu mbalimbali kabisa kama mbingu na ardhi havihusiani kabisa. Huwezi kuulinganisha Muungano wa Tanzania na Urusi na Yugoslavia; huu Muungano wananchi wenyewe wamekubali. Kwanza, wana historia moja na kadhalika na kadhalika, lakini pia Marekani waliosoma historia, Muungano wao ulikuwa wa mabavu ule wa kulazimishwa tu, leo ni watu wenye demokrasia kubwa sana, lakini sisi wenyewe hapa ni wa hiyari ndio maana umedumu miaka 44 hiyo.

Kwa hiyo, Muungano wetu ni halali kabisa na wamezungumza Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba, kulikuwa na *Articles of Unions*, lakini nasema zile ni za kuanzia tu baadaye, Muungano huu unakuwa *dynamic* haubaki hapo ulipo ni lazima utabadilika na wakati na kadhalika maana unaongezeka tu. Kwa mafano, hii ya kuwepo hapa ndani ya Bunge vyama vingi vya siasa, imeingizwa katika Katiba hii kwa sababu ya mabadiliko yanayotokea. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa kama zamani ni lazima itabadilika tu. Nasema Wabunge wana hiyari yao, kama wanaona jambo limeingizwa katika mambo haya ya Muungano ambalo halina maslahi kwetu tutazungumza tutalitoa tu; huu sio msahafu wala biblia, tunaweza kubadilisha wakati wowote ule. Kwa hiyo, la msingi ni kwamba tujengeni hoja, jambo hili hatulitaki tujenge hoja tutalitoa tu; hili liongezwe tutaliongeza,

kwa sababu Muungano huu ni wa ridhaa za pande zote mbili za Muungano. Kwa hiyo, nasema kwamba, Muungano ni halali na kuna haja ya kurekebisha na sio dhambi hata kidogo kurekebisha mambo kama haya. *Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu umeletwa na binadamu si malaika ni lazima kutakuwa na kasoro zake za hapa na pale. Kwa hiyo, kasoro hizi sio makosa kuzionyesha tutazirekebisha lakini sio kulalamika. Binadamu sote wengi hapa tuna familia, tuna mke na watoto; mke na mume mnakaa miaka 50 lakini mnagombana.
Mtu na mke wake nje wanacheka, lakini jana hawajalala usiku kucha wanagombana, lakini nje wanacheka cheka tu. Kwa hiyo, masuala haya ya kimuungano ni sehemu ya maisha yetu. Muungano huu ni *dynamic*, utakuwa na mabadiliko bila shaka. Naomba ndugu zangu tusivunjike moyo na matatizo haya yanayotokea mara kwa mara kuhusu Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumza aina ya Muungano. Muungano wetu ni wa Serikali mbili; Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndivyo tulivyokubaliana uwe hivyo. Ndivyo ulivyoundwa, ndivyo ulivyo na ndivyo ulivyo hivi sasa. Wengine wanasema mbona umefanana na wa nchi gani? Hakuna, kwani ni lazima tuige Ulaya? Huu Muungano umejengwa kwa mujibu wa matakwa yetu, historia yetu na watu wetu si, lazima ufafane na wa nchi nyingine hata kidogo. Haya ni matakwa yetu, ndio Muungano wetu jinsi ulivyo. Kwa hiyo, nasema Muungano wetu huu ni wa kipekee, ambao umejengwa kwa mujibu wa matashi ya viongozi wetu. Njia moja ya kuwaheshimu Viongozi Wakuu; Marehemu Karume na Marehemu Nyerere ni kuuheshimu Muungano huu, sio kuimba tu Baba wa Taifa, hapana.

Urithi mkubwa na muhimu kwa taifa letu ni Muungano huu wa Tanzania. Kwa hiyo, nasema kwamba, yapo wazi na si ajabu baadhi ya Wabunge wanataka nielezee kuhusu majukumu ya kila Wizara. Tunazo Katiba, tumekuwa na Katiba sasahivi tunaelekea kuwa na Katiba ya Muungano, tunajua hili la Zanzibar, lipo wazi kabisa. Kwa hiyo, nasema haina haja mimi kuelezea upya hivi na hivi kwa sababu najua majukumu yapo wazi wazi. Pia tuna kero zake, ambazo ni lazima Wabunge tuwasikilize maoni yenu, tuyapeleke katika Serikali yetu iyashughulikie, ndio maana imeundwa Kamati Maalum inayoongozwa na Makamu wa Rais, kuthamini kwamba ni lazima maoni ya wananchi tuyashirikishwe. Kwa hiyo, matatizo mengi ambayo yamezungumzwa hapa yanahusu zaidi mambo ya michango ya Muungano, mambo ya *BoT, TRA* na kadhalika. Haya tumesema katika hotuba yangu kwamba, tayari Tume ya Pamoja ya Fedha imeyaorodhesha, namna ya kuchangia muungano huu, namna ya kupokea mapato. Sasa hivi yapo kwenye Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Tuwape nafasi Serikali kuyatafakari na baadaye mtaarifiwa matokeo ya jambo hili, tuwe na subira. Tumesubiri miaka 44, kusubiri mwaka mmoja au nusu mwaka inawezekana tu, naomba tupewe nafasi tuweze kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumza juu ya muundo wa Serikali, tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa kumekuwa na chaguzi tatu; mbili nafikiri zimekuwa za Rais Mkapa na moja ya Rais Kikwete. Katika kila uchaguzi, vyama vyetu vinanadi sera yake na moja ya sera muhimu ambayo kila chama imenadi ni aina ya Muundo wa

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wapo watu wamenadi muundo wa majimbo na ndio wengi wapo hapo. Majimbo kwa kutumia helikopta lakini wameporomoka. Wapo watu wamenadi kuwa na Muundo wa Serikali tatu, wameporomoka. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali mbili tumepata 80%, kwa hiyo, muundo wetu unakubalika na wananchi, ndio maana tumeuza sera zetu mara tatu na zote tumeshinda. Si hayo tu, mwaka 1964 tulikuwa na Watanzania 10,000,000 kutoka Bara, 300,000 Zanzibar wakati tunaungana, waliozaliwa hapa zaidi ya theluthi tatu wamezaliwa wanaona Muungano huu ulivyo sasa hivi, hawajui mwingine; wao ni wengi zaidi kuliko sisi tuliobakia wa zamani, zilizopendwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunasema Muungano huu unakubalika kwa sababu wananchi wengi wa Tanzania wamezaliwa ndani ya Muungano wa Serikali mbili wa sasa hivi, tusiwalazimishe jamani tuwaacheni. Kulikuwa na Tume ya Kisanga, alipewa jukumu la kuwauliza Wananchi wa Tanzania nzima hii kwamba, je, wanataka muundo wa Serikali ngapi? Nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge ambao wamesahau takwimu za Jaji Kisanga; kwa Zanzibar wanaotaka mfumo wa Serikali moja ni 0.18%, Zanzibar wanataka Serikali tatu ni 3.48%, Serikali mbili kwa sasa hivi ni 96.26%. Kwa hiyo, hawa wanaosemea Serikali moja au tatu kwa Zanzibar wanatoka wapi; wamewapata watu hawa ambao Jaji Kisanga hajawaona?

Tanzania Bara wanaotaka Serikali moja ni 0.18%, Serikali tatu ni 3.48%, Serikali mbili ni 96.26%. Nawauliza Wabunge wa Bara nani kawatuma? Wengi wapi 96% au 0.18%? Bahati nzuri sijui kwa nini imetokea hapa, lakini ukiangalia takwimu ya Wanzibari wanaotaka Serikali mbili na ya Bara zinafanana zote, sijui kwa nini?

**MJUMBE FULANI:** Ungana!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Niungane, shabash!

Kwa hiyo, nasema kwamba, ndugu zangu tusitwange maji kwenye kinu, wananchi hawataki mfumo wenu wanataka uliopo sasa. Tumeanza kwenye sera za chama, tumezungumza kuhusu idadi ya Watanzania walioazaliwa na tumezungumza juu ya hili la Jaji Kisanga, wote kabisa wanasema sisi tunataka mfumo wa Serikali mbili lakini rekebisheni makosa, tunakubali. (Makofi)

Ndugu zangu za Upinzani wamesema kwamba, wanataka tufanye kura ya maoni, ipi nyingine zaidi ya hii tena? Haina haja.

Pia kwenye Kambi ya Upinzani wamesema kwamba, wanataka niwasaidieje kuhusu mpasuko wa kisiasa Zanzibar na Suluhisho katika mambo yale ni mazungumzo. Nasema hili jambo halihusiani na kwangu mimi hapa, ila waende kwenye vikao vyao vya chama. Serikali haina Mamlaka ya kuingilia mazungumzo yenu, endeleeni kuzungumza na baadaye mlete hapa tutaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi hapa ni kuhusu nafasi ya Makamu wa Rais kwamba, sasa hivi mabadiliko yafanyike lakini kwa ridhaa za wananchi wenyewe. Ilikuja hoja hapa Bungeni kama sijakosea, sijui alikuwa ni Waziri wa Sheria ambaye ni Spika wa sasa hivi, lakini mimi nakumbuka nilikuwepo hapa. Ilikuja hoja hapa Bungeni kufuatana na mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, tukasema kwa sababu yawezekana siku za mbele Mungu apishe mbali kwamba, Kiongozi Mkuu wa Zanzibar au Rais wa Zanzibar akatoka chama kingine na Rais wa Muungano wa chama kingine, Mungu apishie mbali. Ikitokea hivyo, maana yake unakuwa na Serikali ya Muungano, Viongozi wenye itikadi tofauti ambayo ni hatari kwa maendeleo ya nchi yetu, ndiyo siri yake hiyo. Huyu Rais wa Zanzibar, anaweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, endapo Rais hayupo au kadhurika, unampa mpinzani Serikali ya Muungano ni salama hiyo jamani? Ataikuta Serikali yake akirejea? Hataikuta!

Kwa hiyo, mambo yote haya ndiyo tukafikiri jamani tukaona kuna haja ya kufikiria namna ya kubadilisha mfumo huu ili uwezekane.

Hata hivyo, tumesema kwamba, tumeanzisha mfumo wa Mgombea Mwenza, ambaye anakuwa Makamu wa Rais kutoka upande mmoja wa Muungano na mfumo huu unahakikisha kwamba, siku zote utapata ama Rais au Makamu wa Rais kutoka Zanzibar, mfumo huu wa sasa hivi. Kwa hiyo, nasema haina haja ya kulalamika kwa sababu mfumo huu umekuja ili kutoa tahadhari ya mambo haya ya vyama vingi.

Ndugu yangu, Mheshimiwa Ali Said Salim, amenipa kazi ngumu sana, lakini nashukuru nikamwambia aniandikie na akaniandikia pale, lakini nimeshindwa. Ananiambia kwamba, nimpe ufafanuzi wa vifungu mbalimbali kavitaja, yaani ni vingi amevitaja pale, nikasema hii si kazi yangu jamani, mimi si Waziri wa Sheria, si Mahakama na si mtaalamu wa mambo hayo pia, kwa hiyo kumtendea haki nimeamua nimwombe, nayakubali ndugu yangu. Mimi nitamwandikia Barua Waziri wa Katiba na Sheria ili atoe ufafanuzi huo na ampelekee kwa maandishi Bwana Ali Said Salim na ili Wabunge wengine pia wapate kujua mimi nikifanya hapa nitaboronga bure! Si fani yangu hii, yaani mimi si Mwanasheria ila mimi ni mtu wa mashairi tu. Akiniambia nichambue kitabu cha Kusadikika nitamchambulia vizuri sana hapa lakini si Katiba; nitakudanganya Mheshimiwa Ali Said Salim na ninaomba unisamehe kwa hilo. (*Kicheko*)

Vifungu vile vipo wazi; sijui kwa nini inawapa tabu na vimeandikwa kwa Kiswahili fasaha kabisa, lakini ndiyo hivyo naambiwa ukubali nifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, nasema Muungano wetu huu ni wa kipekee na una heshima kubwa sana duniani. Zipo nchi za Afrika ambazo zilijaribu kuungana zimeshindwa, nitataja baadhi yake tena wakati huo Afrika ina Uafrika ule *(Panafricanism).*

Mwezi Mei mwaka 1956, Togo na Ghana waliungana lakini siku ya pili wakaachana; Februari, 1958 Misri na Syria waliungana lakini wakaachana siku ya pili yake; Januari, 1959 Mali na Senegal waliungana siku ya pili wakaachana; Novemba, 1958 Ghana na Mali waliungana na siku ya pili wakaachana. Zipo nchi nyingi tu zilijaribu lakini zimeshindwa, sisi tuone fahari. *(Makofi)*

Wenzetu wanaona wivu sisi, hatuoni fahari hata kidogo. Tuone fahari kwamba, tumeweza kudumisha Muungano huu kwa miaka 44, matatizo yake tutafanikiwa tu kwa sababu ulikuwa Muungano wa kweli kweli na wenye utashi wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri yapo matatizo lakini haya ninayoyasema yapo nje ya Muungano wenyewe. Kengele hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, yapo matatizo ya Muungano ambayo yapo nje ya Muungano wenyewe. Nataka Waheshimiwa Wabunge, mnisikilize kwa makini sana, nitaelezea kwa ufupi. Matatizo haya yanababatizwa kwenye Muungano na matatizo ya kweli.

Kwanza, wale ambao wanajua chimbuko la Muungano huu ; akina Mzee Ngombale Mwiru na wenzake wengi leo hawapo duniani. Hivyo chimbuko la historia wengi hawalijui na wengi ni wapya kabisa. Hilo nalo ni tatizo pia kwa Viongozi wetu Wakuu. Mwalimu Nyerere, Karume na wengine wengi hawapo duniani, ambao ndiyo walioanzisha kwa ari kubwa na kwa uzalendo mkubwa na utaifa makubwa leo hawapo duniani, hilo ni tatizo kubwa.

Wasiojua Muungano huu asili yake na maana yake ni vijana wa leo, wapo wengi na wanaongezeka. Sisi tunazaa sana bwana ; kama mwaka 1964 milioni kumi leo tupo milioni arubaini si kidogo, tunafanya kazi kweli. Kwa hiyo, idadi ya wale ambao wamezaliwa ndani ya Muungano huu, hawajui kingine. Pia hili ni tatizo kwani hatuwezi kuzuia watu wasizae; watazaa na watakufa.

Wapo viongozi wachache wanaoujua Muungano huu, chimbuko lake, asili yake, lakini vigeugeu kwani hawawaambii watu ukweli, wanataka maslahi yao, Taifa hawaliweki mbele. (*Makofi*)

Nitawapa mfano, mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Aboud Jumbe. Yeye alisema anataka mfumo wa Serikali tatu na walewale ambao walimfukuza katika chama hiki leo nao eti pia wanasema Serikali tatu; pale alikuwa mbaya lakini leo mzuri! Wakati haya yanafanyika Dodoma, mimi nilikuwepo CBE hapa. Kwa hiyo, hawasemi ukweli; leo tatu kesho nne, keshokutwa moja haiwezi kuwa hivyo jamani, tuwe wakweli tuwaambie jambo hili ni kadha wa kadha. *(Makofi)*

La pili, kulikuwa na kesi ile Mahakama ya Rufaa na baadhi ya Viongozi walikamatwa; wale Waheshimiwa walivuka kutokuwa wahaini kwa sababu ya Muundo wa Serikali hiyo wakasema kwamba, Serikali hii Zanzibar hawana *sovereignty* yao, wakavuka, imewavusha lakini leo wamesahau. *(*Kicheko*)*

Nimalizie kwa kusema kwamba, lipo lingine pia ambalo ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi huwa nasema hapa lakini ninyi hamuelewi. Kule

Zanzibar sisi tuna matatizo mawili; tuna tatizo la Mapinduzi yetu na Muungano huu. Wapo watu hawataki Mapinduzi ya Zanzibar lakini pia hawataki iliyokuwa *ASP* ya zamani. Sasa wamejiandaa vizuri wanaandika vitabu vingi sana, watu wanaandika vitabu ili kuusema.

Kwa mfano, kuna kitabu hiki cha huyu Bwana anaitwa Ally Muhsin Baruani, ndani yake anasema Muungano huu si halali na kadhalika, nitasema nini alichosema. Hii balaa bwana! Ukurasa wa 33 anasema kwamba: "Hii ni *ASP* baada ya mavamizi ya nchi yetu na kuingia katika madaraka kwa mdomo wa bunduki, ndio iliyouza nchi yetu ya Zanzibar kwa Nyerere katika Aprili, 1964 kwa yale makubaliano ya Nyerere na Karume."

Huyu anasema kwamba, "Zanzibar imevamiwa na Nyerere," sasa watu kama hawa bado mawazo yao yapo. *(Kicheko)*

Ndugu yangu Mudhihir, alisema kuna kitabu; ninayo kopi yake, yupo Mudhihir? Hiki hapa kinaitwa "Ukweli Huu." Huyu Bwana kweli kasema hivi, nanukuu: "Ufisadi mmoja ni huko kuiburura Zanzibar ndani ya Muungano wake, Muungano wa hange, miezi minne tu baada ya kufuzu haya mavamizi yao, hili ni janga kubwa sana." Anasema huyu Bwana Amani Thani Ferouz ushahidi huu hapa, kitabu cha pili hicho.

Kitabu cha tatu kimetungwa na Bwana Issa Bin Nassor El-Ismaily, nasoma nini kasema ukurasa wa 122: "Ni ASP ambayo ilimgaia Zanzibar Nyerere katika mwezi wa Pili mwaka 1964 na ikapoteza kuinyang'anya Zanzibar bendera yake na kiti chake katika Jumuiya ya Madola ni ASP ambayo ilifunga Balozi zote za Zanzibar katika nchi za nje."

Kitabu cha nne, hiki hapa cha Bwana Juma Duni, kiongozi wa CUF. Jina la kitabu ni cha kejeli: "Ni Muungano au usanii na ufisadi wa kisiasa."

Kwa hiyo, jamani tuna mapambano makubwa sana, watu wanatunga vitabu kuhujumu Muungano huu, ushahidi upo hapa vitabu vinne hivi sijui wamepanga pamoja, lakini hii ni hali halisi.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba, Muungano wetu wa Watanzania ni muhimu kwa sababu ni Muungano ambao una asili moja. Wakati tunaunda ASP ni chama cha Waafrika kutoka Bara na kutoka Zanzibar ndiyo asili yake hii. Baadaye tukafanya mapinduzi Zanzibar wengine husema uvamizi, mapinduzi haya yalifanywa na wananchi kutoka Bara na Visiwani.

La tatu, Muungano wa Serikali 1964 ni wa Bara na Visiwani. Nne, TANU na ASP ya Bara na Visiwani. Kwa hiyo, ni mchakato mkubwa sana huu hauwezi kupotea hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba kwamba, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kujenga taifa moja, yanawafika wenzetu kule wa Urusi au Yugoslavia na Chechnya kwa sababu walifanya makosa kama haya.

Mheshimiwa Spika, ulisema kwamba, kunafaa kuwepo na semina hapa, mimi nakubaliana na wewe na sasa ninukuu kauli ya Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere aliyoitoa Julai 6, 1970 hapa Bungeni; alisema hivi, naomba ninukuu: "Bila shaka yoyote, katika mambo yote ya siasa ya Tanzania, jambo lisiloeleweka sana ni matokeo ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar, si kitu sana kama nchi za nje hawaelewi Muungano wetu lakini kwa bahati mbaya mara nyingi hata Watanzania wenyewe hawauelewi."

Mmenielewa jamani? Nasema tena; si kitu sana kama nchi za nje hawaelewi, lakini sisi wenyewe hatuuelewi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na semina ili tuuelewe Muungano huu; faida yake, umuhimu wake na tuuwekee kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Masuala ya Muungano. Natumaini si mchoyo, pengine vitabu hivi unaweza kumkabidhi Katibu wa Bunge ili viwepo katika Maktaba yetu kama rejea ya masuala haya ili tuzidi kuelewa; ni sehemu ya kuelewa Muungano.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 100, itabiti tupitie utaratibu hadi kuiamua. Kwa hiyo, nitamwomba Katibu sasa atutamkie utaratibu huo.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 26 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 - *Administration and General* … … … …. Sh. 2385,526,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Damiano Nyami, hebu ngoja kwanza; ninyi wengi mmezoea kuchukua mishahara tu sasa hapa wataalamu wananiambia ni Mshahara wa Makamu wa Rais labda muusubiri wa Mheshimiwa Waziri au kuna hoja hapa.

**WAJUMBE:** Hapana!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 - *Administration and General* … … … … .. Sh. 3,050,911,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya. Tuanze na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nipate ufafanuzi pale inapotokea kwamba, ramani za jiolojia zinaonyesha kuna madini ambayo yapo na yapo chini ya ardhi ambayo kuna mbuga za wanyama na tungekuwa na lengo la kutaka kujua ni kiasi gani cha madini yapo katika eneo hilo mbali na kuanza kuchimba. Je, utafiti kama huu ili kuweza kuufanikisha na kujua kiasi cha madini hayo yaliyopo unaweza ukaendelea au itakuwa ni vigumu kwa sababu ya hizo mbuga za wanyama?

**MWENYEKITI:** Nadhani ni suala la mazingira hili, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika maeneo ambayo tayari ni ya hifadhi huwa haturuhusu shughuli za uchimbaji, kwa hiyo, kama ni kibali cha kuangalia huwa kinaweza kikatolewa kwa masharti maalum kwa kuzingatia maeneo yale. Kwa maana ya uchimbaji, huwa hairuhusiwi na tayari kupitia ule mkakati wetu wa vyanzo vya maji, tuliweza kuwatoa wachimbaji katika baadhi ya maeneo ambayo walikuwa tayari wanafanya shughuli hizo ndani ya hifadhi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naona amepata jibu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia, nilizungumzia suala zima la mambo ya Muungano na matatizo yake. Nilimtaka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, basi agusie suala moja ambalo lipo wazi na hili si suala la Muungano lakini linafanywa kama ni la Muungano; ni suala la michezo.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, atoe kauli leo kuhusu suala hili ambalo limechukua utata mkubwa sana katika kipindi cha miaka 44. Utata wake ni kwamba, linatumiwa na wenzetu kama suala la Muungano wakati si la Muungano na halijachukuliwa hatua katika kipindi hicho cha miaka 44 kuunda chombo cha Muungano cha Kusimamia mambo hayo. Ni sehemu moja tu ambayo ndiyo inayochukua jukumu hilo ambapo upande mwingine hauna jukumu hilo. Sasa namwomba basi Mheshimiwa Waziri, atoe kauli pamoja na matatizo yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, najua matatizo yapo, lakini yale ya kero basi yawe ya kero hili si la kero wala si utekelezaji wa Katiba, ndiyo swali langu hilo. Mheshimiwa Waziri, hakusema kitu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, tena ni mwenzangu sana huyu bwana, basi tu! Timu yake ya Miembeni au ya Kikwajuni sitakuwa na jawabu leo, lakini Waziri mwenye hiyo dhamana yupo hapa, Mheshimiwa George Mkuchika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la msingi ni kwamba, kuna haja ya Viongozi wenyewe wa michezo waanze kuzungumza kwanza kabla ya Serikali kuingia. Mimi nashauri kwamba, Vyama vya Michezo vya Zanzibar na huku Bara, chini ya mabaraza yao wakutane wazungumze halafu sisi tutasaidia, lakini waanze wao kwanza; si vizuri Serikali kuingia katika mambo ya michezo ambayo ni ya ridhaa zaidi. Huo ndiyo ushauri wangu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh, naona una maelezo tena zaidi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema si suala la vyama vya michezo; katika suala hili la michezo nimezungumza hapa kuna mtu mmoja kahodhi bila ruhusa ya mwingine. Nilichozungumza, Wizara yenyewe iachie suala hili na ikubali kuacha, tatizo ni kwamba, Wizara ya Michezo ya Bara haitaki kuliacha hili suala wanaling'ang'ania au ya Muungano?

Suala ni kwamba, wao waache tuunde chombo cha kitaifa; ni wao wa kutamka si *ZFA* na si *TFF*, lakini ni Wizara yanyewe ndiyo ya kutamka kwamba, kuanzia kesho kiundwe chombo cha kitaifa sisi tutashirikiana ili kuunda chombo cha taifa kiwakilishe Muungano.

Wanahodhi mpaka leo, kila tukisema hawataki, sasa Mheshimiwa Waziri akisema leo *ZFA* au vyama vyenyewe vikae vizungumze; si kweli kwa sababu vyombo vinaweza vikakaa lakini Serikali ikawa haitaki; tutafanya nini? Serikali itamke na iseme kwamba, sasa suala la Muungano liwe peke yake na la Zanzibar liwe peke yake, lakini kiundwe chombo kimoja. Hii ndiyo kauli tuliyoitaja sisi, haitamkwi hii sijui kwa nini na ina ugumu gani maana Mheshimiwa Waziri karudi kutoka China juzi?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa maelezo mazuri aliyoyatoa.

Nalikumbusha Bunge lako kwamba, katika maelezo marefu niliyoyatoa wakati nazungumzia bajeti ya Wizara yangu, kama alivyosema Mheshimiwa Muhammed Seif; yapo mambo ya ukweli tunayaona hatutaki kusema ndivyo yalivyo. Vyama vya Michezo ni Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kama Zanzibar (ZAMARA), wangesema vyama vya mpira tunataka kiwe kimoja tu si kazi ya Serikali ni wao kusema sisi katika mpira

tunataka tuwe chama kimoja, wakialikwa nje kitakuwa kimealikwa chama hicho kimoja; tatizo liko wapi?

Zanzibar wana *ZFA* wanataka waingie *FIFA*; kama Bara kuna *TFF* walikokubalika *FIFA*, *ZFA* haijakubalika kuwa mwanachama wa *FIFA*, inapokuja mialiko ya kwenda nje, anaalikwa yule aliye na uanachama kule na nikaeleza namna gani katika hali kama hiyo vyama vyetu Bara wanavyojitahidi kushirikisha pande zote mbili za Muungano.

Sasa mimi ninashangaa, si jukumu la Serikali kuunda vyama vya hiari, tukifanya hivyo na uanachama wa *FIFA* tutaupoteza, ni jukumu la vyama vyenyewe wakae watapata baraka za Serikali, si jukumu la Serikali kuunda vyama vya michezo iwe ya riadha, *netball* na kadhalika. Kauli ya ndugu yangu, Mheshimiwa Hafidh anataka kujua; je, Serikali msimamo wake utakuwaje? Serikali tutafurahi sana tukisikia vyama hivi vinakaa na tutawaunga mkono kwamba, sasa tunaelekea katika vyama hivi tuandikishe tuingie uanachama mmoja ili matatizo haya yapate kumalizika.

Hili la ndugu yangu Mheshimiwa Hafidh, analiuliza si kama analifahamu ila yeye kabobea kwenye mambo ya mpira, refa wa kimataifa. *TFF* wanamtumia sana kumtumatuma huko nje kama Kamisaa, japo kama yeye hayumo ndani ya *TFF* yupo *ZFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nifanye nyongeza hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. *Order please,* tumsikilize Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka ufafanuzi mdogo tu.

Ninataka ufafanuzi, kwa sababu tunafahamu kwamba, Tanzania tuna Wimbo wa Taifa, sasa nasikia tena kwamba, kuna Wimbo wa Taifa Zanzibar; ninataka kujua kama huo Wimbo kama ni Wimbo Taifa au ni Wimbo wa Zanzibar? Kama ni taifa ni taifa lipi, kwa sababu tunajua kwamba sisi tuna taifa moja? Kwa hiyo, nataka ufafanuzi nijue huu wimbo ni wa taifa lipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutarajia. Kuna wimbo wa Taifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wimbo wa Zanzibar.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza kuhusu suala au hoja niliyoipeleka Wizara ya Fedha na Uchumi na Waziri wa Mazingira aliniambia litajibiwa kwenye hoja ya leo. Suala lenyewe linahusu uondoaji wa kodi kwenye nishati ya motopoa, gesi asilia pamoja na mitungi ya gesi. Wakati ule

nilihoji kwamba, kama ni motopoa Watanzania wengi hawaujui na haifahamiki huko vijijini labda mijini, hata mimi nimekuja kuiona hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kama ni gesi na mitungi yake, ukienda vijijini watu watanunua wapi na hakuna barabara katika sehemu nyingi za vijijini. Ukitoa kodi kwenye gesi na mitungi yake na motopoa; unamlenga nani ambaye anaharibu mazingira; ni mtu wa kawaida vijijini au unamlenga mtu wa mjini? Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa kwamba, kuondoa kodi ile kwenye moto poa au gesi asilia kwa sasa hivi haisaidii kabisa kupunguza athari kwenye mazingira. Alizungumza Mheshimiwa Waziri hapa kwamba, inasaidia sana kwenye mazingira kupunguza athari yake si kweli. Kwa hiyo, tumepunguza kodi kule lakini haisaidii mazingira, nataka ufafanuzi kwenye hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kama ifuatavyo: Kwa kweli nakubaliana naye kwamba, kwa kiasi kikubwa, masuala haya tuliyaanza katika hatua ya kwanza, kwa sababu kama wote mtakubaliana nami, bajeti hii ya fedha imeweza kujielekeza katika masuala ya mazingira. Kwa hiyo, tumeanza kwa kuelekeza kwanza kupunguza matumizi ya mkaa katika maeneo ya mijini, lakini vilevile katika hatua za baadaye na ambayo nimesema katika bajeti yetu hii tumejielekeza kukamilisha tafiti hizo ili makaa ya mawe yaweze kutumika na hii itakuwa ni nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wanatengeneza vumbi hizi za makaa ya mawe kwa kuchanganya na nafaka za mazao. Hao tutashirikiana nao ili kuhakikisha kwamba, shughuli hii wanayoifanya iweze kuwa kwa kiwango kikubwa ili iweze kuwafikia watu wengi vijijini. Kwa hiyo, nasema hatua ya kwanza tumeanza na kila tutakavyozidi kwenda, tutaweza kuwafikia watu wengi zaidi, lakini kila hatua tunayoifanya makusudio ni kuhakikisha kwamba, tunapunguza kwa kiasi kikubwa ukataji miti ovyo na matumizi makubwa ya kuni na mkaa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba ufafanuzi juu ya jambo ambalo nililiandika na Mheshimiwa Waziri amejaribu kuligusia lakini naomba ufafanuzi wa zaidi. Jambo lenyewe linahusu Mradi wa Lake Natron kwa ajili ya kuchimba, kusafisha na kutumia magadi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi moja jirani ina mradi unaofanana na huu tunaouzungumzia na inapata fedha nyingi za kigeni, lakini inapokuja Tanzania vikwazo ni vingi sana; matokeo yake mradi unachelewa na nchi inachelewa kupata faida ya huo mradi. Sasa nilikuwa naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa maana ya *time framework;* wanadhani masuala haya ya *environmental impact assessment* yamepangiwa kuisha lini ili tujue kama nchi tuna mradi au hatuna? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mchango wa Mheshimiwa Kaboyonga. Ni kweli kabisa kwamba, katika masuala ya mazingira, lengo si kuzuia maendeleo lakini ni

kuangalia masuala mazima ya kiuchumi na manufaa kwa jamii na kadhalika. Kwa hiyo, ni kweli tumeruhusu mwekezaji huyu kufanya tathmini ya pili ili tuweze kuona kama yale maeneo ambayo tuliona yatakuwa na athari atayazingatia. Pia na sisi tunafanya tathmini ili kama nchi, tuwe na takwimu za kutosha kuweza kupima na kufanya uperembaji wakati tukipitia hiyo tathmini kutoka kwa mwekezaji na tumepata pia msaada wa *UNEP* ambao wamesema watatusaidia katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tunachoweza kusema ni kipindi ambacho hakitazidi miezi sita. Tutafanya kazi hiyo kwa upande wetu na tutamsubiri mwekezaji, hatujampa *framework* na tunategemea kwamba, kwa sababu ni jambo la manufaa kwa nchi, kuna asilimia arobaini ya Tanzania kama Serikali, Serikali itakuwa na asilimia thelathini na asilimia kumi ya hisa hizo itauzwa kwa wananchi. Kweli ni jambo la manufaa kwa uchumi lakini ni vizuri tukajiridhisha kwamba, haitakuwa na athari na wote tutafaidika.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilielezea kwamba, kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 34; Tume ya Pamoja tayari imekwishaundwa mwaka 2003, ambapo Mwenyekiti wake wa kwanza ni Mheshimiwa Shellukindo, ingawa sheria yake imepita tangu mwaka 1984, Sheria Na. 15, Ibara ya 42. Sasa nikauliza kwamba, kwa mujibu wa Katiba hiyo hiyo kifungu cha 133 na kwa Sheria ile ile inataja akaunti ya fedha ya pamoja. Nimeuliza swali je, akaunti hiyo imekwishafunguliwa na kwa sababu hiyo ni moja ya kero za Muungano ambazo zinapaswa kuondolewa?

Nilitaka pia kujua hisa zikoje katika *BoT*? Tatizo liko wapi na kwamba kama hivyo vitu havipo mpaka leo, huko si kuvunja Katiba makusudi? Naomba ufafanuzi, kama imefunguliwa sina tatizo, kama haijafunguliwa Katiba imevunjwa; kwa nini Katiba inavunjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa hayo ni maoni yako tu, Katiba naisoma hapa haikuweka muda wa mwisho wa kuunda vitu hivyo. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba, Katiba imevunjwa wakati watu bado wanawasiliana na mambo hayo si mepesi. Mheshimiwa Waziri, Katiba haikuvunjwa lakini sasa mbona mnakawia kawia? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunisaidia kufafanua jambo hilo. Najua kwamba, jambo hili ni la siku nyingi sana lakini ni nyeti sana kwa sababu linahusu mchango wa Serikali ya Zanzibar, mchango wa Serikali ya Muungano, mapato, matumizi, hisa kwenye *BoT* na kadhalika. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kwamba, Tume imeundwa, imefanya kazi yake, maoni yao juu ya namna ya mgawanyo huu, upo kwa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, akaunti hii bado haijaanza haina pesa, tusubiri akaunti ianzishwe halafu watu wachangie.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Nashukuru kwa majibu mazuri na kwa kunielewesha kwamba, Katiba haijavunjwa. Nimekubali lakini tangu Tume imeundwa

mwaka 2003 na leo mwaka 2008 na jambo hili ni zuri sana, kuna maendeleo gani au kuna matumaini gani basi kwamba angalau baada ya miaka mingapi huko mbele suala hili litakwisha, maana ni zuri na jinsi tunavyozidi kuchelewa ndivyo kero zinavyozidi kuongezeka; je, litakamilika lini?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Suala hili limekamilika, lipo kwenye ngazi ya Mabaraza ya Mawaziri; Baraza la Mawaziri kwa upande wa Bara na Baraza la Mawaziri la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nadhani wakati wowote itakuwa imekamilika. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Wakati wowote?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ili kuunda akaunti lazima uwe na pesa. Kwa hiyo, kikubwa hapa sio kuunda akaunti; ni kujua vyanzo vya mapato, vyanzo hivyo vimeshaainishwa, vikishaidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa Bara au Serikali ya Muungano ikiidhinishwa na Baraza la Serikali ya Mapinduzi, nadhani wakati wowote akaunti itaundwa na tumeshapanga hata ni nani watakuwa *signatories* wa akaunti hiyo. Nataka kukuhakikishia kwamba, hilo karibu tunalifikisha katika hatma yake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts… … … … … …*Sh. 298,033,400
Kif. 1003 – *Policy and Planning… … … … … … …* Sh. 749,272,000
Kif. 1004 – *Information, Education, Communication Unit… … … … … … … … … … … … …* Sh. 552,214,200
Kif. 1005 – *Internal Audit… … … … … … … … … …* Sh. 152,186,000
Kif. 2001 – *Union Secretariat… … … … … … …* Sh. 24,300,787,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Environment… … … … … … … … … … …* Sh. 6,390,282,200

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 31, Programme 50, Subvote 501, Item 260200* na *Item 260800*. Tukianza na 260200, hapa kunaelekezwa *education material*. Sasa hii ni *environment protection* ambayo nafikiri ni uhifadhi wa mazingira. Nililizungumza nikasema kwamba, kutolewe elimu ya kutosha ili wananchi waelewe umuhimu wa kuhifadhi mazingira, lakini naona fedha iliyotengwa ni Sh. 2,500,000 na hapa kwenye *item* inayofuata ya *training* imewekwa Sh. 2,000,000. Sasa kweli hizi milioni mbili na nusu zitatoa elimu kwa mwaka mzima? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya elimu yapo katika *subvote* 1004, ambayo inazungumzia masuala ya *information, education and communication,* lakini pia katika miradi masuala ya elimu yapo huko na yamezingatiwa katika miradi yote. Kuna mradi

mahususi kabisa kwa ajili ya kutoa elimu ya utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Huo ni mradi mkubwa, una ufadhili wa *DANIDA* na una fedha za kutosha katika programu hii na kama nilivyoeleza katika bajeti yetu, sasa hivi tutakuwa na mkakati mkubwa kabisa wa elimu endelevu kupitia vipindi vya redio, michezo ya kuigiza na vipeperushi vingi sio kama elfu tatu tulivyokuwa tukifanya zamani, lakini mikakati mbalimbali ya kufikisha elimu kama alivyosema Mheshimiwa Komu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration and General…* … … … Sh. 5,685,000,000
Kif. 1003 – *Policy and Planning…* … … … … … … Sh. 500,000,000
Kif. 2001 – *Union Secretariat…* … … … … … … …Sh. 98,474,400
Kif. 5001 – *Environment…* …. … … … … … … Sh. 13,428,518,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa ili kuweka *Hansard* sawa na Bunge letu lisipotoshwe katika *Hansard* zake. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Michezo anasaidia kujibu masuala mbalimbali na ambalo niliinuka kulisemea, alisema kwamba, mimi ni *referee* wa Kimataifa na ni Mechi Kamishna. Kweli ni Mechi Kamishna wa Shirikisho la Mpira la Afrika na Mechi Kamishna wa *FIFA*, halikadhalika ni *instructor* wa *Referees of CECAFA*, lakini Mheshimiwa Waziri akaenda mbali zaidi akasema kwamba, natumwa na *TFF*.

Mheshimiwa Spika, napenda tuweke *Hansard* sawa kwamba, situmwi na *TFF*, mimi ni Mechi Kamishna wa *FIFA*, *CAF* na *CECAFA;* situmwi na *TFF*, naomba *Hansard* ikae sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa hiyo mialiko ya kutoka *FIFA* inapitia wapi, unaletewa moja kwa moja Zanzibar? Hebu fafanua maana yake tunataka kuliweka sawa. *(Kicheko)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Napata mwaliko moja kwa moja kama Hafidh Ali kutoka Zanzibar.

**SPIKA:** Basi ikiwa ni kweli *Hansard* inanukuu hivyo, tukija kuona tofauti, alaa, Mheshimiwa Waziri wa Habari.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa maana ya kuweka kumbukumbu sawa, wanapatikanaje hao Makamisaa; *FIFA* hupeleka taarifa kwa wanachama wa kila nchi na kuwaomba wawapendekeze watu kutoka katika nchi yao, ambao wanaweza kuifanya kazi hiyo. Kamisaa tunayemzungumza kapendekezwa na *TFF*.

Naona sasa limekaa vizuri, kwa hiyo tunaendelea. Mheshimiwa kaa chini tu, hatuwezi kuendelea hivyo. Haiwezekani wewe ndiyo unaalikwa kwa utaratibu wa peke yako. Ni dhahiri *FIFA* inawasiliana na vyombo ambavyo ni wanachama. *(Makofi)*

Hizi ndiyo kero za Muungano. *(Kicheko)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa taarifa, naomba nifanye masahihisho. Nilikosea jina la Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa upande wa Mazingira, anaitwa Ally Khamis Seif siyo Ali Said Salum.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais*
*kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri. Nawashukuru Mawaziri wetu wa Muungano na Mazingira, kwa hoja walizoziwasilisha na jinsi walivyokuja kuhitimisha, kwa kujibu hoja mbalimbali za Wabunge. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, hoja hii haikuwa nyepesi ni nzito, inagusa hisia za Wabunge na Wananchi, lakini nadhani tumeifikisha pazuri. Tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu kwamba, azidi kutusaidia ili Muungano wetu uzidi kuimarika, lakini pia tuweze kuokoa hali ya mazingira ili vizazi vijavyo viweze kuishi katika Tanzania ya kijani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuahirisha Bunge jioni hii kwa kuwa kuna tukio ambalo litahusu Mheshimiwa Rais kuingia humu, yeye si mgeni katika Bunge kwa maana ya Kanuni. Mtaona katika utangulizi wa Kanuni zetu katika yale maeneo ya

ufafanuzi, *interpretation* mgeni maana yake ni mtu yeyote ambaye si Rais na si Mbunge, Katibu au mtumishi yeyote na ambaye hatekelezi kazi rasmi zinazohusu Bunge. Kwa hiyo, huwa hatutengui kanuni kumruhusu Rais kuingia humu, kwa sababu yeye anaingia kama sehemu ya Bunge, ila sasa anapokuja Mheshimiwa Rais haingii humu peke yake, kuna watu ambao hawakutajwa humu kwenye Kanuni nao wanaingia na ni lazima waingie kwa utaratibu na itifaki ya Rais. Isitoshe kesho Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein ataingia humu, sasa yeye inabidi tumwombee ruhusa pamoja na wale wengine.

Ilikuwa pia Jaji Mkuu, Mheshimiwa Agostino Ramadhani awe nasi hapa, lakini kama mnavyofahamu, tumepata habari ya kusikitisha; Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa, Jaji Kaji amefariki dunia hapo jana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jaji Mkuu, inambidi abaki Dar es Salaam dhahiri kusimamia mipango ya mazishi ya Jaji huyo.

Kutokana na hilo pia kuna tatizo la pili, kesho kwa Kanuni si siku ya maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Rais anatua uwanja wa ndege kesho, kipindi kinacholingana na wakati wa maswali. Sasa kwa itifaki, inabidi Mheshimiwa Waziri Mkuu akampokee Mheshimiwa Rais. Kwa yote haya mawili basi, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya Bunge, aweze kutoa hoja kupitia Kanuni ya 150 kutengua Kanuni zinazohusika kwa hayo mambo mawili ili tutakapotengua, shughuli za kesho ziende kwa mujibu wa Kanuni. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na matamshi yako hayo, naomba nitumie Kanuni ya 150(1) ili Kanuni mbili zitenguliwe; kwanza ni Kanuni ya 38, ambayo inahusu maswali kwa Waziri Mkuu kwa sababu ulizozieleza, kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu hataweza kuwa hapa Bungeni kujibu maswali. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Kanuni hii itenguliwe.

Mheshimiwa Spika, pili, kama ulivyoeleza pia kwamba, ataingia Mheshimiwa Makamu wa Rais na wageni wengine watakaoandamana na Mheshimiwa Rais, hivyo, kwa kutumia Kanuni ya 136, naomba pia nayo itenguliwe ili wageni hawa nao waweze kuingia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni zilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa makubaliana hayo, kesho hakutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu na wageni wetu wote watakaokuwa wamefuatana na Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa itifaki, pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais wataingia Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, zaidi ya hivyo, nimewasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ambaye ndiye mtoa hoja wa kesho kwa makadirio ya fedha kwa Wizara ya Mambo ya Nje, amenihakikishia kwamba, hotuba yake ni fupi. Sasa ili tuokoe muda, naomba kusahihisha matangazo yangu ya asubuhi kwamba, baada ya matangazo tuta-*break* kidogo; sivyo hivyo, baada ya matangazo nitamwita mtoa hoja, kwa sababu tunamtarajia Rais muda wa saa tano na kwa kuwa hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje si ndefu na kwa kuwa hapo katikati saa moja itatumika katika shughuli ya Mheshimiwa Rais, tukiahirisha kila kitu tutazidi kukosa hata uchangiaji wa Wizara ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, baada ya matangazo nitamwita Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili aweze kusoma hotuba ya makadirio ya Wizara yake na baada ya hapo ndiyo tutasitisha ili kuweza kupokea wageni halafu utaratibu mwingine utaendelea kwa saa za jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, pamoja na wageni wa Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mbunge wa Mvomero, ambao walikuwa wakija asubuhi hapa, bahati mbaya walipata uharibifu wa gari njiani lakini jioni hii tupo nao hapa. Kwa hiyo, naomba niwatambulishe kama ifuatavyo:-

Wageni wa Mheshimiwa Nibuka ni mkewe, ambaye anaitwa Arafa Khamis, naomba asimame pale alipo na mwanawe ndugu Faisal Mzeru, yule pale amekuja, huyu kweli mwanawe naona kimo ni kile kile. (*Kicheko*)

Wapo pia Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Morogoro Mjini, Mheshimiwa Fikiri Juma, Mwenyekiti, hayupo? Mheshimiwa Nicholaus Mvanga, Katibu wa CCM, Morogoro, yule pale, karibu sana. Ndugu Rukia Bakalemwa, Katibu Msaidizi, Ndugu Kudra Mdengo, Ndugu Hassan Banji, Ndugu Samwel Mhulo, Ndugu Zamoyoni Abdallah, Ndugu Mohamed Lukwele, Ndugu Fatuma Msonga, Ndugu J. J. Kakiziba, Ndugu Thomas Kivuko na Ndugu Mengi Kihanjakiki, sijui jina la Morogoro hili au la Kagera. Basi ndiyo Tanzania yenyewe. Karibu sana Waheshimiwa na tunawashukuru ninyi mliopo katika utumishi wa siasa mnapopenda kuja hapa.

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Suleiman Sadiq ambao ni wanafunzi sitini na tano na Walimu watano kutoka shule ya msingi ya Mtibwa, hawa ndiyo wameondoka, walikuwepo lakini ilibidi kwa muda waliopewa waweze kuondoka.

Baada ya matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.30 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 21 Agosti, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*